SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR








## RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA KIUFUNDI WA MRADI WA USAMBAZAJI WA MIUNDOMBINU YA MAJI SAFI NA SALAMA UNGUJA NA PEMBA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

# KUHUSU UKAGUZI WA KIUFUNDI WA MRADI WA USAMBAZAJI WA MIUNDOMBINU YA MAJI SAFI NA SALAMA UNGUJA NA PEMBA

# KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR**
2 Mtaa wa Tume, 71125 Kilimani Zanzibar, S.L.P 258
Simu/Nukushi: +255 24 223 400, Barua Pepe: info@ocagz.go.tz
Tovuti: www.ocagz.go.tz

**MAREJEO NAM: CAC.132/385/01/4** **TAREHE: 26 MACHI, 2024**

**MHE. DKT HUSSEIN ALI MWINYI,**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI,**
**AFISI YA RAIS IKULU,**
**S.L.P. 437,**
**ZANZIBAR, TANZANIA.**

**KUH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA KIUFUNDI WA MRADI WA USAMBAZAJI WA MIUNDOMBINU YA MAJI SAFI NA SALAMA UNGUJA NA PEMBA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

Ninayo furaha kuwasilisha kwako Ripoti ya Mwaka inayohusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Mradi wa Usambazaji wa Miundombinu ya Maji Safi na Salama Unguja na Pemba kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 kwa mujibu wa kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023.

Naomba kuwasilisha.

Ahsante.

..........................................
**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU**
**WA HESABU ZA SERIKALI**
**ZANZIBAR.**

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

## Mamlaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa za ukaguzi huo angalau mara moja kila mwaka.

## Dira

Kuwa na Taasisi ya ukaguzi iliyo huru na inayoongoza katika kusimamia uwajibikaji na uwazi.

## Dhamira

Kusimamia uwajibikaji wa Taasisi za umma kwa kufanya ukaguzi wa hesabu wenye kuleta tija na kulihakikishia Taifa kwamba rasilimali za Umma zitatumika kama ilivyokusudiwa.

## MISINGI YA MAADILI YA UKAGUZI

1. **Uaminifu** – Kuhakikisha Afisi ina kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala bora unaozingatia Sheria.
2. **Uadilifu** – Kuwa ni Afisi inayozingatia misingi ya uadilifu kwa kutoa huduma bila ya upendeleo.
3. **Kuwa Huru** – Kuwa ni Afisi iliyo huru na inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa Sheria.
4. **Uwezo na Taaluma ya Ukaguzi** – Kuwa ni Afisi yenye kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu.
5. **Kutunza Siri** – Kuwa ni Afisi yenye kutunza siri katika utekelezaji wa kazi zake.
6. **Uwazi na Uwajibikaji** – Kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau ili kuweza kupima uwajibikaji katika matumizi bora ya rasilimali za Umma

# YALIYOMO

YALIYOMO ........ V
ORODHA YA MAJADWELI ........ X
ORODHA YA PICHA ........ XV
VIFUPISHO ........ XVI
SHUKURANI ........ XVII
DIBAJI ........ XIX
MUHTASARI ........ XX
**SURA YA KWANZA** ........ 1
1.0 UTANGULIZI ........ 2
1.1 HISTORIA YA UKAGUZI ........ 2
1.2 CHIMBUKO LA UKAGUZI ........ 2
1.3 MUUNDO WA UKAGUZI ........ 3
1.4 UPEO WA UKAGUZI ........ 3
1.5 VIGEZO VYA TATHMINI ........ 5
1.6 SAMPULI, UKUSANYAJI WA TAKWIMU, NA MBINU ZA UCHAMBUZI WA TAKWIMU ........ 5
1.7 MCHAKATO WA UTHIBITISHAJI WA TAARIFA ........ 8
1.8 VIWANGO VILIVYOTUMIKA KATIKA UKAGUZI ........ 8
1.9 MUUNDO WA RIPOTI YA UKAGUZI ........ 8
**SURA YA PILI** ........ 10
2.0 MFUMO WA USIMAMIZI WA USAMBAZAJI MAJI ZANZIBAR ........ 11
2.1 UTANGULIZI ........ 11
2.2 MFUMO WA SERA NA SHERIA ........ 11
2.3 MALENGO NA MIKAKATI ........ 13
2.4 UHUSIANO KATI YA WATENDAJI WAKUU ........ 14
2.5 MAELEZO YA MIRADI YA MAJI ........ 15

2.6 UGAWAJI WA RASILIMALI ZA FEDHA .......... 16

**SURA YA TATU** .......... 18

3.0 MATOKEO YA JUMLA YA UKAGUZI JUU YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI .......... 18

3.1 UTANGULIZI .......... 18

3.2 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UANZISHWAJI NA UPANGAJI WA MIRADI YA MAJI .......... 18

3.3 MCHAKATO WA UNUNUZI WA MIRADI YA MAJI .......... 21

3.4 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USIMAMIZI WA MKATABA WA MIRADI YA MAJI .......... 25

3.5 KUKAMILIKA KWA MRADI PAMOJA NA UFUNGAJI .......... 26

**SURA YA NNE** .......... 27

4.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA UJENZI WA VITUO VYA UENDESHAJI WA PAMPU ZA MAJI (PUMP CONTROL HOUSE) .......... 28

4.1 UTANGULIZI .......... 28

4.2 MIPANGO ISIYOTOSHELEZA YA UJENZI WA VITUO VYA KUENDESHEA MASHINE ZA MAJI .......... 30

4.3 MCHAKATO WA KUMPATA MKANDARASI HAUKUZINGATIA MATAKWA YA SHERIA YA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA .......... 36

4.4 UTEKELEZAJI WA USIMAMIZI WA MIKATABA YA MIRADI .......... 48

**SURA YA TANO** .......... 53

5.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA UCHIMBAJI NA UJENZI WA VISIMA VIPYA .......... 54

5.1 UTANGULIZI .......... 54

5.2 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA MIPANGO NA USANIFU WA MRADI .......... 55

5.3 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA MAMBO YA UNUNUZI .......... 57

5.4 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USIMAMIZI WA MKATABA .......... 58

**SURA YA SITA** .......... 66

6.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA UJENZI WA MATANGI YA MAJI .......... 67

6.1 UTANGULIZI .......... 67

6.2 MIPANGO NA USANIFU WA MRADI ........ 67
6.3 MANUNUZI YA MKANDARASI ........ 70
6.4 USIMAMIZI WA MKATABA ........ 73
6.5 DOSARI KATIKA USIMAMIZI WA MUDA ........ 74
6.6 DOSARI KATIKA USIMAMIZI WA GHARAMA ZA MRADI ........ 77
6.7 DOSARI KATIKA KUKAMILIKA KWA MRADI PAMOJA NA UFUNGAJI ........ 80

**SURA YA SABA** ........ 82

7.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA KAZI YA UCHIMBAJI NA UFUKIAJI MISINGI ........ 83
7.1 UTANGULIZI ........ 83
7.2 MIPANGO DUNI YA KAZI ZA UCHIMBAJI NA UFUKIAJI WA MISINGI ........ 84
7.3 DOSARI KATIKA MANUNUZI NA MCHAKATO WA UPATIKANAJI WA MKANDARASI ........ 86
7.4 UTEKELEZAJI USIORIDHISHA WA MIRADI KWA KUZINGATIA MUDA, GHARAMA NA UBORA KULINGANA NA MKATABA ........ 87

**SURA YA NANE** ........ 90

8.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA MATENGENEZO YA MATANGI YA MAJI ........ 91
8.1 UTANGULIZI ........ 91
8.2 DOSARI ZILIZOJITOKEZA KATIKA KIPENGELE CHA UNUNUZI ........ 92
8.3 DOSARI KATIKA KIPENGELE CHA USIMAMIZI WA MKATABA ........ 94

**SURA YA TISA** ........ 96

9.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU USAMBAZAJI NA UFUNGAJI WA UMEME ........ 97
9.1 UTANGULIZI ........ 97
9.2 MALIPO YASIYORIDHISHA YA SHILINGI 1,200,000,000 ........ 98
9.3 KUCHELEWA KWA USAMBAZAJI NA UFUNGAJI WA UMEME KATIKA VISIMA VYA MAJI ........ 98

**SURA YA KUMI** ........ 101

10.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU HUDUMA YA USHAURI KATIKA MFUMO WA KUSIMAMIA NA KUDHIBITI UPOTEVU WA MAJI ........ 102

10.1 UTANGULIZI ........ 103
10.2 DOSARI KATIKA UTEKELEZAJI WA MIPANGO ........ 103
10.3 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA UENDESHAJI WA MFUMO ........ 104
**SURA YA KUMI NA MOJA** ........ 106
11.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA HUDUMA ZA USHAURI ELEKEZI PAMOJA NA UJENZI WA MATANGI YA MAJI ........ 107
11.1 UTANGULIZI ........ 107
11.2 DOSARI KATIKA KIPENGELE CHA MIPANGO ........ 108
11.3 DOSARI JUU YA USIMAMIZI WA MKATABA ........ 110
**SURA YA KUMI NA MBILI** ........ 112
12.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA HUDUMA YA USHAURI ELEKEZI NA USIMAMIZI WA UKARABATI NA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAMBAZAJI MAJI ........ 113
12.1 UTANGULIZI ........ 113
12.2 DOSARI KATIKA USIMAMIZI WA USHAURI ELEKEZI ........ 114
**SURA YA KUMI NA TATU** ........ 116
13.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USAMBAZAJI WA MABOMBA YA HDPE KWA LOTI 1 NA LOTI 2 ........ 117
13.1 UTANGULIZI ........ 117
13.2 UPANGAJI WA MIRADI USIYORIDHISHA ........ 118
13.3 DOSARI ILIYOBAINIKA KATIKA MIKATABA YA USAMBAZAJI WA MABOMBA NA VIFAA VYA HDPE ........ 120
13.4 DOSARI KATIKA UTEKELEZAJI WA MKATABA WA MRADI ........ 128
**SURA YA KUMI NA NNE** ........ 135
14.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USAMBAZAJI WA MABOMBA NA VIFAA ........ 136
14.1 UTANGULIZI ........ 136
14.2 DOSARI KATIKA HATI YA MIKATABA ........ 137
14.3 UTEKELEZAJI USIORIDHISHA WA USIMAMIZI WA MKATABA ........ 137

**SURA YA KUMI NA TANO** ........ 139

15.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USAMBAZAJI WA PAMPU ZA VISIMA . 140
15.1 UTANGULIZI ........ 140
15.2 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA UNUNUZI ........ 140
15.3 DOSARI KATIKA UDHIBITI WA UBORA ........ 145

**SURA YA KUMI NA SITA** ........ 149

16.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USAMBAZAJI WA VIFAA VYA MAJI .... 150
16.1 UTANGULIZI ........ 150
16.2 KUSHINDWA KUWASILISHA DHAMANA YA BENKI NA DHAMANA YA UTENDAJI KAZI ........ 150
16.3 MAELEZO YASIOTOSHELEZA YALIYOANDALIWA KWA UNUNUZI WA SLUICE VALVE........ 151

**SURA YA KUMI NA SABA** ........ 153

17.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU USAMBAZAJI WA MITAMBO YA KUCHIMBIA VISIMA ........ 154
17.1 UTANGULIZI ........ 154
17.2 DOSARI ZILIZOBAINIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI........ 154
17.3 UKIUKWAJI WA TARATIBU ZA UTOAJI WA ZABUNI........ 155
17.4 KUCHELEWA KUWASILISHWA KWA MASHINE ZA KUCHIMBIA VISIMA (RIGGS) ........ 156
17.5 DOSARI ILIYOBAINIKA KATIKA MALIPO YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI (VAT) SHILINGI 98,126,285........ 156
17.6 MALIPO YALIYOLIPWA KWA MSAMBAZAJI BILA KUWASILISHA DHAMANA YA BENKI SHILINGI 300,920,608.80........ 157

**SURA YA KUMI NA NANE** ........ 158

18.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USAMBAZAJI WA “GPS RECEIVERS, GENERATORS NA ELECTROFUSION MACHINES” ........ 159
18.1 UTANGULIZI ........ 159
18.2 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA KIPENGELE CHA UNUNUZI ........ 160

## ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli Nambari 1: Orodha ya sampuli ya miradi inayojumuisha miradi ya maji inayofadhiliwa na fedha za UVIKO-19 ............................5

Jadweli Nambari 2: Vitu muhimu vilivyozingatiwa na kuthibitishwa wakati wa uchunguzi wa ziara ya eneo la kazi.................................7

Jadweli Nambari 3:Muundo wa Ripoti ...................................................8

Jadweli Nambari 4: Sheria ya usimamizi wa shughuli za ujenzi..................... 12

Jadweli Nambari 5: Shughuli za Mradi wa Maji........................................... 16

Jadweli Nambari 6: Fedha zilizotengwa na kutolewa kwa ajili ya shughuli za Mradi wa Maji...................................................... 16

Jadweli Nambari 7: Uchambuzi wa utekelezaji wa dhana ya Mradi ................ 19

Jadweli Nambari 8: Kutozingatiwa mapendekezo ya utafiti wa Miamba.......... 20

Jadweli Nambari 9: Wataalamu waliokosekana katika timu ya tathmini.......... 22

Jadweli Nambari 10: Uchambuzi wa mkataba waliopewa wazabuni waliotikia Zabuni .................................................................. 23

Jadweli Nambari 11: Mzabuni aliyepewa mkataba eneo ambalo hakuitikia Zabuni .................................................................. 24

Jadweli Nambari 12:Taarifa ya mkataba wa ujenzi wa kituo cha kuendeshea mashine ya maji kwa Loti ya 1 na Loti .......................... 28

Jadweli Nambari 13: Taarifa ya mkataba wa ujenzi wa vituo ya kuendeshea mashine za maji kwa Loti 3 ......................................... 29

Jadweli Nambari 14: Mabadiliko ya vipimo pamoja na gharama katika uwekaji wa fensi katika vituo vya kuendeshea mashine za maji .. 31

Jadweli Nambari 15: Vipimo ambavyo havikuanishwa katika BoQs ................ 34

Jadweli Nambari 16: Loti zilizotolewa  zabuni kwa Wakandarasi .................... 36

Jadweli Nambari 17: Zabuni ambazo zilizofanyiwa tathmini........................... 38

Jadweli Nambari 18: Loti zilizoombwa na zilizotunukiwa kwa Wakandarasi..... 39
Jadweli Nambari 19: Tofauti katika kielelezo cha kusoma na kiasi cha zabuni. 40
Jadweli Nambari 20: Kiasi cha malipo ya awali na dhamana ya malipo ya awali ..42
Jadweli Nambari 21: Utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ........ 44
Jadweli Nambari 22: Athari za kufanya malipo kwa kuzingatia asilimia........... 46
Jadweli Nambari 23: Hati ya makisio ya gharama za ujenzi na kiasi cha Mkataba........ 47
Jadweli Nambari 24: Uchambuzi wa utekelezaji wa kazi za ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine za maji........ 49
Jadweli Nambari 25: Hali ya malipo kwa Mkandarasi........ 50
Jadweli Nambari 26: Ongezeko la gharama za ziada za upasuaji wa Miamba... 51
Jadweli Nambari 27: Taarifa ya mkataba wa uchimbaji na ujenzi wa Visima vipya ........ 54
Jadweli Nambari 28: Kutozingatia mapendekezo ya utafiti wa Miamba........... 56
Jadweli Nambari 29: Wajumbe wa Kamati ya Tathmini ........ 58
Jadweli Nambari 30: Uchambuzi wa mbinu za malipo........ 59
Jadweli Nambari 31: Malipo yaliyofanywa kwa mkandarasi ........ 59
Jadweli Nambari 32: Uchambuzi wa upimaji wa Visima wa kina (urefu) kwa Unguja........ 60
Jadweli Nambari 33: Uchambuzi wa upimaji wa Visima kwa kina (urefu) Pemba ........ 61
Jadweli Nambari 34: Kiwango cha upatikanaji na uzalishaji wa maji usioridhisha........ 63

Jadweli Nambari 35: Uchambuzi wa upimaji wa Pampu uliofanywa kwa visima vya Sampuli ........ 64
Jadweli Nambari 36: Taarifa za mkataba wa ujenzi wa Mradi wa tangi la maji 67
Jadweli Nambari 37:Tofauti ya idadi ya Nondo kutoka BOQ na idadi halisi ya Nondo ........ 69
Jadweli Nambari 38: Ongezeko la gharama zilizolipwa kwa wakandarasi........ 75
Jadweli Nambari 39: Kuongezeka kwa bei ya mkataba ilitokana na kuongeza kiwango cha Mkandarasi kwa daraja la Zege C40 .......... 78
Jadweli Nambari 40: Ujazo wa zege uliyokadiriwa kutokana na michoro na kiasi kilichoidhinishwa kwa malipo ........ 80
Jadweli Nambari 41: Taarifa ya mkataba kwa ajili ya uchimbaji na ufukiaji wa msingi kwa ajili ya bomba la usambazaji wa maji .......... 83
Jadweli Nambari 42: Taarifa ya mkataba kwa ajili ufukiaji na uchimbaji a mitaro kwa ajili ya kurekebisha bomba la usambazaji wa maji .. 88
Jadweli Nambari 43: Taarifa ya mkataba wa matengenezo ya tangi la maji huko Raha Wete ........ 91
Jadweli Nambari 44: Taarifa ya mkataba wa matengenezo ya matangi ya maji kwa ZAWA........ 92
Jadweli Nambari 45: Muhtasari wa matokeo katika uchunguzi wa awali wa zabuni........ 93
Jadweli Nambari 46: Muhtasari wa matokeo ya awali ya tathmini ya Zabuni... 93
Jadweli Nambari 47:Utaratibu wa malipo ya zabuni kwa mujibu wa mkataba . 95
Jadweli Nambari 48:Nyaraka zinazohitajika kwa malipo kulingana na mkataba: ........ 95
Jadweli Nambari 49: Taarifa za mkataba wa usambazaji na ufungaji wa umeme ........ 97

Jadweli Nambari 50: Uchambuzi wa malipo kwa msambazaji na mfungaji wa umeme ........ 98

Jadweli Nambari 51 :Visima vya mradi vilivyochimbwa kwa Unguja na Pemba ........ 99

Jadweli Nambari 52: Taarifa za mkataba wa huduma ya ushauri na usimamizi........ 102

Jadweli Nambari 53: Uchambuzi wa Wateja wanaotumia na wasiotumia Mita ........ 105

Jadweli Nambari 54: Taarifa za mkataba kwa huduma ya ushauri na usimamizi........ 107

Jadweli Nambari 55: Gharama ya mradi kwa kutumia zege daraja halisi la 40 na daraja la 25 kwa ngazi ........ 109

Jadweli Nambari 56: Uchambuzi juu ya matumizi ya gharama za ziada........ 110

Jadweli Nambari 57: Taarifa za mkataba kwa huduma ya ushauri na usimamizi........ 113

Jadweli Nambari 58: Utaratibu wa awamu za malipo ya utekelezaji wa mradi115

Jadweli Nambari 59: Taarifa za mkataba wa usambazaji wa mabomba ya HDPE Loti ya 1 ........ 117

Jadweli Nambari 60:Taarifa za mkataba kwa ajili ya usambazaji wa vifaa vya HDPE Loti 2........ 118

Jadweli Nambari 61: Uchambuzi wa hali ya wazabuni waliohusika kupewa tuzo ya mkataba ........ 121

Jadweli Nambari 62: Eneo ambalo mzabuni hakuwajibika kupewa tuzo ya mkataba ........ 121

Jadweli Nambari 63: Dosari zilizobainika katika nyaraka za mkataba ........ 122

Jadweli Nambari 64: Tofauti katika asilimia ya malipo ya awali katika hati za Zabuni na hati za mkataba ........ 124

Jadweli Nambari 65: Asilimia ya dhamana ya utendaji kazi katika Zabuni na katika mkataba ........................................................ 125

Jadweli Nambari 66: Kiasi cha mkataba kilichojumuisha VAT na kiasi cha zabuni ambacho hakijajumuisha VAT .................................... 126

Jadweli Nambari 67 : Uchambuzi wa dhamana ya utendaji uliowasilishwa na utendaji unaohitajika katika mkataba ........................ 128

Jadweli Nambari 68: Uchambuzi wa Kiasi kilicholipwa kwa msambazaji kwa loti ya 1 na loti ya 2........................................................ 131

Jadweli Nambari 69: Uchambuzi wa vipimo vilivyofanywa kwenye bomba lililosambazwa ........................................................ 133

Jadweli Nambari 70: Taarifa ya mkataba wa usambazaji wa mabomba na vifaa vyake................................................................ 136

Jadweli Nambari 71: Taarifa ya mkataba wa usambazaji wa pampu ............ 140

Jadweli Nambari 72: Hali halisi ya pampu zilizowasilishwa na wauzaji.......... 147

Jadweli Nambari 73: Maelezo ya mkataba ................................................ 150

Jadweli Nambari 74: Kutokupokelewa kwa Sluice Valve ............................. 152

Jadweli Nambari 75: Malipo yaliyofanyika kwa muuzaji bila kuwasilisha dhamana ya Benki............................................................ 155

Jadweli Nambari 76:Taarifa ya mkataba kwa usambazaji wa GPS Receiver, Electro Fusion Machine............................................ 159

# ORODHA YA PICHA

Picha Nambari 1: Uhusiano kati ya watendaji wakuu katika usimamizi wa huduma za Maji Zanzibar ........ 15

Picha Nambari 2: Kituo cha kuendeshea mashine za maji mbili katika eneo la Mgenihaji ........ 33

Picha Nambari 3: Mchanganyiko wa zege utakao shikilia waya kwenye uzio wa vituo vya Pampu ........ 35

Picha Nambari 4: Maeneo yaliyobainika kujengwa kwa ubora wa kiwango cha chini kwenye eneo la ujenzi lililotembelewa........ 52

Picha Nambari 5: Aina ya Barehole ........ 55

Picha Nambari 6: Ngazi zilizotengwa pembeni ya matangi ya juu ya maji..... 109

Picha Nambari 7: Dondoo ya mchoro uliotumiwa kutoa wingi wa bomba ..... 119

# VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| AO | : | Afisa Mhasibu |
| BoQs | : | Hati za makisio ya gharama za Ujenzi |
| UVIKO– 19 | : | Ugonjwa wa Virusi vya Corona 19 |
| CSR | : | Wajibu wa Jamii |
| EIA | : | Tathmini ya Athari za Mazingira |
| EMP | : | Mipango ya Usimamizi wa Mazingira |
| GCC | : | Masharti ya Jumla ya Mkataba |
| GPS | : | Mfumo wa Nafasi ya Ulimwenguni |
| HDPE | : | Polyethilini ya juu |
| ICT | : | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| ILMS | : | Mfumo wa Usimamizi wa Maktaba Jumuishi |
| IMF | : | Shirika la Fedha la Kimataifa |
| INTOSAI | : | Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi Duniani |
| ISSAIs | : | Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi |
| KW | : | Kilowatt |
| LTD | : | Mdogo |
| MOWEM | : | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| PMU | : | Kitengo cha usimamizi wa ununuzi |
| QTY | : | Kiasi |
| RGoZ | : | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| SAGE | : | Kikundi cha Ushauri wa Mkakati wa Wataalamu juu ya Chanjo |
| SCC | : | Masharti Maalum ya Mkataba |
| TDS | : | Karatasi ya Data ya Zabuni |
| TOR | : | Hadidu Rejea |
| Shilingi /Tsh | : | Shilingi ya Tanzania |
| UPVC | : | Chloride ya Polyvinyl isiyo na plastiki |
| USD | : | Dola ya Kimarekani |
| VAT | : | Kodi ya Ongezeko la Thamani |
| ZAWA | : | Mamlaka ya Maji Zanzibar |
| ZECO | : | Shirika la Umeme Zanzibar |
| ZPPDA | : | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |

## SHUKURANI

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za mara kwa mara anazoendelea kuzichukuwa ikiwa ni pamoja na kuweka msisitizo na kutoa maelekezo katika kufanya marekebisho juu ya dosari mbali mbali zinazobainishwa katika Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali pamoja na hatua anazoendelea kuzichukua kutokana na hoja za ukaguzi zinazoibuliwa kuhusu matumizi ya fedha pamoja na usimamizi wa rasilimali za Umma.

Vile vile napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Viongozi Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwemo Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, pamoja na watendaji mbali mbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano yao wanayokupatia katika utekelezaji wa majukumu yako ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kuwaletea maendeleo endelevu ya nchi yao.

Shukurani zangu za dhati ziende kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kujitolea kwa dhati kujadili na kutoa mapendekezo pamoja na kufuatilia hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuyafanyia kazi mapendekezo yanayotolewa katika Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu kusimamia uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ya watendaji katika sekta mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa kuniunga mkono na kunipa nguvu katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kikatiba, pamoja na jitihada zake anazozichukuwa katika kusimamia misingi ya utawala bora.

Vile vile nitoe shukurani zangu za dhati kwa Bodi ya Utumishi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kusimamia maadili na nidhamu ya wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya kazi zao.

Kwa namna ya kipekee, niwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyengine kuanzia kazi za ukaguzi, ufuatiliaji wa maeneo mbali mbali yaliyokaguliwa hadi kukamilika kwa ripoti hii ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha, nitakuwa mchache wa shukurani kama sitatambua jukumu la vyombo mbali mbali vya habari kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuutambulisha Umma juu ya kazi zinazofanywa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo matokeo na mapendekezo ya kazi hizo huwasilishwa moja kwa moja kwa jamii kupitia vyombo vya habari.

Natumia fursa hii, kuwasihi wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea kuwa na moyo wa dhati katika kufanya kazi kwa bidii na kuongeza mashirikiano kwa ajili ya siku zijazo ili kuendelea kudumisha nidhamu katika utekelezaji wa majukumu yao.

## DIBAJI



Ninafuraha kubwa ya kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi inayohusu Ukaguzi wa kiufundi wa Mradi wa Usambazaji wa Miundombinu ya Maji Safi na Salama Unguja na Pemba kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023. Wasilisho hilo ni kwa mujibu wa Kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria Nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo angalau mara moja kwa kila mwaka.

Ripoti hii imejumuisha mambo mbali mbali yaliyobainika wakati wa ukaguzi ambapo matokeo, athari na mapendekezo ya ukaguzi yameelekezwa kwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini na Mamlaka ya Maji Zanzibar.

Kwa Mujibu wa Mamlaka niliyonayo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ni jukumu langu la kutoa taarifa huru, zilizosahihi na zilizojitosheleza kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusiana na usimamizi wa fedha, matumizi sahihi ya rasilimali za Umma pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hatimae taarifa hizo kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa hatua za utekelezaji.

Ripoti hii inajumuisha mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa kiufundi wa mradi wa usambazaji wa miundombinu ya maji safi na salama katika maeneo ya Unguja na Pemba ambapo nilifanya tathmini kwa kuangalia taarifa za fedha pamoja na nyaraka mbalimbali zinazohusika na miradi, mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu za michakato ya manunuzi na uzingatiaji wa Sheria na Kanuni mbali mbali.

Napenda kuchukuwa fursa hii kuwashukuru wafanyakazi wangu kwa kujitolea kufanya kazi ya ukaguzi pamoja na Uongozi wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini na Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa kutoa ushirikiano wao mzuri ambao umewezesha kukamilisha ripoti hii kwa wakati.

.......................................

**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**
**ZANZIBAR**

## MUHTASARI

### Historia ya Taarifa

Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar ina jukumu la kuhakikisha kunakuwa na huduma ya maji Safi, Salama na ya uhakika kwa wakaazi wa Zanzibar. Wizara inasimamia upangaji, uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji, ikiwa ni pamoja na ujenzi na utunzaji wa mifumo ya usambazaji maji, uchimbaji wa visima vya kalbi na visima vya drili. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepokea fedha kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya kuendeleza ustawi wa jamii wa Taifa chini ya UVIKO-19 na ilikusudia kutumia kuimarisha mfumo wa usambazaji maji.

Chanzo kikuu cha upatikanaji wa maji umetokana na uchimbwaji wa visima 560 Ungula na Pemba. Urefu wa mtandao wa usambazaji wa maji ni Kilomita 3,235. Hata hivyo, chini ya kuimarisha mfumo wa usambazaji wa maji, uzalishaji uliotarajiwa ulikuwa unaongeza uzalishaji wa maji kwa lita 53,264,400 kwa siku. Mtandao wa usambazaji maji kilomita 319 na uhifadhi wa maji kwa lita 9,250,000.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ilipokea jumla ya shilingi 34,200,000,000 kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Fedha (IMF) kuelekea gharama za kuboresha huduma za kijamii chini ya Mradi wa UVIKO-19. ZAWA ilitenga fedha hizo kwa miradi 18 yenye lengo la kuboresha upatikanaji wa maji Zanzibar. Mradi huo ulijumuisha Usambazaji wa vifaa vya maji kama vile Mabomba na vifaa, Pampu, Tangi la Maji, Jenereta, Mashine za kuungia mabomba ya maji (Fusion Machine), na Mitambo ya kuchimbia visima (Rigs). Pia ilihusisha ujenzi wa Matangi ya kuhifadhia maji, Vituo vya kuendeshea mashine ya maji, na Kuchimba visima (Boreholes).

### Lengo na Upeo wa Ukaguzi wa Kiufundi

Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini kama ujenzi wa miradi ya maji Zanzibar ilifanyika kwa ufanisi kwa kuzingatia muda, gharama, upeo na ubora ili kuwezesha kufikia malengo yaliyokusudiwa ya mradi.

Ukaguzi ulizingatia: upangaji wa mradi na usanifu, ununuzi wa vifaa, bidhaa na huduma;makisio, utoaji na matumizi ya fedha za mradi, utekelezaji wa miradi, Usimamizi, na mazingira, usalama na mahitaji ya jamii.

Taasisi zilizokaguliwa ni Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ambazo zilihusika na ujenzi na ununuzi wa vifaa vya usambazaji maji vilivyotekelezwa kupitia Fedha za UVIKO-19.

Ifuatayo ni muhtasari wa hoja kuu za ukaguzi, hitimisho na mapendekezo yaliyotolewa kutoka katika Ukaguzi huu.

## a) Mipango ya Mradi na Usanifu

### Mipango isiyoridhisha ya utekelezaji wa mradi

Ukaguzi ulibaini masuala yafuatayo yanayohusiana na upangaji wa mradi, Upeo usioridhisha wa shimo la Maji taka na Ukubwa wa Uzio katika Ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine za maji.

Ziara tofauti zilizofanyika katika kituo cha Mgenihaji zilibaini kuwa kulikuwa na vituo viwili vya kuendeshea mashine ya maji (Pump Control House) ambavyo vilikuwa karibu sana na vituo vyote viwili na vinatumia shimo moja la maji taka licha ya kwamba mkataba ulibainisha kila kituo cha pampu kuwa na shimo tofauti la maji taka. Kulikuwa na Hatari ya kulipa zaidi ya kiasi cha shilingi 5,980,000 ikijumuisha na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa shimo la maji taka ambalo halikujengwa ambalo lilionyeshwa katika vipengele vya Mkataba ambalo litajengwa katika kila kituo cha kuendeshea mashine ya maji.

Kwa upande mwingine, uhakiki wa eneo la uzio uliojengwa ulibaini ukubwa wa uzio huo haukuwa sawa kama ulivyopangwa kutokana na kuwepo kwa mabadiliko ya urefu wa uzio na idadi ya Nguzo za zege zilizotengenezwa tayari kwa vituo vya pampu zilizojengwa. Hali hii imetokana na Dhana kwamba, eneo lote lilikuwa na ukubwa sawa wa kiwanja wakati viwanja ni tofauti. Hali hii imesababisha ongezeko lisilo la lazima la gharama ya mkataba kwa fungu 3 la kiasi cha shilingi 57,623,569.60 na shilingi 17,440,745.59 kwa fungu 1 na 2 ambalo linaweza kuokolewa na ZAWA.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kufanya ufafanuzi wa kazi iliyofanywa na kurejesha kiasi chote kilicholipwa kwa kazi isiyofanywa kutokana na kupungua kwa ukubwa wa uzio na kwa ajili ya ujenzi wa shimo la maji taka na kuwa na upeo wa kutosha wa kazi katika utekelezaji katika mradi wake ili kuepusha upeo wa juu.

### Mipango isiyotosheleza ya utekelezaji wa mradi wakati wa uchimbaji wa visima

Ripoti ya Utafiti wa miamba ya uzalishaji maji (Hydrogeological) ilipendekeza kwamba visima vitachimbwa kwa kipenyo cha inchi 14 (355mm), na kukamilika kwa inchi 12 kwa mabomba ya UPVC. Ukaguzi ulitembelea eneo la visima vilivyojengwa na kubaini kuwa, visima vilivyochimbwa Unguja vilikuwa na

kipenyo cha nje cha 11 na kipenyo cha ndani cha 10 na visima kwa upande wa Pemba vilikuwa na ukubwa tofauti wa kipenyo kutoka 11" nje na 10" ndani hadi 8" nje na kipenyo cha ndani cha 7" ambacho kilikuwa chini ya kipenyo kilichopendekezwa. Hii imepelekea kupunguzwa kwa ukubwa wa pampu inayoweza kuzamishwa na kutumika katika visima kama hivyo kwa sababu kipenyo cha visima kina ushawishi juu ya uteuzi wa pampu zitakazotumika. Pia, kupunguza kipenyo cha visima hupunguza matengenezo ya visima kwa kupunguza na uingizaji mpya wa mabomba ya UPVC.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kuhakikisha unazingatia ipasavyo uchunguzi wa kijiolojia unaofanywa kwa ajili ya uzalishaji wa maji ili kukabiliana na mahitaji na wingi wa maji.

**Ukosefu wa Tathmini ya Mahitaji ya Maji**

Ukaguzi haukupatiwa tathmini iliyofanyika ili kubaini wingi wa mahitaji ya maji na uwezo wa chanzo kabla ya kupima uwezo wa Matangi ya kuhifadhia maji yaliyopendekezwa. ZAWA ilipendekeza ujenzi wa Matangi kumi ya Maji yenye uwezo wa lita 1,000,000 kila moja bila kuwa na msingi wa uwezo wa Tangi uliopendekezwa.

Hadidu Rejea (TOR) za huduma ya mshauri zilifafanua kuwa, mshauri alipewa kazi ya kufanya uchunguzi wa miamba, kupendekeza aina ya nyenzo, usanifu na kuandaa hati ya zabuni kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa tangi la maji. Hata hivyo, maeneo, ujazo, aina ya tangi ilitambuliwa na ZAWA bila kuwa na uchambuzi wa mahitaji. Ujenzi wa tangi la maji bila kufanya tathmini juu ya mahitaji ya maji na usambazaji ulileta hatari ya kuzidi au kupungua kwa uwezo wa tangi kwa sababu mahitaji ya maji ya jamii hayakujulikana.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa tathmini juu ya mahitaji ya maji na usambazaji inafanywa ili kukadiria uwezo wa tangi la kuhifadhi maji.

**Ubunifu uliopitiliza wa Ujenzi wa Ngazi iliyoimarishwa kwa tangi la maji**

Wakati wa mapitio ya Miundo ya ngazi ilibainika kuwa, ngazi ilitengenezwa kwa muundo wa zege iliyoimarishwa na saruji daraja la C40. Jumla ya muundo wa zege iliyoimarishwa kwa ngazi ilikuwa 350$m^3$ iliyogharimu kiasi cha shilingi 259,424,470.

Kwa upande mwingine uchambuzi wa Wakaguzi wa muundo wa ngazi kwa kutumia daraja la C25 ulifafanua kuwa, ngazi inaweza kutengenezwa kwa

kutumia daraja halisi la C25 na inaweza kukidhi utendaji uliokusudiwa kwa muundo na huduma. Kwa kuwa ngazi haikubeba mzigo wowote isipokuwa uzito wake binafsi na mzigo wa watembea kwa miguu tu, usanifu wa kutumia daraja la zege la C40 ilikuwa hauhitajiki.Kwa kutumia daraja halisi la C25 gharama inaweza kupunguza gharama za mradi kwa shilingi 131,384,470. Hii ilihusishwa na ukaguzi duni wa ripoti za miundo zilizowasilishwa na mshauri ili kuangalia ikiwa zinakidhi matumizi yote yaliyopendekezwa ya muundo na kukidhi mahitaji yote ya mteja.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kwamba miundo ya maji inaundwa ili kukidhi kiwango kinachokubalika cha utoaji huduma na mipaka ya mwisho bila Usanifu wa miundo iliyopitiza.

### b) Ununuzi wa Vifaa, Mshauri Elekezi na Mkandarasi

**Utoaji wa Mkataba kwa Mzabuni asiyestahiki na ambaye hakupendekezwa katika Ripoti ya Tathmini.**

Ripoti ya Tathmini ya Mikataba na Tathmini ilibainisha kuwa, ripoti ya tathmini ya kazi za Uchimbaji na Ujazaji wa misingi ilipendekeza M/S Kifaru Investment Ltd kwa loti zote nne kwa shilingi 2,675,822,950 na alikuwa mzabuni peke yake aliyestahiki kati ya wazabuni 4 waliowasilisha zabuni. Hata hivyo, mkataba huo alipewa M/s Masonry Building Contractor kwa Loti ya 3 tu kwa shilingi 565,112,300 ambae kwa mujibu wa ripoti ya tathmini hakuwasilisha taarifa ya fedha iliyokaguliwa.

Pia, katika mkataba wa usambazaji wa vifaa kwa ajili ya Matengenezo ya Matangi ya Maji, wazabuni wawili waliwasilisha zabuni zao ambao ni, M/S Sapphire Engineering (T) Limited na M/S Mao General Supplier. Wakati wa tathmini wauzaji wote hawakustahiki kupewa zabuni kutokana na kutokukidhi vigezo ambapo kamati ya tathmini ilipendekeza kuitishwa upya kwa zabuni. Hata hivyo, ZAWA ilimpa mkataba Sapphire Engineering Limited kinyume na mapendekezo kutoka kwa kamati ya tathmini.

Kwa Mkataba wa usambazaji wa pampu, kamati ya tathmini ilipendekeza M/S INFRASOL LTD kupewa mkataba wa usambazaji wa Pampu (Submersible). Hata hivyo, ilibainika kuwa mkataba huo ulipewa M/S Sanfransisco LTD kwa loti ya 1 na 4 na M/S Pump for Africa LTD ilipewa loti ya 2, 3 na 5 bila ya uhalali wowote. Wauzaji waliopewa walikuwa wazabuni wasiostahiki kwani walibadilisha mahitaji ya zabuni.

Utoaji wa zabuni kwa wasiostahiki ulihusishwa na tathmini duni ya zabuni zilizowasilishwa. Hii iliiweka ZAWA hatarini kwani mkandarasi aliyepewa tuzo anaweza kushindwa kutekeleza majukumu yake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha uanzingatia mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti ya tathmini wakati wa utoaji wa mkataba ili kuepuka kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma kwa kumteua mzabuni asie na sifa na hatimae kupelekea kushindwa kutekeleza matakwa ya mkataba.

**Kutokuwepo kwa wataalamu wa kutosha katika Kamati ya Tathmini**

Ukaguzi ulipitia ripoti ya tathmini ya zabuni ya mkutano wa Bodi ya Zabuni uliofanyika tarehe 31 Agosti, 2021 na kubainisha kuwa Kamati ya Tathmini ina wajumbe sita kama ilivyowasilishwa na kitengo cha usimamizi wa manunuzi (PMU) lakini baadhi ya wataalamu wamekosekana katika Kamati hiyo, kwa mfano wataalamu wa kisheria, wataalamu wa uchambuzi wa fedha kwa mujibu wa kifungu nambari 32 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016. Hii ilisababishwa na dharura na muda mdogo wa maandalizi ya zabuni ambapo uwezekano mdogo wa kuajiri wataalamu hao ulitokana na uchache wa wataalamu wenye sifa waliopo ZAWA.

Ukosefu wa wataalamu katika timu ya tathmini ulisababisha uchambuzi usiotosheleza wa sehemu ambazo zilihitaji tathmini kamili na taaluma inayohitajika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unazingatia upatikanaji wa wataalamu wenye sifa katika kamati ya tathmini kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

### c) Utekelezaji wa Mradi

**Msambazaji Kutokuwasilisha Dhamana ya Utendaji Kazi**

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa katika mkataba wa usambazaji wa pampu, mabomba na vifaa, Mitambo ya kuchimbia visima, mabomba ya HDPE na vifaa, na Ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine ya maji, mzabuni wa tuzo alitakiwa kuwasilisha dhamana ya benki isiyo na masharti. Hata hivyo, Wazabuni wote hawakuwasilisha dhamana inayohitajika.

Kwa ujenzi wa matangi ya maji, wakandarasi waliwasilisha dhamana ya utendaji kazi kulingana na mahitaji, hata hivyo ukaguzi umebaini dhamana zilizowasilishwa zilipitwa na muda wa matumizi na hadi ukaguzi unakamilika

hakukuwa na jitihada iliyofanywa ya kuhakikisha kunawekwa dhamana mpya inayoendana na muda wa matumizi kwa mazingatio ya kwamba mradi bado unaendelea.

Kutowasilisha dhamana kulihusishwa na usimamizi usiojitosheleza wa utekelezaji wa mkataba ili kuhakikisha uwasilishaji wa wasambazaji kulingana na mkataba unatekelezwa na ilisababisha Ukosefu wa Ulinzi wa Fedha za Mkataba kwa sababu lengo la dhamana ya utendaji kazi lilikuwa kuilinda kisheria (ZAWA) kutokana na upotezaji wa fedha ikiwa mkandarasi atashindwa kutimiza majukumu yake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa, dhamana ya utendaji inawasilishwa na wakandarasi na wauzaji na kuongezewa muda iwapo zimemaliza muda wake.

**Kuchelewa kukamilika mradi kwa wakati**

Mapitio ya mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kuendeshea mashine ya maji ilibainisha kuchelewa kukamilika kwa miradi ikilinganishwa na tarehe iliyopangwa. Ukaguzi umebaini jumla ya miradi 12 kwa loti ya 1 na 2 ilibainika kutokamilika kwa wakati, na kwa upande wa loti ya 3 ukaguzi umebaini miradi ilichelewa kukamilika kwa takriban miezi 8.

Katika mkataba wa ujenzi wa visima, ukaguzi umebaini hadi kufikia Juni, 2023 ucheleweshaji wa kukamilika kwa miradi ulikuwa takriban miezi 10 ambapo kwa ujenzi wa Matangi ya maji kulikuwa na ucheleweshaji wa takriban siku 191 ambazo zilihesabiwa kuanzia tarehe 31 Disemba, 2022 hadi tarehe 10 Julai, 2023. Uchelewaji huo ulitokana na upatikanaji wa vifaa hafifu katika eneo la mradi lililopelekea kutokutekelezeka kwa mradi kwa wakati, kuchelewa kukabidhiwa kwa eneo kwa wakandarasi wa ujenzi wa vituo kutokana na kuchelewa kukamilika kwa kuchimba visima. Vifaa muhimu vya kuharakisha kazi kama vile kreni ya mnara haikuhamishwa na mkandarasi wa ujenzi wa tangi la maji.

Ucheleweshaji huo ulisababisha gharama ya nyongeza ya shilingi 41,157,500 iliyotokana na ZAWA kwa ajili ya kodi na matengenezo ya vituo na Afisi kwa Mhandisi kwa mkataba wa ujenzi wa Matangi ya maji, Gharama za ziada za shilingi 161,547,783.33 zilizotumika na ZAWA ili kuongeza muda wa usimamizi wa mshauri katika Ujenzi wa Matangi ya maji.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unamsimamia mkandarasi kwa ufanisi ili kuhakikisha kuwa mradi unatekelezwa ndani ya muda uliopangwa.

**Kubadilisha Viwango vya zege katika hati ya makisio ya gharama za Ujenzi (BoQs) ambayo iliongeza bei ya Mkataba kwa shilingi 1,474,240,021.75 ikijumuisha na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)**

Mapitio ya Hati ya makisio ya gharama za ujenzi, kwa ajili ya ujenzi wa matangi ya maji ilibainisha kuwa, mkandarasi aliahidi kujenga daraja la zege la C40 kwa kiwango cha Shilingi 450,000 kwa mita za ujazo kwa Matangi manne ya Bubwini, Unguja Ukuu, Mgenihaji, Bambi Uroa kwa upande wa Unguja, na shilingi 460,000 kwa mita za ujazo kwa tangi moja la Tumbatu kwa upande wa Unguja, na Shilingi 540,000 kwa kila mita za ujazo kwa Matangi manne ya Pujini, Makangale, Chanjaani, na Shumbamjini kwa upande wa Pemba pamoja na shilingi 550,000 kwa kila mita za ujazo kwa tangi moja la Kiwani kwa upande wa Pemba.

Mapitio ya taarifa za kikao kwa ajili ya Mkutano wa Kiufundi nambari 3 uliofanywa tarehe 20 Febuari, 2023 umebaini kuwa ZAWA pamoja na Mshauri na Mkandarasi walikubaliana kuongeza kiwango kilichonukuliwa na mkandarasi kwa kutupatia daraja halisi la C40 kutoka shilingi 540,000 hadi shilingi 734,369.01 kwa Matangi yote matano kwa upande wa Pemba, kutoka shilingi 450,000 hadi shilingi 714,460.00 kwa matangi manne (4) kwa upande wa Unguja, na kutoka shilingi 460,000 hadi shilingi 853,979.36 kwa Tangi moja la kisiwa cha Tumbatu ambapo nyongeza ya mabadiliko hayo ilisainiwa tarehe 19 Aprili, 2023.

Kwa mujibu wa nyongeza ya mkataba iliyosainiwa ilieleza ya kwamba sababu iliyotolewa ya kubadilisha viwango vya zege ilitokana na kuagiza mchanga kutoka Tanzania Bara kwa ajili ya ujenzi wa daraja la zege la C40 jambo ambalo lilipelekea kuongezeka kwa gharama za mradi. Ongezeko la gharama hizo ni kinyume na masharti ya mkataba kwani mkandarasi hakustahiki kuongeza daraja lenye kiwango cha C40 kutokana na hati ya zabuni ambayo ilisambazwa kwa mkandarasi ilibainisha kwamba zege inapaswa kujengwa katika kiwango halisi cha daraja la C40.

Kutokana na dosari iliyobainishwa hapo juu ukaguzi umebaini dosari hiyo imesababishwa na usimamizi duni wa mkataba ambao ulisababisha kukubalika kwa pendekezo la mkandarasi juu ya marekebisho ya bei ambayo ilikuwa kinyume na uhalisia wa mkataba jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama za shilingi 1,414,346,394.65 pamoja na VAT ambazo zililipwa kwa mkandarasi kinyume na masharti ya jumla ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa hakuna mabadiliko katika viwango vilivyowasilishwa na wakandarasi au wauzaji baada ya kusaini mkataba kulingana na masharti ya mkataba.

**Kujitokeza kwa hasara ya shilingi 928,153,089.48**

Mapitio ya mkataba wa ujenzi wa visima ilibainisha kuwa hati ya makisio ya gharama za ujenzi (BoQs) ilikuwa na bei inayozingatia kina kilichochimbwa ambacho ni mita 150. Uhakiki wa ziara ya eneo la mradi (site visit) ulibaini kuwa visima vilivyojengwa vilikuwa na kina kutoka mita 17 - 98. Hata hivyo, wakati wa malipo kupunguzwa kwa kina hakukuzingatiwa ili kupunguza kina kisichochimbwa katika kiasi kilicholipwa kwa mkandarasi. Malipo hayo yalifanywa kwa mkandarasi kwa kiasi cha fedha za ziada hivyo mkandarasi alipokea kiasi cha ziada ikilinganishwa na kazi iliyotekelezwa. Uchambuzi wa mkaguzi ulionesha kuwa, kulikuwa na kina cha mita 3309.49 ambazo hazijachimbwa na kiasi cha shilingi 928,153,089.48 ambazo zililipwa kwa mkandarasi kinyume na masharti ya mkataba.

Hii ilisababishwa kushindwa kwa ZAWA kuhakikisha kuwa, malipo kwa mkandarasi hufanywa kulingana na kina halisi cha kuchimba na ukubwa wa visima vilivyojengwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha ulipwaji wa fedha unaendana na utekelezaji halisi wa kazi, hata hivyo ni vyema jitihada za urejeshwaji wa fedha za ziada zilizolipwa zinachukuliwa ili kuokoa fedha za umma.

**Ufikiaji duni wa Malengo ya Mfumo Jumuishi wa Kudhibiti Uvujaji Maji ulioandaliwa na Chuo cha Maji (ILMS)**

Kulingana na ukaguzi wa Muongozo wa uendeshaji wa mtumiaji wa mfumo (ILMS) ilibainika kuwa Mfumo jumuishi wa Udhibiti wa Uvujaji haukuwa na uwezo wa kutoa mfumo mzuri wa usimamizi wa maji kwa kiasi cha maji ya kuvuja. Mfumo huo uliweza kugundua uhusiano wa wateja kwa muda wa muunganisho wa wateja wenye mita na wasio na mita. Mahojiano na afisa wa ZAWA, yalibaini kuwa usimamizi wa kuvuja kwa maji haukuhusishwa katika ILMS kwa sababu inahitaji ufungaji wa kifaa cha utambuzi (sensor) katika mpango wa usambazaji wa maji ambao utafuatilia matumizi ya maji na kuwezesha hesabu ya kuvuja kwa kiasi cha maji na matibabu ya ubora wa maji.

Ukosefu wa uwezo wa mfumo (ILMS) kufuatilia kuvuja kwa maji kwa usimamizi duni wa matumizi ya maji na uzalishaji hivyo kupunguza uwezekano wa ZAWA kufuatilia maji yanayopotea ambayo yanaweza kusababisha kupoteza mapato ya Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kwamba unaweka ufungaji wa kifaa cha utambuzi (sensor) kwa ajili ya kufuatilia upotevu wa maji unaotokana na baadhi ya miundombinu kumwaga maji ovyo katika miradi ya usambazaji wa maji.

**Hitimisho la Jumla**

Kutokana na ukaguzi huu ni kwamba, Mamlaka ya Maji Zanzibar haikusimamia ipasavyo usambazaji wa ujenzi wa vituo vya usambazaji maji vinavyotekelezwa chini ya fedha za UVIKO-19 ili kuhakikisha upatikanaji wa thamani ya fedha. Hii ilithibitishwa na mipango duni ya miundo ya miradi ambayo tathmini ya mahitaji ya maji ilibainishwa, muundo wa kiwango kilichopitiliza wa ngazi za zege uliyoimarishwa kwa Matangi ya maji, na upungufu wa kutosha katika ujenzi wa vituo vya pampu.

Katika ununuzi wa ziada wa wasambazaji ulifanyika kwa mujibu wa Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ambapo vifaa vilivyopewa na wakandarasi havikupendekezwa na kamati ya tathmini. Pia, wazabuni ambao zabuni zao zilizowasilishwa hawakufuata masharti ya zabuni walipewa mikataba badala ya kuondolewa kama wazabuni wasio na sifa.

Aidha, wakati wa utekelezaji, mradi haukusimamiwa vya kutosha ambapo kulikuwa na njia duni za malipo katika ujenzi wa visima na ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji ambazo ulisababisha hasara ya shilingi 928,153,089.48 katika vituo vilivyowekwa pampu za ujenzi, Mabadiliko ya viwango vya mkandarasi kwa daraja halisi la C40 katika ujenzi wa matangi ya kuhifadhia maji ambayo yameongeza gharama za mradi kwa shilingi 1,474,240,021.75 ikijumuisha VAT, kuchelewa kukamilika kwa miradi inayosababisha kuongezeka kwa gharama za mradi kwa shilingi 202,705,283.33 katika ujenzi wa matangi ya maji.

# SURA YA KWANZA



# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Historia ya Ukaguzi

Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar ina jukumu la kuhakikisha kunakuwa na huduma ya maji safi na salama ya uhakika kwa wakaazi wa Zanzibar. Wizara inasimamia upangaji, uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji, ikiwa ni pamoja na ujenzi na utunzaji wa mifumo ya usambazaji maji, visima vya kalbi na visima vya kisasa vya kuchimba kwa drili. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepokea fedha kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya kuendeleza ustawi wa jamii wa Taifa chini ya UVIKO-19 na ilikusudia kuimarisha mfumo wa usambazaji maji.

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ambayo ilianzishwa chini ya Sheria. Na. 4 ya mwaka 2006, ZAWA ni taasisi yenye mamlaka ya kusimamia kwa ujumla huduma za usambazaji maji na usimamizi wa rasilimali za maji Zanzibar. Mamlaka inafanya shughuli zake za kila siku chini ya Bodi ya Wakurugenzi.

Chanzo kikuu cha maji kwa Zanzibar ni maji ya ardhini yaliyotokana na visima 560 vya kina kirefu vilivyoko katika visiwa vyake vikuu (Unguja na Pemba). Urefu wa mtandao wa usambazaji wa maji ni kilomita 3,235. Hata hivyo, chini ya kuimarisha mfumo wa usambazaji wa maji uzalishaji uliotarajiwa ulikuwa unaongeza uzalishaji wa maji kwa lita 53,264,400 kwa siku, mtandao wa maji uliohusishwa ni kilomita 319, na uhifadhi wa maji kwa lita 9,250,000.

## 1.2 Chimbuko la Ukaguzi

Uamuzi wa kufanya Ukaguzi wa Kiufundi ulichochewa na mambo mawili makuu ambayo ni nyenzo kwa kiasi cha fedha kilichotolewa na ustawi wa jamii usiotosha juu ya upatikanaji wa maji. Taarifa hizo ni kama zilivyoelezwa kwa kina hapo chini:

### a) Kiasi kikubwa cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya miradi ya maji

Kupitia mwaka wa fedha (2022/2023) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitenga kutumia jumla ya shilingi Bilioni 34.2 kwa ajili ya usambazaji na ujenzi wa miradi ya maji kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa usambazaji maji kupitia fedha za UVIKO-19 zinazolenga kukuza uhifadhi wa maji na matumizi endelevu ya rasilimali za maji.

### b) Ukosefu wa Ustawi wa Jamii juu ya Upatikanaji wa Maji

Kulingana na makadirio yaliyofanywa na ZAWA wastani wa asilimia 55 ya maji ilizalishwa kwa Unguja na Pemba kabla ya mgao wa fedha za UVIKO-19 kwa kuimarisha mfumo wa usambazaji wa maji. Ingawa baada ya utekelezaji wa mradi wa mfumo wa usambazaji maji, ilikadiriwa kuwa uzalishaji wa maji utaongezeka hadi asilimia 71.

## 1.3 Muundo wa Ukaguzi

### 1.3.1 Lengo la Ukaguzi wa Kiufundi

Lengo la ukaguzi ni kutathmini kama ujenzi wa miradi ya maji Zanzibar ulifanyika kwa ufanisi kwa kuzingatia muda, gharama, upeo na ubora ili kuwezesha kufikia malengo yaliyokusudiwa ya mradi.

### Malengo Maalum

Malengo mahususi ya ukaguzi ni kufanya tathmini kama Wizara ya Maji na Nishati kupitia ZAWA ilihakikisha kuwa:

a) Mipango na usanifu wa miradi ya maji ulifanyika vya kutosha ili kuwezesha kufikia malengo ya mradi;
b) Mchakato wa ununuzi wa Washauri Elekezi, bidhaa na huduma kwa mradi ulifanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni husika za ununuzi;
c) Makisio, utoaji na matumizi ya fedha za mradi ulifanyika kwa mujibu wa miongozo ya kifedha;
d) Utekelezaji wa miradi unafanywa kwa ufanisi ili kufikia muda wa kukamilika, gharama na ubora unaotarajiwa kulingana na masharti ya mkataba; Na
e) Kuendeleza na kutekeleza kikamilifu hatari zinazohusiana na mazingira, usalama na athari za kijamii wakati wa utekelezaji kulingana na mahitaji ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, sheria ya Afya na Usalama Kazini na masharti ya mikataba.

## 1.4 Upeo wa Ukaguzi

Ukaguzi wa Kiufundi ulizingatia mzunguko muhimu wa mradi unaojumuisha usimamizi wa mambo yanayohusiana na mipango, Usanifu, kifedha, ununuzi, usimamizi wa mkataba, kiufundi, mazingira, usalama na athari za kijamii kwenye miradi ya maji iliyotekelezwa.

Hii ilihusisha kukagua na kutathmini michakato na jinsi miradi ilivyopangwa, iliyoundwa, ilivyonunuliwa, kutekelezwa, na pale inapokamilika na kufungwa. Timu ya Ukaguzi pia ilithibitisha viwango vya muundo vilivyotumika, vipimo, ubora na kazi na sehemu zilizojengwa mradi, ubora wa ufundi pamoja na utendaji wao.

Chini ya kipengele cha usimamizi wa kifedha, Timu ya ukaguzi ilitathmini, ufanisi katika utoaji na matumizi ya mfuko wa miradi iliyopangwa/iliyoidhinishwa, kutosha na ufanisi wa udhibiti wa ndani wa kifedha na kuzingatia kanuni za kifedha zinazoongoza na hali ya malipo kama ilivyoonyeshwa katika nyaraka za mradi husika. Uchunguzi wa akaunti ya mwisho ikiwa ni pamoja na utunzaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na madai ya fidia za kazi pia ulihusisishwa.

Kipengele cha usimamizi wa ununuzi kilihusisha tathmini ya uzingatiaji wa taratibu za ununuzi na utoaji wa mikataba kama ilivyoainishwa katika Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 na Kanuni zake za 2020 au sheria yoyote husika au miongozo kama ilivyoonyeshwa katika nyaraka za mradi husika. Shughuli kama vile bajeti ya manunuzi na mipango ya ununuzi, utoshelevu wa uandaaji wa nyaraka za zabuni, mchakato wa zabuni, tathmini ya zabuni na mkataba waliopewa wakandarasi na washauri ikiwa ni pamoja na kusaini mikataba ilizingatiwa. Kipengele cha kiufundi, kilihusisha kutathmini ubora na wingi wa matokeo ya mradi na vifaa vilivyotumiwa kwa kutathmini usahihi na usahihi wa kupanga, Usanifu, kufuata viwango vilivyokusudiwa, ubora wa kazi na utendaji wake. Wakaguzi pia walitathmini utoshelevu na uzingatiaji wa mifumo ya uhakiki wa ubora wa mradi ama udhibiti.

Kwa kufanya hivyo, Wakaguzi walifanya ukaguzi wa kutembelea eneo la mradi wa kazi zilizotekelezwa, mapitio ya matokeo ya vipimo vya maabara ya vifaa na sehemu za kazi zilizokamilishwa. Kama sehemu ya kipengele cha kiufundi, Timu ya Ukaguzi ilifanya vipimo visivyo vya uharibifu wa kazi na miundo iliyojengwa. Kuhusu kipengele cha usimamizi wa mkataba, Timu ya Ukaguzi ilitathmini utoshelevu wa mifumo na michakato ya kusimamia utoaji wa mradi kama vile muda, gharama na ubora.

Hii ni pamoja na tathmini ya mipango ya utekelezaji wa mradi: tathmini ya mradi, upembuzi yakinifu, Usanifu, muda na makadirio ya gharama na vipengele vya kuanzishwa kwa mradi. Vipengele vya usimamizi wa mikataba vinavyohusu usimamizi na ufuatiliaji wa wakandarasi na washauri, kuagiza kufungwa kwa mradi pia vilizingatiwa. Vile vile, ukaguzi wa kiufundi uliangalia ikiwa Wizara ilizingatia kipengele cha shughuli za kujenga uwezo kwa mafundi wa ndani, Wajibu kwa Jamii (CSR) na uhusiano wa kazi kati ya pande zote zinazohusika katika mradi huo. Aidha, Timu ya Ukaguzi ilitathmini upatikanaji na utoshelevu wa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira (EMP) na Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA).

Timu ya Ukaguzi pia ilichunguza kiwango cha kuzingatia utekelezaji wa hatua za kupunguza hatari zinazohusiana na mazingira, afya ya kazi na usalama na athari za kijamii. Mambo makuu ambayo yalitathminiwa ni pamoja na masuala ya usalama kwa wafanyakazi, utunzaji wa udongo na taka ambazo zilizalishwa na kupunguza mmong'onyoko wa udongo.

Vile vile, Timu ya Ukaguzi ilishughulikia shughuli zote na kazi zilizotekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2022/2023 hadi sasa, hasa kwa sababu hiki ndicho kipindi ambacho Wizara ya Maji na Nishati kupitia ZAWA ilianza ujenzi wa miradi hiyo. Kipindi kilichochaguliwa kiliwezesha Timu ya Ukaguzi kutathmini mambo yote muhimu kuanzia awamu ya kupanga na maendeleo yaliyofanywa hadi sasa katika utekelezaji wake.

## 1.5 Vigezo vya Tathmini

Vigezo vya ukaguzi vilitolewa kutoka vyanzo mbalimbali kama vile sheria, viwango, ufanyaji kazi mzuri na nyaraka za Usanifu, Hati za Mipango zilizoidhinishwa, Hati za Usanifu, Maelezo ya Kawaida, Muongozo wa Usanifu na Utafiti wa Mahitaji uliofanywa n.k.

## 1.6 Sampuli, Ukusanyaji wa Takwimu, na Mbinu za Uchambuzi wa Takwimu

### 1.6.1 Njia ya Sampuli

Mbinu za sampuli za makusudi zilitumika kuchagua maeneo ambayo yalichunguzwa yakijumuisha wigo wa mradi ambao umetekelezwa hadi sasa. Vigezo vya uteuzi katika utekelezaji wa mradi vilitegemea mfuko wa fedha za mradi hatarishi (risk project fund) ambao uliingizwa kutokana na fedha za UVIKO-19 ili kuwezesha maji safi na salama. Jadweli hapo chini linawasilisha orodha ya miradi iliyochaguliwa kulingana na vigezo vya uteuzi.

**Jadweli Nambari 1: Orodha ya sampuli ya miradi inayojumuisha miradi ya maji inayofadhiliwa na fedha za UVIKO-19**

| Namba | Shughuli kuu za Mradi | Gharama (Tsh) |
|---|---|---|
| 1. | Uchimbaji wa visima vipya 38 kuzalisha lita 14,187,600 kwa siku | 1,615,000,000 |
| 2. | Ununuzi wa Vifaa vipya | 2,160,148,526 |
| 3. | Ukarabati wa Visima 36 vya RAK kuzalisha lita 15,632,400 kwa siku | 1,536,524,967 |
| 4. | Ukarabati na matengenezo ya Visima 49 (Boreholes) vilivyopo vya kuzalisha lita 23,444,400 kwa siku | 6,781,659,875 |
| 5. | Upanuzi wa msingi wa mtandao wa bomba | 8,425,258,633 |
| 6. | Uchimbaji wa mtaro na ujazaji wa msingi | 1,021,408,000 |
| 7. | Ukarabati wa matangi 3 ya maji | 210,000,000 |
| 8. | Ujenzi wa matangi 9 ya maji | 12,450,000,000 |
| | **Jumla** | **34,200,000,000** |

*Chanzo: Nyaraka za Mkataba*

### 1.6.2 Mbinu za Ukusanyaji wa Takwimu

Timu ya Ukaguzi ilitumia njia tatu za ukusanyaji wa taarifa. Njia hizi ni pamoja na Mapitio ya Hati, Mahojiano na uthibitishaji wa utembeleaji wa eneo la mradi kwa kazi zinazoendelea na zile zilizokamilika. Njia tatu za ukusanyaji wa taarifa ni kama ilivyoelezwa hapa chini:

**a) Mapitio ya Hati**

Timu ya Ukaguzi ilipitia nyaraka mbalimbali ili kupata uelewa wa mradi na kutathmini utoshelevu wa mipango/uhitaji wa tathmini, utekelezaji na ufuatiliaji wa mradi. Hii pia ilifanyika ili kutambua hatari kwa utendaji au sababu za msingi za matatizo ya utendaji ili kuwezesha Timu ya Ukaguzi kuja na matokeo na mapendekezo ya maboresho zaidi. Taarifa zilizokusanywa kupitia nyaraka zilizopitiwa zilitumika kuthibitisha taarifa zilizopatikana zilitokana na mahojiano yaliyofanyika na maafisa wanaohusika na utekelezaji wa mradi.

Nyaraka zilizopitiwa ni zile zilizoangukia ndani ya kipindi kilichokusudiwa na Ukaguzi wa Ufundi kuanzia Juni 2022 hadi Julai 2023 na zilikuwa zile zinazohusiana na upangaji wa mradi, rekodi za kifedha za ununuzi, nyaraka zinazohusiana na utendaji, na mambo ya mazingira.

**b) Mahojiano**

Ili kupata uelewa mpana wa miradi na kutambua changamoto zilizopo za kiufundi, Timu ya Ukaguzi ilifanya mahojiano na majadiliano na viongozi mbalimbali. Mahojiano hayo yalifanyika kwa lengo la kupata taarifa za ziada zinazohusiana na utekelezaji wa miradi ya maji ili kufafanua taarifa zilizopatikana kutokana na nyaraka zilizopitiwa na uhakiki wa kikazi.

**Uthibitishaji Kwa ziara ya kukagua eneo la mradi**

Timu ya Ukaguzi pia ilifanya ziara za kutembelea kwenye maeneo ambayo mradi ulitekelezwa kukagua na kuthibitisha kazi halisi iliyofanywa na kuhakikisha ubora wa kazi kwa kazi zilizotekelezwa. Kupitia ziara ya kutembelea miradi, Timu ya Ukaguzi ilithibitisha ikiwa kazi zilizotekelezwa zilikubaliana na vipimo, michoro, hati za makisio ya gharama za ujenzi (BoQs) na hali yoyote iliyotolewa katika hati za mkataba na muundo. Vipengele muhimu vilizingatiwa pamoja na vyenginevyo visivyo kama hivi kama ifuatavyo: -

(a) Kupima ubora na wingi wa kazi zilizokamilishwa hasa Vipimo visivyo vya uharibifu;
(b) Kupima ubora wa maji yaliyozalishwa.
(c) Uthibitishaji wa kutembelea miradi kwa kazi zilizokamilishwa ikilinganishwa na vitu vilivyoonyeshwa katika Makisio ya gharama za ujenzi.
(d) Vipimo vya idadi halisi ya kazi zilizotekelezwa ikilinganishwa na vipimo vilivyoonyeshwa katika hati za makisio ya gharama za mradi, na
(e) Utembeleaji wa eneo la kazi wa mahitaji ya usalama, mazingira na afya kama ilivyoelezwa katika nyaraka za mradi.

Uchunguzi na uthibitisho wa eneo la kazi ulizingatia idadi ya masuala kama ilivyosimuliwa katika jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 2: Vitu muhimu vilivyozingatiwa na kuthibitishwa wakati wa Uchunguzi wa ziara ya eneo la kazi**

| Kipengele muhimu | Masuala yaliyozingatiwa | Njia |
|---|---|---|
| Hali ya Kukamilisha | Kasi ya utekelezaji ikiwa inakwenda vizuri kulingana na mpango wa kazi | Ukaguzi wa kuona kwa macho na Mapitio ya Hati kwenye eneo la mradi |
| Ubora wa vifaa vya ujenzi | Ubora wa vifaa vinavyotumiwa | Kupima |
| Ubora wa kazi zilizokamilishwa | Hali ya kazi zilizokamilishwa | Kupima |
| Usimamizi wa Mradi | Upatikanaji wa wafanyakazi muhimu | Mapitio ya Hati ya Ukaguzi wa kuona kwenye eneo la mradi |
| | Upatikanaji wa zana zinazohitajika na vifaa ama mashine | Ukaguzi wa kuona kwa macho na Mapitio ya Hati kwenye eneo la mradi |
| Upatikanaji wa maji na ubora | Upatikanaji wa maji | Upimaji na Ukaguzi wa kuona kwa macho |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi, 2023*

### 1.6.3 Mbinu za Uchambuzi wa Takwimu

Ukaguzi ulitumia mbinu mbili za msingi kuchambua taarifa zilizokusanywa wakati wa ukaguzi. Mbinu zilizotumiwa zilikuwa uchambuzi wa taarifa ya kiasi na ubora.

- **Uchambuzi wa Taarifa ya Kiasi (Quantitative)**

  Jadweli za Ms. Excel zilitumika kukusanya na kuchambua taarifa ya kiasi ili kuamua uhalisia unaojitokeza katika muundo wa jadweli. Hali zilizozingatiwa zilielezewa kwa kutumia uhalisia uliobainishwa kama uwiano na/au wastani. "Simple bar and/or pie charts" zilitumika kuonyesha taarifa ya kiasi kwa kuunga mkono hali iliyozingatiwa.

- **Uchambuzi wa Taarifa ya Ubora (Qualitative)**

Uchambuzi wa maudhui ya dhana ulitumika kuchunguza taarifa ya ubora na kuhakikisha kuwepo na mzunguko wa dhana zinazotokana na mahojiano na ukaguzi wa hati. Ukweli uliojulikana uligawanywa kulingana na dhana muhimu katika kila moja ya maswali ya ukaguzi. Kulingana na uchambuzi na uhusiano kati ya makundi ya kificho "Coded Categories" , mambo yaliyopewa kipaumbele yalitambuliwa kwa uhalisia kama yalivyosimuliwa.

## 1.7 Mchakato wa Uthibitishaji wa Taarifa

Vyombo vilivyokaguliwa vilipewa fursa ya kupitia rasimu ya ripoti na kutoa maoni juu ya uhalisia wa habari uliyowasilishwa ndani yake. Wizara ya Maji na Nishati na Mamlaka ya Maji Zanzibar zilithibitisha usahihi wa taarifa na takwimu zilizotumika na kuwasilishwa katika ripoti hii ya ukaguzi.

Kwa njia hiyo hiyo, ripoti ya rasimu iliwasilishwa kwa ukaguzi wa ubora na usimamizi ili kuboresha uwasilishaji na uchambuzi wa ripoti na kuthibitisha yaliyomo kwenye uhalisia wa maelezo yaliyowasilishwa katika ripoti.

## 1.8 Viwango Vilivyotumika katika ukaguzi

Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs) zilizotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI). Viwango hivi vinahitaji kwamba ukaguzi kufanywa ili kupata ushahidi wa kutosha na sahihi wa ukaguzi ili kutoa msingi mzuri wa matokeo na hitimisho kulingana na malengo ya ukaguzi. Kwa ujumla, kulingana na malengo ya ukaguzi, ushahidi uliopatikana ulitoa msingi mzuri wa matokeo na hitimisho lililofikiwa.

## 1.9 Muundo wa Ripoti ya Ukaguzi

Muundo wa ripoti hii umejumuisha sura zifuatazo:

**Jadweli Nambari 3:Muundo wa Ripoti**

| | |
|---|---|
| Sura ya Pili | Mfumo wa Utoaji wa Huduma za Maji Zanzibar |
| Sura ya Tatu | Inawasilisha Matokeo ya Ukaguzi wa Jumla kwa Utekelezaji wa Miradi ya Maji |
| Sura ya Nne | Inawasilisha matokeo ya ukaguzi juu ya ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine za maji |
| Sura ya Tano | Inawasilisha matokeo ya ukaguzi juu ya kuchimba na ujenzi wa visima vipya |
| Sura ya Sita | Inawasilisha matokeo ya ukaguzi juu ya ujenzi wa Matangi ya maji |
| Sura ya Saba | Inawasilisha matokeo ya ukaguzi juu ya kazi ya kuchimba na kujaza misingi |
| Sura ya Nane | Inawasilisha Matokeo ya Ukaguzi juu ya Matengenezo ya Matangi ya Maji |
| Sura ya Tisa | Inawasilisha Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usambazaji na Ufungaji wa Umeme kwenye Matangi ya Maji |
| Sura ya Kumi | Inawasilisha Matokeo ya Ukaguzi juu ya Huduma ya Ushauri kwa Ufungaji wa Mfumo wa ILMS |

| | |
|---|---|
| Sura ya Kumi na Moja | Inawasilisha Matokeo ya Ukaguzi juu ya Huduma ya Ushauri na Usanifu wa Matangi ya Maji |
| Sura ya Kumi na Mbili | Inawasilisha Matokeo ya Ukaguzi juu ya Huduma ya Ushauri na Usanifu juu ya Ukarabati na Usambazaji wa Vifaa Vipya |
| Sura ya Kumi na Tatu | Inawasilisha Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usambazaji wa Mabomba ya HDPE kwa Lot ya 1 na 2 |
| Sura ya Kumi na Nne | Inawasilisha Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usambazaji wa Mabomba na Vifaa |
| Sura ya Kumi na Tano | Inawasilisha Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usambazaji wa Pampu (Submersible) |
| Sura ya Kumi na Sita | Inawasilisha matokeo ya ukaguzi juu ya usambazaji wa motor, paneli ya kudhibiti na valve ya sluice (supply of motor,control panel and sluice valve) |
| Sura ya Kumi na Saba | Inawasilisha Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usambazaji wa Mitambo ya kuchimbia visima |
| Sura ya Kumi na Nane | Inawasilisha Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usambazaji wa GPS, Jenereta na Mashine za Umeme |

# SURA YA PILI



# 2.0 MFUMO WA USIMAMIZI WA USAMBAZAJI MAJI ZANZIBAR

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea mfumo wa usimamizi wa uzalishaji, uhifadhi na usambazaji wa maji Zanzibar. Inaelezea sera na mfumo wa kisheria unaosimamia mfumo wa usimamizi wa maji, pamoja na majukumu na majukumu ya wahusika muhimu wanaohusika. Sura inashughulikia kazi, malengo, na mikakati ya usimamizi wa maji.

## 2.2 Mfumo wa Sera na Sheria

### 2.2.1 Mifumo ya Sera

Zifuatazo ni sera zinazosimamia udhibiti wa elimu ya ufundi na mafunzo nchini Tanzania.

### (a) Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2004

Lengo la sera hii ni kuongoza kuiwezesha Zanzibar kufikia lengo lake la kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wote na watumiaji wengine wa maji ili kutimiza mahitaji ya kupanua shughuli za kijamii na kiuchumi huku wakizingatia uhifadhi wa mazingira. Rasilimali za utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maji hutegemea rasilimali zifuatazo:

#### (i) Rasilimali za Ufundi

Hizi ni pamoja na rasilimali zote zinazochangia upatikanaji wa maji, teknolojia za kirafiki zinazotumiwa, vifaa na miundo.

#### (ii) Rasilimali ya Uchumi

Hizi ni pamoja na ada za watumiaji, michango ya jamii, adhabu, motisha na kila chombo cha kiuchumi kinachotumika kuhakikisha uchimbaji bora na ufanisi, matumizi ya usambazaji na utupaji wa rasilimali na mazingira.

#### (iii) Rasilimali za Utawala

Hizi ni pamoja na mifumo ya habari na miundombinu ya utawala ambayo inasababisha mipango bora na ufanisi, utekelezaji, usimamizi na ufuatiliaji wa kazi za maji ikiwa ni pamoja na miundombinu ya uhifadhi.

#### (iv) Rasilimali za Kisheria

Hizi ni pamoja na mifumo ya kisheria na zana ikiwa ni pamoja na hatua za utekelezaji, leseni, tathmini, viwango, n.k ambazo zinalinda maslahi ya sekta na mazingira.

### (v) Rasilimali za Usimamizi

Inajumuisha miundo yote ya usimamizi na taasisi ambazo zitatoa miongozo na mipangilio ya uwazi katika kutekeleza shughuli tofauti za sekta hiyo.

### 2.2.2 Mifumo ya Sheria

### Sheria ya Ujenzi wa Miradi ya Maji

Kuna sheria tatu tofauti zinazosimamia shughuli za ujenzi Zanzibar kama zilivyowasilishwa katika Jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 4: Sheria ya Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi**

| Sheria | Masharti |
|---|---|
| Sheria nambari 8 ya Usajili wa Wakandarasi Zanzibar ya 2010. | Inamtaka mmiliki wa majengo hayo kuhakikisha jengo lake linajengwa na wakandarasi waliosajiliwa. Sheria hiyo inamtaka mkandarasi kuepuka uzembe wowote unaoweza kusababisha kazi mbaya, kuvunjika au kukosa kazi. |
| Sheria nambari 5 ya Usajili wa Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji wa Majengo ya 2008. | Sheria ndogo zinahitaji mtaalamu kupata mamlaka kutoka kwa mteja kabla ya kuanzisha huduma yoyote au hatua ya kazi na kuidhinisha mabadiliko yoyote ya nyenzo, kuongeza au kutoruhusiwa kutoka kwa muundo ulioidhinishwa. |
| Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 | Sheria inatoa taratibu za kufuatwa wakati wa ununuzi hadi utekelezaji wa mradi. |
| Sheria nambari 4 ya Kodi ya Mapato (R.E) ya 2008. | Sheria inatoa utawala wa masuala yote yanayohusiana na kodi |
| Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016. | Sheria inatoa utawala mambo yote yanayohusiana na malipo na idhini. |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwa Matendo ya Kuheshimu yaliyopitiwa, 2023*

### (a) Sheria nambari 4 ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Maji ya 2006

Sheria hii ni msingi wa kuanzishwa kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) chini ya kifungu cha 3 (1). Sheria inatoa majukumu ya Mamlaka kama ilivyowasilishwa hapa chini:

(i) Kudhibiti, kusimamia na kulinda maeneo yote ya upatikanaji na itakuwa na mamlaka dhidi ya ukiukaji wowote, au kuvuruga au kuingilia maeneo ya upatikanaji;

(ii) Kuhakikisha upatikanaji wa maji nchini;

(iii) Kuandaa na kuendeleza mpango wa maji na kutekeleza miradi mipya ya usambazaji wa maji;

(iv) Kuhamasisha uhifadhi na matumizi sahihi ya rasilimali za maji;

(i) Kukusanya ada kwa ajili ya huduma za maji na huduma zinazotolewa kwa watumiaji;

(vi) Kuainisha viwango vya ubora wa maji, vifaa vya maji na maji kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Sheria hii;

### (b) Kanuni ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Maji ya 2007

Kanuni za Maji hutoa msingi wa utekelezaji wa kazi ya ZAWA kulingana na maendeleo ya rasilimali za maji, mipango ya kutibu maji, huduma ya maji kwa wateja, ujenzi wa miradi ya maji, ushuru wa maji, Kupanga na Usanifu mfumo wa maji, na makosa na adhabu zake. Hizi ni baadhi ya kanuni za maji

## 2.3 Malengo na Mikakati

### 2.3.1 Malengo

ZAWA inaendeshwa na malengo yake ambayo yanaunda maono na dhamira ya mamlaka ambayo ni, kuwa mtoa huduma ya maji inayoongoza katika kanda ambayo inashughulikia mahitaji ya jamii na kiuchumi ya kijamii kwa maendeleo endelevu, na kusaidia maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia utoaji wa huduma za maji ambazo zinapatikana kwa usalama na kwa gharama nafuu kwa njia ya kisasa, endelevu na rafiki kwa mazingira ndani ya Zanzibar.

### 2.3.2 Mikakati

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) iliandaa mpango mkakati wa utekelezaji katika kipindi cha miaka mitano ijayo ili kuhakikisha: (a) usimamizi wa rasilimali za maji unaimarishwa, (b) Huduma ya maji imeboreshwa, (c) Huduma za kibiashara na wateja zimeboreshwa, (d) Uendelevu wa kifedha umeimarishwa, (e) uwezo wa kitaasisi ulioimarishwa na (f) michakato ya utawala na uwajibikaji kuboreshwa kama sehemu ya malengo ya kimkakati kuelekea kufikia kaulimbiu ya ZAWA ambayo ni " Kila Tone la Maji ni Gharama".

## 2.4 Uhusiano Kati ya Watendaji Wakuu

### 2.4.1 Uhusiano Kati ya Watendaji Wakuu

Utekelezaji wa miradi ya maji kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa maji Zanzibar unatekelezwa na watendaji mbalimbali kama ilivyoelekezwa katika majukumu na wajibu wao. Uhusiano muhimu wa wahusika umefupishwa katika picha hapo chini.

**Picha Nambari 1: Uhusiano kati ya Watendaji Wakuu katika Usimamizi wa Huduma za Maji Zanzibar**




## 2.5 Maelezo ya Miradi ya Maji

Mradi wa Maji uligawanywa katika shughuli kama ilivyotengwa na fedha za UVIKO-19 zilizowasilishwa katika Jadweli hapa chini.

**Jadweli Nambari 5: Shughuli za Mradi wa Maji**

| Shughuli kuu | Shughuli Ndogo | Shughuli ya Utoaji | Malengo Tarajiwa | Ugawaji uliopendekezwa (Tsh) |
|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha mfumo wa usambazaji maji | Kuongeza uzalishaji wa maji | Uchimbaji wa visima vipya 38 kuzalisha lita 14,187,600 kwa siku | Uzalishaji wa maji umeongezeka kwa lita 53,264,400 kwa siku | 1,615,000,000 |
| | | Ununuzi wa Vifaa vipya | | 2,160,148,526 |
| | | Ukarabati wa Visima 36 vya RAK kuzalisha lita 15,632,400 kwa siku | | 1,536,524,967 |
| | | Ukarabati na Matengenezo ya Visima 49 vilivyopo kuzalisha lita 23,444,400 kwa siku | | 6,781,659,875 |
| | Uboreshaji wa bomba la maji | Upanuzi wa mtandao wa bomba | Mtandao wa bomba umeongezeka kwa kilomita 319 | 8,425,258,633 |
| | | Uchimbaji na ujazaji wa misingi | | 1,021,408,000 |
| | Kuongeza uhifadhi wa maji | Ukarabati wa matangi 3 ya maji | Uhifadhi wa maji uliongezeka kwa lita 9,250,000 | 210,000,000 |
| | | Ujenzi wa matangi 9 ya maji | | 12,450,000,000 |
| **Jumla Kuu** | | | | **34,200,000,000** |

## 2.6 Ugawaji wa Rasilimali za Fedha

Matumizi bora ya rasilimali fedha na rasilimali watu yanahitajika kwa usimamizi mzuri wa huduma ya maji. Mamlaka ya Maji Zanzibar ina jukumu muhimu katika kudumisha ufanisi na upatikanaji wa huduma za maji Zanzibar. Kwa hivyo, sehemu hii ilishughulikia maelezo juu ya rasilimali zilizotengwa kwa ZAWA.

Mfuko uliopokelewa na ZAWA kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji na usambazaji wa vifaa chini ya maendeleo ya kijamii ya UVIKO-19. Jadweli hapa chini linaonesha fedha zilizotengwa na kupokea.

**Jadweli Nambari 6: Fedha Zilizotengwa na Kutolewa kwa ajili ya Shughuli za Mradi wa Maji**

| Bajeti ya Fedha iliyopangwa (TSh) | Kiasi halisi cha Fedha kilichoingizwa (TSh) |
|---|---|
| 34,200,020,000.00 | 30,585,186,536.62 |

Jadweli hapo juu lilihusisha kuwa kutoka kwa jumla ya mfuko uliopokelewa ni asilimia 89 dhidi ya mfuko wa bajeti kwa utekelezaji wa mradi wa UVIKO-19.

# SURA YA TATU


OFFICE OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL ZANZIBAR
OCAGZ

# 3.0 MATOKEO YA JUMLA YA UKAGUZI JUU YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi yaliyojumuishwa ambayo yalibainishwa katika miradi ya ukaguzi kulingana na mzunguko wa usimamizi wa mkataba kuanzia hatua ya upangaji na ubunifu hadi utekelezaji kwa mujibu wa mkataba kama ilivyowasilishwa hapa chini.

## 3.2 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Uanzishwaji na Upangaji wa Miradi ya Maji

### 3.2.1 Maandalizi ya Dhana ya Mradi (Concept Note) bila kuzingatia mahitaji yaliyopo

Kwa kuzingatia kifungu cha 2.1 na 2.2 cha Muongozo wa Upangaji wa Miradi na Majadiliano ya Kuongeza Mikopo, Kutoa Dhamana na Kupokea Misaada kwa mwaka 2020 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Maelezo yanayotokana na dhana ya uanzishaji wa mradi yanapaswa kujumuishwa mahitaji yaliyopo kwa mradi kwa kuzingatia ukubwa, upeo, faida za sasa na za baadae pamoja na mahitaji ya mradi.

Kulingana na ukaguzi wa Dhana ya Mradi iliyowasilishwa kwa utekelezaji wa Mradi wa wa Mfuko wa UVIKO-19, ukaguzi ulibaini kuwa maandalizi ya dhana ya mradi hayakuhusisha tathmini ya mahitaji kamili ya mfumo wa usambazaji wa maji ili kubaini upeo, mahitaji ya sasa na ya baadae ya mradi lakini kulingana na uzoefu na kumbumbu za utekelezaji wa mradi.

Kwa hivyo wakati wa utekelezaji wa mradi kulikuwa na mahitaji ya ziada ya mradi kama ilivyowasilishwa katika Jadweli hapo chini ambapo baadhi ya vipengele havikuingizwa katika maelezo ya uanzishwaji wa mradi.

**Jadweli Nambari 7: Uchambuzi wa Utekelezaji wa Dhana ya Mradi**

| Kipengele | Dokezo la Dhana ya Mradi | Utekelezaji wa Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|
| Ujenzi wa matangi ya maji | Matangi 9 | Matangi 10 | Tangi la maji la ziada liliongezwa baada ya mchakato wa zabuni (Tangi la Makangale Pemba) |
| Matengenezo ya Matangi ya maji | Matangi 3 | Matangi 2 | Matengenezo kwa tangi la Maji la saateni na kilimani |
| Mfumo wa usambazaji maji | Kilomita 319 | Kilomita 319 | Utafiti na usanifu uliofanywa na mshauri ulionesha kuwa kuna kilomita 479 Unguja na kilomita 133 Pemba |

*Chanzo: Maelezo ya Dhana ya Mradi*

Maandalizi ya dhana ya mradi bila kuzingatia upeo na tathmini ya mahitaji ilichangiwa na maandalizi ya haraka ya kuanzishwa kwa mradi. Hii ilisababisha upatikanaji usioridhisha wa mahitaji ya mtumiaji na mafanikio ya makadirio ya usambazaji wa maji kutoka asilimia 55 ya usambazaji wa maji ya sasa hadi asilimia 71.

### 3.2.2 Kutofuata Mapendekezo ya Utafiti wa Miamba juu ya Uwezo wa Kuzalisha Maji (Hydrogeological)

Kifungu nambari 15.1 cha mkataba wa kuchimba visima na ujenzi wa visima vipya kinahitaji mkandarasi kutegemea ripoti yoyote ya uchunguzi wa eneo litakalochimbwa kisima, ikiongezewa na habari yoyote inayopatikana kwa mzabuni. Wakati wa kuanzisha mradi ya uchunguzi wa kijiolojia inatoa uhakika wa kiasi cha maji kinachokadiriwa ili kukabiliana na mahitaji ya maji katika eneo maalum. Kulingana na mapitio ya Ripoti ya Utafiti wa Miamba juu ya uzalishaji wa maji (Hydrogeological Survey) iliyoandaliwa na M/s Simplex Engineering ya Juni 2022, ukaguzi ulibainisha visima vilivyopendekezwa kuchimbwa kwa kipenyo cha inchi 14 (355mm), na kukamilishwa kwa mifuniko ya UPVC ya inchi 12, na kifurushi cha changarawe katika "VES Point" kilichowekwa chini wakati wa kutembelea maeneo ya mradi.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi ulipofanya ziara ya kikazi uliofanywa wakati wa ukusanyaji wa taarifa ulibaini kutozingatia kwa vipimo vya uchimbaji wa visima kama inavyoonekana katika Jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 8: Kutozingatiwa Mapendekezo ya Utafiti wa Miamba**

| Kigezo (Parameter) | Mapendekezo ya vipimo vya Utafiti wa Miamba (Hydrological) | Uhalisia wa Vipimo wakati wa ukaguzi wa Eneo |
|---|---|---|
| Kipenyo cha kisima (inch) | 14″ | 10″ – 12″ |
| Mfuniko wa plastiki (UPVC) (inch) | 12″ | 8″ – 10″ |
| Urefu wa Kisima (m) | 35 – 75 | 17.44 – 98 |

*Chanzo: Ripoti ya Utafiti wa Miamba na Upimaji wa Eneo*

Jadweli hapo juu linaonyesha kutozingatia visima vyote vilivyochimbwa katika kigezo cha kipenyo (diameter) na urefu wa kisima kwa Unguja na Pemba.

Dosari hii ilitokana na ukosefu wa uwezo na kutekeleza miradi kulingana na uzoefu. Hii ilisababisha ukosefu wa kuzingatia ripoti ya uchunguzi wa kijiolojia kama ilivyoelezwa katika Masharti Maalum ya Mkataba (SCC).

Ukosefu wa kuzingatia mapendekezo ya utafiti wa miamba (hydrogeological) ili kutambua kigezo sahihi cha chanzo cha visima vilivyoathiri kama ifuatavyo: -

a) Upatikanaji wa visima vilivyopasuka (collapsed) na visima vikavu wakati wa utekelezaji wa mradi kama vile;
   - Kisima cha Donge Kipange
   - Kisima cha Kiashangwe
b) Ilipunguza ukubwa unaofaa wa pampu ya chini ya maji ya kisima kwa visima vinavyotoa maji mengi
c) Matengenezo ya visima vya kutosha kwa kupunguza mfuniko na uingizaji mpya wa UPVC; Na
d) Kutozingatia urefu wakati uchimbaji wa visima kwa mujibu wa BoQs, hali hii imesababisha hasara ya shilingi 928,153,089.48 kama gharama ya kina kisichochimbwa cha mita 3309.49 kutoka Unguja na Pemba kama ilivyofafanuliwa katika Sura ya Tano ya ripoti hii.

### 3.2.3 Gharama zilizoongezeka kutokana na usanifu wa ngazi ya zege shilingi 131,384,470

Kulingana na Viwango vya Uingereza (British Standard 8110): Sehemu ya 1:1985, lengo la muundo wa Usanifu ni kufikia uwezekano unaokubalika kwamba miundo inayoundwa itafanya kazi kwa kuridhisha wakati wa maisha yao yaliyokusudiwa na kiwango sahihi cha usalama.

Ukaguzi ulipitia mchoro wa ngazi na kubaini kwamba ZAWA ilitumia muundo wa zege ulioimarishwa daraja halisi la C40 badala ya daraja la C25. Jumla ya ujazo wa zege kwa ngazi ilikuwa 350$m^3$ uliogharimu kiasi cha shilingi 259,424,470.

Aidha, kutokana na mapitio ya ripoti ya muundo ukaguzi ulibaini kuwa na muundo wa ngazi wa mwanzo ulikuwa ngazi za chuma kupitia matangi ya maji yaliyoinuliwa ambayo baadaye yalibadilishwa wakati wa utekelezaji wa mradi na kuekwa ngazi za zege zenye urefu wa mita 15 hadi 20 kwenda juu ambazo zina umbile la ‘U’ iliyotengwa kando ya tangi la maji na haishiriki katika kusaidia kubeba mzigo wa tangi.

Uchambuzi huo ulionyesha kuwa, kwa kutumia daraja halisi la C25 gharama inaweza kuwa shilingi 128,040,000 ambayo ilikuwa shilingi 131,384,470 chini ya gharama ya ngazi kwa kutumia daraja halisi la C40. Hivyo basi, kwa kutumia daraja halisi la C40 katika ngazi hiyo kunagharimu kiasi cha shilingi 259,424,470 wakati kwa kutumia daraja halisi la C25 inaweza kupunguza gharama hadi shilingi 128,040,000 hivyo ZAWA anaweza kuokoa kiasi cha shilingi 131,384,470.

Kutokana na muundo wa kupita kiasi katika ngazi gharama za mradi ziliongezeka kwa shilingi 131,384,470.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa, miundo ya maji imeundwa ili kufikia kiwango kinachokubalika cha huduma na majimbo ya kikomo cha mwisho bila kuunda miundo.

## 3.3 Mchakato wa Ununuzi wa Miradi ya Maji

### 3.3.1 Timu ya Tathmini Haikujumuisha Wataalamu Wanaohitajika

Kanuni ya 118(2) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma 2020, inaitaka Kamati ya Tathmini kuwa na wanachama wenye ujuzi, maarifa na uzoefu unaoendana na mahitaji ya manunuzi ambayo ni pamoja na utaalamu husika wa kiufundi, utaalamu wa manunuzi, utaalamu wa uchambuzi wa usimamizi wa fedha, utaalamu wa kisheria, au mwakilishi kutoka idara ya mtumiaji. Mapitio ya ripoti ya tathmini ya zabuni ya usambazaji wa mabomba na vifaa, ukaguzi ulibaini kuwa sio wataalamu wote wanaohitajika walihusika katika timu ya tathmini. Uchambuzi wa wataalamu wa wanachama ambao wamekosekana katika timu ya tathmini umewasilishwa katika Jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 9: Wataalamu waliokosekana katika Timu ya Tathmini**

| Namba | Nambari ya Zabuni | Jina la Mradi | Mtaalamu Aliyekosekana |
|---|---|---|---|
| 1. | SMZ/No.104/G/ ICB/2020-2021/02 | Usambazaji wa Mabomba na Vifaa | Mtaalamu wa Ununuzi na Sheria |
| 2. | SMZ / IMF / 104 / G / RNCT/2021/2022/01 | Usambazaji wa mabomba ya HDPE, usambazaji wa vifaa vya HDPE na usambazaji wa vifaa vya kichwa cha kisima(well head). | Mtaalamu wa Sheria na Mtaalam wa Uchambuzi wa Usimamizi wa Fedha |
| 3. | SMZ / IMF / 104 / G / RNCT/2021/2022/02 | Usambazaji wa Pampu za Visima (Submersible) Loti ya 1, Loti ya 2, Loti ya 3, Loti ya 4 na Loti 5 | Mtaalamu wa kisheria na mtaalamu wa usimamizi wa fedha |

*Chanzo: Uchambuzi wa Ripoti za Tathmini kutoka katika Zabuni husika uliofanywa na Wakaguzi, 2023*

Jadweli hapo juu linaonesha ukosefu wa wataalamu tofauti katika timu ya tathmini, ambayo ilichangiwa na shindikizo na uharaka wa mchakato wa ununuzi ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya UVIKO-19. Ukosefu wa utaalamu katika timu ya tathmini ulisababisha uchambuzi usiotosheleza wa sehemu ambazo zilihitaji tathmini kamili na taaluma inayohitajika.

### 3.3.2 Zabuni zilitolewa kwa Wazabuni Wasio na sifa

Kanuni ya 118(8)(9) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma 2020, inahitaji kabla ya tathmini ya kina ya zabuni, Kamati ya Tathmini kufanya uchunguzi wa awali wa zabuni ili kubaini kama kila zabuni inakidhi vigezo kwa mujibu wa mahitaji ya nyaraka za zabuni, dhamana zinazohitajika zimetolewa, nyaraka zimesainiwa vizuri, na kwa utaratibu, na nakala za usajili wa kufanya biashara zimetolewa.

Kifungu cha 28.1, 28.2 na 28.5 cha maagizo kwa mzabuni juu ya ufunguzi wa zabuni katika Nyaraka za zabuni inahitaji kabla ya tathmini ya kina ya Zabuni, Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma itaamua kama kila zabuni imekidhi vigezo vya ustahiki, imesainiwa ipasavyo, inaambatanishwa kwa dhamana zinazohitajika na imekidhi vigezo kwa mujibu wa hati ya zabuni.

Zabuni zilizotakiwa kuzingatiwa ni zile zilizokidhi vigezo na masharti yote ya mkataba, masharti na maelezo ya hati ya zabuni kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa. Ikiwa Zabuni haitakidhi vigezo vilivyowekwa haitakubalika na kukataliwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za ununuzi na uondoshwaji wa mali za umma.

Kwa mujibu wa mapitio ya ripoti za tathmini na nyaraka za mikataba ukaguzi ulibaini kuwa mkataba ulitolewa kwa wazabuni ambao hawakuwa na sifa wakati wa tathmini kutokana na kushindwa kurejesha hati ya zabuni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 10: Uchambuzi wa Mkataba waliopewa Wazabuni waliotikia Zabuni**

| Namba | Jina la Mkataba | Jina la Muuzaji aliyepewa Tuzo | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Usambazaji wa Mabomba na Vifaa | M/s Simba Pipe Industries ltd | Kajibu |
| 2. | Usambazaji wa Mabomba ya HDPE Loti ya 1, | M/s Moona Noor Manufacturing and Trading LLC | Hakujibu |
| 3. | Usambazaji wa Vifaa vya HDPE loti ya 2 | M/s GAIA GLOBE ITH. IHR | Hakujibu |
| 4. | Usambazaji wa Pampu za Visima (Submersible) Loti 1 na 4 | M/s Sanfransisco | Hakujibu |
| 5. | Usambazaji wa Pampu za visima (Submersible) Loti ya 2, 3 na 5 | M/s Pumps for Africa | Hakujibu |

*Chanzo: Uchambuzi wa ripoti ya tathmini na Hati za Mkataba*

Jadweli hapo juu linaonesha kwamba wazabuni wawili ambao walipewa mkataba hawakukamilisha baadhi ya vipengele katika zabuni zao na kupelekea kukosa sifa za upewaji wa zabuni. Baadhi ya vipengele hivyo vilivyokosekana ni kama vifuatavyo: -

**Jadweli Nambari 11: Mzabuni Aliyepewa Mkataba Eneo ambalo hakuitikia Zabuni**

| Namba | Jina la Muuzaji aliyepewa Tuzo | Taarifa zilizokosekana katika hati ya dhabuni |
|---|---|---|
| 1. | M/s Moona Noor Manufacturing and Trading LLC | Tax Clearance and Power of Attorney |
| 2. | M/s GAIA GLOBE ITH.IHR | Company registration Certificate, Copy of Audited Financial Statement, Valid Business Licence, Experience at supplying similar material, Tax Clearance, Bid Security, Power of Attorney and Manufacturer Authorisation Certificate. |
| 3. | M/s Amtas Enterprises | Tax Clearance and Power of Attorney |
| 4. | M/s Sanfransisco | Change of Tender Validity Period Non Submission of Tender Security |
| 5. | M/s Pumps for Africa | Amendment of Client's schedule of requirements |

*Chanzo: Ripoti ya Tathmini*

Utoaji wa zabuni kwa Wazabuni ambao hawakujibu ulihusishwa na tathmini duni ya zabuni zilizofanywa na uongozi wa Mamlaka ya Maji. Dosari hiyo inaweza kusababisha upotevu wa fedha za umma pindipo mzabuni atakaposhindwa kutekeleza majukumu yake au kukubali tuzo ya utekelezaji wa kazi kutokana na kuwa na majukumu mengine ya kazi alizopatiwa.

### 3.3.3 Kutokupewa Zabuni kwa Wasambazaji waliopendekezwa na Kamati ya Tathmini

Kwa mujibu wa Kanuni ya 138(1) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020, tuzo hiyo itatolewa ndani ya kipindi cha uhalali wa zabuni kwa mzabuni ambaye zabuni yake imekidhi vigezo kuwa zabuni iliyotathminiwa vizuri. Ukaguzi umefanya mapitio ya ripoti ya tathmini na kubaini kuwa kamati ya tathmini ilimpendekeza mzabuni M/S INFRASOL LTD kupewa mkataba wa usambazaji wa Pampu za visima. Hata hivyo, ilibainika kuwa mkataba huo alipewa mzabuni M/S Sanfransisco LTD kwa Loti ya 1 na 4 na mzabuni M/S Pump for Africa LTD kwa Loti ya 2, 3 na 5 bila ya uwepo wa sababu za msingi zilizopelekea kubadilisha maamuzi ya Kamati ya Tathmini.

Kutokana na dosari iliyobainishwa hapo juu inaweza kupelekea kujitokeza kwa hasara ya fedha za Serikali kutakakosababishwa na baadhi ya wazabuni kukosa sifa na hatimae kuwasilisha vifaa au kutoa huduma isiyo na ubora.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unatoa zabuni kwa wazabuni wenye sifa na waliokidhi vigezo kwa mujibu wa sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

## 3.4 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usimamizi wa Mkataba wa Miradi ya Maji

### 3.4.1 Ubora usiotosheleza wa Pampu zilizosambazwa

#### (i) *Kutokujaribiwa kwa Utendaji wa Pampu zilizosambazwa*

Kifungu nambari 10 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kilieleza kuwa, muuzaji kwa kushirikiana na mnunuzi atafanya vipimo na ukaguzi wa bidhaa zote ili kuthibitisha kuwa sifa na utendaji wa bidhaa zinazingatia kanuni na viwango vya kiufundi vya vipimo chini ya Mkataba.

Mapitio ya Ripoti za Ukaguzi wa pampu zilibainisha kuwa, mnamo tarehe 3 Novemba na tarehe 05 Oktoba, 2022 timu kutoka ZAWA ilitembelea majengo ya wauzaji wa pampu ambao wanatengeneza na kuuza ambapo Wakati wa ziara hiyo wafanyakazi wa kiufundi walikagua vipimo vya pampu na vifaa vyake na kubaini kwamba ZAWA walifanya ukaguzi kwa pampu kuhakikisha zilikuwa zinaendana na sifa zinazohitajika.

Hata hivyo, ukaguzi kupitia mahojiano yaliyofanywa na maafisa wa ZAWA ilibainika kuwa, hakukuwa na vipimo vilivyofanywa kwa mashine za maji zilizotolewa ili kuangalia ikiwa vipimo vya pampu vilivyosemwa vinalingana na utendaji halisi wa pampu zilizosambazwa wakati wa ufungaji. Hata hivyo, ukaguzi uliomba vipimo (vigezo) vilivyotumika wakati wa ununuzi kwa pampu ambazo tayari ziliwekwa katika maeneo ya mradi lakini ukaguzi haukuweza kupatiwa vigezo hivyo.

#### (ii) Uwasilishaji wa Pampu zenye Uwezo wa chini wa kusukuma maji kuliko mahitaji

Ubora wa mipira ya Pampu za maji inayozamishwa chini ya kisima (Grundfos Submersible) ulionyesha kuwa, kiasi cha maji ni sawa na kichwa cha kisima (well head). Ukaguzi uliangalia utendaji wa pampu na kubaini uwepo wa pampu ndogo ambazo hazikukidhi uwezo wa kusukuma kama ilivyoainishwa katika orodha ya mchanganuo wa mahitaji. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa pampu zilizofungwa zilikuwa zinazalisha kiwango kidogo cha maji kuliko mahitaji yaliyokuwa yakihitajika kwa mujibu wa mchanganuo wa mahitaji ulioandaliwa na ZAWA.

Kutokana na dosari hiyo pampu zilizowekwa kusukuma maji kwa urefu ambao uliainishwa katika mchanganuo wa mahitaji itazalisha kiasi kidogo cha maji kuliko inayohitajika kutokana na hali hiyo ujazo wa tangi la kuhifadhia maji utachukuwa masaa mengi hadi kufikia ujazo unaohitajika. Kutokana na hali hiyo upo uwezekano mkubwa wa kujitokeza maharibiko ya mashine hiyo kutokana na kutumia masaa mengi kusukuma kiwango cha maji kinachohitajika.

***(iii) Vipimo Visivyotosheleza vya Valvu ya Maji (sluice valve)***

Kifungu nambari 21.1 kinasema kwamba "Kulingana na kifungu nambari 20 cha GCC, kinafafanua kwamba hakuna tofauti au marekebisho ya masharti ya mkataba yatakayofanywa isipokuwa kwa marekebisho yaliyoandikwa na kusainiwa na wahusika".

Baada ya ukaguzi wa Uainishaji (ikiwa ni pamoja na mchanganuo wa mahitaji na Maelezo ya Kiufundi), na Fomu za Ukaguzi 08 Novemba,2022, Ankara za Kodi namba 0317 ya tarehe 23/06/2022 na Hati za Uwasilishaji namba 0614 ya tarehe 08 Novemba, 2022 ilibainisha kuwa vifaa vya valvu za maji (Sluice Valve) havikuwasilishwa katika Mamlaka ya Maji Zanzibar. Ingawa, baada ya mahojiano na maafisa wa ZAWA ilibainika kuwa baada ya kufanya uhakiki waligundua kuwa nyenzo zilizoainishwa katika mchanganuo wa vipimo hazitoshelezi kwa sababu valvu iliyoagizwa ilikuwa ya chuma kinachopindika (ductile iron) kilichopigwa valvu ya maji kwa hivyo ilipendekezwa kununua valvu za maji (Sluice Valve) na vifaa vya chuma. Walakini, kulingana na ukaguzi wa ankara ya kodi nambari VRN: 40-004781-S ilibainika kuwa kulikuwa na mabadiliko ya valvu moja ya maji itakayokubaliana na kipenyo (diameter) kinachohitajika kutoka 18" hadi 12" kwa hivyo, kwa jumla valvu zitakazokubaliana zitakuwa tatu badala ya nne kulingana na kipenyo cha 18".

## 3.5 Kukamilika kwa Mradi Pamoja na Ufungaji

***(i) Kutowasilishwa kwa Michoro kwa Matangi ya Maji yaliyojengwa***

Kwa mujibu wa kifungu cha 27 cha Masharti Maalum ya Mkataba, mkandarasi atawasilisha michoro iliyochorwa kwa tarehe ya kukamilika kwa vitendo. Pia, meneja wa mradi anaweza kuzuia kiasi cha asilimia 3 ya bei ya mkataba ikiwa wakandarasi hawakuwasilisha michoro iliyobuniwa.

Mapitio ya hati ya mkataba yalibainisha kuwa tarehe ya kukamilika kwa ujenzi wa matangi ilikuwa 10 Julai, 2023 baada ya muda wa siku 191. Walakini hadi tarehe ya ukaguzi huu (28 Julai, 2023) michoro iliyochorwa haikuwasilishwa. Kulingana na masharti ya mkataba meneja wa mradi alikuwa na wajibu wa kuzuia kiasi cha asilimia tatu ya bei ya mkataba ambayo ni sawa na shilingi 393,728,131.9 pamoja na VAT. Hata hivyo, ukaguzi umebaini meneja wa mradi ameshindwa kuzuwia kiasi cha fedha nilichokibainisha hadi ukaguzi unakamilika.

Kutokana na kushindwa kuwasilishwa kwa michoro wakati utekelezaji wa kazi ukiendelea kunaweza kukapelekea kukamilika kwa ujenzi uliokusudiwa pasi na uwepo wa michoro inayohitajika jambo ambalo linaweza kupelekea ukiukwaji wa taratibu za kisheria.

Kutowasilisha michoro iliyochorwa ilionyesha kuwa ZAWA haikuwa na kumbukumbu ya muundo wa tangi la maji lililojengwa kulingana na utekelezaji wa matakwa ya mradi, hivyo huwenda kukajitokeza changamoto kwa siku zijazo kuweza kufanya maboresho ya aina ya tangi jengine kwa sababu ya kukosekana kwa kumbukumbu za awali.

# SURA YA NNE



# 4.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA UJENZI WA VITUO VYA UENDESHAJI WA PAMPU ZA MAJI (PUMP CONTROL HOUSE)

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza matokeo ya ukaguzi juu ya utekelezaji wa mradi kuhusu ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji Unguja na Pemba. Matokeo ya ukaguzi yaligawanywa katika mzunguko wa usimamizi wa mkataba kutoka kwa upangaji na uanzishaji wa mradi hadi utekelezaji wake.

Miradi ya ujenzi wa Vituo vya uendeshaji wa mashine za maji zilipatikana katika visiwa vya Unguja na Pemba. Kazi hiyo inajumuisha ujenzi wa jumla ya vituo 52 vya kuendesha pampu na kazi ziligawanywa katika loti 3. Loti hizi ni Loti ya 1 kwa Unguja Mjini Magharibi, Loti ya 2 kwa Kaskazini na Kusini Unguja inayojumuisha jumla ya vituo 26 vya kuendesha pampu ambazo ziliunda mkataba mmoja. Loti ya 3 ilikuwa kwa upande Kaskazini na Kusini Pemba na jumla ya vituo 26 za kuendesha pampu ambazo ziliunda mkataba mmoja.

Kazi hiyo ilitekelezwa kupitia njia ya manunuzi ya kawaida ambapo Mamlaka ya Maji Zanzibar iliandaa michoro na hati za makisio ya Ujenzi. Kazi hizo zilifanywa na wakandarasi wakuu wawili ambao ni M/s SHAMJO Company Limited na M/s OSAJU Company Limited. Mkandarasi alitakiwa kujenga vituo vya uendeshaji wa pampu kila moja na ukubwa wa jumla takribani mita za mraba 20 zenye jumla ya vyumba viwili na vyoo pamoja na shimo la maji taka. Jadweli nambari 13 na nambari 14 hapo chini kutoa taarifa ya mikataba ya ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji.

**Jadweli Nambari 12:Taarifa ya mkataba wa ujenzi wa kituo cha kuendeshea mashine ya maji kwa Loti ya 1 na Loti**

| Kipengele | Taarifa katika Mkataba |
|---|---|
| Nambari ya Mkataba | SMZ/IMF/No.104/W/RNCT/2021/2022/07 |
| Jina la Mkandarasi | M/S SHAMJO Co. Ltd |
| Tarehe ya Kusaini | 29 Januari, 2022 |
| Tarehe iliyohitajika kuanza | 12 Februari 2022 |
| Tarehe ya Kuanza | |
| Muda wa Mkataba | Miezi 5 |
| Tarehe ya awali ya kukamilika | 13 Julai 2022 |
| Tarehe ya Kukamilisha iliyorekebishwa | 16 Januari 2023 |
| Jumla ya Kiasi cha Mkataba wa awali na VAT | Shilingi 1,383,395,308.00 |
| Jumla ya kiasi cha Mkataba wa awali Uliorekebishwa | Hakuna |
| Maendeleo ya Kazi (%) hadi Julai, 2023 | 85% |

| Kipengele | Taarifa katika Mkataba |
|---|---|
| Malipo ya Kazi hadi kufikia Julai 2023 wakati ukaguzi ulifanyika | Asilimia 90 ya mkataba |
| Kuchelewa kukamilika kwa kazi | Miezi 12.37 |
| Hali ya urejeshwaji wa majanga | Hakuna majanga yaliyotokea licha ya malipo ya awali kufanyika. |
| iba kwa ucheleweshwaji wa malipo | Hakuna |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati ya Mkataba, Vocha ya Malipo na Ripoti ya Maendeleo ya Ujenzi wa Vituo vya mashine (Pump) 1 & 2 uliofanywa na wakaguzi, 2023*

### Jadweli Nambari 13: Taarifa ya mkataba wa ujenzi wa vituo ya kuendeshea mashine za maji kwa Loti 3

| Kipengele | Taarifa katika Mkataba |
|---|---|
| Mkataba wa No. | SMZ/IMF/No.104/W/RNCT/2021/2022/07 |
| Jina la Mkandarasi | KAMPUNI YA M/S OSAJU |
| Tarehe ya Kusaini | Machi 2, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza iliyohitajika | Baada ya ZAWA kukamilisha kuchimba visima |
| Tarehe ya Kuanza ya Ufanisi | 5 Julai 2022 |
| Muda wa Mkataba | Miezi 5 |
| Tarehe ya kukamilika kwa awali | 5 Disemba 2022 |
| Tarehe ya Kukamilisha iliyorekebishwa | 30 Aprili 2023 |
| Jumla ya Kiasi cha Mkataba wa awali na VAT | SHILINGI 1,299,027,097 |
| Mkataba wa Urekebishaji wa Jumla na VAT | Hakuna |
| Maendeleo ya Kazi (%) hadi Julai, 2023 | 80% |
| Malipo ya Kazi hadi kufikia Julai 2023 wakati ukaguzi ulifanyika | 63% ya mkataba |
| Kuchelewa kukamilika kwa kazi | Miezi 7.9 |
| Hali ya athari/majanga yaliyojitokeza mapema | Hakuna licha ya malipo ya awali kufanyika. |
| Riba ya ucheleweshwaji wa malipo | Hakuna |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati ya Mkataba, Hati ya Malipo na Ripoti ya Maendeleo ya Ujenzi wa vituo vya mashine (Pump) Loti ya 3 uliofanywa na wakaguzi, 2023*

Kwa hivyo, ukaguzi ulitathmini ikiwa ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine ya maji ulitekelezwa kwa ufanisi kwa kuzingatia wakati, gharama na ubora. Tathmini hiyo inashughulikia upangaji wa mradi, ununuzi, usimamizi wa muda, gharama na ubora kama ilivyoelezwa hapo chini.

## 4.2 Mipango isiyotosheleza ya Ujenzi wa Vituo vya kuendeshea mashine za maji

Sehemu hii inatoa ufafanuzi juu ya mipango ya ujenzi wa Vituo vya kuendeshea mashine ya maji zinazozingatia wigo wa kazi, Maandalizi ya Uainishaji na Usanifu wa kazi itakayotekelezwa. Mapitio ya miradi ya faili ukaguzi ulibainisha kuwa miradi ilikuwa na mipango ya kutosha kama ilivyoelezwa hapa chini.

### 4.2.1 Mapungufu katika upeo wa kazi

#### (a) Mapungufu katika uwekaji wa uzio (Fence) katika vituo vya kuendeshea mashine za maji

Kwa mujibu wa mkataba hati ya makisio ya gharama za ujenzi (BoQs) ukubwa wa uzio uliozungushwa katika maeneo ya vituo vya kuendeshea mashine za maji ilikua na ukubwa wa mita 195 na kila nguzo (Twiga post) iliyozuia uzio huo ilikua na ukubwa wa mita 65 kwa kila kituo cha kuendeshea mashine ya maji.

Hata hivyo, ukaguzi ulihakiki eneo lililozungushwa fensi na kubaini ukubwa wa fensi haukuwa sawa kama ilivyopangwa. Uchambuzi wa ukaguzi ulibaini ukubwa wa uzio uliojengwa katika vituo vya uendeshaji mashine za maji ulikua hauendani na ukubwa na gharama kwa mujibu wa BoQs jambo ambalo limesababisha uwepo wa mabadiliko ya urefu wa fensi na idadi ya nguzo zilizotumika katika fensi hiyo, Hali halisi ni kama inavyoonekana katika Jadweli lifuatalo: -

## Jadweli Nambari 14: Mabadiliko ya Vipimo pamoja na gharama katika uwekaji wa fensi katika vituo vya kuendeshea mashine za maji

| Vipengele | Loti | Idadi ya Uzio zilizojengwa za vituo vya kuendeshea Pampu za maji | Jumla ya idadi ya nguzo katika Mkataba | Jumla ya idadi ya nguzo zilizothibitishwa eneo la mradi | Tofauti ya idadi ya nguzo baina ya Mkataba Na eneo la mradi | Kiwango cha fedha (Shilingi) | Ongezeko au Kupungua kwa Gharama za Mradi (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya nguzo za Zege za wima | Loti ya 1 & Loti ya 2 | 22 | 1430 | 1604 | -174 | 37,500 | (6,525,000) |
| | Loti ya 3 | 25 | 1625 | 969 | 656 | 30,000 | 19,680,000 |
| Urefu wa waya uliozunguka uzio | Loti ya 1 & Loti ya 2 | 22 | 4290 | 4537 | -247 | 28,446.15 | (7,026,199.05) |
| | Loti ya 3 | 25 | 4875 | 3805 | 1070 | 21,058.97 | 22,533,097.90 |
| Zege iliyozunguka uzio kwa ajili ya kushikilia nguzo na waya. | Loti ya 1 & Loti ya 2 | 22 | 4290 | 4537 | -247 | 11,552.82 | (2,853,546.54) |
| | Loti ya 3 | 25 | 4875 | 3805 | 1070 | 9,452.31 | 10,113,971.70 |
| Waya wa juu uliounganisha waya ulio uzunguka uzio na nguzo za zege ($m^2$) | Loti ya 1 & Loti ya 2 | 24 | 1287 | 1361 | -74 | 14,000 | (1,036,000) |
| | Loti ya 3 | 25 | 1463 | 1142 | 321 | 16,500 | 5,296,500 |

*Chanzo: Uthibitishaji wa Eneo na BoQs za Mkataba*

Jadweli hapo juu linaonesha mabadiliko yaliyosababishwa na uwekaji wa fensi katika maeneo ya mradi ambayo yalisababisha uwepo wa mabadiliko ya kupanda na kupungua kwa gharama za mradi. Takwimu katika mabano hapo juu zinaonesha kuongezeka kwa gharama kutokana na kuongezeka kwa ukubwa wa uzio na takwimu ambazo haziko kwenye mabano zinaonesha kupungua kwa gharama. Hata hivyo, ukaguzi umeshindwa kupatiwa uchambuzi uliofanywa na ZAWA kuhusu mabadiliko hayo na kupeleka ongezeko la gharama za mkataba kupanda kwa kiasi cha Shilingi 57,623,569.60 ambazo zingeweza kuokolewa na ZAWA. Aidha ukaguzi ulibaini ongezeko la gharama za mkataba kwa loti 1 na 2 kwa shilingi 17,440,745.59 ambazo ni gharama za ziada ambazo zingeweza kutumika katika shughuli nyingine za mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unafanya uchambuzi yakinifu wa kazi zilizotekelezwa na kurejesha kiasi chote kilicholipwa kwa ziada kwa kazi isiyotekelezwa, aidha ukaguzi unapendekeza kufanya uchambuzi wa kazi iliyotekelezwa na kurejesha kiasi chote kilicholipwa kwa kazi isiyotekelezwa kutokana na kupungua kwa ukubwa wa uzio kwa loti ya 3.

Aidha, Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kufanya uchambuzi wa kazi iliyotek elezwa na kusababisha uwepo wa kazi ya ziada zilizofanywa na mkandarasi kutokana na kuongezeka kwa ukubwa wa fensi ambapo maamuzi yaliyotolewa kwa kumlipa mkandarasi kwa mujibu wa loti ya 1 &2.

**(b) Kutotekelezwa kwa ujenzi wa shimo la maji taka lenye thamani ya Shilingi 5,980,000**

Kulingana na hati ya mkataba wa Loti ya 1 & 2 wigo wa kazi ni pamoja na ujenzi wa shimo la maji taka kwa kila kituo cha pampu. Hii inamaanisha kuwa mkataba wa Loti ya 1 & 2 kulikuwa na jumla ya mashimo 26 ya maji taka ambayo yalitakiwa kujengwa. Ukaguzi ulifanya ziara ya eneo la mradi Mgenihaji na kubaini uwepo wa vituo viwili vya kuendeshea mashine ya maji ambavyo vilikua karibu sana ambapo kila kituo kilitegemea shimo moja la maji taka ambalo lilikuwepo katika eneo la mradi lenye ukubwa wa mita 1.64 hadi mita 2.7.

Hata hivyo, ukaguzi haukuweza kupatiwa uchambuzi wowote kutoka ZAWA uliofanywa unaoneshwa uwepo wa shimo moja la maji taka ambalo litatumika kwa vituo viwiwli kwa wakati mmoja hali ambayo ni kinyume kwa mujibu wa mchanganuo wa gharama za ujenzi(BoQs) ambazo zilianisha kila kituo cha uendeshaji mashine ya maji kinajitegemea kwa shimo lake la maji taka.

**Picha Nambari 2: Vituo viwili vya kuendeshea mashine ya maji vinavyotumia shimo moja la maji taka - Mgenihaji**




*Chanzo: Picha iliyopigwa na mkaguzi wakati wa ziara katika Vituo vya kuendeshea mashine za maji -Mgenihaji tarehe 21 Julai 2023.*

Kutokufanywa kazi ambazo zilipaswa kufanywa na mkandarasi ambazo ziligharimu jumla ya shilingi 11,960,000 kwa uchimbaji wa mashimo mawili kwa mujibu wa BoQs ambapo mkandarasi huyo alishindwa kutimiza ujenzi huo na badala yake alitumia gharama hizo kwa ujenzi wa shimo moja la maji taka kwa vituo viwili kwa gharama ya shilingi 5,980,000 pamoja na VAT na kufanya uwepo wa ziada ya shilingi 5,980,000 ambapo mkandarasi alizolipwa bila kutekeleza ujenzi wa shimo jengine la maji taka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kunakua na ufatiliaji mzuri kabla ya kufanya malipo ya mwisho kwa mkandarasi kwa mujibu wa shughuli zinazopaswa kutekelewa na mkandarasi huyo ili kijiridhisha kupitia mshauri elekezi kwa mujibu wa makubaliano ya kazi zilizoainishwa ndani ya mkataba wa 1&2 ili kupunguza uwepo wa ziada ya malipo kwa kazi ambazo hazikutekelezwa.

### 4.2.2 Kutokuainishwa kwa vipimo vya ujenzi katika BoQs

Kanuni nambari 102 (1) (c) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, 2020 inahitaji nyaraka za zabuni ambazo ni msingi wa uundaji wa mkataba kuwa na asili na sifa zinazohitajika za kiufundi na ubora, kazi au huduma zinazotolewa, ikiwemo vipimo vya kiufundi vinavyofaa.

Ukaguzi ulipitia nyaraka za mkataba na kubaini loti ya 2 ilihusika kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji kwa Unguja na Pemba na kubaini kuwa hakukuwa na vipimo ambavyo viliambatanishwa na mkataba, ambapo ukaguzi ulifanya mahojiano na mratibu wa mradi na kubaini kuwa vipimo vilivyotolewa kwa ajili ya ujenzi wa fensi na ujenzi wa shimo la maji taka havikuwemo katika BoQs pamoja na kukosekana kwa michoro ambayo ingeliweza kutoa vipimo hivyo. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo: -

**Jadweli Nambari 15: Vipimo ambavyo havikuanishwa katika BoQs**

| Maelezo kwa mujibu wa BoQs | Maelezo | Vipimo vilivyokosekana |
|---|---|---|
| Element no. 7 Plumbing and Drainage | Allow for construction of Septic Tank and all associated chambers for Complete drainage System | Size of septic tank has not been stated, Materials to be used for construction has not been stated, finishing has not been stated and size of chamber and drainage pipe is missing |
| Element no. 8 Fence, Twiga post | Supply and fix Twiga post at interval of 3m arount the fencing area and put support post at every 9m interval | Size of Twiga Post is missing, and size of reinforcement require is missing |
| Element no. 8 Fence, Chainlink Wire | Supply and fix chainlink wire to twiga post | Height of chain link is missing, Material of wire is missing, size of staining wire is missing. |
| Element no. 8 Fence. Burbed Wire | Supply and fix three layer of burbed wire to top of chainlink wire | Size, material, line spacing has not been stated |

*Chanzo: Mkataba wa BoQs, 2023*

Kuathiri mchakato wa zabuni wakati wa utayarishaji unapelekea mkandarasi kuathiri gharama kwenye vipimo kutokana na kutoanishwa kabla ya zabuni jambo ambalo linaweza kusababisha mkandarasi kusambaza vifaa ambavyo vimekosa ubora na kutekeleza kazi aliyopaswa kufanya kwa kiwango cha chini.

Ukaguzi unashuri Uongozi wa ZAWA kusimamia vizuri mchakato wa uandaaji wa BoQs kabla ya kuwasilishwa kwa wakandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

### 4.2.3 Usanifu usiotosheleza wa ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine ya maji.

Kanuni nambari 102(1)(c) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 inahitaji nyaraka za zabuni ambazo ni msingi wa uundaji wa mkataba kuwa na asili na sifa zinazohitajika za kiufundi na ubora, kazi au huduma zinazotolewa, ikiwemo vipimo vya kiufundi vinavyofaa.

Ukaguzi ulipitia nyaraka za mkataba kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine za maji, mashimo ya maji taka, uwekaji wa umeme katika vituo pamoja uwekaji wa fensi katika vituo hivyo, ukaguzi ulibaini ZAWA iliandaa picha za muonekano wa ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine za maji na hakukuwa na michoro ya usanifu ya muundo wa kituo cha kuendeshea mashine ya maji , mashimo mawili ya maji taka pamoja na michoro ya usanifu wa fensi inayoonesha vipengele vya muundo.

Ukosefu wa michoro ya miundo ulisababisha kizuizi katika kufanya ufuatiliaji juu ya kile kinachojengwa kama kinalingana na vipimo vilivyopangwa kwa mujibu wa BoQs pamoja na kukosekana kwa nyaraka muhimu zitakazoweza kuongoza ukaguzi jinsi ya ujenzi ulivyotekelezwa katika vituo vya kuendeshea mashine za maji,ujenzi wa fensi na ukubwa wa shimo la maji taka, hali hii ilibainika wakati wa ziara katika eneo ya Ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine ya maji kwa Lot 1 &2 katika eneo la Mgenihaji ambapo ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na uchimbaji wa misingi ya uwekaji wa fondesheni kwa ajili ya kuzuia waya wa fensi iliyozunguka eneo la kituo cha kuendeshea mashine za maji na badala yake waya wa fensi uliwekwa juu ya ardhi kwa kuambatansihwa na saruji nyembamba jambo ambalo limepelekea utekelezaji wa ujenzi huo kuwa chini ya kiwango ambapo kuna uwezekano wa fensi hiyo kukumbwa na mmong'onyoko wa udongo iwapo mvua itanyesha,hali halisi kama inavyoonekana katika Picha hapo chini.

**Picha Nambari 3: Mchanganyiko wa zege ulioshikilia waya wa fensi katika vituo vya kuendeshea mashine za maji**



*Zege tupu iliyowekwa juu ya ardhi bila ya kuichimbia msingi inayoshikilia waya wa fensi inayokabiliwa na mmong'onyoko wa ardhi*

*Chanzo: picha zilizopigwa na Wakaguzi wakati wa kutembelea eneo la mradi Mgenihaji,2023*

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kusimamia vyema mchakato wa uaandaaji wa michoro yote kabla ya kuanza shughuli za ujenzi.

## 4.3 Mchakato wa kumpata mkandarasi haukuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma

Sehemu hii inatoa matokeo kuhusu mchakato wa kuwapata wakandarasi ni kama ilivyoelezwa hapa chini:

### 4.3.1 Tathmini iliyofanywa kwa loti ambayo haikuwasilishwa wakati ufunguzi wa zabuni

Kanuni nambari 115(4) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 inahitaji zabuni zote zinazokubaliwa na kufunguliwa zipitishwe mara moja, zikiwa na nakala ya kumbukumbu ya zabuni zilizopokelewa na watu hao wanaohudhuria mkutano, kwa Kamati husika ya Tathmini kwa ajili ya tathmini.

Kupitia ripoti ya tathmini ya zabuni juu ya ufunguzi wa nyaraka za zabuni ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na jumla ya loti tatu zenye alama za Loti 1, Loti 2 na Loti 3 zikiwa na jumla ya wakandarasi 7 ambao zabuni zao zilifunguliwa kutoka kwa wazabuni tofauti. Ukaguzi ulipitia Kumbukumbu za kikao cha ufunguzi wa zabuni na kubaini kuwa kwa Loti 1 ilijumuisha jumla ya wazabuni 7, Loti 2 ilijumuisha jumla ya wazabuni 6 na lot 3 ilijumuisha jumla ya wazabuni 5 ambao zabuni zao zilifunguliwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa sio zabuni zote za mikataba ziliwasilishwa kwa kila loti, lakini wakandarasi wote saba walibainika kuwa na zabuni zao ikilinganishwa na makadirio halisi ya wahandisi kwa loti zote zilizofanyiwa tathmini. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika Jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 16: Loti zilizotolewa zabuni kwa Wakandarasi**

| Jina la Mzabuni | Loti ya Zabuni | Loti zilizolinganishwa na Makadirio ya Wahandisi | Loti ya zabuni ambayo mkandarasi hakuiomba |
|---|---|---|---|
| M/S Amos Company LTD | Loti ya tatu (Mstari wa 1, 2&3) | Loti ya tatu (Lot 1, 2&3) | Nil |
| M/S YASIN & Sons Co. LTD | Loti ya tatu (Mstari wa 1, 2&3) | Loti ya tatu (Lot 1, 2&3) | Nil |
| M/S Mwamba Company LTD | Loti ya tatu (Mstari wa 1, 2&3) | Loti ya tatu (Lot 1, 2&3) | Nil |

| Jina la Mzabuni | Loti ya Zabuni | Loti zilizolinganishwa na Makadirio ya Wahandisi | Loti ya zabuni ambayo mkandarasi hakuiomba |
|---|---|---|---|
| M/S Wakandarasi wa Ujenzi wa Kisasa ltd | Loti ya 1 & 2 | Loti ya tatu (Lot 1, 2&3) | Loti ya 3 |
| M/S Grasshoper | Loti ya tatu (Mstari wa 1, 2&3) | Loti ya tatu (Lot 1, 2&3) | Hakuna |
| M/S Osaju Company Ltd | Loti 1 na mengi 2 | Loti ya tatu (Lot 1, 2&3) | Loti ya 3 |
| M/S Shamjo Company LTD | Loti 1 na mengi ya 3 | Loti ya tatu (Lot 1, 2&3) | Loti ya 2 |

*Chanzo: Ripoti ya tathmini, fomu za kufungua zabuni na fomu za Zabuni*

Jadweli hapo juu linaonesha kutolingana kati ya zabuni ya Loti na Mkandarasi ambayo zabuni zilitathminiwa dhidi ya makadirio ya wahandisi kwani, wakandarasi watatu hawakutoa zabuni kwa loti zote lakini zabuni yao ililinganishwa na makadirio ya wahandisi kwa loti zote. Wazabuni hao ni M/S Shamjo Company Ltd kwa loti ya 2 lakini zabuni yake ililinganishwa na makadirio ya mhandisi, M/S Osaju Company ltd na M/S Modern Building Contractors ltd kwa loti ya 3 lakini zabuni zao zililinganishwa na makadirio ya mhandisi.

Hali hii ya tathmini ya wazabuni ambao hawakuwasilisha zabuni walipewa zabuni hizo kwa upendeleo maalum kwa Loti zilizofanyiwa tathmini ambapo matokeo ya tathmini hizo ziliwapendekeza wabuni ambao hawakuwasilisha zabuni za maombi ya loti walizopatiwa, Ukaguzi umebaini M/S Shamjo Company Ltd ambae hakuwasilisha zabuni ya loti ya 2 alipewa mkataba wa loti ya 2 na M/S Osaju Company ltd hakuwasilisha zabuni ya loti ya 3 alipewa mkataba wa loti ya 3 kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 4.3.3 cha ripoti hii.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa inatoa zabuni kulingana na maamuzi ya kamati ya tathmini kwa kuzingatia vigezo na sifa za mzabuni aliyeomba ili kunusuru kujitokeza kwa mzabuni kukosa sifa ya utekelezaji wa kazi aliyopewa.

### 4.3.2 Makosa yaliyojitokeza wakati wa tathmini ya zabuni

Kanuni nambari 123(2) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, 2020 inaitaka Taasisi ya Ununuzi na Utoaji wa Nyaraka kusahihisha makosa ya hesabu ambayo hugunduliwa wakati wa tathmini ya zabuni na Taasisi ya Ununuzi na Kusambaza ili kutoa taarifa ya haraka ya marekebisho yoyote ya aina hiyo kwa mzabuni aliyewasilisha zabuni hiyo.

Ukaguzi umebaini kupitia ripoti ya tathmini jumla ya wazabuni watatu (3) waliyowasilisha zabuni zao walifanyiwa usahihisho wa makosa ya kimahesabu kati ya wazabuni watano (5) walioomba ambapo ilibainika jumla ya wazabuni wawili (2) zabuni zao hazikupitiwa kwa ajili ya kufanyiwa usahihisho wa kimakosa ya kimahesabu jambo ambalo huenda likapelekea kutokeza kwa upotevu wa fedha za umma unatokana na ongezeko la gharama za makisio zilizokua hazikusahihishwa na kufanyiwa tathmini. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 17: Zabuni ambazo zilizofanyiwa tathmini**

| Nambari ya zabuni | Jina la Zabuni | Idadi ya Zabuni zilizopokelewa | Idadi ya Zabuni zilizofanyiwa Uhakiki wa Mahesabu | Zabuni ambayo haikufanyiwa ukaguzi wa hesabu |
|---|---|---|---|---|
| SMZ/IMF/NO.104/W/RNCT/2021/2022/07 | Ujenzi wa Kituo cha kuendeshea mashine ya maji kwa ZAWA | 5 | 3 | 2 |

*Chanzo: Ripoti ya Tathmini*

Jadweli hapo juu linaonesha kuwa zabuni 2 hazikufanyiwa uhakiki wa mahesabu licha ya kuwa wazabuni hao waliwasilisha zabuni zao ambao ni M/s SHAMJO COMPANY ltd na M/S USAJU COMPANY ltd.

Kutokufuata kwa Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ambazo zinahitaji wazabuni wote kufanyiwa ukaguzi wa hesabu wakati wa tathmini ya zabuni.

Aidha, ukaguzi umefanya uchambuzi wa mikataba pamoja na BoQs zilizowasilishwa na wakandarasi ambao ni M/s SHAMJO COMPANY ltd na M/S USAJU COMPANY ltd na kubainika kujitokeza kwa dosari zifuatazo: -

- Mkandarasi M/S Shamjo Company ltd alibainika kujitokeza kwa ongezeko la gharama la shilingi 87,906.00 kwa kuwa kulikuwa na vituo 26 vya pampu kwa mkandarasi kumeweza kupelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama za shilingi 2,285,556 katika BoQ zilizowasilishwa.
- Mkandarasi M/S Osaju Company ltd alibainika kujitokeza kwa ongezeko la gharama za shilingi 257,471.20 kwa kuwa kulikuwa na vituo 26 vya pampu kwa mkandarasi kumeweza kupelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama za shilingi 6,694,251.20 katika BoQ zilizowasilishwa.

Kutokana na dosari zilizobainika hapo juu kwa vile kamati ya tathmini ilishindwa kufanya uhakiki wa mahesabu wa zabuni za wakandarasi hao kumepelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama za ziada zenye thamani ya shilingi

8,979,807.2 ambazo kuna hatari ya wakandarasi hao kufanyiwa malipo ambayo hayaendani na uhalisia wa kazi walizozifanya.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kupitia kamati ya tathmini kuongeza umakini katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuepusha kujitokeza kwa malalamiko kwa baadhi ya wakandarasi au kufanya malipo ya ziada ambayo hayaendani na uhalisia wa utekelezaji wa majukumu ya mikataba yao.

### 4.3.3 Zabuni zilitolewa kwa Mkandarasi kwa Loti ambayo mzabuni hakuwasilisha zabuni

Kwa mujibu wa hati ya mkataba ya ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine ya maji ya ZAWA. Mikataba ya ujenzi wa vituo cha kuendeshea mashine ya maji kwa loti ya 1 ambayo iko Mjini Magharibi-Unguja, Loti 2 iko Kaskazini na Kusini Unguja, na loti ya 3 iko Kusini Pemba.Ukaguzi ulibaini kuwa M/S Shamjo Company Ltd ilipewa mkataba wa loti ya 1 na loti ya 2 wakati loti ya 3 ilipewa M/S Osaju Company Ltd. Mapitio ya fomu ya zabuni iliyowasilishwa na wakandarasi hawa wawili ukaguzi ulibaini kuwa, kulikuwa na loti ambazo hawakuwasilisha zabuni lakini walipewa mikataba ya utekelezaji katika zabuni hizo. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini

**Jadweli Nambari 18: Loti zilizoombwa na zilizotunukiwa kwa Wakandarasi**

| Jina la Mzabuni | Loti aliyoomba | Loti aliyotunukiwa | Loti ambayo hakuomba lakini alitunukiwa |
|---|---|---|---|
| Kampuni ya M/S Shamjo Ltd | Loti 1, Loti 3 | Loti 1 & Loti 2 | Loti ya 2 |
| Kampuni ya M/S Osaju Ltd. | Loti 1, Loti 2 | Loti ya 3 | Loti ya 3 |

*Chanzo: Fomu ya Zabuni na Ripoti ya Tathmini*

Jadweli hapo juu linaonesha kuwa loti ya 2 na loti ya 3 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kuendeshea mashine ya maji zilitolewa kwa mkandarasi ambae hakuomba zabuni kulingana na fomu ya zabuni. Kutokana na dosari hiyo ukaguzi umebaini kamati ya tathmini na bodi ya zabuni iliridhia uwepo wa dosari hizo na hakukuwa na sababu yoyote iliyotolewa na ZAWA iliyopelekea kutunukiwa kwa mkataba kwa wakandarasi hao.

Kutokuzingatiwa kwa taratibu na sheria za ununuzi kunaweza kukapelekea kujitokeza kwa athari ya kuwatunukia wakandarasi mikataba ya utekelezaji wa kazi ambazo hazitakuwa na ubora au kukidhi vigezo vilivyotakiwa kwa mujibu wa zabuni husika. Aidha hali hiyo inaweza kupelekea kuwanyima fursa wakandarasi wengine wenye sifa na uwezo wa utekelezaji wa kazi hiyo.

Uongozi unashauri uongozi wa ZAWA kuzingatia sheria na kanuni za uondoshaji wa mali za umma ili kunusuru kujitokeza kwa viashiria vya ukiukwaji wa maadili na hatimae kupelekea kuitia hasara Serikali.

### 4.3.4 Tofauti ya bei wakati wa ufunguzi wa zabuni ukilinganisha na fomu ya tuzo kwa Mkandarasi

Kanuni nambari 44 (5) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 zinahitaji bei ya kusoma wakati wa ufunguzi wa zabuni iwe ni bei halisi iliyobainishwa katika nyaraka za zabuni inahitaji kusomwa katika ufunguzi wa zabuni ili iwe kiasi kilichoandikwa katika fomu ya zabuni kama ilivyowasilishwa na wakandarasi. Mapitio ya fomu ya zabuni na wakati wa ufunguzi wa zabuni haikuwa sawa. Uchambuzi wa kusoma kwa kampuni iliyopewa ni kama ilivyowasilishwa katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 19: Tofauti katika Kielelezo cha Kusoma na Kiasi cha zabuni**

| Mkandarasi | Jina la Mkataba | Loti | Gharama halisi ya zabuni (A) | Gharama iliyosomwa wakati wa ufunguzi wa zabuni (B) | Tofauti iliyobainika (Tshs) (A) – (B) | Mabadiliko ya Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M/S Osaju Company Ltd | Ujenzi wa Vituo vya kuendeshea mashine ya maji kwa ZAWA | Loti ya 1 | 1,312,148,583.2 | 706,541,544.80 | 605,607,038.40 | 46 |
| | | Loti ya 2 | 1,312,148,583.2 | 605,607,038.40 | 706,541,544.80 | 54 |
| | | Loti ya 3 | | 1,312,148,583.2 | - | |
| M/S Shamjo Campany Ltd | Ujenzi wa Vituo vya kuendeshea mashine ya maji kwa ZAWA | Loti 1 | 714,916,441 | 767,343,640. | (52,427,199) | -7 |
| | | Loti 2 | | - | - | |
| | | Loti ya 3 | 1,239,189,365 | 1,425,066,760 | (185,877,395) | -15 |

Jadweli hapo juu linaonesha tofauti katika kiasi cha fomu ya zabuni na katika ufunguzi wa zabuni kusoma kiasi kwa wazabuni wawili ambao walipewa mkataba. Kwa M/S Osaju Company Ltd kuna kupungua kwa asilimia 46 na asilimia 54 kwa loti ya 1 na loti ya 2 kutoka kwa kiasi cha fomu ya zabuni. Kwa kesi ya M / S Shamjo Company ltd kulikuwa na ongezeko la asilimia 7 na asilimia 15 kwa loti ya 1 na loti ya 3 kwa mtiririko huo kiasi cha fomu ya zabuni.

Kutotumia fomu ya zabuni wakati wa ufunguzi wa zabuni ilisomwa ambayo ilichangiwa na uzingatiaji duni wa Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Hii ilisababisha uwezekano wa makosa katika kiasi cha mkataba kilichoingia ambacho huleta dalili ya udanganyifu wa mchakato mzima wa ununuzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unasimamia matumizi ya fomu ya zabuni wakati wa ufunguzi na usomaji wa zabuni ili kuepuka kujitokeza dosari ya kiasi cha zabuni kinachoripotiwa.

### 4.3.5 Utoaji wa Mkataba kwa mzabuni ambaye hakupendekezwa katika Ripoti ya Tathmini

Kanuni nambari 45(3) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, 2020 inaitaka Bodi ya Zabuni kupitia upya tathmini na mapendekezo yaliyowasilishwa na Kitengo cha Ununuzi na Uondoshaji na inaweza ama kuidhinisha mapendekezo hayo, kupendekeza tuzo ya mkataba kwa Afisa Masuuli au kukataa kuidhinisha mapendekezo ya tuzo ya zabuni na kuitisha zabuni mpya au kufanya tathmini upya au kuchukuwa hatua nyengine inayofaa.

Kutokana na mapitio ya ripoti ya tathmini kwa upande wa Unguja na Pemba (Lot 1, 2) kwa ajili ya vituo vya Pampu ukaguzi umebaini kujitokeza kwa dosari za kumtunukia zabuni mzabuni ambae hakupendekezwa na kamati ya tathmini.

Kwa mujibu wa ripoti ya tathmini ukaguzi umebaini kampuni ya M/S Osaju Company ltd ilishinda kwa loti zote kwa thamani ya shilingi 2,645,722,788.80. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kuwa kampuni ya M/S Osaju Company ltd ilitunukiwa zabuni yenye thamani ya shilingi 1,299,027,097 na kampuni ya M/S Shamjo Company Ltd ilitunukiwa zabuni yenye thamani ya shilingi 1,383,395,308 na kupelekea kujitokeza kwa ongezeko la shilingi 36,699,616 ambapo ilifanya jumla ya zabuni kufikia shilingi 2,682,422,405.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unatekeleza mapendekezo ya kamati ya tathmini kwa mzabuni aliyeshinda kupewa tuzo ya zabuni ili kuepusha kupewa tuzo mzabuni asie na sifa, au asie na vigezo vya utekelezaji wa kazi aliyopatiwa.

### 4.3.6 Upungufu wa Nyaraka za Mkataba

#### (a) Tofauti iliyobainika kati ya Malipo ya awali na malipo ya hati ya dhamana

Kifungu nambari 54.1 cha masharti ya jumla ya mkataba kinamtaka mkandarasi kuwasilisha malipo ya awali kwa njia ya dhamana ya benki isiyo na masharti katika fomu na kwa benki inayokubalika kwa mwajiri kwa kiasi na sarafu sawa na malipo ya awali kama ilivyoelezwa katika mashati maalum ya mkataba.

Mapitio ya masharti maalum ya mkataba yalibainisha kiasi cha dhamana ya malipo ya awali hakikuwa sawa na kiasi cha malipo ya awali yanayohitajika kulipwa. Jadweli hapo chini linatoa uchambuzi wa asilimia ya malipo ya awali na asilimia ya dhamana ya malipo ya awali.

### Jadweli Nambari 20: Kiasi cha Malipo ya awali na dhamana ya Malipo ya awali

| Nam. | Jina la Mkataba | Nambari ya Mkataba | Asilimia ya Malipo ya Awali ya Kulipwa kulingana na Mkataba | Thamani ya dhamana ya Malipo ya Awali iliyohitajika kuwasilishwa kulingana na Mkataba |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji kwa ZAWA Lot ya 3 | SMZ/No.104/G/RNCT/2021/2022/07 | Asilimia 20 ya mkataba | Asilimia 10 ya malipo ya awali kwa njia ya dhamana ya benki |
| 2. | Ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji kwa ZAWA Loti ya 1 na Loti ya 2 | SMZ/No.104/G/RNCT/2021/2022/07 | Asilimia 20 ya mkataba | Mkandarasi alitakiwa kuwasilisha tamko la Dhamana bila kusema thamani yake |

*Chanzo: Nyaraka za Mkataba*

Jadweli hapo juu linaonesha kwamba kwa mkataba wa pili kiasi cha kulipwa cha malipo ya awali kilikuwa asilimia 20 ya bei za mkataba. Lakini uwasilishaji unaohitajika wa dhamana ulikuwa asilimia 10 ya malipo ya awali kwa loti ya 3 kwa njia ya dhamana ya benki. Kwa loti ya 1 na 2 kiasi cha malipo ya awali mkandarasi alitakiwa kuwasilisha tamko la dhamana bila kusema thamani yake. Dhamana hizi zote sio sawa na kiasi cha malipo ya awali yanayohitajika.

Kutozingatia kile kinachohitajika katika masharti ya jumla ya mkataba wakati wa kujaza masharti maalum ya mkataba.

Malipo ya awali ya kwa mkandarasi hayakuzingatiwa vya kutosha na kutoa orodha ya kutorejesha kiasi cha malipo ya awali ikiwa kutajitokeza changamoto kwa mkandarasi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha inazingatia masharti maalum ya mikataba ili kuepuka kujitokeza kwa hasara ya kutokukamilika kwa kazi pindipo mkandarasi atakaposhindwa kutekeleza matakwa ya utekelezaji wa kazi zake kwa mujibu wa mkataba.

### (b) Hati ya Zabuni na Hati ya Mkataba iliyo na kiasi tofauti cha Dhamana ya Utendaji

Taratibu bora zinahitaji Dhamana ya Utendaji ilioelezwa katika hati za zabuni kuwa sawa katika hati za mkataba ili kudumisha muda katika mchakato wa zabuni. Ukaguzi ulifanya mapitio ya nyaraka za Zabuni na kubaini kuwa kifungu cha 26 cha masharti maalumu ya hati ya zabuni kinahitaji Dhamana ya Utendaji kuwa asilimia 10 ya bei ya mkataba. Pia, kifungu cha jumla ya mkataba kinamtaka mkandarasi kutoa Dhamana ya Utendaji kwa mwajiri kwa namna na kwa benki au uhakika unaokubalika kwa mwajiri.

Masharti maalum ya mkataba yalimtaka mkandarasi kuwasilisha dhamana ya utendaji kwa njia ya uhakikisho wa utendaji uliotolewa na mkandarasi ambae hakuwa aliyetajwa katika nyaraka za zabuni na katika hali ya jumla ya mkataba. Hii inaonesha mkandarasi alitakiwa kutoa hakikisho mwenyewe lakini sio sehemu ya tatu kama inavyotakiwa katika masharti ya jumla ya mkataba.

Ukaguzi umebaini utendaji wa kazi wa mkandarasi haukuzingatia masharti maalum ya mkataba jambo ambalo linaweza kupelekea kuisababishia hasara Serikali pindipo mkandarasi atakaposhindwa kutekeleza majukumu yake ya kazi kwa mujibu wa utaratibu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unazingatia masharti maalum ya mikataba ili kuongeza uaminifu kwa wakandarasi katika mchakato wa kufanya manunuzi

### (c) Kutokuzingatiwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu

Kanuni nambari 47(2) & (4) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 inamtaka Afisa Masuuli, ndani ya siku saba (7) baada ya kutoa uamuzi wa kuwasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali rasimu ya mkataba wa kuridhia. Afisa Masuuli anahitajika, baada ya kupokea maoni juu ya rasimu ya mkataba kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuyaingiza maoni hayo katika rasimu ya mkataba.

Mapitio ya nyaraka za mkataba na ushauri kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ukaguzi ulibaini kuwa kuna maoni ambayo yalitolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali lakini hayakuingizwa kwenye utekelezaji wa mkataba. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 21: Utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

| Nam. | Mkataba | Maoni muhimu kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji kwa ZAWA Loti ya 3. | Fomu ya zabuni ni ya tarehe 27 Disemba 2021 wakati barua ya taarifa ya tuzo ni ya tarehe 24 Februari 2021. Hii inahitaji kurekebishwa. | Yamefanyiwa kazi. |
| | | Fomu ya zabuni inaonesha mkandarasi aliomba loti ya 1 Unguja lakini taarifa ya tuzo imetolewa kwa loti ya 3. ZAWA inapaswa kufanya mapitio juu ya hili. | Hakuna maboresho yaliyofanywa. |
| | | BoQs na taarifa za kumbukumbu za kikao cha mapatano zimetajwa kuwa ni sehemu ya mkataba lakini hazikuambatanishwa katika mkataba. Hivyo, kutoambatanishwa kwa BoQs inapelekea ugumu wa kujua jinsi gani ilivyofikiwa bei iliyoelezwa. | Kumbukumbu za kikao zimeambatanishwa lakini BoQs hazikuambatanishwa |
| | | Uwepo wa Anwani mbili za mawasiliano ambazo ni anuani ya Makao makuu ya ZAWA na anuani ya Afisi ya ZAWA Pemba inaweza kusababisha kuchelewa kwa mawasiliano, kuna haja ya kuweka anwani moja. | Haijatekelezwa |
| | | Mkataba haukufuata malipo ya kawaida kama ilivyoelezwa katika hali ya jumla ya mkataba badala yake malipo yanapaswa kufanywa kwa msingi. Mkandarasi anatakiwa kulipwa malipo ya awali ya asilimia 20 ya kiasi cha mkataba lakini hakuna ahueni. Pia kifungu cha 25 cha SCC kinahitaji dhamana ya malipo ya awali kuwa katika mfumo wa tamko la dhamana tunapendekeza mkandarasi kuwasilisha dhamana ya benki ya malipo ya awali bila masharti kwa sababu tamko la dhamana sio salama ikiwa mkandarasi atakosa kutumia malipo ya awali. | Fomu ya dhamana ya malipo ya awali imerekebishwa lakini utaratibu wa malipo haujabadilishwa na hakuna urejeshaji wa malipo ya awali |
| | | Kiwango cha chini cha cheti cha malipo ya muda kisichotumika badala yake malipo yatategemea hatua za ujenzi hasa kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 4 ya fomu ya mkataba. | Eneo hilo halijatekelezwa badala yake limeeleza asilimia ya malipo kulingana na hatua iliyokamilishwa au kipengele cha kazi kama ilivyoelezwa katika mkataba. |

| Nam. | Mkataba | Maoni muhimu kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| 2. | Ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji kwa ZAWA Loti 1 na Loti 2 | Barua ya kukubalika, barua ya taarifa ya tuzo na michoro ni miongoni mwa nyaraka zinazounda sehemu ya mkataba lakini hazijaambatanishwa | Mchoro umeambatishwa lakini umeambatishwa haujakamilika kwani mchoro wa usanifu tu kwa Vituo vya kusimamia mashine za maji umeambatishwa lakini mchoro wa usanifu kwa uzio haujaambatanishwa na michoro yote ya muundo wa uzio na Vituo vya kusimamia mashine za maji haijaambatishwa |
| | | Kifungu cha 20 cha SCC na aina ya mkataba kinasema kuwa malipo yatakuwa kwa asilimia ya kazi iliyokamilishwa. Ofisi inashauri sehemu hii kubadilishwa na malipo kufanywa kulingana na kazi iliyokamilishwa kama ilivyothibitishwa na msimamizi wa mradi. | Kifungu hicho hakijatekelezwa sehemu ya uzio walioongeza kazi ili kuidhinishwa na Mhandisi wa ZAWA lakini utaratibu wa malipo haujabadilika. |
| | | Kifungu cha 26 cha Dhamana ya Utendaji wa SCC kinahitaji kurekebishwa Dhamana ya Utendaji ili kuwa katika mfumo wa dhamana ya benki isiyo na masharti badala ya tamko. Pia malipo ya awali ni asilimia 20 ya bei ya mkataba, ofisi inashauri dhamana kuwa sawa na kiasi cha malipo ya awali | Haijatekelezwa |
| | | Hadidu rejea za vikao vya mapatano ni miongoni mwa nyaraka zinazounda sehemu ya mkataba lakini hazija sainiwa | Haijatekelezwa kama mwenyekiti alivyosaini. |

*Chanzo: Hati za Mkataba na Maoni kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Loti zote mbili Unguja na Pemba*

Jadweli hapo juu linaonesha kwamba, ushauri kutoka kwa Mwanasheria mkuu haukuingizwa katika mkataba. Ukaguzi ulifanya uchambuzi juu ya vitu ambavyo vina maana ya gharama ya moja kwa moja kwa mkataba ambavyo haukuingizwa. Vitu hivi ni malipo ya kuwa katika suala la asilimia ya kazi iliyokamilishwa badala ya kuwa msingi wa kazi iliyotekelezwa. Hii itasababisha malipo ya dharura moja kwa moja bila idhini ya mteja na malipo ya gharama kwa ajili ya kuchimba mwamba ambayo ni sehemu ya mkataba na malipo yake hutegemea upatikanaji wa mwamba na juu ya kiasi chake na marekebisho ya uchimbaji ya kawaida inayohusiana.

Uchambuzi wa gharama ya kutojumuisha ushauri Mkuu wa Mwanasheria katika mkataba hasa juu ya malipo kwa wakandarasi kwa muda wa asilimia ya kipengele kilichokamilishwa kwa bei ya mkataba itasababisha malipo ya vitu ambavyo vinahitaji idhini ya mteja. Vitu ambavyo vitalipwa zaidi ni vya ziada kwa kuchimba ya mwamba na dharura. Uchambuzi wa gharama umewasilishwa katika Jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 22: Athari za kufanya malipo kwa kuzingatia asilimia**

| Nam. | Jina la Mkataba | Nambari ya Mkataba | Kipengele | Gharama ya jumla katika Mkataba (VAT Inclusive) kwa Vituo 26 za vya kuendeshea mashine ya maji |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji kwa ZAWA Loti ya 3 | SMZ/No.104/G/ RNCT/2021/2022/07 | Ziada juu ya uchimbaji wa mwamba | 888,118.81 |
| | | | Hali ya dharura | 125,978,321.8 |
| 2. | Ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji kwa ZAWA Lot 1 na Lot 2 | SMZ/No.104/G/ RNCT/2021/2022/07 | Ziada juu ya uchimbaji wa mwamba | 996,666.67 |
| | | | Hali ya dharura | 111,577,260.95 |
| **Jumla ya Kiasi** | | | | **239,440,368.23** |

*Chanzo: Hati ya Mkataba na Hati za Zabuni*

Jadweli hapo juu linaonesha kuwa kutokana na malipo kufanyika kwa asilimia ya bei ya mkataba shilingi 239,440,368.23 zinatarajiwa kuwa ni malipo ya ziada kwa wakandarasi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unatekeleza kikamilifu ushauri unaotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu ili kuepuka hasara inayoweza kujitokeza kwa kutozingatia maelekezo ya kisheria.

### (d) Kutojitosheleza kwa nyaraka za bei ya Mkataba

Kifungu nambari 40.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinahitaji hati ya makisio ya gharama za ujenzi kutumika kuhesabu bei ya mkataba. Inahitaji mkandarasi kulipwa kwa kiasi cha kazi iliyofanywa kwa kiwango cha hati ya makisio ya gharama za ujenzi kwa kila kitu. Aidha, taratibu zilizo bora zinahitaji bei ya mkataba kuunganishwa na masharti ya jumla ya kiasi kilichotolewa katika muhtasari wa mazungumzo na BoQ.

Mapitio ya nyaraka za mkataba yalionyesha kuwa jumla ya kiasi kilichowasilishwa katika BoQ ikizidishwa na idadi ya kazi zilizotekelezwa, ukitoa na punguzo lililowekwa matokeo yake si sawa na bei ya mkataba iliyopo. Hali hii imejitokeza katika moja ya mikataba miwili iliyotengenezwa kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 23: Hati ya makisio ya gharama za ujenzi na Kiasi cha Mkataba**

| Jina la Mkandarasi | Idadi ya Kazi | Gharama kwa kila Kazi na VAT (Tsh) | Jumla ya Gharama (Tsh) | Punguzo Wakati wa mapatano (%) | Jumla ya gharama na Punguzo (Tsh) | Kiasi cha Mkataba (Tsh) | Ongezeko la Gharama kulingana na punguzo (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M/s Shamjo Company Limited | 26 | 54,810,260 | 1,425,066,760 | 5 | 1,357,206,438.1 | 1,383,395,308 | 26,188,869.90 |
| M/S Usaju Company Limited | 26 | 50,467,253 | 1,312,148,578 | 1 | 1,299,157,007.92 | 1,299,027,097 | NIL |

*Chanzo: Nyaraka za Mkataba*

Jadweli hapo juu linaonesha kuwa kutokana na kutokuwapo kwa nyaraka za kutosha za bei ya mkataba kumepelekea uwepo wa ongezeko la shilingi 26,188,869.90 zaidi ya kiasi cha gharama za mkataba baada ya kutoa punguzo.

Ukaguzi ulibaini kuwa fomu ya mkataba na masharti maalum ya mkataba kifungu cha 20 zilibainisha kuwa malipo yatafanywa kwa awamu ambapo asilimia 20 ya bei ya mkataba italipwa baada ya kusaini mkataba, asilimia 40 baada ya kukamilika kwa kazi, asilimia 30 italipwa baada ya kukamilika kwa usanifu wa ujenzi, uwezekaji na uwekaji wa plasta, asilimia 5 italipwa baada ya kukamilika kwa uzio na asilimia 5 iliyobakia italipwa baada ya kumalizika kwa muda wa dhima ya kasoro.

Ukaguzi umebaini nyaraka hizi za mkataba ni kinyume na kifungu cha 40.2 cha masharti ya jumla ya Mkataba ambacho kinamtaka mkandarasi kulipwa kwa kiasi cha kazi iliyofanywa kwa hati ya makisio ya gharama kwa kila kitu.

Kufanyika malipo ya mkandarasi kwa kuzingatia asilimia ya bei ya mkataba kumepelekea mkandarasi kulipwa gharama za dharura za shilingi 239,440,368.23 pamoja na shilingi 26,188,869.90 na kupelekea kutokuwepo kwa mahusiano baina ya hati ya makisio ya gharama na bei ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha katika miradi ijayo utazingatia masharti maalum ya mkataba na hayatakinzana na vifungu vyengine vya mkataba ili kunusuru kujitokeza kwa malipo yasiyo na tija.

## 4.4 Utekelezaji wa Usimamizi wa Mikataba ya Miradi

### 4.4.1 Kutojitosheleza kwa dhamana ya utendaji kazi kwa Mkandarasi

Kifungu nambari 55.1 cha Mkataba kinahitaji, mkandarasi kuwasilisha Dhamana ya Utendaji si zaidi ya tarehe iliyoainishwa barua ya kukubali tuzo ya zabuni na kuwa katika hali inayokubalika na Mwajiri.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya kumbukumbu za mradi na hati za mikataba na kubaini kwamba dhamana ya utendaji kazi haikuwasilishwa na mkandarasi katika mikataba yote miwili jambo ambalo linaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma pindipo mkandarasi atakaposhindwa kutekeleza mradi katika kiwango kinachokubalika au kufilisika wakati wa utekelezaji wa mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi ya ZAWA kuhakikisha unazingatia matakwa ya mkataba ya uwasilishwaji wa hati ya dhamana ili kuweza kurejesha gharama zitakazotumiwa na Serikali pindipo mkandarasi atakaposhindwa kutekeleza mradi katika kiwango kilichoainishwa kwa mujibu wa mkataba.

### 4.4.2 Ucheleweshwaji wa ujenzi wa Vituo vya kuendeshea mashine za maji

Kwa mujibu wa kifungu nambari 1 cha masharti maalum ya mkataba kinahitaji kazi za ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine zikamilishwe ndani ya kipindi cha miezi minne kwa Loti 3 na ndani ya kipindi cha miezi mitano kwa Loti 1 na Loti 2.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya nyaraka za mikataba na majalada ya mradi na kubaini uwepo wa ucheleweshwaji wa kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine za maji kwa wakati, hadi ukaguzi unakamilika mnamo tarehe 18 Julai 2023 vituo hivyo havikukamilika kama ilivyotarajiwa na kupelekea baadhi ya vituo kufikia takriban kati ya miezi 8 na siku 14 hadi mwaka 1 na siku 6.
Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 24: Uchambuzi wa utekelezaji wa kazi za ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine za maji**

| Nambari ya Loti | Nambari ya Mkataba | Tarehe ya kuanza kwa mkataba | Muda wa utekelezaji wa mradi (Mwezi) | Tarehe ya Kukamilika kwa mradi | Muda wa ucheleweshwaji wa mradi (Mwezi) |
|---|---|---|---|---|---|
| Loti ya 1 & Loti ya 2 | SMZ/No.104/G/ RNCT/2021/2022/07 | 12 Februari 2022 | 5 | 11-Julai 2022 | 12.6 |
| Loti ya 3 | SMZ/No.104/G/ RNCT/2021/2022/07 | 5 Julai 2022 | 4 | 4 Novemba 2022 | 8.14 |

*Chanzo: Hati za mkataba na barua kwa Mkandarasi kwa ajili ya Upanuzi wa Muda*

Aidha, kutokana na majadiliano na baadhi ya watendaji ilibainika kwamba sababu kuu iliyopelekea kutokamilika kwa mradi kwa wakati kulitokana na ZAWA kuchelewa kukabidhi maeneo ya utekelezaji wa mradi kwa wakandarasi kulikosababishwa na ucheleweshwaji wa uchimbwaji wa visima.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kabla ya kusainiwa kwa mikataba ni vyema kufanya upembuzi yakinifu ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uchimbwaji wa visima ili kuweza kuleta tija kwa wananchi kwa wakati.

### 4.4.3 Udhibiti usiojitosheleza wa gharama za ujenzi wa vituo vya pampu

Kwa mujibu wa kifungu cha 40.2 cha masharti ya jumla ya mkataba kinaeleza gharama za mkataba zitakokotelewa kwa kuzingatia BoQ. Hivyo Mkandarasi atahitajika kulipwa kwa mujibu wa kazi aliyoifanya kulingana na thamani halisi ya BoQ kwa kila kazi atakayoifanya.

Aidha, kigezo cha malipo kilichotumika cha asilimia 20 ya malipo ya awali, asilimia 40 baada ya kukamilika kwa kazi, asilimia 30 italipwa baada ya kukamilika kwa usanifu wa ujenzi, uwezekaji na uwekaji wa plasta, asilimia 5 italipwa baada ya kukamilika kwa uzio na asilimia 5 iliyobakia italipwa baada ya kumalizika kwa muda wa dhima ya kasoro.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya hati za malipo pamoja na vielelezo vilivyotumika kufanyia malipo na kubaini wakandarasi walifanyiwa malipo kwa kigezo cha asilimia ya gharama ya mkataba baada ya kukamilika kwa kazi aliyoitekeleza. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 25: Hali ya malipo kwa mkandarasi

| Nam. | Jina la Mkataba | Nambari ya Mkataba | Kiasi cha Mkataba | Jumla ya malipo hadi Julai 2023 | asilimia iliyolipwa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji kwa ZAWA Loti ya 3 | SMZ/No.104/G/ RNCT/2021/2022/07 | 1,229,027,097.00 | 779,416,257.80 | 63 |
| 2. | Ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji kwa ZAWA Loti ya 1 na Loti ya 2 | SMZ/No.104/G/ RNCT/2021/2022/07 | 1,383,395,307.84 | 1,245,055,278.00 | 90 |

*Chanzo: Hati za Malipo*

Jadweli hapo juu linaonesha kuwa mkandarasi nambari 2 amelipwa asilimia 90 ya bei ya mkataba kwa ajili ya Ujenzi wa Vituo vya kuendeshea Pampu kwa Loti 1 na loti 2 na asilimia 63 ya bei ya mkataba wa Ujenzi wa Vituo vya kuendeshea mashine ya maji kwa Loti 3. Malipo yalifanywa kulingana na asilimia ya kazi iliyotekelezwa jambo ambalo ni kinyume na masharti ya jumla ya mkataba.

Kutokana na dosari iliyobainishwa hapo juu imepelekea kujitokeza kwa malipo ya dharura ambayo hayajapata idhini na kuthibitishwa kwa kazi mpya iliyofanywa pamoja na malipo ya uchimbaji wa mwamba ambao ulikuwa unahitaji uthibitisho wa mwajiri kwa thamani ya fedha ambayo ilipaswa kulipwa jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa ongezeko la malipo ya dharura yenye thamani ya shilingi 181,242,392.44 yanayotokana na gharama za upasuaji wa mwamba bila ya uwepo wa uthibitisho wa kazi iliyotekelezwa. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 26: Ongezeko la gharama za ziada za upasuaji wa Miamba

| Nam. | Jina la Mkataba | Kipengele | Gharama za malipo kwa mujibu wa BoQs (Tsh) | Asilimia ya ziada ya malipo iliyolipwa | Malipo ya ziada yaliyolipwa (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji kwa ZAWA Lot 3 | Kazi ya ziada ya uchimbaji mwamba | 888,118.81 | 63 | 559,514.85 |
| | | Kazi ya dharura | 125,978,321.8 | 63 | 79,366,342.73 |
| 2. | Ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji kwa ZAWA Loti 1 na Loti 2 | Kazi ya ziada ya uchimbaji mwamba | 996,666.67 | 90 | 897,000.00 |
| | | Kazi ya dharura | 111,577,260.95 | 90 | 100,419,534.86 |
| **Jumla ya kiasi kilicholipwa** | | | | | **181,242,392.44** |

*Chanzo: Hati ya Malipo na makisio ya Gharama ya Mkataba*

Ukaguzi unaushauri uongozi ZAWA kuhakikisha kuwa kuna nyaraka za kutosha za mkataba na vile vile malipo yanafanyika kwa kuzingatia kazi zilizotekelezwa na matumizi yoyote ya dharura ili kuweza kupata uthibitisho wa shughuli zilizotekelezwa.

### 4.4.4 Udhibiti usiojitosheleza wa ubora wa kazi kulingana na Masharti na Vigezo vya Mkataba

Kifungu nambari 36.1 cha masharti maalum ya mkataba kinahitaji meneja wa mradi kuangalia kazi ya mkandarasi na kumjuulisha juu ya dosari yoyote itakayobainika wakati wa utekelezaji wa mradi. Kutokana na hali hiyo kazi ya ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine za maji ilihitaji kupimwa kwa kuangalia ubora wa zege, uimara wa nguzo pamoja na paa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya kumbukumbu za mradi na kubaini kuwa hakuna vipimo vilivyofanyika katika jaribio lililofanywa pamoja na mahojiano na Mratibu juu ya miradi yote ya UVIKO-19 iliripotiwa na kubaini kuwa hakukufanyika jaribio katika ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine ya maji. Aidha, imebainika hakukuwa na udhibiti wa ubora wa ujenzi wa Vituo vya kuendeshea mashine za maji.

Aidha, kwa upande wa vituo vilivyopo Mgenihaji, ukaguzi ulibaini kwamba ujenzi wa zege iliyowekwa kwa ajili ya kushikilia waya wa uzio wa vituo vilivyojengwa kwa loti 1 na 2 ilibainika kutokua na ubora kutokana na ujenzi huo kutokukidhi vigezo vinavyohitajika jambo ambalo huenda likapelekea kujitokeza kwa mmong'onyoko wa udongo na kupelekea kuharibika wakati wa mvua kubwa. Picha nambari 3 ya ripoti hii inaonesha ujenzi wa uzio uliokuwa haukukidhi vigezo.

Kutokana na ziara iliyofanywa na wakaguzi katika maeneo mengine ya miradi ya vituo vya kuendeshea mashine ya maji ikiwemo eneo la Kironjo II, Ng'ambwa darajani, Chambani kwapopo, na kubainika uwepo wa miundombinu ya uwekaji wa mabomba ya maji machafu ambayo hayakufukiwa ardhini na kupeleka kupigwa na jua kwa kipindi chote jambo ambalo huenda mabomba hayo yakachakaa,kupasuka na kuanza kumwaga maji machafu ambayo hayatakua salama katika vyanzo vya maji safi na hatimae kuenda yakasababisha kujitokeza kwa mripuko wa maradhi mbalimbali kwa yale maeneo yaliyokaribu na wananchi. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha hapo chini: -

**Picha Nambari 4: Maeneo ya vituo vya kuendeshea mashine ya maji yaliyobainika kujengwa kwa kiwango cha chini**

| | | |
|---|---|---|
|  |  |  |
| *Dari ya zege inayovuja katika eneo la Kironjo II* | *Bomba la maji machafu linalopigwa na mwanga wa Jua katika eneo la Kwa popo* | *Bomba la maji machafu linalopigwa na mwanga wa Jua katika eneo la Ng'ambwa Darajani* |

*Chanzo: Eneo lililotembelewa na Wakaguzi tarehe 26 na 27 Julai, 2023 Pemba Zanzibar*

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha inaweka utaratibu wa kutosha wa udhibiti bora bila ya kujali ukubwa wa miradi ili kuhakikisha miradi inajengwa kwa ubora uliokusudiwa pamoja na kuhakikisha nyaraka za mkataba zimewekewa maelezo ya kutosha ya vitu vyote vya kazi vinavyotarajiwa kutekelezwa.

# SURA YA TANO



# 5.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA UCHIMBAJI NA UJENZI WA VISIMA VIPYA

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi juu ya mradi wa maji wa uchimbaji na ujenzi wa visima vipya Thalathini na nane (38) vilivyokusudiwa kuongeza uzalishaji wa maji katika mfumo wa usambazaji wa maji safi na salama kwa Unguja na Pemba.

Mamlaka ya Maji Zanzibar katika malengo ya kuongeza na kuboresha uzalishaji wa maji ilifunga mkataba na mkandarasi M/S Simplex Engineering kwa ajili kufanya kazi ya uchimbaji na ujenzi wa visima vipya 38, kati ya hivyo visima vipya 11 kwa upande wa Unguja na visima vipya 27 kwa Pemba. Hali halisi ya taarifa ya mkataba wa uchimbaji wa visima hivyo ni kama inavyoonekana katika Jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 27: Taarifa ya Mkataba wa uchimbaji na Ujenzi wa Visima Vipya**

| Kipengele cha Mkataba | Mkataba wa uchimbaji na ujenzi wa visima vipya kwa Loti ya 1; loti ya 2; na Loti ya 3 |
|---|---|
| Nambari ya Mkataba | SMZ/IMF/No.104/G/RNCT/2021/2022/04 |
| Jina la Mkandarasi | M/S Simplex EngineeringLimited |
| Tarehe ya Kusaini | Machi 9, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza | Machi 16, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza ya Ufanisi | Machi 16, 2022 |
| Muda wa Mkataba | Miezi 5 |
| Tarehe ya awali ya kukamilika | Agosti 17, 2022 |
| Tarehe halisi ya Kukamilisha | Juni 4, 2023 |
| Jumla ya kiasi cha Mkataba wa awali na VAT | Shilingi 1,630,102,815.00 |
| Jumla ya Kiasi cha Mkataba wa Urekebishaji na VAT | - |
| Maendeleo ya Kazi (%) hadi Julai 2023 | Asilimia 100 |
| Maendeleo ya Malipo (%) hadi Julai 2023 | Asilimia 86 |
| Kuchelewa kukamilika kwa kazi | Miezi 10 |
| Riba ya kuchelewa malipo | - |

*Chanzo: Nyaraka za Mkataba*

Ukaguzi huo ulithamini juhudi zilizofanywa hadi sasa kuhakikisha uendelevu katika uzalishaji wa maji na uanzishwaji wa chanzo kipya cha maji. Hata hivyo, mapungufu yafuatayo yalibainika wakati wa utekelezaji wa mradi huo.

## 5.2 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Mipango na Usanifu wa Mradi

### 5.2.1 Kutokuwepo kwa Uzingatiaji wa Mipango ya Utekelezaji wa Mradi

Kifungu cha 15.1 cha GCC cha mkataba wa uchimbaji na ujenzi wa visima vipya kinamtaka mkandarasi kutegemea ripoti yoyote ya uchunguzi wa eneo la ujenzi, ikiongezewa na habari yoyote inayopatikana kwa mzabuni.

Wakati wa uanzishwaji wa mradi ripoti ya uchunguzi wa kijiolojia inatoa uhakika wa kiasi cha maji kinachokadiriwa ili kukabiliana na mahitaji ya maji katika eneo maalum. Kulingana na ukaguzi wa Ripoti ya Utafiti wa miamba iliyoandaliwa na M/s Simplex Engineering ya Juni 2022, ukaguzi ulibaini kuwa ilipendekezwa kuwa visima vitachimbwa kwa kipenyo cha **inchi 14** (355mm), na kukamilika na **12 "inchi** bomba za UPVC kama inavyoonyeshwa katika Picha ifuatayo.

**Picha Nambari 5: Aina ya kisima**




**Key**: bgl = below ground level

*Source: Ripoti ya Utafiti wa Miamba*

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa eneo la mradi uliofanywa wakati wa ukusanyaji wa taarifa ilibainika kutozingatia uchimbaji wa visima kama ilivyowasilishwa katika Jadweli hapa chini.

**Jadweli Nambari 28: Kutozingatia mapendekezo ya utafiti wa Miamba**

| Kisima | Mapendekezo ya Utafiti wa Miamba | | Vipimo Halisi | |
|---|---|---|---|---|
| | Kipenyo cha Kisima(Inch) | Vifuniko vya UPVC (Inch) | Kipenyo cha Kisima (Inch) | Vifuniko vya UPVC (Inch) |
| Visima vya Unguja | | | | |
| Uroa/Bambi BH1 | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Uroa/Bambi BH2 | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Mgeni Haji BH1 | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Mgeni Haji BH2 | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Unguja Ukuu BH1 | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Unguja Ukuu BH2 | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Kiashangwe | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Donge Kipange BH1 | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Kaburi Kikombe BH1 | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Kaburi Kikombe BH2 | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Visima vya Pemba | | | | |
| Sharifu Ali BH1 | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Sharifu Ali BH2 | 14″ | 12″ | 8″ | 7″ |
| Sharifu Ali BH3 | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Sharifu Ali BH4 | 14″ | 12″ | 8″ | 7″ |
| Mkoroshoni | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Shamiani | 14″ | 12″ | 8″ | 7″ |
| Jaani | 14″ | 12″ | 8″ | 7″ |
| Mwambe | 14″ | 12″ | 8″ | 7″ |
| Kiwani | 14″ | 12″ | 8″ | 7″ |
| Mbiji BH1 | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Mbiji BH2 | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Manyaga | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Mtuhaliwa | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Ngwachani | 14″ | 12″ | 8″ | 7″ |
| Mjimbini | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Chambani | 14″ | 12″ | 11″ | 10″ |
| Ng’ombeni | 14″ | 12″ | 8″ | 7″ |

*Chanzo: Ripoti ya Utafiti wa Miamba na Vipimo halisi*

Jadweli hapo juu linaonesha kutozingatia mapendekezo ya utafiti wa miamba juu ya kipenyo cha visima ambapo kwa visima kutoka Unguja vilionekana kuwa na kipenyo cha nje chenye inchi 11 na kipenyo cha ndani chenye inchi 10 na kisima kutoka Pemba kilikuwa na ukubwa tofauti wa kipenyo kutoka 11 " nje na 10" ndani hadi 8" nje na kipenyo cha ndani cha 7".

Kutokana na dosari iliyobainishwa hapo juu huenda ilisababishwa na uwepo wa mipango hafifu iliyochangiwa na utekelezaji wa miradi kulingana na kazi kimazoea. Hii ilisababisha kutozingatia ripoti ya uchunguzi wa miamba kama ilivyoelezwa katika masharti maalum ya mkataba.

Ukosefu wa kuzingatia ripoti ya utafiti wa miamba ili kutambua kigezo sahihi cha vyanzo vya visima viliathiri mambo yafuatayo: -

e) Upatikanaji wa visima vilivyoharibika na visima vikavu wakati wa utekelezaji wa mradi;
f) Kupunguza ukubwa sahihi wa visima vya pampu
g) Matengenezo yasiotosheleza ya visima kwa kupunguza kifuniko na uingizaji mpya wa UPVC.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kuhakikisha unafuatilia ipasavyo uchunguzi wa miamba iliyofanywa kwa ajili ya uzalishaji wa maji ili kukabiliana na mahitaji ya wingi wa maji.

## 5.3 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Mambo ya Ununuzi

### 5.3.1 Kamati ya Tathmini kukosa Utaalamu wa Kutosha

Kwa mujibu wa kifungu nambari 118(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016, kilisema kuwa "Bila kuathiri kifungu cha 32(4) cha Sheria, Kamati ya Tathmini itajumuisha wanachama wenye ujuzi, maarifa na uzoefu unaohusiana na mahitaji ya ununuzi na inaweza kujumuisha: (a) utaalamu husika wa kiufundi; (b) utaalamu wa ununuzi; (c) utaalamu wa uchambuzi wa fedha; (d) utaalamu wa kisheria; au (e) mwakilishi kutoka idara ya mtumiaji

Ukaguzi ulipitia ripoti ya tathmini ya zabuni ya mkutano wa Bodi ya Zabuni uliofanyika tarehe 31 Agosti, 2021 na kubaini kuwa Kamati ya Tathmini ina wajumbe sita kama ilivyowasilishwa na kitengo cha usimamizi wa manunuzi (PMU) lakini baadhi ya wataalamu wamekosekana katika Kamati, kama vile mtaalamu wa sheria, mtaalamu wa uchambuzi wa fedha kwa mujibu wa kifungu Na. 32 cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

**Jadweli Nambari 29: Wajumbe wa Kamati ya Tathmini**

| Nam. | Majina | Taaluma | Taasisi | Nafasi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mr. Moh'd O. Moh'd | Afisa wa Ununuzi | ZPRA | Mwenyekiti |
| 2. | Mr. Hussein A. Juma | Uhandisi wa Umeme | ZAWA | Mjumbe |
| 3. | Mr. Ali H. Haji | Afisa wa mabomba | ZAWA | Mjumbe |
| 4. | Mr. Hassan Z. Haji | Mchimbaji wa visima | ZAWA | Mjumbe |
| 5. | Mr. Hassan H. Kongo | Mtaalamu wa Umeme | ZAWA | Mjumbe |
| 6. | Mr. Moh'd A. Khatib | Mchimbaji wa visima | ZAWA | Mjumbe |

*Chanzo: Ripoti ya tathmini ya Zabuni*

Jadweli hapo juu linaonesha kuwa muundo wa kamati ya tathmini haukuwa na wataalam waliobobea katika uchambuzi wa kisheria na kifedha.

Kukosekana kwa baadhi ya wajumbe wenye sifa kwenye kamati ya tathmini ilisababisha uwepo wa mapendekezo ya tuzo ya wauzaji ambao hawana sifa na kusababisha gharama kwa serikali.

Ukaguzi unashauri mamlaka ya Maji Zanzibar Kitengo cha usimamizi wa manunuzi kinapaswa kuzingatia wataalamu wote wa kitaalamu katika kamati ya tathmini.

## 5.4 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Usimamizi wa Mkataba

### 5.4.1 Malipo ya awali yaliyofanyika bila kuwasilisha dhamana ya Benki na Dhamana ya Utendaji

Kwa mujibu wa kifungu nambari 54 cha GCC, Mwajiri atafanya malipo ya awali kwa mkandarasi baada ya kuwasilisha dhamana ya benki kwa fomu na kwa benki inayokubalika kwa mwajiri kwa kiasi na sarafu sawa na malipo ya awali.

Pia, kwa mujibu wa kifungu nambari 55 cha GCC kilisema kuwa, "Dhamana ya Utendaji utatolewa kwa mwajiri kabla ya tarehe iliyoainishwa katika barua inayokubalika na itatolewa kwa kiasi na fomu na benki au uhakika unaokubalika kwa mwajiri."

Ukaguzi ulibaini kuwa, Mamlaka ya Maji Zanzibar ililipa malipo ya awamu ya kwanza kwa Kampuni ya M/S Simplex Engineering Ltd bila kupata dhamana ya benki na Dhamana ya Utendaji kutoka kwa Muuzaji kama mkataba uliosainiwa.

Kufanya malipo bila ya kuzingatia uwasilishwaji wa dhamana ya benki na dhamana ya utendaji kunaweza kupeleka uwepo wa udhibiti duni wa kifedha ambao uliruhusu malipo kufanywa bila kuzingatia mahitaji ya mkataba.

Ukosefu wa Dhamana ya mradi kwa utekelezaji wa kazi, kwani kukosekana kwa Dhamana ya Utendaji inapelekea Dhamana ndogo kwa ZAWA ikiwa mkandarasi atashindwa kutekeleza kazi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji kuhakikisha miradi ijayo Wazbuni wote wanawasilisha dhamana ya utendaji pamoja na dhmana ya benki ili kunusuru kuitia hasara Serikali pindipo mkandarasi atakaposhindwa matakwa ya mkataba wake**.**

### 5.4.2 Ukiukwaji wa taratibu za Malipo na kupelekea hasara ya shilingi 928,153,089.48

Kifungu nambari 20 cha masharti maalum (SCC) kinachobainisha kifungu nambari 47.1(m) cha masharti ya jumla ya mkataba GCC cha uchimbaji na ujenzi wa visima vipya kilibainisha kwamba malipo yaliyofanywe kwa asilimia dhidi ya hatua ya mradi kama ifuatavyo;

**Jadweli Nambari 30: Uchambuzi wa Mbinu za Malipo**

| Njia ya Malipo (%) | Maendeleo ya Kazi (%) |
|---|---|
| 30 | 10 |
| 30 | 50 |
| 30 | 90 |
| 5 | Baada ya kukamilika kwa asilimia 100 |
| 5 | Baada ya kukamilika kwa DLP |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka Hati za Mkataba*

Aidha, kifungu nambari 45.3 cha GCC cha uchimbaji na Ujenzi wa Visima Vipya kwa ajili ya kumtaka Meneja wa Mradi kuamua thamani ya kazi inayotekelezwa kwa ajili ya uthibitisho wa malipo kulingana na thamani ya vitu vilivyo katika hati za makisio ya gharama za mradi iliyokamilishwa. Kwa kuwa BoQs ilieleza kuwa uchimbaji wa visima vyote vipya 38 ulipaswa kuwa na kina cha kipenyo cha mita 150 na inchi 12.

Kwa kuzingatia ukaguzi wa cheti cha malipo kilichotolewa na timu ya ukaguzi, ilibainika kuwa malipo hayo yalifanywa kwa mujibu wa kifungu nambari 20 cha SCC kama ilivyowasilishwa katika jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 31: Malipo yaliyofanywa kwa mkandarasi**

| Namba | Nambari ya hati za malipo | Kiasi cha Malipo (Tsh) | Asilimia ya (%) |
|---|---|---|---|
| 1. | PV2000215 | 489,030,844.50 | 30 |
| 2. | PV2000261 | 489,030,844.00 | 30 |
| 3. | PV2000395 | 415,676,271.00 | 26 |
| | **Jumla** | **1,393,737,959.50** | **86** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka Hati za Malipo*

Hata hivyo, Ukaguzi ulibaini uwepo wa malipo yaliyofanywa kwa kuzingatia gharama za makisio ya ujenzi ambayo yalikuwa chini ya kazi halisi iliyotekelezwa kama ilivyoelezwa katika Jadweli hapa chini.

**Jadweli Nambari 32: Uchambuzi wa upimaji wa visima wa kina (urefu) kwa Unguja**

| Eneo | Urefu wa kisima kulingana na BoQs (m) | Kipimo cha urefu kama ilivyo katika ziara ya ukaguzi (m) | Urefu wa kisima usiochimbwa (m) |
|---|---|---|---|
| Uroa/Bambi BH1 | 150 | 79.00 | 71.00 |
| Uroa/Bambi BH2 | 150 | 69.65 | 81.35 |
| Mgeni Haji BH1 | 150 | 17.44 | 132.56 |
| Mgeni Haji BH2 | 150 | 38.60 | 111.40 |
| Unguja Ukuu BH1 | 150 | 26.60 | 123.40 |
| Unguja Ukuu BH2 | 150 | 33.00 | 117.00 |
| Kiashangwe | 150 | 69.20 | 80.80 |
| Donge Kipange BH1 | 150 | 50.15 | 99.85 |
| Donge Kipange BH2 | 150 | Nil[1] | Nil’ |
| Kaburi Kikombe BH1 | 150 | 42.00 | 108.00 |
| Kaburi Kikombe BH2 | 150 | 42.00 | 108.00 |
| **Jumla** | | **467** | **1033.36** |

*Chanzo: Hati ya Mkataba na Upimaji wa kina uliofanywa na wakaguzi,2023*

Kipimo cha kina cha visima 27 kutoka Pemba vilikuwa kama ilivyowasilishwa katika Jadweli hapo chini.

1 Kisima kipya kilichochimbwa kilianguka, na kufanya kutoweza kupima kisima hicho

### Jadweli Nambari 33: Uchambuzi wa Upimaji wa visima kwa Kina (urefu)-Pemba

| Eneo | Urefu wa kisima kulingana na BoQs (m) | Kipimo cha urefu kama ilivyo katika ziara ya ukaguzi (m) | Urefu wa kisima usiochimbwa (m) |
|---|---|---|---|
| Mapofu 1 | 150 | 45.30 | 104.70 |
| Mapofu 2 | 150 | 65.30 | 84.70 |
| Mapofu 3 | 150 | 44.80 | 105.20 |
| Kironjo | 150 | 68.70 | 81.30 |
| Kiuyu Manda 1 | 150 | 45.00 | 105.00 |
| Kiuyu Manda 2 | 150 | 50.30 | 99.70 |
| Saninga | 150 | 34.00 | 116.00 |
| Wande | 150 | 65.00 | 85.00 |
| Kijuki | 150 | 25.00 | 125.00 |
| Uwondwe | 150 | 78.30 | 71.70 |
| Sharifu Ali BH1 | 150 | 98.00 | 52.00 |
| Sharifu Ali BH2 | 150 | 52.70 | 97.30 |
| Sharifu Ali BH3 | 150 | 78.20 | 71.80 |
| Sharifu Ali BH4 | 150 | 63.00 | 87.00 |
| Mkoroshoni | 150 | 97.00 | 53.00 |
| Shamiani | 150 | 98.00 | 52.00 |
| Jaani | 150 | 87.00 | 63.00 |
| Mwambe | 150 | 66.00 | 84.00 |
| Kiwani | 150 | 55.62 | 94.38 |
| Mbiji BH1 | 150 | 90.00 | 60.00 |
| Mbiji BH2 | 150 | 90.00 | 60.00 |
| Manyaga | 150 | 88.90 | 61.10 |
| Mtuhaliwa | 150 | 41.40 | 108.60 |
| Ngwachani | 150 | 25.00 | 125.00 |
| Mjimbini | 150 | 88.50 | 61.50 |
| Chambani | 150 | 71.10 | 78.90 |
| Ng’ombeni | 150 | 61.75 | 88.25 |
| **Jumla** | | | **2,276.13** |

***Chanzo***: *Hati ya Mkataba na Upimaji wa uchimbaji na Ujenzi wa Visima Vipya*

Jadweli 33 na 34 linaonesha kupungua kwa kina cha visima kutokana na kina kilichopendekezwa katika BoQs, na kuacha kina kisicho na maji kuwa 1033.36 kwa Unguja na 2276.13 kwa Pemba. Hali hii ilithibitika kutokana na mapitio ya ripoti ya uchimbaji wa visima na vipimo vya kina vilivyochukuliwa wakati wa

ukusanyaji wa taarifa ambao ulifafanua kina kidogo cha kuchimba kuliko BoQs na kupelekea kujitokeza upotevu wa shilingi 928,153,089.48 kama gharama ya kina kisichochimbwa cha 3309.49m kutoka Unguja na Pemba.

Kutokana na dosari iliyobainishwa hapo juu huenda ilitokana na uongozi wa ZAWA kutokuhakikisha vyeti vya malipo kwa mujibu wa visima halisi vilivyochimbwa na kujengwa, ambapo malipo yaliyofanywa hayakuzingatia kima halisi cha uchimbaji wa visima kwa mujibu wa masharti ya mkataba.

Udhibiti usiotosheleza wa malipo kulingana na kazi iliyotekelezwa ulisababisha uwepo wa gharama za ziada ambazo hazikutekelezwa kama ni gharama za uchimbaji wa visima kwa mujibu wa BoQs kunapelekea viashiria vya uwepo wa malipo ambayo hayatagharamia kazi iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kwamba fedha zilizolipwa kwa kazi isiyotekelezwa zinarejeshwa ili kuweza kupangiwa matumizi mapya ya serikali.

### 5.4.3 Kuchelewa kukamilika kwa Mradi wa Uchimbaji wa visima

Kifungu nambari 1 cha SCC cha Mkataba wa uchimbaji na ujenzi wa visima vipya kilihitaji kukamilika kwa mkataba kwa kazi nzima kuwa miezi mitano (5) kutoka tarehe ya kuanza ambayo ilikuwa siku saba baada ya kusaini mkataba. Kutokana na mapitio ya Ripoti ya Maendeleo ya Mradi ya Machi 2023, ukaguzi ulibaini kuwa kazi nzima ilikuwa ni asilimia 90 tu ya visima vyote vinavyohitajika, hii ina maana kati ya visima vipya 38 vilivyochimbwa na kujengwa visima 34 vilikamilika na visima vinne ambavyo bado havijakamilika viliyopo kisiwani Pemba.

Aidha, imebainika ucheweleshwaji wa kukamilika kwa uchimbaji na ujenzi wa visima ni baina ya miezi 10 na zaidi ambapo hadi ukaguzi unakamilika Juni,2023 bado baadhi ya visima havijakamilika kama inavyobainishwa katika jadweli hapo juu.

Kuchelewa kukamilika kwa uchimbaji wa visima hivyo vipya kulisababishwa na ukosefu wa uzalishaji wa maji kwa baadhi ya maeneo ambayo hayakuwa na maji kabisa. Hata hivyo, ilisababishwa na uchelewaji wa ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine za kusukumia maji kutokana na kutokuwepo kwa visima vilivyokamilika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unaongeza makini katika usimamiaji ikiwemo kuwahimiza wakandarasi kutekeleza majukumu yao kwa umakini ili kuepuka kujitokeza kwa dosari ya kutokukamilika kwa mitadi kwa wakati

### 5.4.4 Uwepo wa Visima Vikavu na visivyozalisha maji

Kulingana na lengo la dhana ya mradi huo ambayo ililenga kuongeza uzalishaji wa maji kutoka asilimia 55 hadi 71 ili kukidhi mahitaji ya sasa ya usambazaji wa maji kwa Unguja na Pemba kwa kuchimba visima vipya. Ukaguzi umefanya mapitio ya ripoti ya majaribio ya pampu kwa visima vilivyochimbwa kwa Unguja na Pemba na kubaini uwepo wa visima vilivyochimbwa visivyo na tija kutokana na kushindwa kuzalisha kiwango cha maji kilichokusudiwa kama inavyobainishwa katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 34: Kiwango cha upatikanaji na uzalishaji wa maji usioridhisha**

| Namba | Eneo | Makadirio ya upatikanaji wa Maji (lita kwa saa) | Matokeo yaliyoripotiwa (lita kwa saa) | Tofauti ya kiwango cha uzalishaji wa maji (lita kwa saa) |
|---|---|---|---|---|
| | | **Unguja** | | |
| 1. | Donge Kipange | 60,000 | Kisima Kikavu na kilibomoka | 60,000 |
| 2. | Kaburi Kikombe | 80,000 | 60,000 | 20,000 |
| 3. | Kiashangwe | 77,000 | 40,000 | 37,000 |
| 4. | Uroa/Bambi BH1 | 66,000 | 35,000 | 31,000 |
| | **Jumla** | **283,000** | **135,000** | **148,000** |
| | | **Pemba** | | |
| 5. | Msuka-Dodea | 40,000 | 15,000 | 25,000 |
| 6. | Chambani Kwapopo | 20,000 | 16,000 | 4,000 |
| 7. | Mkanyageni | 60,000 | 18,000 | 42,000 |
| 8. | Pindua | 40,000 | 15,000 | 25,000 |
| | **Jumla** | **160,000** | **64,000** | **69,000** |

*Chanzo: Ripoti ya Uchimbaji na Ripoti ya Vipimo vya uzalishaji maji na pampu juu ya kusukuma maji*

Kutokana na jadweli hapo juu ilikadiriwa kwa upande wa uchimbaji wa visima vipya vya Unguja vizalishe lita 283,000 kwa saa ambapo imebainika kuzalisha kiwango kidogo cha lita 135,000 kwa saa na kupelekea tofauti ya kiwango cha lita 148,000 kwa saa zilizokua hazikuzalishwa.

Aidha, kwa upande wa uchimbaji wa visima vipya vya Pemba vizalishe lita 160,000 kwa saa ambapo imebainika kuzalisha kiwango kidogo cha lita 64,000 kwa saa na kupelekea tofauti ya kiwango cha lita 69,000 zilizokua hazikuzalishwa.

Kutokana na uzalishwaji mdogo wa maji usiokidhi makusudio ya kiwango kilichohitajika kinaweza kupelekea kushindwa kufikia malengo ya Serikali waliojipangia ya kuongeza uzalishaji wa maji safi na salama kwa asilimia 71, jambo ambalo linaweza kuipelekea Serikali kutumia gharama ya ziada ya uchimbaji wa visima vyengine vipya ili kukidhi kiwango kilichokusudiwa.

Pamoja na uwepo wa dosari ya kutokukidhi kwa kima cha maji kilichohitajika ukaguzi ulihakiki vipimo kwa baadhi ya visima vilivyochimbwa na kubaini uwepo wa ubora wa maji yaliyozalishwa na yanafaa kwa matumizi kama ilivyobainishwa katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 35: Uchambuzi wa upimaji wa pampu uliofanywa kwa visima vya Sampuli**

| Namba | Eneo | Makadirio ya uzalishaji Maji (lita kwa saa) | Matokeo ya Vipimo vya Pampu (lita kwa saa) | Uchambuzi wa Ubora wa Maji |
|---|---|---|---|---|
| **Unguja** | | | | |
| 1. | Mgeni Haji BH1 | 60,000 | 110,000 | Inafaa kwa matumizi |
| 2. | Mgeni Haji BH2 | 60,000 | 110,000 | Inafaa kwa matumizi |
| 3. | Kiashange | 77,000 | 45,600 | Inafaa kwa matumizi |
| 4. | Donge Kipange | 60,000 | 1,900 | Inafaa kwa matumizi |
| **Pemba** | | | | |
| 5. | Ng’ambwa | 60,000 | 64,000 | Inafaa kwa matumizi |
| 6. | Jaani | 40,000 | 23,000 | Inafaa kwa matumizi |
| 7. | Junguni | 40,000 | 6,000 | Inafaa kwa matumizi |
| 8. | Kiungoni | 40,000 | 3,600 | Inafaa kwa matumizi |

*Chanzo: Ripoti ya Vipimo vya Kusukuma maji kwa Visima vya Sampuli*

Kutoka Jadweli hapo juu, lilibainika kuwa kutokana na ukaguzi wa upimaji wa pampu uliofanywa visima vitatu (3) vilikuwa na kina kikubwa cha uzalishaji wa maji zaidi ya uzalishaji uliokadiriwa, hata hivyo uwepo wa visima vingine vitano (5) vilikuwa na kina kidogo cha uzalishaji wa maji chini ya kiwango cha makadirio.

Uwepo wa uzalishaji wa maji kwa baadhi ya visima visivyokidhi kiwango cha makadirio inawezekana ulitokana na uhafifu wa uchunguzi wa miamba na kushindwa kubaini uwezekano wa visima ambavyo vinaweza kuzalisha kima halisi au zaidi cha maji kilichokadiriwa.

Uwepo wa visima vyenye uzalishaji mdogo wa maji vinaweza kupelekea kuathiri kiasi cha maji cha kutosha kwa eneo lililokusudiwa ambalo litasababisha kutofikia malengo ya mradi wa kuongeza uzalishaji wa maji hadi asilimia 71, kwa hivyo mahitaji ya usambazaji wa maji hayawezi kukidhi mahitaji ya wanajamii katika eneo huisika kwa kipindi kirefu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unafanya upembuzi yakinifu kuweza kujua uwezo wa uzalishaji wa maji katika eneo kabla ya kuchimbwa kwa visima, uchunguzi wa miamba kwa maeneo ambayo yatakua na uchache wa upatikanaji wa maji pamoja na kufanya marekebisho kwa baadhi ya maeneo ambayo yalibainika visima vyake kutokukidhi mahitaji yalioyokusudiwa au kukauka.

# SURA YA SITA



# 6.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA UJENZI WA MATANGI YA MAJI

## 6.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi juu ya ujenzi wa Matangi ya maji ya Unguja na Pemba yanayojumuisha mzunguko mzima wa usimamizi wa mradi hadi hatua ya maendeleo ya mradi wakati wa ukaguzi. Taarifa ya mradi ilikuwa kama inavyoonyeshwa katika Jadweli hapa chini.

**Jadweli Nambari 36: Taarifa za Mkataba wa Ujenzi wa Mradi wa Tangi la Maji**

| | |
|---|---|
| Jina la Mradi | Ujenzi wa Matangi ya Maji ya chini na ya Juu katika Visiwa vya Unguja na Pemba chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Ustawi wa Jamii wa Taifa chini ya UVIKO-19 (LOTI 1 na 2) |
| Nambari ya Mkataba: | SMZ/IMF/H03/W/EP-RNCT/2021/2022/09 (LOTI 1 na LOTI 2) |
| Mkandarasi | M/S Simba Developers LTD |
| Mshauri | M/S Nimeta Consult (T) Ltd |
| Muda wa Mradi | Miezi 9 |
| Tarehe ya Kuanza | Machi 21, 2022 |
| Tarehe ya kukamilika ya awali | Januari 1, 2023 |
| Tarehe ya Kukamilisha Iliyobadilishwa | Julai 10, 2023 |
| Upeo wa Mradi | Ujenzi wa Matangi kumi ya Maji yenye uwezo wa kuhifadhi lita 1,000,000 kila moja, Matangi matano Unguja na mengine matano Pemba |

*Chanzo: Mkataba wa Ujenzi wa Matangi ya Maji*

Wakati wa ukaguzi masuala yafuatayo yanayohusiana na Mipango na Usanifu, Ununuzi wa Mkandarasi, na Utekelezaji wa Mkataba yalibainishwa.

## 6.2 Mipango na Usanifu wa Mradi

### *(i) Kukosekana kwa Tathmini ya Mahitaji ya Maji*

Kwa mujibu wa muongozo wa Usanifu wa Maji, Makadirio ya uwezo wa uhifadhi wa tangi ya maji hupaswa kuzingatia mahitaji ya maji kwa nyakati mbalimbali za siku na upatikanaji wa maji kutoka kwenye mpango wa usambazaji maji ili kupatikanwa kwa maji wakati mahitaji yanapokuwa makubwa. Ujazo wa Tangi huhesabiwa kama ni kiwango cha juu cha maji ukitoa kiwango cha chini cha maji, ukitoa kiasi cha mwisho.

Kupitia ombi la ripoti ya utafiti wa uwezekano, ilibainika kwamba, hakuna tathmini iliyofanywa ili kutambua idadi ya mahitaji ya maji na uwezo wa chanzo cha kutosha kabla ya kuongeza uwezo wa shimo ya kuhifadhi maji iliyopendekezwa.

Ilibainika kuwa, ZAWA ilipendekeza ujenzi wa Matangi kumi ya Maji yenye uwezo wa lita 1,000,000 kwa kila moja bila kuwa na msingi wa uwezo wa Tangi uliopendekezwa. Kwa mujibu wa maafisa wa ZAWA, ukubwa wa Matangi hayo ulifanywa kwa kuzingatia uzoefu wao katika utoaji wa huduma za maji kwa jamii.

Mapitio ya Hadidu Rejea (TOR) kwa huduma ya ushauri yalibainisha kuwa, mshauri alipewa kazi ya kufanya uchunguzi wa miamba, kupendekeza aina ya nyenzo, Usanifu na kuandaa hati ya zabuni kwa mradi wa ujenzi wa tangi la maji. Hata hivyo, maeneo, kiasi, aina ya tangi ilitambuliwa na ZAWA bila kuwa na uchambuzi wa mahitaji.

Upangaji usioridhisha wa utekelezaji wa mradi huo uliosababisha kutotekelezwa kwa utafiti wa uwezekano wa ujenzi wa Matangi ya maji. Hii ilihusishwa na vikwazo vya muda kwa ajili ya kuanza kwa mradi.

Ujenzi wa tangi la maji bila kufanya tathmini juu ya mahitaji ya maji na usambazaji husababisha hatari ya kuzidi au kupungua kwa uwezo wa tangi kwa sababu mahitaji ya maji kwa wananchi hayakujulikana.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa inafanya tathmini juu ya mahitaji ya maji na usambazaji ili kukadiria uwezo wa tangi la kuhifadhi maji.

### *(ii) Makadirio yasiyotosheleza ya Makisio ya gharama za vifaa vya ujenzi (BoQs)*

Kulingana na njia ya kawaida ya kipimo cha kazi za Uhandisi, kiasi kitahesabiwa kutoka kwenye michoro isipokuwa kama ilivyoelezwa vinginevyo katika Mkataba, na hakuna posho itakayofanywa kwa ajili ya matumizi yaliyozidi, kupungua au kutotumika.

Wakati wa mapitio ya gharama za ujenzi na michoro iliyotumika katika ujenzi wa Matangi ya maji, yafuatayo yalibainika.

### *(iii) Idadi ya Nondo kwenye mchanganuo haikulingana na Idadi katika Hati za makisio ya gharama za Ujenzi (BoQs)*

Nondo za chuma zilizokadiriwa kutokana na mchanganuo wa nondo zilizopinda, zilionyesha kuwa ubora wa nondo kwa msingi wa tangi la maji, nguzo, mihimili, slab na ukuta ulitoa matokeo ya tone 442.283 na tone 475.62 kwa loti 1 na loti 2.

Kwa upande mwingine kiasi cha nondo za chuma katika BOQs kwa msingi wa tangi la maji, nguzo, mihimili, slab na ukuta ulitoa matokeo ya toni 412.089 na toni 481.97 kwa loti 1 na loti 2. Jadweli hapo chini linaonesha tofauti katika idadi ya nondo katika kiasi cha nondo zilizopinda na iliyowasilishwa katika BOQs.

**Jadweli Nambari 37:Tofauti ya idadi ya nondo kutoka BOQ na idadi halisi ya nondo**

| Tangi | Idadi katika BOQ (Tons) | Idadi halisi (Tons) | Idadi ya kulipwa (kama kwa IPC No. 10) (Tons) |
|---|---|---|---|
| **Loti ya 1** | | | |
| Tumbatu | 95.19 | 101.62 | 94.831 |
| Bumbwini | 95.494 | 103.16 | 95.052 |
| Unguja Ukuu | 95.495 | 102.61 | 95.04 |
| Mgenihaji | 97.52 | 106.11 | 97.082 |
| Bambi Uroa | 28.39 | 28.783 | 28.38 |
| **Jumla** | **412.089** | **442.283** | **410.385** |
| **Loti ya 2** | | | |
| Pujini | 103.22 | 107.731 | 98.68 |
| Shumbamjini | 122.6 | 117.43 | 116 |
| Kiwani | 96.4 | 93.657 | 92.39 |
| Makangale | 122.6 | 128.23 | 119.68 |
| Chanjaani | 37.15 | 28.572 | 24.59 |
| **Jumla** | **481.97** | **475.62** | **451.34** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi juu ya Mchoro na Cheti cha Malipo*

Kutokana na Jadweli hapo juu ya idadi ya nondo za chuma kutoka kwenye mchanganuo wa nondo zilizopinda ilikuwa tofauti na ile iliyowasilishwa katika BoQs. Kwa loti 1 jumla ya idadi katika BoQs ilikuwa chini ya ile katika mchanganuo wa nondo zilizopinda ambazo zilitoa matokeo ya tone ya 30.194 wakati kwa loti 2 jumla ya idadi kutoka BoQs ilikuwa juu kuliko ile katika mchanganuo wa nondo kwa matokeo ya tani 6.35. Kutokana na tofauti iliyobainishwa hapo juu huwenda ilikuwa kinyume na njia ya kawaida ya kipimo ambayo ilihitaji kiasi katika BoQs kutolewa kutoka kwenye michoro bila ya uwepo wa matumizi ya ziada yaliyofanywa kwa matumizi yaliyozidi, kupungua au kutotumika, kwa hivyo kiasi katika BoQs kilihitajika kuwa sawa na katika michoro.

Ukaguzi ulibaini kuwa kiwango cha nondo za chuma katika vyeti vya malipo kilikuwa tani 410.385 na tani 451.34 kwa loti 1 na loti 2 ambapo ni chini ya ile iliyowasilishwa katika BoQs kwa tani ya 1.7 na tani 30.6 kwa loti 1 na loti 2.

Ukaguzi ulifanya mahojiano na wafanyakazi wa mshauri elekezi na kubaini kuwa malipo hayo yalifanywa kwa kuzingatia utekelezaji halisi. Hata hivyo, mchoro ulioandaliwa haukupatikana kwa wakaguzi kuthibitisha kiasi kulingana na utekelezaji uliofanyika. Aidha, wakati wa ziara ya eneo la ujenzi, ilibainika kuwa, nondo za chuma tayari zilikuwa zishafunikwa na saruji kwa hivyo uthibitishaji kwenye eneo la ujenzi haukuwezekana.

Kutokana na tofauti iliyobainika huwenda ilipelekea kujitokeza kwa idadi ya nondo za chuma katika BoQs na idadi halisi ya nondo zilizopindwa ilitokana na kiasi kidogo cha vitu kutoka kwa michoro ya usanifu.

Tofauti ya kiasi katika BoQs inaweza kupelekea kujitokeza kwa tofauti ya utekelezaji wa mradi kwani kiasi kilichokadiriwa hakitaonekana katika uhalisia wake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa idadi ya vifaa katika BoQs inaendana na uhalisia wa utekelezaji wa mradi kwa mujibu wa michoro ili kuepusha kujitokeza kwa tofauti wakati wa utekelezaji wa mradi na kupelekea kujitokeza kwa gharama za ziada za vifaa.

## 6.3 Manunuzi ya Mkandarasi

### 6.3.1 Kutoa mkataba kwa wakandarasi wasioomba zabuni

Kwa mujibu wa Kanuni nambari 138(1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya 2020, tuzo itatolewa ndani ya kipindi cha uhalali wa zabuni kwa mzabuni ambaye zabuni yake imedhamiriwa kuwa zabuni iliyotathminiwa vizuri.

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa katika ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Matangi ya kuhifadhia maji, ZAWA ilichagua njia ya ununuzi yenye masharti maalum "restricted tender" na wakandarasi 23 walichaguliwa kushiriki katika mchakato wa zabuni hiyo.

Kwa mujibu wa ripoti ya tathmini ilibainisha kuwa wakandarasi 15 walialikwa kuchukuwa zabuni kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa matangi ya maji. Hata hivyo, wakati wa ufunguzi wa zabuni wakandarasi wawili tu ambao ni M/S Salem Construction Ltd na M/S Simba Developers LTD waliwasilisha zabuni zao.

Mapitio ya ripoti ya ndani kuhusu maendeleo ya manunuzi yalibaini kuwa baada ya wazabuni wawili tu kuitikia mwaliko ZAWA iliamua kufuta mchakato wa ununuzi na kutoa mwaliko wa pili. Sababu za kufutwa ni malalamiko kutoka kwa wazabuni wengine kwamba hawakupata hati ya zabuni ambayo ilitumwa kwao kupitia barua pepe. Katika mwaliko wa pili hati za zabuni zilipelekwa kwa wakandarasi watano ambao ni M/S Estim Ltd, M/S Advent Ltd, M/S CRJE East Africa Ltd, M/S Shanxi Engineering Ltd, na M/S MAC Construction Company Ltd. Hata hivyo, kampuni ya M/S Simba Developers Ltd na M/S Salem Ltd hazikualikwa kuwasilisha zabuni zao kwa kuwa tayari mchakato wa ununuzi wa kwanza ulikuwa umefutwa.

Wakati wa tathmini ya zabuni zilizowasilishwa, kamati ya tathmini ilipendekeza M/S CRJE East Africa Ltd apewe Loti 1 na M/S Advent Company Ltd apewe loti 2 ya mradi huo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa mapitio ya mkataba wa ujenzi wa matangi ya kuhifadhia maji ukaguzi ulibaini kampuni ya M/S Simba Developer Ltd ilipewa mkataba wa utekelezaji wa ujenzi wa matangi ya kuhifadhia maji ambapo kampuni hiyo haikushiriki katika mchakato wa pili wa utoaji wa zabuni.

Mahojiano na maafisa wa ZAWA yalibainisha kuwa hakukuwa na sababu za msingi zilizosababisha ZAWA kumchagua mkandarasi kutoka kwenye mchakato wa ununuzi uliofutwa jambo ambalo huwenda likasababisha malalamiko kwa wakandarasi walioomba zabuni kwa mchakato wa mara ya pili.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya kazi za ujenzi unafuata taratibu za manunuzi zilizoainishwa katika kusimamia Kanuni za Ununuzi ili kuhakikisha uteuzi wa haki wa wazabuni unafanyika.

### 6.3.2 Taarifa ya nia ya tuzo haikutolewa kwa Wazabuni

Kwa mujibu wa kanuni nambari 137(2), baada ya kupokea mapendekezo ya uamuzi wa tuzo kutoka Bodi ya Zabuni, Afisa Masuuli atajiridhisha kuwa taratibu sahihi zimefuatwa na ndani ya kufanya kazi siku tatu, atatoa taarifa ya nia ya kutoa mkataba kwa wazabuni wote walioshiriki katika zabuni husika kuwapa siku kumi ndani ya kuwasilisha malalamiko ikiwa yapo.

Mapitio ya kumbukumbu za ununuzi yalibaini kuwa, hakukuwa na idhini ya bodi ya zabuni juu ya mapendekezo kutoka kwa kamati iliyotathminiwa ambayo ilipendekeza M/S CRJE East Africa LTD na M/S Advent LTD kupewa Loti 1 na Loti 2. Vile vile, hakukuwa na kumbukumbu zilizoonyesha kuwa wazabuni walijuulishwa juu ya nia ya kutoa mkataba kwa M/S Developers LTD ambae amepewa mkataba kinyume na utaratibu.

Kutokana na dosari iliyobainika hapo juu imepelekea kujitokeza kwa kutozingatiwa kwa mapendekezo ya kamati ya tathmini ambapo uongozi wa ZAWA ulitoa tuzo ya mkataba kwa wakandarasi ambao hawakuhusika katika mchakato wa ununuzi wa zabuni.

Kushindwa kuwajulisha wazabuni juu ya nia ya kutoa zabuni kunaweza kupelekea kujitokeza kwa hatari ya kukosa ushindani wa wazabuni katika miradi mengineyo kutokana na kukosekana kwa morali kwa baadhi ya wazabuni ambao hawakujuulishwa juu ya dhana ya kukoseshwa kwa zabuni hiyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa mapendekezo ya kamati ya tathmini yanapitiwa na bodi ya zabuni na wazabuni wanaarifiwa juu ya nia ya kutoa mkataba.

### 6.3.3 Kipindi kidogo cha zabuni

Kwa mujibu wa kifungu nambari 50 cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016, kipindi cha zabuni kitatosha kuruhusu wazabuni kuandaa na kuwasilisha zabuni zao na hawatapunguzwa kwa lengo la kupunguza ushindani.

Pia, Kanuni nambari 105 (1) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma zinaeleza kuwa, muda unaoruhusiwa kwa ajili ya maandalizi ya zabuni utategemea ukubwa na ugumu wa manunuzi yaliyokusudiwa na kwa hali yoyote ile, hautakuwa mfupi kuliko muda uliowekwa katika Jadweli la Nne ya Kanuni hizi. Jadweli la nne ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ilieleza kuwa, kwa Zabuni ya Ndani ya Wazi, kipindi cha zabuni kilichopendekezwa kitakuwa siku 14 hadi 21.

Mapitio ya kumbukumbu za ununuzi yalibaini kuwa mwaliko wa wakandarasi, ziara ya eneo la ujenzi na mkutano wa kabla ya zabuni ulipangwa tarehe 5 Februari, 2023 na wazabuni walitakiwa kuwasilisha zabuni zao tarehe 7 Februari, 2023 ambayo ilikuwa siku mbili tangu siku ya ziara.

Aidha, mapitio ya barua pepe za mwaliko zilizotumwa kwa wazabuni zilibainisha kuwa, tarehe 9 hadi 11 Februari, 2022 ZAWA ilituma barua pepe ya mwaliko wa pili kwa wazabuni wenye nyaraka za zabuni zilizoambatishwa, baada ya kufutwa kwa mchakato wa kwanza kutokana na malalamiko ya wazabuni kwamba hawakupata mwaliko. Katika mwaliko huo, wazabuni walitakiwa kuwasilisha maombi yao tarehe 15 Februari, 2022 ambayo ilikuwa siku 4 tangu siku ya mwaliko. Tarehe ya kuwasilisha iliongezwa hadi 18 Februari, 2022 na ziara ya eneo la ujenzi na mkutano wa kabla ya zabuni ulipangwa mnamo 14 Februari, 2022 kwa Unguja na tarehe 15 Februari, 2022 kwa Pemba.

Ukaguzi ulibaini kuwa muda uliotengwa kwa wazabuni kuandaa na kuwasilisha zabuni zao umebainisha kuwa, kuanzia siku ya kutembelea eneo la utekelezaji wa mradi na mkutano wa zabuni kabla ya tarehe 14 na 15 Februari, 2022 mkandarasi alipewa siku 3 kuandaa na kuwasilisha nyaraka zao za zabuni kinyume na kanuni za manunuzi ya umma ambazo zinahitaji muda wa zabuni kuwa angalau siku 14 kwa Zabuni za ndani zilizowekewa vikwazo.

Kwa upande mwingine, mapitio ya barua pepe za mwaliko zilibainisha malalamiko ya mkandarasi juu ya kipindi cha zabuni na kuomba mteja kuongeza kipindi cha zabuni. Hata hivyo, hakukuwa na majibu ya wazi kwa ZAWA kuhusu kuongezwa kwa kipindi cha zabuni.

Bodi ya zabuni iliidhinisha hati ya zabuni bila kuangalia ikiwa muda wa kutosha ulitengwa kwa zabuni.

Kutokana na kubainika kwa dosari hiyo athari zifuatazo ziliweza kujitokeza: -

- ***Si wakandarasi wote walioalikwa waliwasilisha maombi yao***

Uchambuzi wa zabuni zilizowasilishwa na wakandarasi hao umebainisha kuwa katika mualiko wa kwanza wa makandarasi wawili (2) kati ya kumi na tano (15) walioalikwa sawa na asilimia 13 waliwasilisha zabuni zao. Katika mwaliko wa pili wakandarasi wanne (4) kati ya watano (5) walioalikwa waliwasilisha zabuni zao. Wakaguzi walikuwa na maoni kwamba kipindi cha zabuni ndogo hupunguza uwezekano wa wakandarasi kukamilisha na kuwasilisha zabuni zao.

- ***Hatari ya kupunguza ushindani katika mchakato wa zabuni***

Kutenga muda mdogo wa zabuni, hupunguza uwezekano wa wakandarasi kukamilisha na kuwasilisha zabuni zao kwa wakati. Kama matokeo idadi ya wazabuni walishindwa kuwasilisha zabuni yao ambao kwa upande wake kupunguza ushindani na mteja alikuwa na nafasi ndogo ya kuchagua mkandarasi mwenye uwezo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kwamba, wanatoa kipindi cha kutosha cha zabuni kabla ya idhini na usambazaji wa hati za zabuni.

## 6.4 Usimamizi wa Mkataba

### 6.4.1 Kumalizika kwa Dhamana ya Utendaji

Kwa mujibu wa Kifungu nambari 55.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba, Dhamana ya Utendaji itatolewa kwa Mwajiri kabla ya tarehe iliyoainishwa katika Barua ya Kukubali na itatolewa kwa kiasi na fomu na benki au uhakika unaokubalika kwa Mwajiri, na kuainishwa katika aina na uwiano wa sarafu ambazo Bei ya Mkataba inalipwa. Dhamana ya Utendaji utakuwa halali hadi tarehe 28 siku kutoka tarehe ya kutolewa kwa Cheti cha Kukamilisha katika kesi ya Dhamana ya Benki, na hadi mwaka mmoja kutoka tarehe ya kutolewa kwa Cheti cha Kukamilisha katika kesi ya Dhamana ya Utendaji.

Mapitio ya jalada la mkataba yalibainisha kuwa, mkandarasi aliwasilisha Dhamana ya Benki yenye kumbukumbu Namba. 0010GTZ22000007 ya tarehe 27 Aprili, 2022 ambayo isiyo na masharti na kumalizika tarehe 30 Januari, 2022. Mapitio zaidi ya mkataba yalibainisha kuwa tarehe ya kukamilika kwa mkataba wa awali ilikuwa tarehe 31 Disemba, 2022 ambayo ilifanyiwa mabadiliko na kuongezwa hadi tarehe 10 Julai 2023. Ukaguzi umebaini hati ya dhamana ilimaliza muda wa matumizi bila ya kuongezwa muda ili kufidia wakati ulioongezwa.

Kutokuongezwa muda wa matumizi wa hati ya dhamana kunaweza kupelekea kuisababishia hasara Serikali inayotokana na kushindwa kutekelezwa kwa miradi ya maendeleo kwa mkandarasi pindipo akishindwa kutekeleza masharti ya mkataba au kufilisika wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa dhamana ya utendaji kwa miradi ya ujenzi inaongezwa muda kulingana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

## 6.5 Dosari katika Usimamizi wa Muda

### 6.5.1 Kuchelewa kukamilika kwa mradi

Mapitio ya mkataba wa Mradi yalibaini kuwa, mkataba wa ujenzi wa matangi ya maji ulitakiwa kukamilika tarehe 31 Disemba, 2022 ambayo ilikuwa miezi tisa tangu tarehe ya kuanza. Mapitio ya barua na ref. no. ZAWA/U.5/5/VOL 1/29 ya tarehe 10 Januari, 2023 ilibainisha kuwa, ZAWA ilitoa muda wa miezi mitatu (3) kwa mkandarasi kukamilisha kazi hiyo hadi tarehe 10 Machi 2023.

Hata hivyo, mkandarasi huyo hakufanikiwa kukamilisha mradi huo ndani ya muda wa miezi mitatu. Kupitia barua yenye kumbukumbu namba ZAWA/U.5/5/VOL 1/40 ya tarehe 11 Aprili, 2023, ZAWA ilitoa nyongeza ya pili ya muda hadi Julai 10, 2023. Uchambuzi wa Mkaguzi juu ya upanuzi wa muda uliotolewa kwa mkandarasi ulibainisha kuwa, mradi ulicheleweshwa kukamilika kwa siku 191 (tarehe 31 Disemba, 2022 hadi 10 Julai, 2023).

Mapitio ya Barua yenye kumbukumbu namba. HQ / ZAWA/2022/CS08/021 ya tarehe 20 Disemba, 2022 juu ya mapendekezo ya mshauri juu ya upanuzi wa muda alibainisha kuwa, kuchelewa kukamilika kwa mradi kulisababishwa na mambo yafuatayo: -

- Kuchelewa kwa mkandarasi kutambua eneo la kupata vifaa vya ujenzi kama mchanga na kokoto ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya utengenezaji wa zege wenye kiwango cha daraja la C40, hata hivyo ilichukuwa muda wa siku 30 kupatikana kwa mchanganyiko wa zege yenye kiwango cha daraja la C30.
- Kuchelewa upatikanaji wa muunganiko wa maji na umeme katika maeneo ya utekelezaji wa mradi ambapo ilibainika kuwa katika maeneo hayo huduma ya maji iliweza kuunganishwa katika kipindi cha wiki ya kwanza ya mwezi wa Juni 2022 kwa kuunganisha matangi mawili tu ya maji.
- Upungufu wa vifaa vya ujenzi kwenye eneo la ujenzi ambapo ilipelekea uwepo wa ucheleweshwaji wa utekelezaji wa kazi za mradi.
- Kutokuwepo kwa vifaa muhimu vinavyorahisisha utekelezaji wa mradi ikiwemo krini (crane) ya mnara ambapo mkandarasi alitegemea zaidi matumizi ya krini ya kukodi.

### 6.5.2 Ongezeko la gharama ya mradi shilingi 41,157,500 inayotokana na kodi za ujenzi wa vituo vya mashine za maji

Mapitio ya Hati ya Malipo Nambari 10 yalibaini kuwa, kutokana na kushindwa kwa mkandarasi kukamilisha mradi ndani ya kipindi cha mkataba kilichopendekezwa cha miezi 9 imepelekea kuongezwa kwa siku 191 ambapo ilisababisha kuongezeka kwa gharama ya shilingi 41,157,500 ambazo zililipwa kwa mkandarasi kama kitangulizi cha malipo. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 38: Ongezeko la gharama zilizolipwa kwa wakandarasi**

| Nambari ya Kipengele | Maelezo | Idadi (mwezi) | Ongezeko la muda (mwezi) | Tofauti ya ongezeko la muda<br>A | Kiwango (Tsh)<br>B | Ongezeko la gharama (Tsh)<br>AxB |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **LOTI ya 1: Ujenzi wa matangi ya maji Unguja** | | | | | | |
| 9.1 | Kukodi nyumba aina ya I kwa Mhandisi | 9 | 14 | 5 | 1,500,000 | 7,500,000 |
| 9.2 | Kukodi nyumba aina ya III kwa Mhandisi | 9 | 12 | 3 | 1,500,000 | 4,500,000 |
| 9.3 | Kudumisha nyumba aina ya I kwa Mhandisi | 9 | 14 | 5 | 150,000 | 750,000 |
| 9.4 | Kudumisha nyumba aina ya III kwa Mhandisi | 9 | 12 | 3 | 150,000 | 450,000 |
| 10.1 | Afisi ya kupumzika kwa Mhandisi | 9 | 14 | 5 | 1,000,000 | 5,000,000 |
| 10.2 | Kudumisha/ Huduma kwa Afisi ya Mhandisi | 9 | 14 | 5 | 700,000 | 3,500,000 |
| 11.3 | Kuendesha na kudumisha gari kwa ajili ya usimamizi | 9 | 14 | 5 | 200,000 | 1,000,000 |
| **LOTI ya 2: Ujenzi wa Matangi ya Maji Pemba** | | | | | | |
| 9.1 | Kukodi nyumba aina ya I kwa ajili ya Mhandisi | 9 | 13 | 4 | 1,725,000 | 6,900,000 |
| 9.2 | Kukodi nyumba aina ya III kwa ajili ya Mhandisi. | 9 | 12 | 3 | 1,725,000 | 5,175,000 |
| 9.3 | Kudumisha nyumba aina ya I ya Mhandisi. | 9 | 13 | 4 | 172,500 | 690,000 |
| 9.4 | Kudumisha nyumba aina ya III ya Mhandisi. | 9 | 12 | 3 | 172,500 | 517,500 |

| Nambari ya Kipengele | Maelezo | Idadi (mwezi) | Ongezeko la muda (mwezi) | Tofauti ya ongezeko la muda A | Kiwango (Tsh) B | Ongezeko la gharama (Tsh) AxB |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 10.1 | Afisi ya kupumzika kwa Mhandisi | 9 | 12 | 3 | 1,150,000 | 3,450,000 |
| 10.2 | Kudumisha/ Huduma kwa Afisi ya Mhandisi | 9 | 10 | 1 | 805,000 | 805,000 |
| 11.3 | Kuendesha na kudumisha gari kwa ajili ya usimamizi | 9 | 13 | 4 | 230,000 | 920,000 |
| | **Jumla ya Kiasi kilicholipwa kwa Mkandarasi kutokana na ongezeko la Muda** | | | | | **41,157,500** |

*Chanzo: Cheti cha Malipo ya Muda Namba. 10*

Jadweli hapo juu linaonesha kuwa jumla ya shilingi 41,157,500 zimelipwa kwa Mkandarasi kwa hati ya malipo nambari 10 kutokana na uwepo wa ongezeko la muda katika utekelezaji wa mradi.

### 6.5.3 Ongezeko la gharama la shilingi 161,547,783.33 kwa ajili ya kuongeza muda wa usimamizi kwa mshauri elekezi

Kifungu nambari 6.2 (b) cha GCC cha mkataba wa huduma ya ushauri kwa ajili ya utoaji wa usanifu na usimamizi wa ujenzi wa matangi ya maji ya ardhini na ya juu Unguja na Pemba kinaeleza kuwa kiasi cha mkataba kilikuwa shilingi 890,000,000 pamoja na VAT.

Vile vile, kifungu nambari 2.3 cha GCC kama ilivyoainishwa katika SCC ya mkataba wa huduma ya ushauri kwa ajili ya utoaji wa muundo na usimamizi wa ujenzi wa Matangi ya maji ya ardhini na ya juu Unguja na Pemba kilihitaji kipindi cha mkataba kuwa miezi 23, ambapo miezi 3 ya Usanifu na nyaraka za zabuni, Miezi 8 kwa usimamizi wa kazi na miezi 12 kwa Kipindi cha Dhima ya Kasoro.

Hata hivyo, kwa kuzingatia mapitio ya Ripoti ya Maendeleo ya Kila Mwezi Nambari 13 ya Mei 2023 na hati za malipo kwa huduma ya ushauri ilibainika kuwa kwa awamu ya Usanifu na Usimamizi malipo yaliyofanywa yalizidi kiasi cha mkataba hadi shilingi 1,051,339,346.17 sawa na ongezeko la shilingi 161,547,783.33 kama gharama ya ziada iliyotokana na nyongeza ya muda wa ziada wa miezi sita kwa mkandarasi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa katika hatua zote za utekelezaji wa mradi unaimarisha usimamizi wa kandarasi ili kuepusha kujitokeza kwa kwa malipo yatokanayo na fidia ya ongezeko la muda jambo ambalo linaweza kusababisha kuitia hasara Serikali.

## 6.6 Dosari katika usimamizi wa gharama za Mradi

### 6.6.1 Mabadiliko ya viwango vya zege katika BoQs ambayo yameengeza bei ya mkataba kwa shilingi 1,474,240,021.75 pamoja na VAT

Kwa mujibu wa kifungu nambari 39.2 Makisio ya Gharama za vifaa vya ujenzi yatatumika kuhesabu gharama za Mkataba na Mkandarasi atalipwa kwa kiasi cha kazi aliyofanya kwa kiwango cha Bili ya Makisio ya Gharama za Vifaa kwa kila kitu.

Mapitio ya Hati ya makisio ya gharama za ujenzi, kwa ajili ya ujenzi wa matangi ya maji ilibainisha kuwa, mkandarasi aliahidi kujenga daraja la zege la C40 kwa kiwango cha shilingi 450,000 kwa mita za ujazo kwa Matangi manne ya Bubwini, Unguja Ukuu, Mgenihaji, Bambi Uroa kwa upande wa Unguja, na shilingi 460,000 kwa mita za ujazo kwa tangi moja la Tumbatu kwa upande wa Unguja, na Shilingi 540,000 kwa kila mita za ujazo kwa Matangi manne ya Pujini, Makangale, Chanjaani, na Shumbamjini kwa upande wa Pemba pamoja na shilingi 550,000 kwa kila mita za ujazo kwa tangi moja la Kiwani kwa upande wa Pemba.

Mapitio ya taarifa za kikao kwa ajili ya Mkutano wa Kiufundi namba 3 uliofanywa tarehe 20 Febuari, 2023 umebaini kuwa ZAWA, Mshauri na Mkandarasi walikubaliana kuongeza kiwango kilichonukuliwa na mkandarasi kwa kutupatia daraja halisi la C40 kutoka shilingi 540,000 hadi shilingi 734,369.01 kwa Matangi yote matano kwa upande wa Pemba, kutoka shilingi 450,000 hadi shilingi 714,460.00 kwa matangi manne (4) kwa upande wa Unguja, na kutoka shilingi 460,000 hadi shilingi 853,979.36 kwa tangi moja la kisiwa cha Tumbatu ambapo nyongeza ya mabadiliko hayo ilisainiwa tarehe 19 Aprili, 2023.

Kwa mujibu wa nyongeza ya mkataba iliyosainiwa ilieleza ya kwamba sababu iliyotolewa ya kubadilisha viwango vya zege ilitokana na kuagiza mchanga kutoka Tanzania Bara kwa ajili ya ujenzi wa daraja la zege la C40 jambo ambalo lilipelekea kuongezeka kwa gharama za mradi. Ongezeko la gharama hizo ni kinyume na masharti ya mkataba kwani mkandarasi hakustahiki kuongeza daraja lenye kiwango cha C40 kutokana na hati ya zabuni ambayo ilisambazwa kwa mkandarasi ilibainisha kwamba zege inapaswa kujengwa katika kiwango halisi cha daraja la C40.

Kutokana na dosari iliyobainishwa hapo juu ukaguzi umebaini dosari hiyo imesababishwa na usimamizi duni wa mkataba ambao ulisababisha kukubalika kwa pendekezo la mkandarasi juu ya marekebisho ya bei ambayo ilikuwa kinyume na uhalisia wa mkataba jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama za shilingi 1,414,346,394.65 pamoja na VAT ambazo zililipwa kwa mkandarasi kinyume na masharti ya jumla ya mkataba. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 39: Kuongezeka kwa bei ya Mkataba Ilitokana na Kuongeza Kiwango cha Mkandarasi kwa Daraja la Zege C40**

| Loti | Eneo la Ujenzi | Ongezeko (Tsh) kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha zege katika BoQs | Kiasi cha fedha kilicholipwa kwa Mkandarasi (Tsh) |
|---|---|---|---|
| Loti ya 1 | Tumbatu | 228,315,849.06 | 221,181,043.42 |
| | Bumbwini | 158,033,362 | 152,866,210 |
| | Unguja Ukuu | 151,189,137 | 146,814,969 |
| | Mgeni Haji | 151,421,862 | 146,751,393 |
| | Bambi Uroa | 72,953,936 | 71,849,693 |
| **Jumla Ndogo (A)** | | **761,914,146** | **739,463,309** |
| Loti ya 2 | Pujini | 115,729,252 | 107,848,388 |
| | Makangale | 132,674,343 | 124,442,382 |
| | Shumbamjini | 130,730,652 | 122,197,073 |
| | Chanjani | 47,536,829 | 46,909,989 |
| | Kiwani | 93,362,623 | 89,005,290 |
| **Jumla Ndogo (B)** | | **520,033,699** | **490,403,122** |
| **Jumla bila ya VAT (A+B)** | | **1,281,947,845** | **1,229,866,431** |
| **Kodi ya VAT (15%)** | | **192,292,176.75** | **184,479,964.65** |
| **Jumla Kuu (Pamoja na VAT)** | | **1,474,240,021.75** | **1,414,346,395.65** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi wa IPC no. 10*

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa hakuna mabadiliko katika viwango vilivyowasilishwa na wakandarasi au wauzaji baada ya kusaini mkataba kulingana na masharti ya mkataba.

### 6.6.2 Ongezeko la malipo ya awali kutoka asilimia 15 hadi asilimia 30 baada ya uteuzi wa Mkandarasi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 26.0 cha Nyaraka za zabuni ambacho kilieleza kuwa malipo ya awali ya zabuni yatakuwa asilimia 15 ya bei ya mkataba.

Mapitio ya kumbukumbu za vikao yalieleza kuwa, mkandarasi aliomba asilimia ya malipo ya awali kuongezwa kutoka asilimia 15 hadi asilimia 40 jambo ambalo timu ya majadiliano ilikubali kuongeza hadi asilimia 30.

Licha ya ukweli kwamba malipo ya awali yalilipwa kwa mkandarasi baada ya kuwasilisha dhamana ya malipo ya awali, kuongeza kiasi cha malipo ya awali baada ya uteuzi wa mkandarasi kutoa zabuni ilileta dalili ya nia ya kupunguza ushindani katika mchakato wa zabuni.

Ikiwa kiasi cha malipo ya awali kilibainishwa mapema katika hati ya zabuni kama asilimia 30 badala ya asilimia 15, wazabuni zaidi wangeshajihika zaidi na zabuni kwa jambo ambalo lingesababisha kuwepo kwa ushindani mkubwa ambao kwa upande wake ungetoa fursa ya kuchagua mkandarasi mwenye sifa za ziada.

Kubadilisha malipo ya awali wakati wa mazungumzo kilisababishwa na ukosefu wa tathmini ya kutambua ikiwa asilimia 15 iliyoainishwa katika hati ya zabuni ilikuwa kiasi cha kutosha ikilinganishwa na ugumu wa kazi ya utekelezaji wa mradi kwa kuzingatia eneo la mradi, upeo wa kazi na muda unaohitajika kukamilisha mradi huo.

Ukaguzi ulibaini kuwa hali hiyo ilisababisha kukosekana kwa ushindani kwa wazabuni kuwasilisha zabuni zao kama ilivyobainishwa katika mwaliko wa kwanza ambapo jumla ya wazabuni wawili waliwasilisha zabuni zao ambao ni kampuni ya M/s Salem Construction Ltd na M/S Simba Developers Ltd kati ya wakandarasi 15 walioalikwa waliwasilisha zabuni zao.

Katika mwaliko wa pili wakandarasi wanne kati ya wakandarasi watano waliwasilisha zabuni zao. Wakaguzi walikuwa na maoni kwamba, idadi ya wazabuni ingeliweza kuongezeka pindipo hati ya zabuni ingelibainisha mapema ya kwamba kiasi cha malipo ya awali kitakuwa asilimia 30 badala ya asilimia 15 iliyoainishwa katika hati ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa unakuwa makini katika kubainisha asilimia ya awali ya malipo ili kuweza kuvutia waombaji na hatimae kupata mkandarasi mwenye sifa za ziada ambae atatekeleza miradi ya maendeleo kwa ufanisi na kwa vigezo kubalifu.

### 6.6.3 Makadirio hafifu ya kiasi halisi cha zege daraja la C40

Ukaguzi wa vyeti vya malipo Nambari 10 ulibaini kuwa kiwango cha daraja halisi C40 ambacho kiliidhinishwa kwa malipo kilikuwa 561.73m$^3$, 558.63m$^3$, 555.15m$^3$, 271.12m$^3$ na 627.57m$^3$ kwa Tumbatu, Bumbwini, Unguja Ukuu, Bambi Uroa na ShumbaMjini.

Aidha, dondoo ya Mkaguzi wa zege kutoka kwenye michoro ya Tangi zimebaini kiwango cha daraja la C40 kilikuwa 535.78m$^3$, 535.96m$^3$, 547.68m$^3$, 248.35m$^3$ na 619.23m$^3$ kwa Tumbatu, Bumbwini, Unguja Ukuu, Bambi Uroa, na ShumbaMjini. Jadweli hapo chini linaonesha tofauti ya ujazo nilioubainisha hapo juu kutokana na michoro na kutoka kwenye vyeti vya malipo.

**Jadweli Nambari 40: Ujazo wa zege uliyokadiriwa kutokana na michoro na kiasi kilichoidhinishwa kwa malipo**

| Tangi | Makadirio yaliyofanywa na wakaguzi kutokana na michoro ($m^3$) | Malipo kwa mujibu wa (IPC No. 10) ($m^3$) | Tofauti ($m^3$) | Kiasi (Tsh) |
|---|---|---|---|---|
| Tumbatu | 535.78 | 561.73 | 25.95 | 22,160,755 |
| Bumbwini | 535.96 | 558.63 | 22.67 | 16,196,808 |
| Unguja Ukuu | 547.68 | 555.15 | 7.47 | 5,337,016 |
| Bambi Uroa | 248.35 | 271.12 | 22.77 | 16,268,254 |
| Shumbamjini | 619.23 | 627.57 | 8.34 | 6,124,638 |
| **Jumla** | | | **87.2** | **66,087,471** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi juu ya michoro na vyeti vya malipo*

Kutoka Jadweli hapo juu limebainisha ya kwamba kiwango cha saruji daraja la C40 iliyoidhinishwa kwa malipo katika ujenzi wa Tumbatu, Bumbwini, Unguja Ukuu, Bambi Uroa, na ShumbaMjini tangi la maji lilizidi kiasi kilichokadiriwa kutokana na michoro ya usanifu kwa ujazo wa 87.2$m^3$ sawa na shilingi 66,087,471.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa Mshauri anafanya kipimo cha kazi zilizotekelezwa katika ujenzi wa Matangi ya maji kabla ya idhini ya malipo ya mwisho kwa mkandarasi, na ziada yoyote inapaswa kukatwa kutoka kwa malipo ya mwisho.

## 6.7 Dosari katika kukamilika kwa mradi pamoja na ufungaji

### 6.7.1 Kutowasilishwa kwa michoro kwa matangi ya maji yaliyojengwa shilingi 393,728,131.9 pamoja na VAT

Kwa mujibu wa kifungu nambari 27 cha Masharti Maalum ya Mkataba, mkandarasi atawasilisha michoro iliyochorwa kwa tarehe ya kukamilika kwa vitendo. Pia, meneja wa mradi anaweza kuzuia kiasi cha asilimia 3 ya bei ya mkataba ikiwa wakandarasi hawakuwasilisha michoro iliyobuniwa.

Mapitio ya hati ya mkataba yalibainisha kuwa tarehe ya kukamilika kwa ujenzi wa matangi ilikuwa 10 Julai, 2023 baada ya muda wa siku 191. Hata hivyo, hadi tarehe ya ukaguzi huu (28 Julai, 2023) michoro iliyochorwa haikuwasilishwa. Kulingana na masharti ya mkataba meneja wa mradi alikuwa na wajibu wa kuzuia kiasi cha asilimia tatu ya bei ya mkataba ambayo ni sawa na shilingi 393,728,131.9 pamoja na VAT. Hata hivyo, ukaguzi umebaini meneja wa mradi ameshindwa kuzuwia kiasi cha fedha nilichokibainisha hadi ukaguzi unakamilika.

Kutokana na kushindwa kuwasilishwa kwa michoro wakati utekelezaji wa kazi ukiendelea kunaweza kukapelekea kukamilika kwa ujenzi uliokusudiwa pasi na uwepo wa michoro inayohitajika jambo ambalo linaweza kupelekea ukiukwaji wa taratibu za kisheria.

Kutowasilisha michoro iliyochorwa ilionyesha kuwa ZAWA haikuwa na kumbukumbu ya muundo wa tangi la maji lililojengwa kulingana na utekelezaji wa matakwa ya mradi, hivyo huwenda kukajitokeza changamoto kwa siku zijazo kuweza kufanya maboresho ya aina ya tangi jengine kwa sababu ya kukosekana kwa kumbukumbu za awali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa michoro iliyochorwa inawasilishwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya kumbukumbu za baadae. Vile vile, uongozi unapaswa kufanya zuio la shilingi 393,728,131.9 pamoja na VAT wakati wa malipo ya mwisho kulingana na masharti ya mkataba.

# SURA YA SABA



# 7.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA KAZI YA UCHIMBAJI NA UFUKIAJI MISINGI

## 7.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi juu ya uchimbaji na kazi za ufukiaji wa bomba la aina ya HDPE lenye unene wa nchi 6 na kipenyo cha nchi 10 likiwa na urefu wa kilomita za mraba 57.812.

Kazi hiyo ilitekelezwa kupitia njia ya manunuzi ya kawaida ambapo Mamlaka ya Maji Zanzibar iliandaa michoro na makisio ya gharama ambapo mkandarasi M/S Masonry Building Contractors Ltd alitekeleza kazi hiyo kama inavyobainishwa hapo chini: -

**Jadweli Nambari 41: Taarifa ya mkataba kwa ajili ya uchimbaji na ufukiaji wa msingi kwa ajili ya bomba la usambazaji wa maji**

| Kipengele | Taarifa katika Mkataba |
|---|---|
| Mkataba namba | SMZ/IMF/104/W/RNCT/2021/2022/11 |
| Jina la muuzaji | M/S Masonry Building Contractors Ltd |
| Tarehe ya Kusaini | Juni 27, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza Inahitajika | 04 Julai 2022 |
| Tarehe ya Kuanza ya Ufanisi | 04 Julai 2022 |
| Muda wa Mkataba | Miezi 2 |
| Tarehe ya kukamilika kwa mradi | 03 Septemba 2022 |
| Tarehe ya Kukamilisha iliyorekebishwa | Hakuna |
| Mkataba wa awali wa jumla na VAT | shilingi 565,112,300 |
| Mkataba wa Urekebishaji wa Jumla na VAT | Hakuna |
| Maendeleo ya Kazi (%) hadi Julai, 2023 | |
| Malipo ya Maendeleo (%) hadi Julai 2023 wakati Ukaguzi ulifanyika | 65% ya mkataba wa mkataba |
| Kuchelewa kukamilika kwa kazi hadi Julai 2023 | Miezi 11 |
| Dhamana ya malipo ya awali | Hakukuwa na malipo ya awali |
| Riba ya malipo yaliyochelewa | Hakuna |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati ya Mkataba na hati ya Malipo uliofanywa na Wakaguzi,2023*

Wakati wa ukaguzi masuala yafuatayo yanayohusiana na uchimbaji na ufukiaji wa bomba za maji yalizingatiwa kama ifuatavyo: -

## 7.2 Mipango duni ya kazi za uchimbaji na ufukiaji wa misingi

Sehemu hii inatoa ufafanuzi juu ya mipango ya kuchimba na ujazaji wa misingi ya usambazaji wa mabomba ya maji safi na salama.

Sehemu hiyo inashughulikia upangaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi, Mipango ya usimamizi na mpangilio wa kudhibiti ubora na kufanya tathmini ya Mazingira na athari za miradi. Ukaguzi ulifanya mapitio ya kumbukumbu za miradi na kubaini uwepo wa dosari zifuatazo: -

### 7.2.1 Upangaji duni wa makadirio ya gharama za Miradi

Mpango wa ununuzi ulitenga jumla ya shilingi 1,020,800,000 kutekeleza shughuli za uchimbaji na ufukiaji wa mabomba ya maji. Mapitio ya ripoti ya tathmini ya ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya uchimbaji na kazi ya ufukiaji wa mabomba Ukaguzi ulibaini kuwa, ZAWA ilimteua mkandarasi kutoa zabuni kwa Kazi za ufukiaji kwa lot 3. Loti hizi ziligawanyika katika loti 4 na zilikuwa ziko katika maeneo yafuatayo Lot 1 ilikuwa kwa Chakechake Pemba, Lot 2 ilikuwa kwa Mkoani Pemba, Lot 3 ilikuwa ya Micheweni Pemba na Lot 4 ilikuwa ya Wete Pemba. Ripoti ya tathmini ilitolewa pamoja na mapendekezo yake kwa loti zote 4

Aidha, ukaguzi umebaini mkataba wa uchimbaji na ufukiaji wa misingi ya mabomba ya maji ya lot 1 ilirekebishwa na kusainiwa kwa lot 3 kwa mujibu wa mahojiano na mratibu wa mradi, jambo ambalo limepelekea kusainiwa kwa mkataba wa lot 1 ambao ulibainika kuwa na upungufu wa fedha za kufadhili miradi iliyojumuisha loti zote.

Ukaguzi ulipitia hati ya dhamana iliyowasilishwa pamoja na ripoti ya kamati ya tathmini na kubaini jumla ya gharama iliyopangwa kwa ajili ya uchimbaji na ufukiaji wa misingi ilikuwa shilingi 1,021,408,000 kwa kilomita 319 hii ni sawa na shilingi 3,201.91 kwa kila mita kwa kazi za uchimbaji na ufukiaji wa misingi kima ambacho kilikua chini ya gharama kwa kila mita moja kwa mujibu wa kiwango cha mkataba kilichotolewa cha asilimia 62.

Kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi iliyopangwa inatokana na mipango duni iliyoandaliwa awali jambo ambalo linapelekea ugumu na ucheleweshwaji wa utoaji wa huduma kwa jamii ambapo mpango huu kwa wilaya nne za Pemba kati ya hizo Wilaya moja tu ndiyo iliyofanikiwa kutekelezwa kwa mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha inafanya makadirio ya kutosha ya miradi ili kuwa na mpango halisi wa kazi utakaoweza kutekelezwa na kufikia lengo lililopangwa.

### 7.2.2 Mpango wa utekelezaji wa Mradi usiojitosheleza

Mbinu bora za utekelezaji wa miradi ni kuwepo kwa mteja (mfanyakazi), Mkandarasi na Mshauri elekezi ambao watashirikiana katika utekelezaji wa shughuli za mradi ambapo mkandarasi na mshauri elekezi wanaajiriwa na mwajiri kwa ajili ya utekelezaji wa kazi, mkandarasi husimamiwa kazi zake na mshauri elekezi na mwajiri anapaswa kusimamia utekelezaji wa kazi zinazofanywa na mkandarasi na mshauri elekezi kulingana na mikataba iliyotayarishwa.

Katika utekekelezaji wa kazi za uchimbaji na ufukiaji wa mabomba yanayosambaza maji kazi ambayo ilisimamiwa na mshauri elekezi alieteuliwa na Mamlaka ya Maji (ZAWA) ukaguzi umebaini mkandarasi alikuwa akifanya kazi za uchimbaji na ufukiaji wa mabomba ya maji na Mamlaka ya Maji (ZAWA) ilikuwa ikifanya kazi za ufungaji wa mabomba ambapo imepelekea mshauri elekezi kusimamia kazi za mwajiri wake.

Aidha, ukaguzi umebaini mshauri elekezi hakupaswa kusimamia kazi zinazofanywa na mwajiri wake jambo ambalo limepelekea kutokuwepo kwa mpangilio maalum katika usimamizi wa kazi zilizotekelezwa katika mradi.

Kutokana na dosari ya uwepo wa kazi ambazo zilipaswa kufanywa na mkandarasi tofauti, kitendo cha ZAWA kufanya kazi alizopaswa kufanya mkandarasi kunaweza kukapelekea ugumu kuchukuliwa hatua pindipo kazi hiyo isipotekelezwa kwa mujibu wa viwango vya mkataba na mshauri elekezi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kwamba kunakuwa na usimamizi mzuri wa kazi katika utekelezaji wa miradi kwa mujibu wa masharti ya mkataba.

### 7.2.3 Utekelezaji wa Mradi bila ya kufanya tathmini ya Athari za Mazingira na Kijamii

Kanuni nambari 144(3) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma za 2020 inaitaka Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kufanya tathmini ya athari za mazingira ya kazi yoyote katika hatua ya upangaji wa mradi na kwa hali yoyote kabla ya kuanza kwa taratibu za manunuzi.

Mapitio ya kumbukumbu za mradi zilibainisha kuwa, tathmini ya athari za mazingira kwa kuchimba na ufukiaji wa bomba la usambazaji wa maji kwa ZAWA haikufanyika. Kutokufanyika kwa tathmini ya kupima athari za kimazingira huwenda ilisababishwa na kutokamilika kwa mipango ya mradi kabla ya utekelezaji wake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unatoa kipaombele cha ufanyaji wa tathmini zinazotokana na athari za kimazingira na kijamii kabla ya utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha wanapunguza uwezekano wa kujitokeza kwa athari ambazo zitapelekea ongezeko la gharama za mradi jambo ambalo litasababisha hasara kwa Serikali kutokana na kuharibika kwa miundombinu ya mradi.

## 7.3 Dosari katika Manunuzi na Mchakato wa upatikanaji wa Mkandarasi

### 7.3.1 Utoaji wa Mkataba kwa Mzabuni asiyestahiki na ambaye hakupendekezwa katika Ripoti ya Tathmini

Ripoti ya Tathmini ya Mikataba na Tathmini ilibainisha kuwa, ripoti ya tathmini ya kazi za Uchimbaji na Ujazaji wa misingi ilipendekeza M/S Kifaru Investment Ltd kwa loti zote nne kwa shilingi 2,675,822,950 na alikuwa mzabuni peke yake aliyestahiki kati ya wazabuni 4 waliowasilisha zabuni. Hata hivyo, mkataba huo alipewa M/s Masonry Building Contractor kwa Loti ya 3 tu kwa shilingi 565,112,300 ambae kwa mujibu wa ripoti ya tathmini hakuwasilisha taarifa ya fedha iliyokaguliwa.

Pia, katika mkataba wa usambazaji wa vifaa kwa ajili ya Matengenezo ya Matangi ya Maji, wazabuni wawili waliwasilisha zabuni zao ambao ni, M/S Sapphire Engineering (T) Limited na M/S Mao General Supplier. Wakati wa tathmini wauzaji wote hawakustahiki kupewa zabuni kutokana na kutokukidhi vigezo ambapo kamati ya tathmini ilipendekeza kuitishwa upya kwa zabuni. Hata hivyo, ZAWA ilimpa mkataba Sapphire Engineering Limited kinyume na mapendekezo kutoka kwa kamati ya tathmini.

Kwa Mkataba wa usambazaji wa pampu, kamati ya tathmini ilipendekeza M/S INFRASOL LTD kupewa mkataba wa usambazaji wa Pampu (Submersible). Hata hivyo, ilibainika kuwa mkataba huo ulipewa M/S Sanfransisco LTD kwa loti ya 1 na 4 na M/S Pump for Africa LTD ilipewa loti ya 2, 3 na 5 bila ya uhalali wowote. Wauzaji waliopewa walikuwa wazabuni wasiostahiki kwani walibadilisha mahitaji ya zabuni.

Utoaji wa zabuni kwa wasiostahiki ulihusishwa na tathmini duni ya zabuni zilizowasilishwa. Hii iliiweka ZAWA hatarini kwani mkandarasi aliyepewa tuzo anaweza kushindwa kutekeleza majukumu yake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unazingatia mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti ya tathmini wakati wa utoaji wa mkataba ili kuepuka kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma kwa kumteua mzabuni asie na sifa ha hatimae kupelekea kushindwa kutekeleza matakwa ya mkataba.

## 7.4 Utekelezaji usioridhisha wa Miradi kwa kuzingatia Muda, Gharama na Ubora kulingana na mkataba

### 7.4.1 Kutowasilisha Dhamana ya Utendaji na Mkandarasi

Kifungu nambari 55.1 cha Mkataba kinahitaji, mkandarasi kuwasilisha Dhamana ya Utendaji si zaidi ya tarehe iliyoainishwa barua ya kukubali tuzo ya zabuni na kuwa katika hali inayokubalika na Mwajiri.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya kumbukumbu za mradi na hati za mikataba na kubaini kwamba dhamana ya utendaji kazi haikuwasilishwa na mkandarasi licha ya utekelezaji wa mradi ukiwa umechelewa kukamilika kwa kipindi cha miezi 11 jambo ambalo linaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma pindipo mkandarasi atakaposhindwa kutekeleza mradi katika kiwango kinachokubalika au kufilisika wakati wa utekelezaji wa mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi ya ZAWA kuhakikisha unazingatia matakwa ya mkataba ya uwasilishwaji wa hati ya dhamana ili kuweza kurejesha gharama zitakazotumiwa na Serikali pindipo mkandarasi atakaposhindwa kutekeleza mradi katika kiwango kilichoainishwa kwa mujibu wa mkataba.

### 7.4.2 Kutokujitosheleza kwa muda wa utoaji wa Mikataba

Kulingana na mkataba wa kazi za uchimbaji na ufukiaji wa misingi ya mabomba ya maji ilibainika kwamba kazi hizo zinapaswa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 2 kutoka tarehe 4 Julai 2022.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 31.1 cha masharti ya jumla ya mkataba kinaeleza ya kwamba meneja wa mradi kuongeza muda wa kukamilika kwa mradi ikiwa kutajitokeza kwa mabadiliko ya kazi au jambo lolote ambalo litapelekea kujitokeza kwa kikwazo cha kukamilika kwa kazi bila ya mkandarasi kuchukua juhudi za kuharakisha kukamilika kwa mradi.

Ukaguzi umefanya mapitio ya majalada ya kumbukumbu za mradi na kubaini ya kwamba hadi kufikia Julai 2023 mradi ulikua haujakamilika. Hii inatoa taaswira ya kuchelewa kukamilika kwa mradi kwa muda wa miezi 10 na siku 9.

Hata hivyo, mapitio mengine ya majalada ya kumbukumbu za mradi yalifanyika na kubainika ya kwamba hakukua na maombi ya nyongeza ya muda kwa ajili ya kukamilika mradi yalioyofanywa na mkandarasi au mwajiri. Kumbukumbu za nyaraka za mradi hazioneshi uwepo wa ongezeko la muda uloombwa na mkandarasi, hii ilibainisha ya kwamba mradi ulikua ukitekelezwa wakati mkataba ulishapitiwa na muda wa matumizi, jambo ambalo ni kinyume na kifungu nambari 31.1 cha masharti ya jumla ya mkataba.

Pamoja na uwepo wa dosari hizo ukaguzi haukuuona jitihada zilizochukuliwa na mkandarasi kutoa taarifa mapema kwa uongozi wa ZAWA jambo ambalo linakwenda kinyume na kifungu nambari 35.1, Vilevile ukaguzi umebaini ZAWA hawakuonyesha nia ya kutoza tozo ya adhabu kwa mkandarasi kushindwa kukamilisha mradi kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa ZAWA uhakikishe miradi yote iliyotekelezwa inakamilika kwa wakati ili kuweza kutoa huduma za maji safi na salama kwa wakati kwa jamii kama ilivyopangwa.

### 7.4.3 Kuwepo kwa udhibiti mdogo wa gharama za vituo vya kuoendeshea mashine ya maji

Kifungu nambari 20 cha masharti maalum ya mkataba kinamtaka mkandarasi kulipwa asilimia 15 ya bei ya mkataba baada ya kukamilika asilimia 20 ya kazi ya bei ya mkataba.

Malipo ya pili asilimia 35 ya bei ya mkataba yatalipwa baada ya kukamilika kwa asilimia 50 ya kazi, na malipo ya tatu ya asilimia 15 ya bei ya mkataba yatalipwa baada ya kukamilika kazi kwa asilimia 80, malipo ya nne ya asilimia 30 ya bei ya mkataba yatalipwa baada ya kukamilika kwa kazi kwa asilimia 100, na malipo ya mwisho ya asilimia 5 ya bei ya mkataba yatalipwa baada ya kukamilika kwa kipindi cha dhima ya mpito.

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa vyeti vya malipo vilivyolipwa kwa wakandarasi na kubaini jumla ya shilingi 367,322,995.00 sawa na asilimia 65 ya bei ya mkataba zilizopwa. Hali halisi ni kama inavyoonekena katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 42: Taarifa ya mkataba kwa ajili Ufukiaji na Uchimbaji wa Mitaro kwa ajili ya kurekebisha bomba la usambazaji wa maji**

| Nambari ya Malipo | Kiasi kilicholipwa (Tsh) | Asilimia inayohitajika kwa bei ya mkataba | Asilimia ya Bei ya Mkataba Kulipwa | Inahitajika Kujumlisha<br>Asilimia ya Kukamilisha Kazi katika Mkataba | Asilimia halisi ya Kukamilisha | Asilimia ya kazi za jumla ambazo hazijafikiwa kama Kwa Mkataba |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Malipo ya 1 | 84,766,845 | 15 | 15 | 20 | 15 | 5 |
| Malipo ya 2 | 197,789,305 | 35 | 35 | 50 | 50 | 0 |
| Malipo ya 3 | 84,766,845 | 15 | 15 | 80 | 65 | 15 |

*Chanzo: Hati za Mkataba, Maombi ya Malipo na Mkandarasi na Vocha ya Malipo*

Jadweli hapo juu linaonesha kwamba jumla ya hati tatu za malipo zilizolipwa kwa mkandarasi, malipo ya hati mbili hayakufikia asilimia inayohitajika ya kukamilika

lakini bado malipo yaliendelea kufanywa. Malipo hayo ni hati nambari 1 ambapo mkandarasi alilipwa chini ya asilimia ya kukamilisha kazi kwa asilimia 5, na hati nambari 3 mkandarasi alilipwa chini ya asilimia ya kukamilsha kazi kwa asilimia 5.

Hali hii ilisababishwa kutokana na kutokufanyika kwa malipo kulingana na asilimia inayohitajika kulipwa kwa mujibu wa kazi iliyofanyika kulingana na bei ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakiksiha kuwa unasimamia vyema malipo ya wakandarasi kwa kufanya malipo kulingana na kiwango kilichoainishwa katika mkataba.

# SURA YA NANE



# 8.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA MATENGENEZO YA MATANGI YA MAJI

## 8.1 Utangulizi

Sura hii inahusiana na matokeo ya ukaguzi wa matengenezo ya Matangi ya maji katika eneo la Saateni na Mnara wa mbao kwa upande wa Unguja na Raha Wete kwa upande wa Pemba. Maelezo yanayohusiana na matengenezo ya matangi ya maji katika maeneo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini.

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ilisaini mkataba na mkandarasi M/S Saphire Engineering (T) Limited kwa ajili ya matengenezo ya tangi la maji lililopo Raha Pemba kwa thamani ya shilingi 212,501,600. Taarifa ya mkataba wa matengenezo ya tangi hilo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini: -

**Jadweli Nambari 43: Taarifa ya mkataba wa matengenezo ya tangi la maji Raha Wete**

| Kipengele cha Mkataba | Usambazaji na Utoaji wa Vifaa kwa ajili ya Matengenezo ya Matangi ya Maji –Raha Pemba |
|---|---|
| Nambari ya mkataba | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/10 |
| Jina la Mkandarasi | M/S Saphire Engineering (T) Limited |
| Tarehe ya Kusaini | Aprili 13, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza | Aprili 13, 2022 |
| Muda wa Mkataba | Miezi 2 |
| Tarehe ya kukamilika kwa awali | Juni,2022 |
| Tarehe halisi ya Kukamilisha | Haujakamilika |
| Mkataba wa awali wa jumla na VAT | Shilingi 212,501,600 |
| Mkataba wa Urekebishaji wa Jumla na VAT | - |
| Maendeleo ya Kazi (%) hadi Julai 2023 | - |
| Maendeleo ya Malipo (%) hadi Julai 2023 | 90% |
| Kuchelewa kukamilika kwa kazi | Miezi 13 |
| Tozo ya ucheleweshwaji wa malipo | - |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka Hati za Mkataba, 2023*

Pia, Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ilisaini mkataba na mkandarasi M/S Humble Engineering & General Supply Ltd kwa ajili ya matengenezo ya matangi ya maji katika eneo la Saateni na Kilimani Mnara wa Mbao kwa thamani ya shilingi 119,224,339. Taarifa ya mkataba wa matengenezo ya tangi hilo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini: -

### Jadweli Nambari 44: Taarifa ya Mkataba wa Matengenezo ya Matangi ya Maji kwa Zawa

| Kipengele cha Mkataba | Matengenezo ya Matangi ya Maji kwa Zawa katika Saateni na Kilimani Mnara wa Mbao |
|---|---|
| Nambari ya mkataba | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/10 |
| Jina la Mkandarasi | M/S Humble Engineering & General Supply Ltd |
| Tarehe ya Kusaini | Juni 8, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza | Juni 15, 2022 |
| Muda wa Mkataba | Siku 60 |
| Tarehe ya kukamilika inayotarajiwa | Agosti 15, 2022 |
| Tarehe halisi ya kipindi cha kibali cha kukamilika | - |
| Mkataba wa awali Sum na VAT Inclusive | Shilingi 119,224,339 |
| Mkataba wa Urekebishaji wa Jumla na VAT | - |
| Maendeleo ya Malipo (%) kama ya 30th Juni 2023 | Asilimia 100 |
| Kuchelewa kukamilika kwa kazi | - |
| Tozo ya ucheleweshwaji wa malipo | - |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka Hati za Mkataba, 2023*

Wakati wa ukaguzi masuala yafuatayo yanayohusiana na utengenezaji wa matangi ya maji, ukaguzi ulibaini dosari zifuatazo: -

## 8.2 Dosari zilizojitokeza katika Kipengele cha Ununuzi

### 8.2.1 Uteuzi usiofaa wa Msambazaji wa Vifaa vya Matengenezo ya Matangi ya Maji Raha Wete Pemba

Kanuni nambari 118(8) (9) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, 2020, inahitaji kabla ya tathmini ya kina ya zabuni, Kamati ya Tathmini kufanya uchunguzi wa awali wa zabuni ili kubaini kama kila zabuni inajibu kwa kiasi kikubwa mahitaji ya nyaraka za zabuni, dhamana zinazohitajika zimetolewa, nyaraka zimesainiwa vizuri, zabuni kwa ujumla zimefuata utaratibu na nakala za usajili wa kufanya biashara zimetolewa.

Ukaguzi ulipitia ripoti ya tathmini ya zabuni ya Usambazaji wa Vifaa kwa ajili ya matengenezo ya Matangi ya maji Januari 2022 ambapo jumla ya wazabuni wawili waliwasilisha zabuni zao ambao ni, M/S Mao General Supplier kwa thamani Shilingi 54,843,300 na M/S Midodoni Hardware kwa thamani ya Shilingi

68,241,000 na baadaye kufunguliwa, Bodi ya Zabuni ilichunguza nyaraka zilizotolewa za wazabuni hao wawili kulingana na vigezo vilivyowekwa, ukaguzi umebaini wazabuni wote hao hawakustahili kufanyiwa tathmini ya kina na badala yake walipaswa kufanyika zabuni upya. Hali halisi ya matokeo ya uchunguzi wa awali wa zabuni hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 45: Muhtasari wa matokeo katika Uchunguzi wa Awali wa zabuni**

| Name of Bidders | Verification (a) | Eligibility (b) | Completeness (c) | Substantial Responsiveness (d) | Acceptance Detailed Examination (e) |
|---|---|---|---|---|---|
| M/S Mao General Supplier | NO | YES | NO | NO | NO |
| M/S Midodoni Hardware | NO | YES | YES | NO | NO |

*Chanzo: Ripoti ya zabuni ya tathmini*

Ukaguzi ulipitia ripoti ya tathmini ya zabuni ya pili pamoja na mapendekezo yake ya usambazaji wa vifaa kwa ajili ya matengenezo ya Matangi ya maji Machi 2022, ambapo ukaguzi ulibaini jumla ya wazabuni wawili waliwasilisha zabuni zao ambao ni, M/S Sapphire Engineering (T) Limited yenye thamani ya shilingi 212,501,600 ambazo ni sawasawa na (Dola za Kimarekani 80,000 @ shilingi 2,309.80) na mkandarasi M/S Mao General Supplier hakua na bei ya zabuni iliyoanishwa na baadaye zabuni hiyo ilifunguliwa, ambapo Bodi ya Zabuni ilichunguza nyaraka zote zilizotolewa na wazabuni hao kulingana na vigezo vilivyowekwa,ambapo ilibainika Wazabuni hao kutokua na sifa zinazohitajika kutekeleza matengenezo hayo na walipaswa ZAWA kufanya zabuni upya.

Hali halisi ya matokeo ya tathmini ya awali kwa wazabuni hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 46: Muhtasari wa matokeo ya awali ya Tathmini ya Zabuni**

| Name of Bidders | Verification (a) | Eligibility (b) | Completeness (c) | Power of Attorney (c) | Substantial Responsiveness (d) | Acceptance Detailed Examination |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M/S Sapphire Engineering (T) Ltd | NO | YES | NO | NO | NO | NO |
| M/S Mao General Supplier | NO | YES | NO | YES | NO | NO |

Ukaguzi umebaini uwepo wa wazabuni ambao hawakufaulu wakati wa kufanyiwa tathmini ya kwanza na ya pili ya zabuni ambapo ZAWA bado iliendelea kumchagua mzabuni M/S Saphire Engineering (T) Ltd ambapo aliandikiwa barua ya mualiko wa kikao cha mapatano yenye kumbukumbu namba ZAWA/U/10/VOLII/81 ya tarehe 25 Machi,2022 na pia alipewa taarifa ya uteuzi yenye kumbukumbu namba ZAWA/U/10/VOLII/81 ya tarehe 25 Machi,2022 kwa mujibu wa mkataba namba SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/10.

Kuteua wazabuni ambao wamekosa sifa wakati wa kufanyiwa tathmini kunaweza kupelekea Serikali kuingia katika gharama za ziada.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kamati za tathmini zinafanya uchambuzi kwa kuzingatia vigezo vyote vilivyomo katika mkataba kabla ya kuchaguliwa kwa mzabuni.

## 8.3 Dosari katika Kipengele cha Usimamizi wa Mkataba

### 8.3.1 Kuchelewa kuwasilishwa kwa Tangi la Maji - Raha Wete Pemba

Kwa mujibu wa kifungu nambari 21 cha masharti maalum ya Mkataba (SCC) ambacho kilimtaka mzabuni kuwasilisha Tangi moja la kuhifadhia maji katika eneo la Raha Wete ndani ya kipindi cha wiki 8 kuanzia Aprili 13, 2022 hadi Juni 2022

Ukaguzi umebaini mzabuni huyo alichelewa kuwasilisha tangi hilo katika eneo la mradi kwa mujibu wa mkataba ambapo utekelezaji wake ulichelewa kwa miezi 13 hadi ukaguzi unakamilika mwezi wa Julai 2023, tangi hilo halijawasilishwa katika eneo la mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa unazingatia masharti yote ya mikataba ili kuepusha kujitokeza kwa uharibifu au hasara kwa Serikali.

### 8.3.2 Kutowasilisha dhamana ya Benki ya Malipo ya awali na Dhamana ya Utendaji

Mamlaka ya Maji Zanzibar ilipokea mgao wa fedha za Ahueni ya UVIKO-19 shilingi 212,501,600. Fedha hizo zilitengwa kufanya ukaguzi maalum kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za UVIKO-19. Kampuni ya M/S Saphire Engineering (T) Ltd ililipwa awamu ya kwanza ya shilingi 106,250,800 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za mradi.

Ukaguzi ulibainisha kuwa, muuzaji aliwasilisha nambari ya Dhamana ya Utendaji BICL/LUT/534705/22/PB kutoka Kampuni ya Bima ya Bumaco badala ya dhamana ya Benki kama maelekezo ya mkataba. Pia, ukaguzi ulibaini kuwa, Mamlaka ya Maji Zanzibar iliendelea kulipa awamu ya kwanza kwa M/S Sapphire Engineering (T) Ltd bila kupata dhamana ya benki na Dhamana ya Utendaji kutoka kwa msambazaji kama mkataba uliosainiwa. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 47:Utaratibu wa malipo ya zabuni kwa mujibu wa mkataba

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Malipo ya awali | 50% ya bei ya mkataba ambayo itafanywa baada ya uwasilishaji wa dhamana ya benki isiyo na masharti ya bei sawa iliyolipwa. |
| 2. | Wakati wa Uwasilishaji | 50% ya bei ya mkataba italipwa kwa muuzaji ndani ya siku 30 baada ya upokeaji na uchunguzi wa bidhaa. |

### Jadweli Nambari 48:Nyaraka zinazohitajika kwa malipo kulingana na mkataba:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Dhamana ya Benki ya Juu | 50% ya malipo ya mkataba (GCC Clause 18) |
| 2. | Dhamana ya Utendaji | 10% ya Dhamana ya Utendaji wa mkataba (GCC Clause 9) |

Utekelezaji wa mradi huo ulikuwa hatarini kwa kuwa mradi haukulindwa kwa utendaji wowote mbaya kutoka kwa muuzaji.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa katika manunuzi yajayo wanaongeza umakini katika kufanya ufuatiliaji wa kina ili kuweza kumpata msambazaji mwenye sifa zinazokubalika.

# SURA YA TISA



# 9.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU USAMBAZAJI NA UFUNGAJI WA UMEME

## 9.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi kuhusu kazi ya usambazaji na ufungaji wa umeme inavyotekelezwa na ZECO kwa mujibu wa mkataba nambari SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/12 wenye thamani ya shilingi 118,122,214.62 kwenye vituo vyenye visima vya kuendeshea mashine ya maji kama invyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 49: Taarifa za mkataba wa usambazaji na ufungaji wa Umeme**

| Kipengele cha Mkataba | Usambazaji na ufungaji wa Umeme |
|---|---|
| Mkataba wa No. | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/12 |
| Jina la muuzaji | M/S Shirika la Umeme Zanzibar |
| Tarehe ya Kusaini | Juni 27, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza | Juni 15, 2022 |
| Muda wa Mkataba | Siku 60 |
| Tarehe ya kukamilika inayotarajiwa | 15 Agosti, 2022 |
| Tarehe halisi ya Kukamilika | |
| Thamani ya Mkataba pamoja na VAT | Shilingi 118,122,214.62 |
| Mkataba wa Urekebishaji wa Jumla na VAT | Hakuna |
| Malipo yaliyolipwa hadi tarehe 30 Juni, 2023 | 100% |
| Kuchelewa kukamilika kwa kazi | Hakuna |
| Riba kwa kuchelewa malipo | Hakuna |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka Hati za Mkataba, 2023*

Wakati wa ukaguzi masuala yafuatayo yanayohusiana na usambazaji na ufungaji wa umeme yalizingatiwa kama ifuatavyo: -

## 9.2 Malipo yasiyoridhisha ya shilingi 1,200,000,000

Kifungu nambari 46 (1) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 kinaeleza kuwa, Afisa Masuuli atasimamia mkataba kwa kuzingatia hali ya ufanisi, kiuchumi ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha inapatikana katika utekelezaji na usimamizi wa shughuli za mradi kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 pamoja na Kanuni zake.

Ukaguzi ulipitia nyaraka za mikataba pamoja na hati za malipo nambari PV20000632 yenye kiasi cha shilingi 1,200,000,000 zilizolipwa kwa ajili ya usambazaji na ufungaji wa umeme katika vituo vya uendeshaji wa mashine za maji Pemba. Hata hivyo ukaguzi haukuweza kupatiwa nyaraka zinazothibitisha kufanyika kwa malipo hayo.

**Jadweli Nambari 50: Uchambuzi wa Malipo kwa Usambazaji na Ufungaji wa Umeme**

| Namba | Hati za Malipo | Kiasi kilicholipwa (Tsh) |
|---|---|---|
| 1. | PV2000283 | 59,061,107.31 |
| 2. | PV2000387 | 40,916,747.69 |
| 3. | PV2000623 | 1,200,000,000 |
| | **Jumla** | **1,299,977,855** |

*Chanzo: Hati za Malipo*

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa, ZECO ililipwa jumla ya shilingi 99,977,855 kwa ajili ya usambazaji na ufungaji wa umeme chini ya kiwango cha mkataba cha shilingi 118,122,214.62 ambacho kilikuwa kikubwa zaidi kwa mujibu wa hati za malipo zilizoainishwa hapo juu zenye thamani ya shilingi 1,299,977,855 fedha ambazo zililipwa kwa ZECO. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini hati ya malipo yenye namba PV2000623 iliyotumika kumlipa ZECO yenye kiasi cha shilingi 1,200,000,000 ilikosa vielelezo vinavyothibitisha kuwa malipo hayo yalifanyika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unaimarisha udhibiti wa ndani katika mfumo wa usimamizi wa fedha ili kuhakikisha malipo yote yanayofanywa yanaambatanishwa na nyaraka husika.

## 9.3 Kuchelewa kwa Usambazaji na Ufungaji wa Umeme katika visima vya maji

Mamlaka ya Maji Zanzibar iliingia mkataba na ZECO wenye namba SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/12 kwa ajili ya kazi ya usambazaji na ufungaji wa umeme katika maeneo yote yaliyochimbwa visima vya maji Unguja na Pemba kwa lengo la kuimarisha uzalishaji wa maji kutoka eneo la visima hadi kwenye matangi ya kusambazia maji.

Kulingana na muda wa mkataba kazi hiyo ilitakiwa kutekelezwa kwa siku 60 kuanzia tarehe 15 Juni hadi 15 Agosti, 2022. Hata hivyo, wakati wa ziara ya eneo la mradi ukaguzi ulibaini kuwa kati ya visima 38, ni visima 6 tu sawa na asilimia 16 ambavyo viliweza kuunganishwa na huduma ya umeme na kufanya kazi kwa uzalishaji wa maji na visima 32 sawa na asilimia 84 havikuunganishwa na umeme, hali halisi ya visima hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 51 :Visima vya mradi vilivyochimbwa kwa Unguja na Pemba**

| Mkoa | Eneo | Idadi |
|---|---|---|
| **Visima Vipya** | | |
| Kusini Unguja | Uroa (Bambi Uroa) 1 | 2 |
| | Uroa (Bambi Uroa) 2 | |
| | Mgeni Haji Bh2 | 2 |
| | Mgeni Haji Bh1 | |
| | Unguja Ukuu Bh1 | 2 |
| | Unguja Ukuu Bh2 | |
| Kaskazini Unguja | Kiashangwe | 1 |
| | Donge Kipange 2 | 2 |
| | Donge Kipange 1 | |
| | **Kaburi Kikombe Bh1** | 2 |
| Mjini | Kaburi Kikombe Bh2 | |
| **Jumla ya Visima Unguja** | | **11** |
| Kaskazini Pemba | Mapofu 1 | 3 |
| | Mapofu 2 | |
| | Mapofu 3 | |
| | Kironjo | 1 |
| | Kiuyu Manda 1 | 2 |
| | Kiuyu Manda 2 | |
| | Saninga | 1 |
| | **Wande** | 1 |
| | Kijuki | 1 |
| | Uwondwe | 1 |
| Kusini Pemba | Kwa Sharifu Ali 1 | 4 |
| | Kwa Sharifu Ali 2 | |
| | Kwa Sharifu Ali 3 | |
| | Kwa Sharifu Ali 4 | |

| | | |
|---|---|---|
| Kusini Pemba | Mkoroshoni | 1 |
| | Shamiani | 1 |
| | Jaani | 1 |
| | Mwambe | 1 |
| | Kiwani | 1 |
| | Mbiji 1 | 2 |
| | Mbiji 2 | |
| | Manyaga | 1 |
| | Mtuhaliwa | 1 |
| | Ngwachani | 1 |
| | Mjimbini | 1 |
| | Chambani | 1 |
| | Ng'ombeni | 1 |
| **Jumla ya Visima Pemba** | | **27** |
| **Jumla Kuu Visima Vipya (Unguja+Pemba)** | | **38** |

Hali hii imepelekea kuchelewa kwa uzalishaji wa maji kulikotokana na kukosekana kwa maji katika matangi ya maji iliyosababishwa na ukosefu wa umeme.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kufanya uchunguzi wa kina wa usambazaji wa umeme kutoka ZECO ili kuhakikisha visima vyote vinaunganishwa na huduma ya umeme kwa lengo la upatikanaji wa maji safi na salama kwa matumizi ya wananchi.

# SURA YA KUMI


Water Management System
monitor and manage water & wastewater infrastructure
Automation
Plant Monitoring
Energy Optimization
Water treatment plant
Quality & Level Monitoring
Reservoir
Water tower
Leakage sensors
Flow, Pressure, Quality Monitoring
Smart meters-Advanced Metering
Consumer
Rain
Real time data and analysis on water usage, water availability patterns and accurate forecasting helps in supply planning
Wastewater
Rain overflow basin
River, lake
Automated Groundwater access: reduce environmental impact
Groundwater/Source
Water Quality & Quantity Monitoring
River, lake
OFFICE OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL ZANZIBAR
OCAGZ

# 10.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU HUDUMA YA USHAURI KATIKA MFUMO WA KUSIMAMIA NA KUDHIBITI UPOTEVU WA MAJI

## 10.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi kuhusu kazi ya ushauri elekezi katika ufungaji wa mfumo wa kusimamia na kudhibiti upotevu wa maji katika maeneo yote yaliyosambazwa maji ambapo ZAWA iliingia mkataba na Chuo cha Maji wenye kumbukumbu nambari SMZ / IMF / NO.104 / CS / RNCT / 2021. 2022 /01 kwa thamani ya shilingi 242,822,500. Maelezo ya huduma za ushauri na usimamizi yamewasilishwa katika jadweli hapa chini:

**Jadweli Nambari 52: Taarifa za Mkataba wa Huduma ya Ushauri na Usimamizi**

| Kipengele cha Mkataba | Huduma ya Ushauri kwa Ufungaji wa Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Uvujaji wa Maji (ILMS) |
|---|---|
| Nambari ya Mkataba | SMZ/IMF/NO.104/CS/RNCT/2021.2022/01 |
| Jina la Mkandarasi | M/S Chuo cha Maji |
| Tarehe ya Kusaini Mkataba | 05 Juni, 2022 |
| Tarehe ya kuanza ujenzi | Juni 20, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza ya Ufanisi | Juni 20, 2022 |
| Muda wa Mkataba | Miezi 3 |
| Tarehe ya awali ya kukamilika | 22 Septemba, 2022 |
| Tarehe halisi ya Kukamilisha | Oktoba, 2022 |
| Kiasi cha Mkataba wa awali ikijumuisha VAT | Shilingi 242,822,500.00 |
| Kiasi cha Mkataba uliorekebishwa ikijumuisha VAT | Hakuna |
| Maendeleo ya Kazi (%) hadi Julai, 2023 | Asilimia 100 |
| Maendeleo ya Malipo (%) hadi Julai, 2023 | Asilimia 101.4 |
| Kuchelewa kukamilika kwa kazi | - |
| Riba ya kuchelewa kulipa | Hakuna |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka katika hati za Mkataba, 2023*

Ukaguzi unatambua juhudi zinazofanywa na ZAWA katika mabadiliko ya mfumo wa taarifa za usimamizi ili kuimarisha ufanisi katika utoaji wa huduma ya maji Zanzibar. Pamoja na jitihada zilizofanywa na ZAWA Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:

## 10.2 Dosari katika utekelezaji wa Mipango

### 10.2.1 Kukosekana kwa Mpango Mkakati wa TEHAMA wa Taasisi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 2.3 cha muongozo wa Serikali Mtandao wa, 2017 kinazitaka taasisi za umma kuandaa na kutekeleza Mkakati wa TEHAMA wa Taasisi ili kuweka mkazo wa wazi katika kutumia TEHAMA kwa utoaji huduma bora na kufikia thamani bora ya uwekezaji katika Viwango vya Kiufundi. Pia, kuhakikisha kuwa mipango yote ya maendeleo na matumizi ya TEHAMA inaendana na malengo na maelekezo ya kimkakati ya Taasisi.

Ukaguzi ulifanya mahojiano na maafisa wa ZAWA na kubaini kuwa kulikuwa na ukosefu wa mpango mkakati wa TEHAMA, jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa muelekeo wa mipango imara ya TEHAMA ambayo ingezingatia ufungaji wa mfumo jumuishi wa usimamizi wa upotevu wa maji kutokana na miundombinu ya kusambazia maji ya ZAWA kwa maendeleo ya jamii.

Kukosekana kwa mpango mkakati wa TEHAMA kulisababisha kutokamilika kwa mpango wa mabadiliko ya matumizi ya TEHAMA kwa ajili ya maendeleo katika utoaji wa huduma za Mamlaka ya Maji Zanzibar.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unaweka kipaumbele kwa kuandaa mpango mkakati wa TEHAMA ili kuweza kuisaidia ZAWA katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za maji kupitia mifumo ya TEHAMA.

### 10.2.2 Kukosekana kwa Mpango wa Kukabiliana na Maafa “Disaster Recovery Plan” katika Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Upotevu wa maji

Kwa mujibu wa kifungu nambari 4.3.3 cha Muongozo wa Maendeleo ya Usanifu wa Usalama wa Taasisi wa Muongozo wa Serikali Mtandao wa 2022, unaeleza kwamba ili kuimarisha Usanifu wa Usalama wa Serikali Mtandao, Taasisi za Umma zinatakiwa kuandaa Mpango wa Kukabiliana na Maafa, kwa lengo la kuweka taratibu za kurejesha na kulinda mifumo na miundombinu ya TEHAMA bila ya kupoteza taarifa wakati janga litakapotokezea.

Hata hivyo, kulingana na mahojiano na maafisa wa ZAWA ilibainika kuwa hakukuwa na mpango wa kukabiliana na maafa katika Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Uvujaji wa maji uliowekwa kwa ajili ya ulinzi dhidi ya upoteaji au uharibifu wa taarifa kama ilivyoelezwa katika Muongozo wa Usanifu wa Usalama.

Kukosekana kwa mpango wa kukabiliana na maafa kwa Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Uvujaji wa Maji husababisha kukosekana kwa usalama wa taarifa jambo ambalo linaweza kupelekea kupoteza taarifa muhimu za upotevu wa maji endapo janga likitokezea katika Taasisi husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kuhakikisha unaongeza udhibiti na usimamizi wa taarifa za maji zilizomo kwenye mifumo ya maji kwa kuandaa mpango imara wa kukabiliana na maafa ili kuepuka upotevu na uharibifu wa taarifa za maji.

## 10.3 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Uendeshaji wa Mfumo

### 10.3.1 Kukosekana kwa muingiliano (integration) baina ya mfumo wa Usimamizi wa Upotevu wa Maji (ILMS) na mifumo mengine

Kifungu nambari 3.4.3 cha Muongozo wa Serikali Mtandao wa Zanzibar wa 2022 kinaeleza kwamba Taasisi za Umma kutumia huduma za mashirikiano na muunganiko wa mifumo inayoendeshwa na Serikali ili kuweza kubadilishana taarifa katika taasisi zote kwa kuangalia kiwango cha muingiliano wa taarifa pamoja na kuzingatia usalama wa kubadilishana taarifa hizo.

Kulingana na mahojiano na maafisa wa ZAWA ukaguzi ulibaini kuwepo kwa mifumo mingine ya usimamizi wa taarifa inayotumiwa na ZAWA ikiwa ni pamoja na Mfumo wa Usimamizi wa Bili za Maji, Mfumo wa kusimamia taarifa za matumzi ya fedha pamoja na mfumo wa kusimamia taarifa za rasilimali watu.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kukosekana kwa muingiliano (integration) baina ya Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Upotevu wa Maji (ILMS) na mifumo mengine iliyopo katika Mamlaka (ZAWA) jambo ambalo limepelekea kupungua kwa ufanisi wa utendaji kazi wa Mamlaka katika usimamizi na utoaji wa huduma bora za maji kwa jamii.

Kukosekana kwa muingiliano wa mifumo ya ZAWA kunaweza kusababisha kutopatikana kwa taarifa za uhakika kutokana na mifumo kushindwa kubadilishana taarifa na hatimae kupelekea kupungua kwa ufanisi wa utendaji kazi wa Mamlaka katika kutoa huduma bora za maji kwa wananchi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unaweka muingiliano baina ya mfumo wa udhibiti wa upotevu wa maji pamoja na mifumo mengine husika ya TEHAMA ya ZAWA ili mifumo hiyo iweze kusomana na kurahisisha zoezi la ubadilishanaji wa taarifa na hatimae kuongezeka kwa ufanisi wa ukushanyaji wa mapato.

### 10.3.2 Kutofikiwa kikamilifu lengo la uanzishwaji wa Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Upotevu wa Maji (ILMS)

Kulingana na hadidu rejea ya Ufungaji wa Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Uvujaji wa maji kwa ajili ya kusimamia Miundombinu ya ZAWA, ilibainisha kwamba lengo la kuanzishwa kwa mfumo huo ni kusaidia katika usimamizi na udhibiti wa matumizi ya maji.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya muongozo wa matumizi na uendeshaji wa Mfumo wa ILMS na kubaini kwamba Mfumo huo haukuwa na Jumuishi wa Usimamizi wa Uvujaji wa maji haukuwa na uwezo wa kusimamia ipasavyo upotevu wa rasilimali za maji ili kuweza kupatikana ujazo mzuri na kiwango bora cha maji safi na salama kwa wananchi.

Kulingana na ukaguzi uliofanyika kwa wateja kuhusu uungwaji na upatikanaji wa huduma za maji kupitia mfumo wa ILMS imebainika kuwa mfumo huo uliweza kugundua uwepo wa wateja walioungiwa na wasioungiwa mita za maji. Kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 53: Uchambuzi wa Wateja wanaotumia na wasiotumia Mita

| Namba | Aina ya Wateja | Idadi |
|---|---|---|
| | Wanaotumia mita | 3,577 |
| | Wasiotumia mita | 63,456 |
| | **Jumla** | **67,033** |

*Chanzo: Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Uvujaji wa maji*

Hata hivyo, kulingana na mahojiano na Afisa wa ZAWA, ukaguzi ulibaini kuwa usimamizi wa kiasi cha maji yanayovuja haukubainishwa katika mfumo wa ILMS kwani hakukuwa na vifaa vya utambuzi katika matangi ya kuhifadhia maji na kifungio chake (gate valve) ili kufuatilia mwenendo wa matumizi ya maji kwa kuweza kuhesabu kiwango cha upotevu wa maji unaoripotiwa.

Pia, ilibainika kuwa, mfumo jumuishi wa usimamizi wa upotevu wa maji kwa pamoja hautoi ripoti za uvujaji wa maji ndani ya mfumo kutokana na kuchezewa kwa mashine za maji na wananchi au kuharibika ama kuchakaa kwa miundombinu ya kusambazia na kuhifadhi maji.

Kukosekana kwa mfumo wa usimamizi wa ufuatiliaji wa matumizi ya kiasi cha maji kuvuja na kutibu ubora wa maji kunapelekea uwepo wa usimamizi duni wa uzalishaji na utumiaji wa huduma ya maji jambo ambalo linapelekea upotevu wa mapato na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa unaboresha na kuongeza kasi ya usimamizi wa mifumo ya maji ili kuweza kuongeza ufanisi katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za maji kwa jamii.

# SURA YA KUMI NA MOJA



# 11.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA HUDUMA ZA USHAURI ELEKEZI PAMOJA NA UJENZI WA MATANGI YA MAJI

## 11.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza matokeo ya ukaguzi kuhusiana na huduma za ushauri elekezi juu ya ujenzi wa matangi ya maji ya juu na ya ardhini. Ukaguzi ulifanya tathmini ya juu ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kuhakikisha ZAWA inatoa huduma bora za upatikanaji wa maji kutokana na miundombinu iliyowekwa ya kuhifadhia na kusambaza maji kwa maeneo ya Unguja na Pemba.

Mamlaka ya Maji Zanizbar iliingia mkataba na kampuni ya M/S Nimeta Consult (T) wenye nambari SMZ/IMF/No.104/CS/RNCT/2021/2022/08 tarehe 07 Febuari, 2022 ambapo mkataba huo ulikuwa na thamani ya shilingi 890,000,000 pamoja na VAT, baadae kupitia mkataba huo ZAWA ilifanya marekebisho na kupelekea thamani hiyo kubadilika na kufikia jumla ya shilingi 1,051,339,346.17 pamoja na VAT huduma za Ushauri elekezi juu ya ujenzi wa matangi ya maji ya juu na ya ardhini. Hali halisi ya mkataba huo ni kama invyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 54: Taarifa za Mkataba kwa Huduma ya Ushauri na Usimamizi**

| Kipengele cha Mkataba | Huduma ya Ushauri elekezi kwa ajili ya Usanifu na Usimamizi wa Ujenzi wa Matangi ya Maji |
|---|---|
| Nambari ya Mkataba | SMZ/IMF/No.104/CS/RNCT/2021/2022/08 |
| Jina la Mkandarasi | M/S NIMETA CONSULT (T) |
| Tarehe ya Kusaini | 7 Febuari, 2022 |
| Tarehe ya kuanza | 14 Febuari, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza ya Ufanisi | 14 Febuari, 2022 |
| Muda wa Mkataba | Miezi 23 |
| Tarehe ya awali ya kumaliza kazi | 7 Januari, 2024 (ikiwa ni pamoja na usimamizi wa DLP) |
| Tarehe halisi ya Kukamilisha kazi | |
| Jumla ya kiasi cha awali cha Mkataba na ikijumuisha VAT | Shilingi 890,000,000.00 |
| Thamani ya Mkataba pamoja na VAT | Shilingi 1,051,339,346.17 |
| Maendeleo ya Kazi (%) hadi Julai, 2023 | Asilimia 100 |
| Maendeleo ya Malipo (%) hadi Julai, 2023 | Asilimia 100 |
| Kuchelewa kukamilika kwa kazi | - |
| Riba kwa kuchelewa malipo | - |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka katika hati za mkataba, 2023*

Wakati wa ukaguzi masuala yafuatayo yanayohusiana na huduma za ushauri elekezi kuhusu ujenzi wa matangi ya kuhifadhia maji yalizingatiwa kama ifuatavyo: -

## 11.2 Dosari katika Kipengele cha Mipango

### 11.2.1 Gharama zilizoongezeka kutokana na usanifu wa ngazi ya zege shilingi 131,384,470

Kwa mujibu wa Viwango vya Uingereza (British Standard 8110): Sehemu ya 1:1985, lengo la muundo wa Usanifu ni kufikia uwezekano unaokubalika kwamba miundo inayoundwa itafanya kazi kwa kuridhisha wakati wa maisha yao yaliyokusudiwa na kiwango sahihi cha usalama.

Ukaguzi ulipitia mchoro wa ngazi na kubaini kwamba ZAWA ilitumia muundo wa zege ulioimarishwa daraja halisi la C40 badala ya daraja la C25. Jumla ya ujazo wa zege kwa ngazi ilikuwa $350m^3$ uliogharimu kiasi cha shilingi 259,424,470.

Aidha, kutokana na mapitio ya ripoti ya muundo ukaguzi ulibaini kuwa na muundo wa ngazi wa mwanzo ulikuwa ngazi za chuma kupitia matangi ya maji yaliyoinuliwa ambayo baadae yalibadilishwa wakati wa utekelezaji wa mradi na kuekwa ngazi za zege zenye urefu wa mita 15 hadi 20 kwenda juu ambazo zina umbile la 'U' iliyotengwa kando ya tangi la maji na haishiriki katika kusaidia kubeba mzigo wa tangi.

Uchambuzi huo ulionyesha kuwa, kwa kutumia daraja halisi la C25 gharama inaweza kuwa shilingi 128,040,000 ambayo ilikuwa shilingi 131,384,470 chini ya gharama ya ngazi kwa kutumia daraja halisi la C40. Hivyo basi, kwa kutumia daraja halisi la C40 katika ngazi hiyo kunagharimu kiasi cha shilingi 259,424,470 wakati kwa kutumia daraja halisi la C25 inaweza kupunguza gharama hadi shilingi 128,040,000 hivyo ZAWA anaweza kuokoa kiasi cha shilingi 131,384,470. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha nambari 6 hapo chini: -

### Picha Nambari 6: Ngazi zilizotengwa pembeni ya matangi ya maji ya juu




*Chanzo: Picha iliyopigwa na Mkaguzi wakati wa ukaguzi wa eneo tarehe 20 Julai, 2023*

Aidha, Jadweli hapo chini linaonesha mlinganisho wa gharama za zege kwenye ujenzi wa ngazi katika matangi ya maji kwa kutumia daraja la C40 na daraja la C25 lenye kuonesha uimara wa zege iliyowekwa. Hali halisi ni kama ifuatavyo:-

### Jadweli Nambari 55: Gharama ya mradi kwa kutumia zege daraja halisi la 40 na daraja la 25 kwa ngazi

| Eneo la Ujenzi wa Tangi | Kiwango cha ujazo wa Zege ($m^3$) (Tsh) (A) | Gharama kwa Kiwango cha ujazo wa Zege kwa daraja la C40 (Tsh) (B) | Jumla ya Gharama za uwekaji zege kwa daraja la C40 (Tsh) (AxB) | Gharama kwa Kiwango cha ujazo wa Zege katika daraja la C25 (Tsh) (C) | Jumla ya Gharama za uwekaji zege kwa daraja la C25 (Tsh) (AXC) |
|---|---|---|---|---|---|
| Pujini | 45 | 734,369 | 33,046,605 | 396,000 | 17,820,000 |
| Makangale | 55 | 734,369 | 40,390,295 | 396,000 | 21,780,000 |
| Shumba Mjini | 55 | 734,369 | 40,390,295 | 396,000 | 21,780,000 |
| Kiwani | 35 | 734,369 | 25,702,915 | 396,000 | 13,860,000 |
| Tumbatu | 40 | 853,979 | 34,159,160 | 330,000 | 13,200,000 |
| Bubwini | 40 | 714,460 | 28,578,400 | 330,000 | 13,200,000 |
| Uguja Ukuu | 40 | 714,460 | 28,578,400 | 330,000 | 13,200,000 |
| Mgeni Haji | 40 | 714,460 | 28,578,400 | 330,000 | 13,200,000 |
| Jumla | **350** | | **259,424,470** | | **128,040,000** |
| **Tofauti katika gharama ya C40 na C25 = 259,424,470 - 128,040,000** | | | | | **131,384,470** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kuhusu makisio ya gharama za ujenzi wa matangi ya maji*

Jadweli hapo juu linaonesha ZAWA alitumia zege daraja la C40 katika ujenzi wa ngazi na kugharimu kiasi cha shilingi 259,424,470 ukilinganisha na utumiaji wa zege daraja la C25 ambapo gharama za ujenzi zimepungua hadi kufikia shilingi 128,040,000, hivyo kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 131,384,470 fedha ambayo ingeweza kuokolewa na ZAWA pindipo pangekuwa na uangalifu katika matumizi ya vigezo vya ujenzi wa matangi hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kwamba miundombinu ya ujenzi wa matangi ya maji inafanywa kwa mujibu wa makubaliano ya mikataba ili kufikia kiwango kinachokubalika na kupelekea upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi.

### 11.3 Dosari juu ya Usimamizi wa Mkataba

#### 11.3.1 Kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa mafunzo ya mradi 200,000,000

Kifungu nambari 6.2 (b) cha Masharti ya Jumla ya Mkataba cha huduma ya ushauri kwa ajili ya utoaji wa usanifu juu ya usimamizi wa ujenzi wa matangi ya maji ya juu na ardhini kwa Unguja na Pemba kinaeleza kwamba kiasi cha mkataba kilikuwa shilingi 890,000,000 pamoja na VAT na hivyo pamoja na kiasi cha shilingi 200,000,000 zilizotumika kwa ajili ya mafunzo na gharama za uendeshaji wa mradi kwa kikosi kazi cha ZAWA.

Ukaguzi ulipitia ajenda nambari 7 inayoainisha makubaliano ya kazi za mradi na kubaini uwepo wa nyongeza ya gharama za uendeshaji wa mradi pamoja na mafunzo kwa kiasi cha shilingi 200,000,000 ambapo ilipelekea fedha hizo kuongezeka hadi kufikia kiasi cha shilingi 690,000,000 jambo ambalo limeongeza gharama za mkataba na kufikia kiasi cha shilingi 890,000,000 pamoja na VAT.

Aidha, ukaguzi ulibaini gharama za ziada katika mkataba zilisababishwa kutokana hadidu rejea namba 11. Gharama ya ziada zilikuwa kama ilivyowasilishwa katika Jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 56: Uchambuzi juu ya matumizi ya gharama za ziada**

| Namba | Kipengele | Nambari | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Bodi ya Wakurugenzi Mafunzo | 7 | 16,452,500.00 |
| 2. | Mafunzo ya Usimamizi | 18 | 12,290,500.00 |
| 3. | Posho ya kazi ya ziada kwa ufatiliaji | - | 4,913,043.48 |
| 4. | Mafunzo ya Idara ya Mipango | 7 | 10,000,000.00 |
| 5. | Ununuzi wa vishkwambi kwa Bodi ya Mkurugenzi | 6 | 12,950,000.00 |
| 6. | Ununuzi wa Kompyuta, Printa na vifaa vingine vya kielektroniki | - | 46,407,000.00 |

| Namba | Kipengele | Nambari | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 7. | Ununuzi wa vifaa vya Ofisi vya PRO | - | 50,900,000.00 |
| 8. | Matengenezo ya gari | - | 20,000,000.00 |
| | **Jumla ndogo** | | **173,913,043.48** |
| | Kodi ya VAT (15%) | | 26,086,956.52 |
| | **Jumla Kuu** | | **200,000,000.00** |

*Chanzo: Pendekezo la Matumizi ya Gharama za Ziada*

Jadweli hapo juu, linaonesha jumla ya shilingi 130,257,000.00 zilitumika kwa ajili ya shughuli ambazo hazihusiani na gharama za uendeshaji na mafunzo kama zilivyoainishwa katika hadidu rejea nambari 11 ambapo malipo haya yalifanywa kupitia ankara iliyoibuliwa na mshauri Elekezi.

Ukaguzi ulipitia matumizi ya gharama za ziada zilizohusiana na uendeshaji wa mafunzo na kubaini kujitokeza kwa malipo ya ziada ambapo ilitokana na ZAWA kushindwa kuziweka gharama hizo kupitia mpango wake wa utekelezaji wa mradi.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa uongozi wa ZAWA haukufanya tathmini ya mahitaji ili kubaini mapungufu ya watumishi kwa mahitaji ya kuwajengea uwezo wa mafunzo.

Hali hii ya ukosefu wa mipango ya matumizi ya gharama za ziada ilipelekea kuwepo kwa matumizi yasiyo na uhalali na yasiyopangwa kwa fedha ambazo zinaweza kutumika kwa lengo la kupunguza tofauti nyingine za gharama katika utekelezaji wa mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unatayarisha mipango ya kutosha ya utekelezaji wa mradi pamoja na kuhakikisha kwamba unafanya tathmini ya kutosha inayohusiana na mahitaji halisi ya wafanyakazi ili kuepusha kujitokeza kwa matumizi ya ziada yanayoweza kuepukika.

# SURA YA KUMI NA MBILI



# 12.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSIANA NA HUDUMA YA USHAURI ELEKEZI NA USIMAMIZI WA UKARABATI NA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAMBAZAJI MAJI

## 12.1 Utangulizi

Sura hii inahusu matokeo ya ukaguzi juu ya Huduma ya Ushauri elekezi kuhusiana na Usanifu na Usimamizi wa Ukarabati na Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji. Maelezo ya taarifa ya mkataba kwa huduma za ushauri kwa ajili ya utafiti, usanifu na usimamizi yamewasilishwa katika Jadweli hapo chini.

Mamlaka ya Maji Zanzibar iliingia mkataba na Chuo cha Maji cha Dar-es-Salaam wenye nambari SMZ/IMF/No.104/CS/RNCT/2021/2022/01-A wa tarehe 27 Juni, 2022 kwa thamani ya shilingi 704,025,000 pamoja na VAT kuhusiana na huduma za Ushauri elekezi kuhusiana na ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji. Hali halisi ya mkataba huo ni kama invyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 57: Taarifa za Mkataba kwa Huduma ya Ushauri na Usimamizi**

| **Kipengele cha Mkataba** | **Huduma ya ushauri kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa usambazaji mpya wa maji** |
|---|---|
| Nambari ya Mkataba | SMZ/IMF/N o.104/CS/RNCT/2021/2022/01-A |
| Jina la Mkandarasi | M/S Chuo cha Maji cha Dar-es-Salaam |
| Tarehe ya Kusaini Mkataba | Juni 27, 2022 |
| Tarehe ya kuanza kazi | 11 Julai, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza ya Ufanisi | 11 Julai, 2022 |
| Muda wa Mkataba | Miezi, 12 |
| Tarehe ya awali ya kukamilika | 11 Julai, 2023 |
| Tarehe halisi ya Kukamilika | |
| Thamani ya Mkataba wa awali pamoja na VAT | shilingi 704,025,000 |
| Jumla ya kiasi cha Mkataba uliorekebishwa na VAT | Hakuna |
| Maendeleo ya Kazi (%) hadi Julai, 2023 | |
| Maendeleo ya Malipo (%) hadi Julai, 2023 | Asilimia 25 |
| Kuchelewa kukamilika kwa kazi | |
| Riba ya kuchelewa kwa malipo | Hakuna |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka katika Hati za Mkataba, 2023*

Wakati wa ukaguzi masuala yafuatayo yanayohusiana na huduma za ushauri elekezi kuhusu ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji yalizingatiwa kama ifuatavyo: -

### 12.1.1 Kukosekana kwa ushindani katika Mchakato wa upatikanaji wa Mshauri Elekezi

Kifungu nambari 68(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016, inazitaka taasisi za umma kuhakikisha kuwa wanaweka ushindani katika kuwapata wakandarasi.

Ukaguzi ulibaini kuwa katika mchakato wa mshauri elekezi hakukuwa na ushindani ambapo ilipelekea zabuni hiyo kutofanyiwa tathmini na hivyo ilifanya uteuzi wa chanzo kimoja tu cha zabuni kutokana na mzabuni huyo kualikwa moja kwa moja bila uwepo wa ushindani wa mzabuni mwengine. Hali hii imepelekea uwepo wa upendeleo uliochangiwa na kutokuwepo kwa udhibiti mzuri katika mchakato wa kumpata mshauri elekezi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kwamba wanazingatia Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 katika mchakato wa kumpata mshauri elekezi ili kuepusha uwepo wa upendeleo miongoni mwa wazabuni wanaotambulika kisheria.

## 12.2 Dosari katika Usimamizi wa Ushauri Elekezi

### 12.2.1 Kuchelewa kwa utolewaji wa huduma za Ushauri elekezi katika miundombinu ya Usambazaji wa Maji

Kifungu nambari 14.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaeleza kwamba muda wa mkataba ni miezi kumi na mbili (12) baada ya kuwasilisha Mpango kazi wa mshauri elekezi pamoja na cheti cha Bima.

Pia, kulingana na kifungu nambari 13.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinaeleza kwamba huduma hiyo ilipaswa kufanyika ndani ya wiki mbili baada ya kusainiwa kwa mkataba tarehe 11 Julai, 2022.

Ukaguzi ulipitia hati za malipo pamoja na ripoti za utekelezaji wa mradi na kubaini kazi za usambazaji wa miundombinu ya maji imetekelezwa chini ya usimamizi wa mshauri elekezi licha ya kumalizika kwa muda wa mkataba wa miezi 12 ambapo ukaguzi ulithibitisha kwamba utekelezaji wa mradi kwa mujibu wa mkataba ulikua ni asilimia 100 na maendeleo ya utekelezaji wa kazi hiyo ilifikia asilimia 55 ingawa ukaguzi haukuweza kuthibitisha muda ulioongezwa kwa mshauri elekezi.

Kukosekana kwa ufanisi katika utekelezaji wa mradi kulitokana na kutokuwepo kwa usimamizi imara unaotokana na mshauri elekezi hali iliyopolekea kuchelewa kupatikana kwa huduma ya maji kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unaweka usimamizi mzuri kwa washauri elekezi katika utekekelezaji wa miradi ya maendeleo ili iweze kukamilika kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa kwa wananchi.

### 12.2.2 Ucheleweshwaji wa Malipo kwa Huduma za Ushauri

Kifungu nambari 41.2 cha mkataba wa huduma ya ushauri kilibainisha utaratibu wa awamu za malipo ya utekelezaji wa mradi kama ifuatavyo;

**Jadweli Nambari 58: Utaratibu wa awamu za Malipo ya utekelezaji wa mradi**

| Asilimia | Mahitaji |
|---|---|
| **Awamu ya I** | |
| 25% | Baada ya kuwasilisha mpango kazi |
| 35% | Baada ya kuwasilisha ripoti ya usanifu wa mradi |
| **Awamu ya II** | |
| 30% | Wakati wa kuanza kwa kazi ya usimamizi |
| 10% | Baada ya kukamilika kwa kazi na uwasilishaji wa ripoti ya mwisho inayokubalika pamoja na mchoro |

Hata hivyo, kwa kuzingatia ukaguzi wa hati za malipo namba 200036 ilibainika kuwa mshauri alikuwa tayari ameshalipwa asilimia 25 ya kiasi cha mkataba ambayo ilikuwa ni malipo kwa kazi ya usanifu.

Aidha, pamoja na kwamba ripoti ya usanifu iliweza kuwasilishwa kwa wakati ukaguzi umebaini malipo yanayohusiana na kazi hiyo ambayo ni sawa na asilimia 35 hayakulipwa kwa wakati. Vilevile malipo ya asilimia 30 ambayo yalipaswa yalipwe kwa ajili ya usimamizi wa kazi za mradi malipo hayo hayakulipwa kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unafanya malipo kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba ili kuepusha kujitokeza kwa malipo ya tozo ya adhabu jambo ambalo linaweza kupelekea ongezeko la gharama za mradi pamoja na kutokukamilika mradi kwa wakati.

# SURA YA KUMI NA TATU



# 13.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USAMBAZAJI WA MABOMBA YA HDPE KWA LOTI 1 NA LOTI 2

## 13.1 Utangulizi

Kazi ya usambazaji wa mabomba ya HDPE na vifaa vya HDPE imegawanywa katika loti mbili. Loti hizi ni loti 1 kwa usambazaji wa mabomba ya HDPE na loti ya 2 kwa usambazaji wa vifaa vya HDPE. Kwa bomba la HDPE muuzaji alitakiwa kusambaza bomba la PN 10 la ukubwa tofauti kuanzia kipenyo cha 53mm hadi kipenyo cha 315mm na urefu wa jumla wa mita 318,879. Kwa vifaa vya HDPE muuzaji alitakiwa kutoa jumla ya vifaa vya bomba la 150,001 PN16 HDPE.

Kazi hiyo ilitekelezwa kupitia njia ya manunuzi ya kawaida ambapo Mamlaka ya Maji Zanzibar iliandaa mchanganuo wa mahitaji. Kazi hiyo ilifanywa na wasambazaji wawili. Wasambazaji walitakiwa kusambaza mabomba na vifaa vya HDPE hadi ZAWA.

Majadweli hapo chini yanayonesha taarifa ya mikataba ya Usambazaji wa Mabomba na vifaa vya HDPE.

**Jadweli Nambari 59: Taarifa za mkataba wa usambazaji wa mabomba ya HDPE Loti ya 1**

| Kipengele | Taarifa katika Mkataba |
|---|---|
| Nambari ya Mkataba | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/01 |
| Jina la Msambazaji | M/S Moona Noor Manufacturing and Trading LLC |
| Tarehe ya Kusaini mkataba | 29 Januari, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza kazi | 29 Januari, 2022 |
| Muda wa Mkataba | Hakuna muda wa mkataba ulioelezwa |
| Tarehe ya awali ya kukamilika kazi | |
| Tarehe iliyorekebishwa ya Kukamilisha kazi | Hakuna |
| Jumla ya kiasi cha Mkataba cha awali bila VAT | Dola za Marekani (USD) 2,535,548.25 |
| Kiasi cha Mkataba uliorekebishwa pamoja na VAT | Hakuna |
| Maendeleo ya Kazi (%) hadi Julai, 2023 | |
| Maendeleo ya malipo (%) hadi Julai, 2023 wakati Ukaguzi ulifanyika | Asilimia 100 |
| Kuchelewa kukamilika kwa kazi hadi Julai 2023 | - |
| Riba ya kuchelewa kwa malipo | Hakuna |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati ya Mkataba na hati ya Malipo uliofanywa na Wakaguzi*

### Jadweli Nambari 60:Taarifa za Mkataba kwa ajili ya Usambazaji wa vifaa vya HDPE Loti 2

| Kipengele | Taarifa katika Mkataba |
|---|---|
| Nambari ya Mkataba | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/01 |
| Jina la Msambazaji | M/S GAIA GLOBE ITH. IHR INONU 0504/3 Turkey |
| Tarehe ya Kusaini mkataba | 29 Januari, 2022 |
| Tarehe inayotakiwa ya Kuanza kazi | 29 Januari, 2022 |
| Muda wa Mkataba | Hakuna muda wa mkataba ulioelezwa |
| Tarehe ya awali ya kukamilika kazi | Hakuna |
| Tarehe iliyorekebishwa ya Kukamilisha kazi | Hakuna |
| Jumla ya Kiasi cha awali cha Mkataba pamoja na VAT | USD 769,607.76 |
| Jumla ya kiasi cha Mkataba Uliorekebishwa pamoja na VAT | Hakuna |
| Maendeleo ya Kazi (%) hadi Julai, 2023 | |
| Maendeleo ya malipo (%) hadi Julai, 2023 wakati Ukaguzi unafanyika | Asilimia 100 |
| Kuchelewa kukamilika kwa kazi hadi Julai, 2023 | - |
| Riba kwa malipo yaliyochelewa | Hakuna |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Hati ya Mkataba na Hati za Malipo*

Kwa hivyo, ukaguzi ulitathmini ikiwa ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine za usambazaji wa maji ulitekelezwa kwa ufanisi kwa kuzingatia Mipango, wakati, gharama na ubora. Tathmini hiyo inashughulikia upangaji wa mradi, ununuzi, usimamizi wa muda, gharama na ubora kama ilivyoelezwa chini.

## 13.2 Upangaji wa Miradi Usiyoridhisha

Mbinu bora zinahitaji miradi yoyote ya maji kutekelezwa kupitia hatua zifuatazo za utafiti wa upembuzi yakinifu, hatua ya usanifu, hatua ya ununuzi na hatua za utekelezaji. Utafiti wa upembuzi yakinifu na hatua ya usanifu imewekwa pamoja katika hatua ya kupanga miradi.

Katika mapitio ya kumbukumbu za mradi, ukaguzi ulibaini kuwa ZAWA iliingia mkataba na wauzaji kusambaza mabomba ya HDPE na vifaa vya HDPE. Lakini hakukuwa na upembuzi yakinifu wowote ambao ulibainika kuwa ulifanyika ili kubaini idadi ya watu wa eneo hilo waliotakiwa kupewa maji, vyanzo vya maji, utabiri wa mahitaji ya maji wakati wa usanifu wa muda wa miradi, makadirio ya gharama za miradi na ukubwa wa miundombinu mbalimbali inayotarajiwa kujengwa wakati wa utekelezaji wa miradi kama vile matangi ya kuhifadhi maji.

Vile vile ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na ripoti ya usanifu iliyopatikana inayoonyesha ukubwa wa tofauti ya mabomba yaliyonunuliwa.

Wakati wa ukaguzi, ZAWA ilitoa mchoro kwa mkaguzi ambao ulisemekana kutumika kuonyesha wingi wa bomba. Hata hivyo, mchoro huo haukuwa na vipimo ambavyo vilikuwa na ukubwa wa mabomba. Hii inafanya vigumu kwa mkaguzi kufanya ukaguzi juu ya michoro na wingi wa mabomba na vifaa ambapo ZAWA aliingia mkataba na wauzaji. Mfano wa michoro iliyowasilishwa kwa wakaguzi ni kama mchoro inavyoonekana katika picha hapo chini:-

**Picha Nambari 7: Dondoo ya Mchoro uliotumiwa kutoa Wingi wa Bomba**




*Chanzo: Dondoo ya michoro iliyowasilishwa*

Kama inavyoonyesha taswira kutoka katika mchoro hapo juu kutumika kuandaa kiasi cha bomba zitakazonunuliwa inaonesha tu saizi ya bomba inayohitajika. Mchoro hauonyeshi urefu wa bomba inayohitajika kwa saizi tofauti ya mabomba.

Kutokana na dosari iliyobainika hapo juu kunaweza kupelekea kujiotokeza kwa athari zifuatazo:-

a) Kuna hatari ya kuweka idadi ndogo ama idadi kubwa ya mabomba na vifaa vyake kwa sababu haijulikani kiasi cha idadi kilichopatikana.
b) Kuna hatari ya kuzidi au kupungua ukubwa wa bomba kutokana na kutokujulikana kwa vipimo halisi vya bomba vilivyoandaliwa ndani ya BoQ.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unaweka mipango imara ya mradi kwa kuhakikisha kunafanyika upembuzi yakinifu kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi.

## 13.3 Dosari iliyobainika katika mikataba ya usambazaji wa mabomba na vifaa vya HDPE

### 13.3.1 Timu ya tathmini kutokujumuisha wataalamu wanaohitajika

Kanuni nambari 118(2) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020, inaitaka Kamati ya Tathmini kuwa na wajumbe wenye ujuzi, maarifa na uzoefu unaoendana na mahitaji ya manunuzi ambayo ni pamoja na utaalamu husika wa kiufundi, utaalamu wa manunuzi, utaalamu wa uchambuzi wa usimamizi wa fedha, utaalamu wa kisheria, au mwakilishi kutoka idara ya mtumiaji.

Mapitio ya ripoti ya tathmini ya zabuni ya usambazaji wa mabomba na vifaa, ukaguzi ulibaini kuwa sio wataalamu wote wanaohitajika walihusika katika timu ya tathmini.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha inafuata Kanuni ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2020 kwa kuhakikisha kila mtaalamu anayehitajika kuwa sehemu ya tathmini anateuliwa.

### 13.3.2 Utolewaji wa Zabuni kwa wazabuni wasio na sifa

Kanuni nambari 118(8)(9) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma 2020, inahitaji kabla ya tathmini ya kina ya zabuni, Kamati ya Tathmini kufanya uchunguzi wa awali wa zabuni ili kubaini kama kila zabuni inakidhi vigezo kwa mujibu wa mahitaji ya nyaraka za zabuni, dhamana zinazohitajika zimetolewa, nyaraka zimesainiwa vizuri, na kwa utaratibu, na nakala za usajili wa kufanya biashara zimetolewa.

Vifungu nambari 28.1, 28.2 na 28.5 vya maagizo kwa mzabuni juu ya ufunguzi wa zabuni katika Nyaraka za zabuni inahitaji kabla ya tathmini ya kina ya zabuni, Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma itaamua kama kila zabuni imekidhi vigezo vya ustahiki, imesainiwa ipasavyo, inaambatanishwa kwa dhamana zinazohitajika na imekidhi vigezo kwa mujibu wa hati ya zabuni.

Zabuni zilizotakiwa kuzingatiwa ni zile zilizokidhi vigezo na masharti yote ya mkataba, masharti na maelezo ya hati ya zabuni kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa. Ikiwa zabuni haitakidhi vigezo vilivyowekwa haitakubalika na kukataliwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za ununuzi na uondoshwaji wa mali za umma.

Kwa mujibu wa mapitio ya ripoti za tathmini na nyaraka za mikataba ukaguzi ulibaini kuwa mkataba ulitolewa kwa wazabuni ambao hawakuwa na sifa wakati wa tathmini kutokana na kushindwa kurejesha hati ya zabuni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 61: Uchambuzi wa Hali ya Wazabuni waliohusika kupewa Tuzo ya Mkataba**

| Nam | Jina la Mkataba | Nambari ya Mkataba | Jina la Msambazaji aliyepewa tuzo | Hali ya majibu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Usambazaji wa Mabomba ya HDPE Loti 1, | SMZ/IMF/104/G/ RNCT/2021/2022/01 | M/s Moona Noor Manufacturing and Trading LLC | Haikujibiwa |
| 2. | Usambazaji wa vifaa vya HDPE Loti | SMZ/IMF/104/G/ RNCT/2021/2022/01 | M/s GAIA GLOBE ITH. IHR | Haikujibiwa |

*Chanzo: Uchambuzi wa ripoti ya tathmini na Hati za Mkataba*

Jadweli hapo juu linaonesha kuwa wasambazaji wawili ambao walipewa mkataba hawakuwa na sifa ambao ni M/s Moona Noor Manufacturing and Trading LLC na M/S Gaia Globe Ith. Ihr Inonu 0504/3 Turkey.

Kutokana na mchakato wa uteuzi wa wazabuni uliofanyika imebainika kuwepo kwa mapungufu mbali mbali kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 62: Eneo ambalo mzabuni hakuwajibika kupewa tuzo ya mkataba**

| Namba | Jina la Mzabuni | Dosari zilizobainika |
|---|---|---|
| 1. | M/s Moona Noor Manufacturing and Trading LLC | Tax Clearance and Power of Attorney |
| 2. | M/s GAIA GLOBE ITH.IHR | Company registration Certificate, Copy of Audited Financial Statement, Valid Business Licence, Experience at supplying similar material, Tax Clearance, Bid Security, Power of Attorney and Manufacturer Authorisation Certificate |

*Chanzo: Ripoti ya Tathmini*

Kutokana na jadweli hapo juu imebainisha kuwa wasambazaji walioainishwa hawakuwa na sifa zilizohitajika kwa ajili ya kupewa tuzo ya zabuni wakati wa tathmini jambo ambalo limepelekea kuongezeka kwa gharama zilizotokana na uingizaji wa mizigo bandarini.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha tuzo za mkataba zinatolewa kwa wazabuni ambao wamekidhi sifa na vigezo vya zabuni vinavyohitajika.

### 13.3.3 Uhaba wa nyaraka za Zabuni

Masharti ya jumla ya mkataba hutoa taarifa ambazo hazijakamilika na ukamilifu wake unahitaji kutolewa katika masharti maalum ya mkataba.

Ukaguzi ulipitia nyaraka za zabuni na kubaini kuwa taarifa muhimu katika kipengele cha Masharti Maalum ya Mkataba zilitaka nyaraka zijazwe ambapo imebainika dosari ya kutokujazwa kwa taarifa hizo. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 63: Dosari zilizobainika katika nyaraka za mkataba**

| Nam. | Jina la Mkataba | Nambari ya Mkataba | Dosari zilizobainika katika mkataba |
|---|---|---|---|
| 1. | Usambazaji wa Mabomba ya HDPE Loti 1, | SMZ/IMF/104/G/ RNCT/2021/2022/01 | Eneo la Mradi halikuelezwa, utaratibu wa malipo ulikuwa katika makundi matatu ambayo ni Malipo ya awali, malipo Baada ya Usafirishaji, na malipo baada ya kukubali Zabuni zinazotolewa lakini asilimia ya malipo haikuelezwa na eneo la kujaza asilimia inayohitajika lilikuwa tupu (haikujazwa). |
| 2. | Usambazaji wa vifaa HDPE Loti 2 | SMZ/IMF/104/G/ RNCT/2021/2022/01 | Eneo la Mradi haikuelezwa, utaratibu wa malipo ulikuwa katika makundi matatu ambayo ni Malipo ya awali, malipo Baada ya Usafirishaji, na malipo baada ya kukubali Zabuni zinazotolewa lakini asilimia ya malipo haikuelezwa na eneo la kujaza asilimia inayohitajika lilikuwa tupu (haikujazwa). |

*Chanzo: Hati ya Zabuni*

Kutokana na dosari zilizobainishwa hapo juu kunaweza kukapelekea uwezekano wa mkandarasi kupandisha bei ya mkataba kwa lengo la kufidia tofauti ya baadhi ya bei za wakandarasi zilizowasilishwa kutokana na kutokujulikana kwa utaratibu wa malipo utakaofanyika jambo ambalo linaweza kupelekea kupunguza ushindani wa wazabuni wengine wanaotarajiwa kushiriki katika zabuni hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha Masharti yote ya Mkataba yanajazwa ipasavyo kwa mujibu wa utaratibu ili kuepusha kujitokeza kwa vitendo vya udanganyifu.

### 13.3.4 Kutojumuisha gharama za kutoa mzigo bandarini na gharama za usafirishaji hadi ZAWA

Kwa mujibu wa kifungu nambari 15.6 (i) cha hati ya zabuni kinaeleza kwamba bei iliyonukuliwa ilitakiwa kuzingatia utoaji wa mzigo mpaka katika maghala kama ilivyoainishwa katika mkataba.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya nyaraka za mkataba na kubaini kwa mujibu wa barua za kukubali kutoka kwa wasambazaji ambayo ni sehemu ya mkataba, barua hizo zilisisitiza kuwa bei yao iliyonukuliwa ni (CIF) mpaka bandari ya Zanzibar na haijumuishi kibali cha ushuru cha Zanzibar, Kodi na Usafiri wa Ndani kwenda Ofisi Kuu ya ZAWA. Hii inaonesha kwamba wasambazaji waliunda masharti yao wenyewe kinyume na kile kilichokuwa katika hati ya zabuni ambayo ilihitaji mzabuni kuufikisha mzigo katika Ofisi Kuu ya ZAWA. Wasambazaji hawa walitakiwa kutoshinda zabuni kwani hawakukidhi mahitaji ya matangazo ya zabuni yaliyowekwa katika Hati za Zabuni.

Kutokana na dosari ya upungufu wa nyaraka za mkataba ukaguzi umebaini dosari hiyo imesababishwa na uwepo wa mapitio hafifu ya taarifa zilizowasilishwa na mkandarasi ili kuhakikisha kuwa wanaweka kile kinachohitajika katika nyaraka za zabuni kabla ya kusaini mkataba ambapo ilisababisha gharama za ziada kwa ZAWA kwa gharama za kutoa mzigo, Kodi na Usafiri wa ndani hadi Ofisi Kuu ZAWA jambo ambalo kwa mujibu wa hati ya mkataba ZAWA hakuhusika na ubebaji wa gharama za utoaji na usafirishaji wa mabomba hayo. Kufanya hivyo ni kuisababishia Serikali kuingia gharama zisizo na tija.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha mahitaji yaliyotolewa katika hati ya zabuni yanatekelezwa kikamilifu na mkandarasi ambaye anapewa mkataba vyenginevyo ni vyema kusimamia urejeshwaji wa gharama kwa mkandarasi atakaeshindwa kutekeleza matakwa ya mkataba.

### 13.3.5 Kuongezeka kwa Malipo ya awali tofauti na ile iliyo katika Hati za Zabuni

Kulingana na hati za zabuni malipo ya awali yalitakiwa kuwa asilimia 10 ya bei ya mkataba na kiwango cha juu cha malipo ya awali kilikuwa asilimia 15 ya bei ya mkataba.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya nyaraka za mkataba na kubaini kwamba asilimia ya malipo ya awali yaliyowasilishwa katika nyaraka za zabuni na katika nyaraka za mkataba hazikuwa sahihi. Jadweli hapo chini linaonesha tofauti ya asilimia ya malipo ya awali katika nyaraka za zabuni na nyaraka za mkataba.

**Jadweli Nambari 64: Tofauti katika asilimia ya malipo ya awali katika hati za zabuni na hati za mkataba**

| Nam. | Jina la Mkataba | Nambari ya Mkataba | Asilimia ya juu ya malipo ya awali katika hati ya zabuni | Asilimia ya Malipo ya awali katika Hati ya Mkataba | Asilimia ya ziada katika mkataba |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Usambazaji wa Mabomba ya HDPE Loti 1, | SMZ/IMF/104/G/ RNCT/2021/2022/01 | 15 | 50 | 35 |
| 2. | Usambazaji wa vifaa vya HDPE Loti | SMZ/IMF/104/G/ RNCT/2021/2022/01 | 15 | 50 | 35 |

*Chanzo: Nyaraka za Zabuni na Hati za Mkataba*

Jadweli hapo juu linaonesha kuwa katika miradi miwili kati ya mitatu, malipo ya awali katika nyaraka za zabuni ambapo tofauti na zile zilizo katika hati za mkataba kwa asilimia 35 zaidi ya mahitaji.

Ukaguzi ulibaini uwepo wa dosari hiyo ulisababishwa na wakandarasi kupitia nyaraka za hati ya mkataba bila kuzingatia kipengele kilichotolewa katika nyaraka za zabuni jambo ambalo limepelekea kuongezeka kwa gharama za malipo ya awali pamoja na kujitokeza kwa waombaji wachache kutokana na uwepo wa kiasi kidogo cha malipo ya awali yaliyotolewa katika hati ya zabuni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unaweka asilimia ya malipo ya awali katika hati ya zabuni na katika hati za mkataba ili kuepusha kujitokeza malalamiko kwa baadhi ya wazabuni ambao wameshindwa kuwasilisha hati za zabuni kutokana na kutokuoneshwa kwa malipo ya awali katika hati ya zabuni zilizotangazwa.

### 13.3.6 Kupunguza kiasi cha dhamana ya utendaji kazi katika nyaraka za mkataba

Kifungu nambari 9.1 cha masharti maalum katika hati ya zabuni kinahitaji kiasi cha dhamana ya utendaji kazi kuwa asilimia 20 ya bei ya mkataba.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya nyaraka mbali mbali za mkataba na kubaini kuwa kiasi cha dhamana ya utendaji kazi kilichowasilishwa kilikuwa chini ya asilimia 20 iliyobainishwa katika bei ya mkataba.

Jadweli hapo chini linaonesha asilimia ya dhamana ya utendaji kazi katika nyaraka za zabuni na ambazo zimeingizwa kwenye nyaraka za mkataba.

**Jadweli Nambari 65: Asilimia ya Dhamana ya Utendaji Kazi katika Zabuni na katika Mkataba5**

| Nam. | Jina la Mkataba | Nambari ya Mkataba | Asilimia katika Waraka wa Zabuni | Asilimia katika Hati ya Mkataba |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Usambazaji wa Mabomba ya HDPE Loti 1, | SMZ/IMF/104/G/ RNCT/2021/2022/01 | 20 | 10 |
| 2. | Usambazaji wa vifaa vya HDPE Loti 2 | SMZ/IMF/104/G/ RNCT/2021/2022/01 | 20 | 10 |

*Chanzo: Hati za Mkataba na Hati za Zabuni*

Kupunguza kiasi cha asilimia ya dhamana ya utendaji kazi katika hati ya mkataba kutoka kwa kile kilichohitajika wakati wa zabuni kunaweza kupelekea kukosekana kwa ufanisi wa kazi unaotokana na kutokuwepo kwa ushindani wa wazabuni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unaainisha asilimia ya dhamana ya utendaji kazi katika hati ya zabuni na katika hati za mkataba ili kutoa fursa kwa wakandarasi kujitokeza na kuomba hati za zabuni kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.

### 13.3.7 Kutokuwepo kwa muda wa mkataba katika nyaraka za mkataba

Muda wa mkataba ni kipengele kinachotumika kuelezea kipindi ambacho mkataba utakaa. Hii inaweza pia kueleweka kama kipindi kati ya tarehe ya kuanza mkataba na tarehe ya mwisho ya kumalizika kwa mkataba, ambayo yote kwa kawaida huainishwa ndani ya mkataba na itakubaliwa na pande zote mbili.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya nyaraka za mkataba na kubaini kutokuwepo kwa muda wa mkataba wa Usambazaji wa Mabomba ya HDPE Loti 1 na Usambazaji wa vifaa vya HDPE loti 2 kwa mujibu wa mkataba SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/01 uliosainiwa tarehe 29 Januari, 2022.

Kutokana na kukosekana kwa muda wa utekelezaji wa mkataba ni vigumu kudhibiti muda wa utekelezaji wa mkataba kwani kuna muda wa kutumika kama kumbukumbu ikiwa kuna ucheleweshaji wa wasambazaji katika utoaji wa Zabuni. Vile vile ZAWA itashindwa kutoza malipo ya ucheleweshwaji ama kushindwa kumaliza kazi kwa wasambazaji.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kila mkataba una muda wa utekelezaji wake kwa miradi ijayo.

### 13.3.8 Dosari zilizobainika baina ya mkataba na hati ya zabuni

Katika ukaguzi uliofanyika ilibainika kupitia ripoti ya tathmini ya zabuni (tender document) iliyowasilishwa kwa wazabuni ilibainisha kwamba thamani ya zabuni haitajumuisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT Exclusive) ambapo gharama ya zabuni ni sawa na Dola za Kimarekani USD 2,535,548.25 kwa ajili ya usambazaji wa mabomba ya HDPE kwa loti 1 na Dola za Kimarekani USD 769,607.76 kwa ajili ya usambazaji wa vifaa vya HDPE kwa loti 2 bila ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT Exclusive.)

Aidha, ukaguzi ulibaini kupitia hati ya mkataba (contract document) iliyowasilishwa kwa wazabuni ilibainisha kwamba thamani ya zabuni itajumuisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT Inclusive) ambapo gharama ya zabuni ni sawa na Dola za Kimarekani USD 2,535,548.25 kwa ajili ya usambazaji wa mabomba ya HDPE kwa loti 1 na Dola za Kimarekani USD 769,607.76 kwa ajili ya usambazaji wa vifaa vya HDPE kwa loti 2 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT Inclusive).

Kutokana na taarifa zilizowasilishwa baina ya hati ya zabuni na hati ya mkataba zilibainika kujitokeza kwa dosari za utendaji kwa kuripotiwa thamani ya mkataba kuwa ni sawa na thamani halisi ya hati ya zabuni jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa malalamiko wakati wa malipo kwa wazabuni.

Kutokana na dosari iliyobainika hapo juu ukaguzi ulifanya mapitio ya kumbukumbu ya nyaraka za malipo (payment vouchers) na kubaini malipo yaliyofanyika kwa wazabuni yalijumuisha makato ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) jambo ambalo lilipelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama ya mkataba ya shilingi 381,820,496 zilizolipwa Mamlaka ya Mapato (ZRA).

Dosari ya kiasi cha mkataba kilichobainishwa pamoja na hati ya zabuni ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 66: Kiasi cha mkataba kilichojumuisha VAT na kiasi cha zabuni ambacho hakijajumuisha VAT**

| Nam. | Jina la Mkataba | Nambari ya Mkataba | Kiasi cha Mkataba kilichojumuisha VAT (USD) | Kiasi cha Zabuni ambacho hakijajumuisha VAT (USD) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Usambazaji wa Mabomba ya HDPE Loti 1, | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/01 | 2,535,548.25 | 2,535,548.25 |
| 2. | Usambazaji wa vifaa vya HDPE Loti 2 | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/01 | 769,607.76 | 769,607.76 |

*Chanzo: Hati za Mkataba na Ripoti ya Tathmini*

Matokeo yake wakati wa malipo kwa wasambazaji, malipo yalifanywa kwa kuzuia VAT ambacho kiasi hiki hakikuwa sehemu ya mkataba. Kutokana na kuzuia kiasi cha VAT ambayo haikuwa sehemu ya mkataba ilisababisha ZAWA kufanya malipo ya kodi ya Ongezeko la thamani la shilingi 381,820,496 iliyolipwa kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa hati namba PV2000197 na PV2000198 kwa mkataba wa loti 1 kupitia stakabadhi namba 0992591 ya ZRA.

Kutokana na kitendo cha uongozi wa ZAWA kukata kodi ya Ongezeko la thamani kwa mzabuni kinyume na makubaliano ya hati ya zabuni imepelekea Mzabuni kuwasilisha barua yenye kumbukumbu namba MNMT/ZAWA/002-2022 ya tarehe 7 Aprili 2022 kwenda ZAWA ikidai kurejeshewa kiwango cha fedha kilichozuiwa kimakosa kinyume na makubaliano ya hati ya zabuni ambapo ZAWA ilirejesha malipo hayo kwa hati ya malipo nambari PV2000203 ya tarehe 05 Mei 2022.

Hali hii imepelekea kuathiri bajeti ya ZAWA kutokana na kufanyika malipo mara mbili na hivyo kuitia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unakuwa makini katika kuandaa hati za mikataba na zabuni ili kuepusha kujitokeza kwa mgongano wakati wa kufanyika kwa malipo pamoja kuepusha kujitokeza kwa malalamiko kwa wazabuni.

### 13.3.9 Uwepo wa malipo yaliyozuiliwa kimakosa shilingi 131,345,275

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia hati za malipo zenye kumbukumbu namba PV2000201 na PV2000200 za tarehe 24 Februari 2022 ilibainika jumla ya shilingi 131,345,275 kuwa ni kodi ya zuio iliyolipwa ZRA na TRA kupitia mkataba wa Loti 2. Kutokana na mapitio ya mkataba yalibainisha zabuni iliyotolewa haitajumuisha kodi. Hata hivyo ZAWA ilifanya zuio ya kiasi cha fedha kilichobainishwa hapo juu kimakosa jambo ambalo huwenda likapelekea kwa mzabuni kudai kurejeshewa kiwango cha fedha kilichozuiliwa.

ZAWA ilibaini uwepo wa dosari niliyoibainisha hapo juu ambapo kiasi cha malipo ya awamu ya mwisho yalifanywa kupitia hati namba PV2000287 ya tarehe 15 Oktoba 2022 bila ya uwepo wa zuio la kodi (VAT) baada ya kubaini zuio hilo limefanyika kimakosa katika cheti cha awali cha malipo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unazidisha umakini katika uandaaji na uwasilishaji wa mapitio ya rasimu ya mkataba ili kuepusha kujitokeza kwa mgongano wa taarifa zinazohusiana na kodi ya zuio.

## 13.4 Dosari katika utekelezaji wa mkataba wa mradi

### 13.4.1 Uwasilishwaji duni wa dhamana ya utendaji kazi na muuzaji

Kifungu nambari 9.1 na 9.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinahitaji, ndani ya siku thelathini (30) za kupokea taarifa ya kupatiwa Mkataba, Mzabuni aliyofanikiwa kutoa kwa Mnunuzi dhamana ya utendaji katika kiasi kilichoainishwa katika Masharti Maalumu ya Mkataba (SCC) na itakuwa katika fomu ya Dhamana ya Benki au fomu nyingine yoyote iliyoonyeshwa katika SCC.

Kutokana na mapitio ya majalada na mikataba ya mradi ukaguzi ulibaini uwepo wa dhamana tofauti uliowasilishwa mbali na ule unaohitajika katika mkataba. Uchambuzi wa mkataba uliopitiwa na dhamana wa utendaji kazi unaohitajika na usalama wa utendakazi uliowasilishwa kama inavyoonyeshwa.

**Jadweli Nambari 67 : Uchambuzi wa dhamana ya utendaji uliowasilishwa na utendaji unaohitajika katika mkataba**

| Namba | Jina la Mkataba | Dhamana inayohitajika | Dhamana iliyowasilishwa |
|---|---|---|---|
| 1. | Usambazaji wa Mabomba na Vifaa | Dhamana ya Benki isiyo na masharti ya dhamana ya Utendaji kazi | Dhamana ya Utendaji iliyotolewa na Kampuni ya Bima |
| | | Dhamana ya Benki isiyo na masharti ya malipo ya awali | Dhamana ya Benki isiyo na masharti |
| 2. | Usambazaji wa Mabomba ya HDPE Loti ya 1 | Dhamana ya Utendaji wa barua ya uhakikisho wa Utendaji | Haijawasilishwa |
| | | Dhamana ya Benki isiyo na masharti ya malipo ya awali | Haijawasilishwa |
| 3. | Usambazaji wa vifaa vya HDPE loti ya 2 | Aina za Dhamana ya Utendaji ambayo haikutajwa lakini thamani ilielezwa | Haijawasilishwa |
| | | Dhamana ya Benki isiyo na masharti ya malipo ya awali | Haijawasilishwa |
| 4. | Usambazaji wa mitambo ya kuchimbia visima (Rigs). | Dhamana ya Benki isiyo na masharti ya dhamana ya Utendaji kazi | Haijawasilishwa |
| | | Dhamana ya Benki isiyo na masharti ya malipo ya awali | Haijawasilishwa |
| 5. | Ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji kwa ZAWA Loti ya 3 | Uhakikisho wa Utendaji uliotolewa na Mkandarasi bila kutaja asilimia inayohitajika | Haijawasilishwa |

| Namba | Jina la Mkataba | Dhamana inayohitajika | Dhamana iliyowasilishwa |
|---|---|---|---|
| 6 | Ujenzi wa Vituo vya kusimamia mashine za maji kwa ZAWA Loti ya 1 na Loti ya 2 | Uhakikisho wa Utendaji uliotolewa na Mkandarasi bila kutaja asilimia inayohitajika | Haijawasilishwa |
| 7 | Kazi za Uchimbaji na Ufukiaji wa misingi kwa maeneo ya Pemba | Asilimia 10 ya bei ya mkataba lakini katika fomu haikuelezwa | Haijawasilishwa |
| 8 | Ujenzi wa matangi ya juu yaliyoinuliwa na ya ardhini | Dhamana ya Utendaji wa barua ya uhakikisho wa Utendaji | Imewasilishwa lakini imeisha muda kabla ya mwisho wa mkataba |
| | | Dhamana ya Benki isiyo na Masharti ya Malipo ya Awali | Imewasilishwa lakini imeisha muda kabla ya mwisho wa mkataba |
| 9 | Usambazaji wa Pampu za Visima vya Submersible Loti ya 1, Loti ya 2, Loti ya 3, Loti ya 4 na Loti ya 5 | Dhamana ya Utendaji wa barua ya uhakikisho wa Utendaji | Haijawasilishwa |
| | | Dhamana ya Benki isiyo na Masharti ya Malipo ya Awali | Haijawasilishwa |

Jadweli hapo juu lilionyesha kuwa mzabuni pekee aliyepewa tuzo ambaye aliwasilisha dhamana ya utendaji unaohitajika na dhamana ya malipo ya awali ilikuwa kwa ujenzi wa tangi la maji la chini na tangi la maji la juu. Hata hivyo, juu ya kuongeza muda wa dhamana zilizowasilishwa hazikufanywa upya ili kuhusisha muda ulioongezwa wakati wasambazaji wengine hawakuwasilisha Dhamana ya Utendaji unaohitajika na dhamana ya malipo ya awali.

Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa ZAWA kupitia barua yenye kumbukumbu namba ZAWA/10/9/VOL 11/59 na ZAWA/10/9/VOL 11/58 zote za tarehe 06 Septemba 2022 zilimwandikia msambazaji M/s Moona Noor Manufacturing and TRADING LLC kwa Usambazaji wa Mabomba ya HDPE Loti ya 1 na M/S Gaia Globe Ith. Ihr. Barua hiyo ilikuwa ni kuwajulisha wasambazaji kuwa asilimia 50 ya malipo (malipo ya awali) yamefanyika na kuwakumbusha wasambazaji kuhakikisha kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi kuwawezesha kulipwa baada ya kukamilika uwasilishwaji wa bidhaa. Ukaguzi umebaini kutokana na hali hiyo ni kwamba kwa kipindi cha takriban miezi saba baada ya kusainiwa kwa hati ya mkataba na kulipwa kwa malipo ya awali bila ya kuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji ZAWA ilichukuwa jukumu la kuwakumbushia wazabuni hao. Hata hivyo, hadi ukaguzi unakamilika hakuna jitihada zilizochukuliwa na wasambazaji hao.

Kutokana na dosari iliyobainishwa hapo juu kuna uwezekano mkubwa wa kujitokeza kwa dosari zifuatazo:-

**(a) Mkataba kukosa ulinzi wa kifedha**

Kwa kuwa lengo la Dhamana ya Utendaji Kazi lilikuwa kulinda ZAWA kutokana na upotezaji wa kifedha ikiwa msambazaji atashindwa kutimiza majukumu yake, ZAWA ilikuwa katika hatari ya upotezaji wa kifedha ambao unaweza kutokea kama matokeo ya wasambazaji kushindwa kukamilisha kazi au kutofikia viwango vinavyohitajika.

**(b) Vibali visivyothibitishwa kwa pampu zilizosambazwa**

Kutowasilisha Dhamana ya Utendaji Kazi kwa vifaa vya mradi wa maji vilivyotolewa kama pampu za maji zilisababisha kibali kisichothibitishwa cha pampu za maji ambazo zilipaswa kuwa miezi kumi na mbili tangu tarehe ya kuwasilisha bidhaa. Kwa sababu ya kukosekana kwa Dhamana ya Utendaji Kazi, hakukuwa na kiasi cha fedha ambacho kilichozuiliwa na ZAWA ili kugharamia gharama za ucheleweshwaji pindipo atakaposhindwa mzabuni kuwasilisha bidhaa katika kipindi cha dhamana.

### 13.4.2 Udhibiti usiofaa wa muda wa mkataba

Mbinu bora zinahitaji hati ya mkataba kuonesha kipindi cha kuanza utekelezaji wa usambazaji wa Zabuni na muda wa shughuli zake. Hii itawezesha chombo cha ununuzi kudhibiti muda ili kuhakikisha miradi inakamilika ndani ya muda uliotajwa katika mkataba.

Mapitio ya nyaraka za mkataba na faili za mradi ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na muda wa utekelezaji wa mkataba uliohitajika. Hii inaonesha wasambazaji walikuwa huru kusambaza mabomba muda wowote wanaotaka.

Zaidi ya hayo, ukaguzi wa mradi huo ulibaini kuwa hakukuwa na ripoti yoyote ya maendeleo ya mradi na hakuna ripoti yoyote ya kukamilika.

Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa ZAWA kupitia barua yenye nambari ya kumbukumbu ZAWA/10/9/VOL 11/59 na ZAWA/10/9/VOL 11/58 zote mbili za tarehe 06 Septemba, 2022 waliwaandikia wasambazaji M/s Moona Noor Manufacturing and Trading Llc kwa Usambazaji wa Mabomba ya HDPE Loti 1 na M/S Gaia Globe Ith. Ihr. Barua hiyo ilikuwa inawajuulisha wasambazaji kwamba asilimia 50 ya malipo (malipo ya awali) yamefanywa na kuwakumbusha wasambazaji kuhakikisha wanawawasilisha dhamana ya utendaji kazi ili kuwawezesha kulipwa baada ya kukamilika kwa usambazaji wa Zabuni. Hii inaonesha kuwa miezi 7 baada ya kusaini mkataba wa usambazaji wa Zabuni haukukamilika wakati mkandarasi alitakiwa kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi siku 30 baada ya kusaini mkataba.

Udhibiti wa muda usiofaa husababisha kuchelewa kwa utoaji wa huduma kwa jamii.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unaweka udhibiti wa kutosha wa muda wakati wa utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma kwa wakati.

### 13.4.3 Udhibiti usiofaa wa gharama wakati wa utekelezaji wa mkataba wa usambazaji wa mabomba na vifaa vya HDPE

Kifungu nambari 18 cha masharti maalum ya Mkataba kinahitaji malipo kufanywa kwa kuzingatia awamu za asilimia ya bei za mkataba. Hii inamaanisha kuwa malipo ya jumla yanahitajika kuwa sawa na bei za mkataba. Ukaguzi umebaini mambo yafuatayo:-

Ukaguzi ulifanya mapitio ya vocha za malipo ya wasambazaji na kubaini uwepo wa malipo yaliyofanyika zaidi kwa msambazaji kwa loti 1. Kutokana na mapitio ya mkataba huo bei ya mkataba ilikuwa USD 2,535,548.25 kwa Loti 1 bila ya VAT na USD 769,607.76 kwa Loti ya 2 bila ya VAT. Mapitio ya hati ya upokeaji wa Zabuni (Delivery Note) ilibainika msambazaji kwa Loti 1 kwa mabomba ya HDPE alisambaza kiasi chote kinachohitajika cha bomba ambacho kilikuwa na jumla ya mita 318,879. Pia msambazaji alisambaza jumla ya vifaa 150,000 kati ya 150,001 vinavyohitajika. Kifaa ambacho hakikusambazwa kama ripoti ya upokeaji inavyosema kilikua ni HDPE Kipunguzaji PN10 ambayo gharama yake ilikuwa Dola za Marekani 11.75. Ukaguzi ulifanya uchambuzi wa kiasi kilicholipwa ambacho kinawasilishwa katika Jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 68: Uchambuzi wa Kiasi kilicholipwa kwa msambazaji kwa loti ya 1 na loti ya 2**

| Tarehe | Hati ya Malipo | Kiasi kilicholipwa (Tsh) (A) | Kiwango cha ubadilishaji fedha (B) | Kiasi kilicholipwa (USD) (A/B) |
|---|---|---|---|---|
| 24-Feb-22 | PV2000196 | 2,494,560,571.00 | 2,309.00 | 1,080,364.04 |
| 29-Juni-22 | PV2000237 | 595,093,186.01 | 2,347.00 | 253,554.83 |
| 05-Mei-22 | Ililipwa na Wizara ya Fedha | 2,735,823,492.00 | 2,309.00 | 1,184,852.10 |
| 01-Machi-22 | PV2000203 | 50,909,399.00 | 2,309.00 | 22,048.25 |
| **Jumla ya malipo yaliyofanyika Loti ya 1 (Dola za Marekani)** | | | | **2,540,819.21** |
| 15-Okt-22 | PV 2000287 | 896,593,040.00 | 2,330 | 384,803.88 |
| 24-Feb-22 | PV 2000199 | 757,166,884.00 | 2,309 | 327,919.83 |
| **Jumla ya malipo yaliyofanywa Loti ya 2 (Dola za Marekani)** | | | | **712,723.71** |

*Chanzo: Hati ya Malipo*

Jadweli hapo juu linaonesha kuwa jumla ya malipo yaliyofanyika kwa msambazaji kwa loti 1 ilikuwa **USD 2,540,819.21** wakati kiasi cha jumla ya mkataba wake ilikuwa **USD 2,535,548.25.** Hii inaonesha uwepo wa malipo ya ziada ya **USD 5,270.96** wakati faili ya mradi haijaonyesha upeo wowote wa kazi za ziada.

Aidha, jadweli ilionyesha kuwa kwa mkataba wa loti ya 2 msambazaji alilipwa kiasi cha dola za Marekani 712,723.71 wakati mkataba wake ulikuwa kiasi cha USD 769,607.76 bila VAT ambapo inaonesha uwepo wa malipo pungufu kwa USD 56,884.05. Upungufu huo ulibainika kuwa ni kiasi cha fedha kilichozuiliwa kimakosa kutokana na mkataba kukatwa malipo ya kodi ya zuio kinyume na uhalisia. Kiasi hicho kilizuiliwa kwenye malipo nambari 1 kupitia hati nambari PV 2000201 na PV 2000200 ambayo iliwasilishwa TRA na ZRA.

Hata hivyo pamoja na uwepo wa uzuwiaji wa fedha hizo kimakosa ukaguzi umebaini mzabuni wa loti 2 alishamaliza utekelezaji wa mkataba wake ingawa kifaa cha aina ya HDPE Kipunguzaji PN10 chenye gharama ya USD 11.75 kilikuwa bado hakikuwasilishwa.

Pia ukaguzi ulibaini kuwa nje ya mkataba ZAWA ilitumia gharama za ziada kutokana na tozo za barua ya dhamana ya kupata mkopo benki (Letter of Credit) na Benki ya Watu wa Zanzibar Limited kwa mkataba wa loti 1 unaofikia kiasi cha shilingi 9,038,090.71 zilizolipwa kupitia nambari ya hati ya malipo PV2000237 ya tarehe 29 Juni 2022. Hakukuwa na mfuko wa fedha wowote ambao ulitengwa kwa barua ya dhamana ya kupata mkopo lakini katika kipengele cha masharti maalum cha mkataba kifungu cha 18. Ilihitajika malipo ya mwisho (asilimia 10 ya bei ya mkataba) kulipwa kupitia barua ya dhamana ya kupata mkopo benki.

Kutokana na maelezo ya hapo juu ukaguzi umebaini uwepo wa athari zifuatazo:-

(a) Malipo yaliyolipwa zaidi kiasi cha USD 5,270.96 kwa mkataba wa loti 1 kutokana na maandalizi duni ya malipo.

(b) Malipo yaliyolipwa chini ya kiwango kiasi cha USD 56,376.29 (Kiasi kilicholipwa chini ya kiwango USD 56,884.05 ukitoa kiasi cha fedha kilicholipwa ambacho Zabuni haikusambazwa cha USD 11.75, ukitoa USD 496.01 ambazo zina makosa katika hati za makisio ya ujenzi (BoQs) kwa mkataba wa loti 2.

(c) Ongezeko la gharama za miradi kutokana na Barua ya dhamana ya mkopo wa benki (Letter of Credit) yenye thamani ya shilingi 9,038,090.71

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha mikataba inaandaliwa na kupitiwa vya kutosha ili kuepuka mkataba kuwa na makosa. Vile vile kufanya tathmini ya kutosha ya malipo ili kuepuka malipo ya ziada kwa wazabuni.

### 13.4.4 Kutokujitosheleza kwa ubora wa udhibiti wa vipimo kwa mujibu wa vigezo na masharti ya mkataba

Kifungu nambari 5.2 cha Vigezo vya Kiufundi katika hati ya zabuni kinahitaji mzabuni kuwasilisha nakala tano za vyeti zilizosainiwa zinazoonesha vipimo na matokeo ya vipimo hivyo kama inavyohitajika. Hata hivyo nakala hizo zinatakiwa kuonyesha kiwango halisi kilichopatikana kutokana na kipimo kwa kila kiwango kilichotumika (unit) kwa mujibu wa vigezo, na sio kuthibitisha kama ni mahitaji yametimizwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya kumbukumbu ya vyeti vya vipimo na kubaini kwamba baadhi ya vipimo vilivyofanywa havikuonesha thamani halisi ya kipimo kama kilivyoelezwa katika mkataba. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 69: Uchambuzi wa vipimo vilivyofanywa kwenye bomba lililosambazwa**

| S/N | Name of Contract | Pipe Required to be Supplied | Available Test Report |
|---|---|---|---|
| 1. | Supply of HDPE Pipes Lot 1 | 50mm HDPE Pipe 10 Bar Pressure | There is test report but value of test result in term of pressure is not Known |
| | | 63mm HDPE Pipe 10 Bar Pressure | There is test report but value of test result in term of pressure is not Known |
| | | 90mm HDPE Pipe 10 Bar Pressure | There is test report but value of test result in term of pressure is not Known |
| | | 110mm HDPE Pipe 10 Bar Pressure | There is test report but value of test result in term of pressure is not Known |
| | | 160mm HDPE Pipe 10 Bar Pressure | Hydrostatic strength the result indicated that no failure during the test. The value of test result in term of pressure is not Known |
| | | 200mm HDPE Pipe 10 Bar Pressure | Hydrostatic strength the result indicated that no failure during the test. The value of test result in term of pressure is not Known |
| | | 250mm HDPE Pipe 10 Bar Pressure | Hydrostatic strength the result indicated that no failure during the test. The value of test result in term of pressure is not Known |
| | | 315mm HDPE Pipe 10 Bar Pressure | Hydrostatic strength the result indicated that no failure during the test. The value of test result in term of pressure is not Known |
| 2. | Supply of HDPE Fitting lot 2 | 50mm HDPE Pipe 10 Bar Pressure | There is test report but value of test result in term of pressure is not Known |

*Chanzo: Mahitaji ya Ratiba ya Mkataba*

Jadweli hapo juu linaonesha kwamba vipimo vilifanyika lakini vipimo vya hydrostatic havikuweza kuonesha uhalisia wa kipimo kilichosomwa wakati wa upimaji wa mabomba ya viwango vya HDPE. Hata hivyo baadhi ya vipimo kama vile kipenyo (diameter) na upana wa mabomba uliweza kuwasilishwa.

Kwa kesi ya vifaa vya mabomba ya HDPE ukaguzi haukuweza kubaini ripoti ya majaribio iliyofanywa na kuwasilishwa jambo ambalo huwenda likapelekea kukosekana kwa uhimilivu wa msukumo wa maji katika mabomba hayo.

Kutokana na dosari zilizobainishwa hapo juu huwenda ikapelekea kujitokeza kwa athari zifuatazo:-

(a) Kutokuoneshwa kwa vipimo halisi vilivyosomwa kama vinavyohitajika katika hati ya mkataba kunatia shaka juu ya ubora wa mabomba yaliyowasilishwa.

(b) Kutowasilishwa kwa hati ya vipimo na mzabuni kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wa zabuni ya usambazaji wa vifaa vya mabomba kunatia shaka juu ya ubora kulingana na viwango vilivyohitajika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha hati ya vipimo vya ubora katika usambazaji wa vifaa zimeainisha taarifa zote zinazohitajika kwa mujibu wa masharti ya mkataba, pamoja na kuhakikisha wasambazaji wote kwenye mkataba wa usambazaji wanawasilisha cheti cha kupima ubora wa Zabuni kulingana na masharti katika mkataba ili kupata uhakika juu ya ubora wa Zabuni zinazotolewa.

# SURA YA KUMI NA NNE



# 14.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USAMBAZAJI WA MABOMBA NA VIFAA

## 14.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea taarifa za ukaguzi zinazohusiana na usambazaji wa vifaa pamoja na mabomba ambapo msambazaji alitakiwa kusambaza mabomba aina ya PN10 HDPE yenye ukubwa kuanzia inchi 6 hadi inchi 3/4. Msambazaji alitakiwa kusambaza bomba lenye urefu wa kilomita 220 kwa Unguja na kilomita 26.5 kwa Pemba.

Kazi hiyo ilitekelezwa kupitia njia ya kawaida ya manunuzi ambapo Mamlaka ya Maji Zanzibar ilifanya matayarisho ya mahitaji ya vifaa ambapo kazi hiyo ilifanywa na mzabuni mmoja kwa ajili ya uwasilishaji wa vifaa na mabomba kwa ZAWA. Hali halisi ya mkataba huo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 70: Taarifa ya mkataba wa usambazaji wa mabomba na vifaa vyake**

| Kipengele | Taarifa katika Mkataba |
|---|---|
| Nambari ya Mkataba. | SMZ/No.104/G/ICB/2020-2021/02 |
| Jina la muuzaji | M/S Simba Pipe Industries Ltd |
| Tarehe ya Kusaini mkataba | 20 Julai, 2021 |
| Tarehe ya Kuanza kazi | 20 Julai, 2021 |
| Muda wa Mkataba | Mwezi mmoja(1) |
| Tarehe ya awali ya kukamilika | 19 Agosti 2021 |
| Tarehe iliyorekebishwa ya Kukamilisha | Hakuna |
| Jumla ya kiasi cha Mkataba wa awali pamoja na VAT | shilingi 1,867,132,965.58 |
| Jumla ya kiasi cha Mkataba uliorekebishwa pamoja na VAT | - |
| Maendeleo ya Kazi (%) hadi Julai, 2023 | |
| Maendeleo ya malipo (%) hadi Julai 2023 wakati Ukaguzi ulipofanyika | Asilimia 40 |
| Kuchelewa Kukamilika kwa Kazi hadi 25 Mei 2022 Wakati malipo ya mwisho yalifanywa malipo yalikuwa hadi 40% ya bei ya Mkataba | 279 |
| Riba kwa malipo yaliyochelewa | - |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati ya Mkataba na Hati ya Malipo uliofanywa na Wakaguzi*

Kwa hivyo, ukaguzi ulitathmini ikiwa ujenzi wa vituo vya kuendeshea mashine za maji (pump control house) ulitekelezwa kwa ufanisi kwa kuzingatia Mipango, wakati, gharama, na ubora.Tathmini hiyo inashughulikia upangaji wa mradi, ununuzi, usimamizi wa wakati, gharama, na ubora kama ilivyoelezwa hapa.

## 14.2 Dosari katika hati ya mikataba

### 14.2.1 Kushindwa kusaini Mkataba ndani ya Kipindi cha Uhalali wa Zabuni

Kulingana na nyaraka za zabuni Kipindi cha uhalali wa zabuni inamaanisha kipindi kinachofuata hadi tarehe ya kufungwa na kuwasilisha zabuni ambazo bei ya zabuni na masharti ya zabuni hayatakuwa chini ya mabadiliko yoyote na mzabuni. Muda halali wa zabuni ya usambazaji wa mabomba na vifaa ulikuwa siku tisini (90).

Katika mapitio ya ripoti ya tathmini na nyaraka za mkataba ukaguzi ulibaini kuwa ufunguzi wa zabuni ulikuwa tarehe 13 Januari 2021 na mwisho wa kipindi cha uhalali wa zabuni ulikuwa 13 Aprili 2021 . Mkataba huo ulisainiwa tarehe 20 Julai 2021 ambao unaonesha kucheleweshwa kwa siku 98.

Mapitio zaidi ya kumbukumbu za mradi ukaguzi ulibaini kuwa ZAWA kupitia barua yenye nambari ya kumbukumbu ZAWA/A.10/10/106 ya tarehe 23 Aprili 2021 iliongeza uhalali wa zabuni kwa siku nyengine tisiini (90). Wakati ambapo barua ya nyongeza ya muda wa uhalali wa zabuni ilikuwa siku kumi (10) baada ya kumalizika kwa kipindi cha uhalali wa zabuni ambacho kilisambazwa kwa wazabuni wote.

Kutokana na hali hiyo, mzabuni aliefanyiwa tathmini alikubali taarifa ya tuzo na mabadiliko ya bei kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba PLASCO/ZAWA/20052021/51 ya tarehe 20 Mei 2021 pamoja na kwamba tarehe hiyo ilishapitiliza kipindi cha uhalali wa zabuni. Vile vile bei zilizopendekezwa na mzabuni aliyetathminiwa zilionekana kufikia shilingi 152,180,301.10 ukilinganisha na bei ya zabuni ya shilingi 340,464,072.50 ya mzabuni aliyewasilisha ombi la zabuni ndani ya wakati jambo ambalo limepelekea ongezeko la gharama za ziada kwa kiasi cha shilingi 188,283,771.40.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha manunuzi yanafanyika pale ambapo kuna uhakika wa fedha za utekelezaji wa mradi na kuhakikisha mkataba unasainiwa kwa kipindi cha uhalali wa zabuni.

## 14.3 Utekelezaji Usioridhisha wa Usimamizi wa Mkataba

### 14.3.1 Kuchelewa kukamilika kwa miradi kwa siku 211 bila kutoza fidia ya malipo ya ucheleweshwaji wa Zabuni (liquidated damage)

Kulingana na mkataba wa usambazaji wa vifaa vya mabomba ulipaswa kukamilika ndani ya mwezi mmoja kutoka tarehe 20 Julai, 2021 mpaka 19 Agosti, 2021.

Kifungu nambari 21 cha masharti maalum ya mkataba kiwango kinachotumika cha kufidia ucheleweshwaji ni asilimia 0.2 kwa siku moja ambapo ingepaswa kulipwa kulingana na bei ya zabuni. Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 280,069,944.84 ikiwa ni dhamana ya utendaji kazi ambazo hazijawasilishwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya kumbukumbu za mradi na kubaini kuwa hakukuwa na ripoti ambayo inaonesha muda wa mradi ulipokamilika. Vile vile imebainika malipo ya mwisho ambayo yalifanyika wakati usambazaji ulikuwa asilimia 40 ya bei ya mkataba yalifanyika mnamo 18 Machi 2022. Jambo ambalo lilipelekea ucheleweshaji wa siku 211 za utekelezaji wa mradi pamoja na kwamba hakukuwa na muda wa ziada ulioidhinishwa kwa mzabuni.

Kutokana na dosari iliyobainika hapo juu ZAWA ilitakiwa kutoza fidia ya malipo ya ucheleweshwaji wa Zabuni yenye thamani ya shilingi 280,069,944.84 ambapo hadi ukaguzi unakamalika hatukuweza kuthibitisha tozo ya fidia iliyotozwa kwa mzabuni jambo ambalo huwenda likapeleka kujitokeza kwa ucheleweshwaji wa utekelezaji wa mradi kwa wakati na hatimae kukosekana kwa tija iliyokusudiwa kwa wananchi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha mkataba unatekelezwa ndani ya kipindi cha mkataba na utekelezaji wowote wa kazi nje ya kipindi cha mkataba kutoza fidia ya ucheleweshwaji wa Zabuni kulingana na sheria na masharti ya mkataba.

### 14.3.2 Kukosekana kwa Ripoti ya Kukamilika kwa Mkataba

Kutokana na mapitio ya hati za malipo yaliyofanyika hadi kipindi cha Julai 2023 ukaguzi ulibaini jumla ya shilingi 746,313,944.63 zililipwa kwa mzabuni ambapo ni sawa na asilimia 40% ya gharama za mkataba. Aidha, ilibainika tarehe 18 Machi 2022 ni kipindi ambacho malipo ya mwisho yalifanyika ambapo baada ya malipo hayo hakukua na hati yoyote ya malipo inayohusiana na kufanyika kwa malipo hayo.

Ukaguzi ulifanya mahojiano na afisa manunuzi na kubainisha ya kwamba baada ya malipo ya asilimia 40% Mamlaka ilichukua maamuzi ya kusitisha mkataba, ingawa hakukua na usitishwaji rasmi wa mkataba na mzabuni, na wala hakukuwa na sababu zilizoelezwa kusitishwa kwa mkataba huo.

Kutokana na kukosekana kwa sababu zilizopelekea kusitishwa kwa mkataba kunaweza kupelekea kwa mzabuni kuendelea na usambazaji wa mabomba jambo ambalo huenda likapelekea kujitokeza kwa changamoto baina ya mzabuni na ZAWA.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unapoamua kuvunja mkataba unazingatia masharti ya mkataba sambamba na utayarishaji wa ripoti zilizopelekea kuvunjwa kwa mkataba ili kunusuru kujitokeza malalamiko kwa mzabuni na hatimae kuitia hasara Serikali.

# SURA YA KUMI NA TANO



# 15.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USAMBAZAJI WA PAMPU ZA VISIMA

## 15.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea taarifa za ukaguzi zinazohusiana na usambazaji wa pampu za visima ambazo ni kama ifuatavyo: -

*Supply of Assorted Submersible Bore Hole Pumps - 13 Pumps; Supply of Assorted Submersible Bore Hole Pumps - 23 Pumps; Supply of Assorted Submersible Bore Hole Pumps - 20 for Replacement Pumps in Pemba; Supply of Assorted Submersible Bore Hole Pumps - 38 Pumps for new Boreholes in Unguja and Pemba; and Supply of Assorted Submersible Bore Hole Pumps - 29 for replacement Pumps in Unguja.*

Kutokana na usambazaji wa pampu hizo ZAWA iliingia makubaliano ya Mkataba na wazabuni uligawanywa katika loti tano (5) ambapo msambazaji M/S SAN FRANSCISCO alipewa loti 1 na 4 ikiwa na jumla ya pampu 51 za kuzamisha chini ya kisima wakati M/S Pampu for Africa alipewa loti 2, 3, na 5 ikiwa ni jumla ya pampu 72 zinazoweza kuzamishwa chini ya kisima kama ilivyowasilishwa katika Jadweli hapa chini.

**Jadweli Nambari 71: Taarifa ya mkataba wa usambazaji wa pampu**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Jina la Mkataba** | Usambazaji wa Pampu (Submersible Pumps) Loti ya 1, Loti ya 2, Loti ya 3, Loti ya 3, Loti ya 4, na Loti ya 5. | | | |
| **Nambari ya Mkataba.** | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/02 | | | |
| | | | | |
| **Loti za Mikataba** | **Msambazaji aliyepewa tuzo** | **Bei ya Mkataba (Dola za Marekani)** | **Tarehe ya mkataba** | **Kipindi cha Utekelezaji** |
| Loti ya 1 | M/S Sanfransisco | 269,326 | **09/02/2022** | Haijabainishwa |
| Loti ya 2 | M/S Pumps for Africa | 436,424.63 | **09/3/ 2022** | Wiki 20 |
| Loti ya 3 | | 247,064.48 | | |
| Loti ya 4 | M/S Sanfransisco | 664,909 | **29/01/ 2022** | Haijabainishwa |
| Loti ya 5 | M/S Pumps for Africa | 676,483.12 | **09/3/ 2022** | Wiki 20 |

*Chanzo: Hati za Mikataba ya Ununuzi wa Pampu*

## 15.2 Matokeo ya ukaguzi juu ya ununuzi

Ununuzi wa Pampu 123 za kuzamisha chini ya kisima kwa ajili ya uboreshaji wa Huduma za Usambazaji Maji Zanzibar ulifanyika kupitia njia isiyo ya wazi ya zabuni (restricted tender). Katika kuanzisha ununuzi wasambazaji tisa(9) walichaguliwa na walialikwa kushiriki katika mchakato wa zabuni. Ukaguzi ulitathmini mchakato wa ununuzi na mchakato wa utekelezaji ambapo mapungufu yafuatayo yalibainishwa:

### 15.2.1 Zabuni zilitolewa kwa wazabuni wasio na sifa

Kanuni nambari 118(8)(9) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma 2020, inahitaji kabla ya tathmini ya kina ya zabuni, Kamati ya Tathmini kufanya uchunguzi wa awali wa zabuni ili kubaini kama kila zabuni inakidhi vigezo kwa mujibu wa mahitaji ya nyaraka za zabuni, dhamana zinazohitajika zimetolewa, nyaraka zimesainiwa vizuri, na kwa utaratibu, na nakala za usajili wa kufanya biashara zimetolewa.

Vifungu nambari 28.1, 28.2 na 28.5 vya maagizo kwa mzabuni juu ya ufunguzi wa zabuni katika Nyaraka za zabuni inahitaji kabla ya tathmini ya kina ya Zabuni, Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma itaamua kama kila zabuni imekidhi vigezo vya ustahiki, imesainiwa ipasavyo, inaambatanishwa kwa dhamana zinazohitajika na imekidhi vigezo kwa mujibu wa hati ya zabuni.

Zabuni zilizotakiwa kuzingatiwa ni zile zilizokidhi vigezo na masharti yote ya mkataba, masharti na maelezo ya hati ya zabuni kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa. Ikiwa Zabuni haitakidhi vigezo vilivyowekwa haitakubalika na kukataliwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za ununuzi na uondoshwaji wa mali za umma.

Kwa mujibu wa mapitio ya ripoti za tathmini na nyaraka za mikataba ukaguzi ulibaini kuwa mkataba ulitolewa kwa wazabuni M/S Sanfansisco na M/S. Pumps for Afrika hawakuwa na sifa kutokana na kushindwa kuzingatia mahitaji yafuatayo ya zabuni:-

**i. Mabadiliko ya kipindi cha uhalali wa zabuni**

Kifungu nambari 17.1 cha taarifa ya tathmini ya zabuni (Zabuni data sheet) iliyotolewa kwa wazabuni ilieleza kuwa kipindi cha uhalali cha zabuni kitakuwa siku 120. Pia, Sehemu ya 17 ya Maagizo kwa wazabuni ilieleza kuwa zabuni itabaki halali kwa kipindi kilichoainishwa katika tathmini ya takwimu ya zabuni baada ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha zabuni iliyoagizwa na Taasisi ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma chini ya ITB Kifungu nambari 22. zabuni halali kwa kipindi kifupi itakataliwa na Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji kama ni zabuni isiyokidhi vigezo.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya zabuni zilizowasilishwa na waombaji na kubainika kwamba kampuni ya M/S SAN FRANSISCO iliwasilisha zabuni iliyoonyesha muda uliokubalika wa siku 30 na kampuni ya Pumps for Africa iliwasilisha zabuni iliyoonyesha muda uliokubalika wa siku tano(5) badala ya siku 120 zilizoanishwa katika taarifa ya tathmini ya zabuni

Mapitio ya zabuni iliyowasilishwa na wauzaji waliopewa mkataba huo yalibainisha kuwa M/S SANFRANSISCO ilitoa kipindi cha uhalali wa zabuni ya siku 30 na Pampu for Afrika ilitoa kipindi cha uhalali wa zabuni ya siku 5 badala ya siku 120

zilizoainishwa Hii ilionyesha kuwa baada ya siku 30 na siku 5 kutoka tarehe ya kuwasilisha, zabuni iliyowasilishwa na M/S SAN FRANCISCO na M/S Pumps for Afrika kwa mtiririko huo ilikosa vigezo vya ushindani kutokana na zabuni hizo kuwa nje ya kipindi cha uhalali wa zabuni jambo ambalo huenda likapelekea wazabuni hao kuondoa zabuni zao baada ya kumalizika kwa kipindi cha uhalali wa zabuni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa mzabuni ambaye hakuzingatia mahitaji ya zabuni anachukuliwa kama zabuni iliyokosa ushindani kutokana na kutokukidhi vigezo.

### ii. Kutowasilishwa kwa dhamana ya Zabuni (Tender Security)

Kulingana na Kifungu nambari 18.1 cha ITB, Mzabuni atatoa kama sehemu ya zabuni yake, Dhamana ya zabuni katika fomu ya awali na kwa kiasi na sarafu iliyoainishwa katika tathimini ya taarifa ya zabuni au Azimio la Kuhifadhi zabuni kama ilivyoelezwa katika tathmini ya taarifa ya zabuni. Kifungu cha 1.1 cha tathmini ya taarifa ya zabuni (BDS) kilisema kuwa; zabuni lazima iambatane na dhamana ya zabuni ya asilimia 2.5 ya bei iliyonukuliwa katika hundi ya Dhamana ya Benki.

Pia, Kifungu nambari 18.6 cha ITB kilionesha kuwa, zabuni yoyote ambayo haitaambatanishwa na dhamana ya zabuni kulingana na ITB kifungu kidogo cha 18.1 au 18.3 itakataliwa na Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kama iliyokosa vigezo.

Mapitio ya zabuni iliyowasilishwa na wasambazaji waliopewa mkataba ilibainisha kuwa hakuna hata mmoja wao aliyewasilisha dhamana ya zabuni katika hati ya dhamana ya benki kama ilivyoelezwa katika tathmini ya taarifa ya zabuni. Ukaguzi ulibaini kuwa msambazaji aliwasilisha fomu ya tamko la zabuni tu.

Mchakato wa zabuni ulikuwa hatarini kwani taasisi ya ununuzi haikuwa na kiasi chochote cha kudai kama fidia ikiwa mzabuni aliondoa zabuni yake au alishindwa kukubali tuzo ikiwa alikuwa mzabuni aliyefanikiwa kuchaguliwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa mzabuni ambaye hakuzingatia mahitaji ya zabuni anachukuliwa kama zabuni isiyo na sifa na kuondoshwa katika mchakato wa ushindani.

### iii. Marekebisho ya mchanganuo wa mahitaji ya mteja

Mchanganuo wa mahitaji katika hati ya zabuni ilimtaka mzabuni kuwasilisha nukuu ya kuwasilisha pampu katika Afisi za Mamlaka ya Maji.

Hata hivyo, mapitio ya kumbukumbu zilizowasilishwa na M/S SAN FRANCISCO yalibainisha kuwa muuzaji aliwasilisha kumbukumbu hiyo kwa sharti kwamba, Uchukuzi (Freight) na ufungaji utatozwa tofauti ambayo ilikuwa kinyume na

mahitaji ya mteja ambayo ilimtaka muuzaji kuwasilisha ofa ya kupeleka pampu katika Afisi kuu ZAWA. Uwasilishaji wa muuzaji ulihitajika kuchukuliwa kama zabuni isiyokidhi vigezo kwani haikuzingatia mahitaji ya zabuni.

Kutokana na mzabuni kupewa hati ya zabuni isiyokidhi vigezo ilipelekea kujitokeza kwa gharama za ziada za USD 6,000 kwa ajili ya utoaji na uchukuzi wa mizigo ambayo ilikua nje ya mpango kazi uliowasilishwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa zabuni zinazotolewa zinakidhi vigezo vilivyowekwa ili kuepusha kujitokeza kufanyika kwa malipo ya ziada,Aidha kutokutoa zabuni kwa wazabuni wasio na sifa kunaweza kupelekea kuokoa kiwango cha fedha ambacho kimelipwa kwa mkandarasi kutokana na kukosa sifa.

### 15.2.2 Ukiukwaji wa maamuzi ya kamati ya tathmini

Kwa mujibu wa Kanuni nambari 138(1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya 2020, tuzo hiyo itatolewa ndani ya kipindi cha uhalali wa zabuni kwa mzabuni ambaye zabuni yake imedhamiriwa kuwa zabuni iliyotathminiwa vizuri .

Mapitio ya ripoti ya tathmini ilionesha kuwa kamati ya tathmini ilipendekeza kwamba M/S INFRASOL LTD apewe tuzo ya mkataba wa usambazaji wa pampu (Submersible). Hata hivyo, ilibainika kuwa mkataba huo alipewa M/S SANFRANSISCO LTD kwa loti 1 na 4 na M/S Pump for Africa LTD akapewa loti 2, 3, na 5 bila ya kuzingatia maamuzi ya kamati ya tathmini.

Wakati wa tathmini, M/S SAN FRANCISCO aliondolewa katika tathmini ya awali kama mzabuni asiyekidhi vigezo wakati M/S Pumps for Afrika iliondolewa katika tathmini ya kina kwani zabuni yake haikuzingatia mahitaji ya zabuni.

Kwa upande mwingine, mahojiano na maafisa wa ZAWA yalibainisha kuwa hakukuwa na kikao cha bodi ya zabuni ambacho kiliidhinisha mkataba wa zabuni kwa M/S SAN FRANCISCO na M/S Pumps for Afrika jambo ambalo limetiashaka juu ya upatikanaji wazabuni hao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unazingatia maamuzi ya kamati ya tathmini ili kuweza kuwapata wazabuni wenye uwezo na sifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.

### 15.2.3 Kuongezeka kwa malipo ya awali kutoka asilimia 10 hadi 50 baada ya mchakato wa zabuni

Kwa mujibu wa sehemu ya 43.1 na 43.2 ya tathmini ya taarifa ya zabuni, Malipo ya awali asilimia ndogo itakua asilimia 10 ya Bei ya Mkataba na kiwango cha juu cha malipo ya awali kitakuwa asilimia 15 ya Bei ya Mkataba.

Mapitio ya Mikataba iliyosainiwa na wauzaji wa pampu ilibainisha kuwa, kiasi cha malipo ya awali kilibadilishwa kuwa asilimia 50 ya bei ya mkataba. Kutokana na kutokuwepo kwa vikao vya makubaliano (negotiation minutes) zilizoombwa na Wakaguzi, Wakaguzi hawakuweza kutathmini ikiwa malipo ya awali yalijadiliwa wakati wa mkutano wa makubaliano. Hata hivyo kanuni ya 134(2) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020, inazuia majadiliano ambayo yatasababisha kubadilisha vipengele na masharti ya mkataba ulioelezwa katika hati ya zabuni.

Mapitio ya kumbukumbu zilizowasilishwa na M/S SAN FRANCISCO zilibainisha kuwa, malipo ya awali ya asilimia 50 yalikuwa katika hati iliyotolewa na muuzaji katika zabuni zilizowasilishwa, ZAWA ilikubali masharti hayo kinyume na kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020.

Kutokana na kuwekwa kwa asilimia 10 ya malipo ya awali katika hati ya zabuni kulipelekea kujitokeza kwa ushindani mdogo wa wazabuni wanne (4) waliojitokeza ambao ni sawa na asilimia 45 kati ya wazabuni tisa (9) walioalikwa na kuwasilishiwa hati ya zabuni.

Kuongeza asilimia ya malipo ya juu baada ya mchakato wa zabuni hupunguza ushindani kwa wazabuni wengine kwani pindipo hati ya zabuni ikiainisha malipo ya awali ya asilimia 50 inaweza kupelekea kujitokeza kwa ushindani mkubwa na kuwapata wazabuni wenye sifa wa utekelezaji wa mradi kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa kiasi cha kutosha cha malipo ya awali kimeainishwa katika nyaraka za zabuni ili kushajihisha upatikanaji wa wazabuni wenye sifa na uwezo wa utekelezaji wa miradi iliyopangwa.

### 15.2.4 Malipo ya awali yasiyokua na dhamana ya benki USD 1,147,103.615 (shilingi 2,654,130,419)

Kwa mujibu wa kifungu nambari 18.6 cha masharti maalum ya mkataba, malipo ya awali yatalipwa ndani ya siku thelathini (30) za kusaini mkataba, na baada ya kuwasilisha madai na dhamana ya benki kwa kiasi kinacholingana ambapo bidhaa zitapokelewa kama ilivyobainishwa katika hati ya zabuni.

Mapitio ya hati ya mkataba yalibainisha kuwa, wazabuni wote wa pampu hawakuwasilisha dhamana ya malipo ya awali kama ilivyobainishwa katika mkataba.

Aidha, ukaguzi umebaini hakukuwa na hatua yoyote iliyochukuliwa kwa upande wa ZAWA kutokana na wasambazaji hao kutoweza kufuata vigezo na masharti ya mkataba.

Licha ya ukweli kwamba, mkataba ulimruhusu mteja kushikilia malipo hadi muuzaji azingatie masharti yaliyobainishwa kwenye mkataba, ZAWA ilifanya malipo ya awali kwa wazabuni kinyume na masharti ya mkataba.

Kutokana na kutowasilishwa kwa dhamana ya malipo ya awali ya asilimia 50 ya bei ya mkataba (asilimia 50 ya USD 2,294,207.23) sawa na USD 1,147,103.615 (shilingi 2,654,130,419) ambayo ililipwa kwa mzabuni bila ya kuzingatia vigezo na masharti yaliyoainishwa katika mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa unasimamia ipasavyo masharti yaliyoainishwa katika mkataba ili kuepusha kujitokeza kwa hasara itokanayo na kufanyika kwa malipo kwa mzabuni ambae hakukidhi vigezo vya kufanyiwa malipo.

## 15.3 Dosari katika udhibiti wa ubora

### 15.3.1 Wauzaji hawakutoa hati ya dhamana kwa pampu zilizotolewa

Kulingana na Kifungu nambari 11 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SSC), wakati wa usambazaji wauzaji walitakiwa kuwasilisha hati ya dhamana (warrant certificates) kutoka kwa mtengenezaji au muuzaji. Pia Kifungu cha 16 cha SSC kinasema kwamba, kipindi cha udhamini kitakuwa miezi 12 kutoka tarehe ya kusambaza Zabuni, muuzaji atazingatia dhamana za utendaji zilizoainishwa katika mkataba.

Kupitia mahojiano na maafisa wa ZAWA ilibainika kuwa, licha ya kushindwa kwa muuzaji kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi ambao ulipaswa kutumika kushughulikia hati ya muuzaji, wauzaji wa pampu hawakuwasilisha hati za dhamana kulingana na kifungu nambari 11 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC).

Hati ya dhamana ya pampu zilizonunuliwa haikuthibitishwa kwa sababu hakuna kitu chochote kinachoweza kumlazimisha msambazaji kuwajibika iwapo hakuweza kutekeleza vyema majukumu yake kama ilivyoainishwa katika mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa vifaa vilivyonunuliwa vinakuwa na hati za dhamana kutoka kwa mtengenezaji au msambazaji ili kuepusha kujitokeza kwa hasara inayotokana na vifaa vilivyokosa sifa.

### 15.3.2 Kutofanyiwa majaribio ya utendaji kazi kwa pampu zilizowasilishwa

Kifungu nambari 10 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) kilieleza kuwa msambazaji kwa kushirikiana na mnunuzi atafanya vipimo vyote na ukaguzi wa Zabuni ili kuthibitisha kuwa sifa na utendaji wa Zabuni zinazingatia kanuni na viwango vya kiufundi vya vipimo chini ya Mkataba.

Mapitio ya ripoti za ukaguzi wa pampu yalibainisha kuwa, mnamo tarehe 3 Novemba na 05 Oktoba, 2022 timu ya wafanyakazi wa Ufundi kutoka ZAWA ilitembelea majengo ya msambazaji kukagua pampu zilizotengenezwa chini ya ununuzi. Wakati wa ziara hiyo, wafanyakazi wa kiufundi walikagua vipimo vya pampu na vifaa vyao.

Ilibainisha zaidi kuwa, wakati wa uwasilishaji wa pampu wafanyakazi wa kiufundi wa ZAWA walikagua pampu zilizowasilishwa. Ukaguzi uliofanywa kulingana na usomaji wa vipimo vya pampu zilizowasilishwa ili kutathmini ikiwa zilikubaliana na mahitaji ya mnunuzi.

Hata hivyo, kupitia mahojiano yaliyofanywa na maafisa wa ZAWA walibaini kuwa hakukuwa na vipimo vilivyofanywa kwenye pampu zilizowasilishwa ili kuangalia ikiwa vipimo vya pampu vilivyoainishwa vinalingana na utendaji halisi wa pampu.

Kulingana na maafisa wa ZAWA, kwa kawaida hufanya vipimo kwenye pampu vilivyowasilishwa wakati wa ufungaji. Hata hivyo, wakaguzi waliomba matokeo ya majaribio kwa pampu ambazo tayari ziliwekwa lakini matokeo hayakupatikana.

ZAWA ilikubali kupokea pampu kulingana na vipimo vilivyoonyeshwa katika BoQ , ingawa pampu hizo hazikufanyiwa majaribio ya utendaji kazi ili kupata uthibitsho wa kuwa mashine zilizoagizwa ndio ambazo zilitakiwa kwa mujibu wa mkataba, badala yake mashine hizo zilisambazwa kwenye visima na kuanza kutumika bila ya kufanyiwa vipimo vya majaribio.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa majaribio yanafanywa kwenye pampu zilizonunuliwa ili kutathmini hali ya utendaji wa pampu ukilinganisha na mahitaji yaliyoainishwa kwa mujibu wa mkataba.

### 15.3.3 Uwasilishaji wa pampu zenye uwezo wa chini wa kusukuma maji kuliko mahitaji

Ubora wa mipira ya Pampu za maji inayozamishwa chini ya kisima (Grundfos Submersible) ulionyesha kuwa, kiasi cha maji ni sawa na kichwa cha kisima (well head). Ukaguzi uliangalia utendaji wa pampu na kubaini uwepo wa pampu ndogo ambazo hazikukidhi uwezo wa kusukuma kama ilivyoainishwa katika orodha ya mchanganuo wa mahitaji. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa pampu zilizofungwa zilikuwa zinazalisha kiwango kidogo cha maji kuliko mahitaji yaliyokuwa yakihitajika kwa mujibu wa mchanganuo wa mahitaji ulioandaliwa na ZAWA.

Kutokana na dosari hiyo pampu zilizowekwa kusukuma maji kwa urefu ambao uliainishwa katika mchanganuo wa mahitaji itazalisha kiasi kidogo cha maji kuliko inayohitajika kutokana na hali hiyo ujazo wa tangi la kuhifadhia maji utachukuwa masaa mengi hadi kufikia ujazo unaohitajika. Kutokana na hali hiyo upo uwezekano mkubwa wa kujitokeza maharibiko ya mashine hiyo kutokana na kutumia masaa mengi kusukuma kiwango cha maji kinachohitajika.

Jadweli hapa chini linaonesha hali ya pampu zilizowasilishwa na wauzaji zenye uwezo wa kusukuma kuliko ilivyoainishwa.

### Jadweli Nambari 72: Inaonesha hali ya pampu zilizowasilishwa na wauzaji

| ZAWA requirements | Supplied pumps | Remarks |
|---|---|---|
| **Pumps Supplied by Sanfransisco** | | |
| Submersible Bore Hole Pump of 22KW capable of producing 58m3/h @ 105 m head. | Submersible Bore Hole Pump, capable of producing 58m3/h @ 90 m head (SP 60-11) | At the required head of 105m the supplied pump will not produce 58m3/h as per requirement instead it will produce around 48m3/h which is 10 m3/h less than the required quantity of water. |
| Submersible Bore Hole Pump of 15kW, capable of producing 45m3/h @ 100m head | Submersible Bore Hole Pump of 15kW, capable of producing 45m3/h @ 87m head (SP 46-10) | At the required head of 100m the supplied pump will not produce 45m3/h as per requirement instead it will produce around 37m3/h which is 8 m3/h less than the required quantity of water. |
| Submersible Bore Hole Pump of 15kW, capable of producing 50m3/h @ 100m head | Submersible Bore Hole Pump of 15kW, capable of producing 50m3/h @ 93m head (SP 46-12) | At the required head of 100m the supplied pump will not produce 45m3/h as per requirement instead it will produce around 47m3/h which is 3 m3/h less than the required quantity of water. |
| **Pump Supplied by Pumps for Africa** | | |
| Submersible Bore Hole Pump of 15kW, capable of producing 46m3/h @ 100m head | 15C21910 SP46-10N RP3 6” 3x380-415/50 15KW | At the required head of 100m the supplied pump will not produce 46m3/h as per requirement instead it will produce around 37m3/h which is 9 m3/h less than the required quantity of water. |
| Submersible Bore Hole Pump of 11kW, capable of producing 30m3/h @ 120m head | 13C01913 SP30-13N RP3 6” 3X380-415/50 11KW | At the required head of 120m the supplied pump will not produce 30 m3/h as per requirement instead it will produce around 21m3/h which is 9m3/h less the required quantity of water. |
| Submersible Bore Hole Pump of 15kW, capable of producing 46m3/h @ 120m head | 15C21910 SP46-10N RP3 6” 3X380-415/50 15KW | At the required head of 120m the supplied pump will not produce 46m3/h as per requirement instead it will produce around 20m3/h which is 26m3/h less than the required quantity of water. |

| ZAWA requirements | Supplied pumps | Remarks |
|---|---|---|
| Submersible Bore Hole Pump of 11kW, capable of producing 30m3/h @ 120m head | 13C01913 SP30-13N RP3 6"3X380-415/50 11KW | At the required head of 120m the supplied pump will not produce 30 m3/h as per requirement instead it will produce around 21m3/h which is 9m3/h less than the required quantity of water. |
| Submersible Bore Hole Pump of 15kW, capable of producing 35m3/h @ 130m head | 13C01917 SP30-17N RP3 6"3X380-415/50 15KW | At the required head of 130m the supplied pump will not produce 35 m3/h as per requirement instead it will produce around 30m3/h which is 5 m3/h less than the required quantity of water. |
| Submersible Bore Hole Pump of 15kW, capable of producing 40m3/h @ 100m head | 15C21910 SP46-10N RP3 6" 3X380-415/50 15KW | At the required head of 130m the supplied pump will not produce 40m3/h as per requirement instead it will produce around 37m3/h which is 3m3/h less than the required quantity of water. |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi wa kumbukumbu za upokeaji wa pampu*

Jadweli hapo juu linaonyesha kwamba katika pampu zilizoainishwa hazitoweza kusukuma na kuzalisha kiasi cha maji kwa mujibu inavyohitajika.

Hali hii imetokana na kushindwa kufuatwa kwa mahitaji na maelekezo ya mnunuzi wakati wa uwasilishaji wa pampu zilizonunuliwa jambo ambalo limepelekea uwepo wa uzalishaji mdogo wa maji unaochukuwa muda mrefu kujaza matangi ya kuhifadhia maji

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa unazingatia vigezo vilivyowekwa kwenye mkataba kuhusiana na ununuzi wa pampu za maji zinazoendana na mahitaji kwa lengo la kupima ubora wa utendaji utakaopelekea kiwango kikubwa cha uzalishaji wa maji na hatimae kupatikana kwa tija iliyokusudiwa kwa wananchi.

# SURA YA KUMI NA SITA



# 16.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USAMBAZAJI wa vifaa vya maji

## 16.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi maalum kwa miradi iliyokaguliwa juu ya usambazaji wa vifaa vya maji kwa utekelezaji wa miradi.

Kutokana na usambazaji wa vifaa vya usambazaji wa maji ikiwemo kusambaza Submersible Pumps, Motor na Control Panel, MP204 na Sluice Valve na kampuni ya M/S Saphire Engineering (T) Limited kwa thamani ya shilingi 330,518,625 kama ilivyowasilishwa katika Jadweli hapa chini.

**Jadweli Nambari 73: Maelezo ya mkataba**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jina la Mkataba** | Supply for Submersible Pumps, Motor and control Panel, MP204, and Sluice Valve for Emergency Procurement | | |
| **Nambari ya Mkataba** | SMZ/ZAWA/13/JUNE/G/EP/2021-2022/147. | | |
| | | | |
| **Msambazaji aliyepewa tuzo** | **Bei ya Mkataba (Shilingi)** | **Tarehe ya mkataba** | **Kipindi cha Utekelezaji** |
| **M/S Saphire Engineering (T) Limited** | 330,518,625 | 27/06/2022 | Wiki 2 |

*Chanzo: Hati ya Mkataba*

Ukaguzi huo unatambua juhudi zinazofanywa na ZAWA katika utoaji wa huduma ya dharura kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa maji safi, salama na ya uhakika kwa wakaazi wa Zanzibar. Pamoja na jitihada zilizofanywa na ZAWA Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:

## 16.2 Kushindwa kuwasilisha dhamana ya benki na dhamana ya utendaji kazi

Kifungu nambari 9.1 na 9.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinahitaji, ndani ya siku thelathini (30) za kupokea taarifa ya kupatiwa Mkataba, Mzabuni aliyofanikiwa kutoa kwa Mnunuzi dhamana ya utendaji katika kiasi kilichoainishwa katika Masharti Maalumu ya Mkataba (SCC) na itakuwa katika fomu ya Dhamana ya Benki au fomu nyingine yoyote iliyoonyeshwa katika SCC.

Kutokana na mapitio ya majalada na mikataba ya mradi ukaguzi ulibaini uwepo wa dhamana tofauti uliowasilishwa mbali na ule unaohitajika katika mkataba. Uchambuzi wa mkataba uliopitiwa na dhamana wa utendaji kazi unaohitajika na usalama wa utendakazi uliowasilishwa kama inavyoonyeshwa.

Kifungu nambari 9.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kinasema kuwa "Kiasi cha dhamana ya utendaji kazi itakuwa asilimia kumi (10) ya Bei ya Mkataba ambapo taarifa ya tuzo yenye kumbukumbu namba. ZAWA / U.10/2/VOL.148

ya tarehe 19 Juni 2022 inaeleza kwamba Wakati wa mchakato wa malipo ni lazima iwasilishwe dhamana ya Benki ya asilimia 50 ya bei ya mkataba pamoja na dhamana ya utendaji kazi kwa asilimia 10 ya Bei ya Mkataba kutoka kwa Benki ya Biashara yenye sifa inayotambulika.

Baada ya mahojiano na maafisa wa ZAWA ukaguzi ulifanya uhakiki wa hati za malipo na kubaini na uwepo wa malipo ya shilingi 165,259,312.50 sawa na asilimia 50 ya bei ya mkataba ambayo yalilipwa kwa mzabuni bila kuwasilisha dhamana ya benki na dhamana ya utendaji kazi kulingana na mahitaji ya mkataba.

Kutokana na dosari hiyo ikiwa msambazaji atashindwa kuwasilisha zabuni au kuzingatia hali yoyote ya mkataba au hasara yoyote itakayotokana na kushindwa kwa mzabuni kukamilisha majukumu yake chini ya Mkataba ZAWA haitaweza kumfungulia mashtaka wala jambo ambalo linaweza kupelekea ZAWA kupata hasara.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa unazingatia sheria na masharti ya mkataba na kuhakikisha kwamba malipo yanafanywa kwa kuzingatia masharti maalum ya mkataba yaliyoainishwa.

## 16.3 Maelezo yasiotosheleza yaliyoandaliwa kwa ununuzi wa Sluice Valve

Kifungu nambari 21.1 kinasema kwamba "Kulingana na kifungu cha 20 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC), hakuna tofauti au marekebisho ya masharti ya mkataba yatafanywa isipokuwa kwa marekebisho yaliyoandikwa na kusainiwa na pande zote mbili.

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa vipimo vilivyobainishwa katika mchanganuo wa mahitaji , maelezo ya kiufundi na fomu za Ukaguzi za tarehe 08 Novemba 2022, Ankara ya Kodi yenye namba 0317 ya tarehe 23/06/2022, na hati za utoaji Zabuni (delivery note) yenye namba 0614 ya tarehe 08 Novemba, 2022 na kubaini kwamba vifaa vinavyohusiana na uchujaji wa maji (Sluice Valve) havikuwasilishwa katika Afisi za ZAWA.

Aidha, baada ya mahojiano na maafisa wa ZAWA ukaguzi ulibaini vifaa vilivyowasilishwa katika mchanganuo wa vipimo vilikuwa vya plastiki na kupendekezwa kununuliwa vifaa vya chuma (Sluice Valve) jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika marekebisho hayo hayakuweza kufanyika.

### Jadweli Nambari 74: Kutokupokelewa kwa Sluice Valve

| | Eneo | Jina la Kipengele | vipimo | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| **Unguja** | Saateni Tangini – Mjini | Butterfly Flanged Sluice Valve | DN450 – DI Blue Color-18" | 2 |
| | Amani Mjini | Butterfly Flanged Sluice Valve | DN300 – DI Blue Color-12" | 2 |
| | Amani Mjini | Butterfly Flanged Sluice Valve | DN350 – DI Blue Color-14" | 1 |
| **Pemba** | Tangini Machomanne | Butterfly Flanged Sluice Valve with adopter DN16 - DI Blue Color-12" | DN16 – DI Blue Color-12" | 2 |
| | Tangi la Taifu na Mtemani | Butterfly Flanged Sluice Valve with adopter DN16 - DI Blue Color-10" | DN16 – DI Blue Color-10" | 2 |

*Chanzo: Maelezo ya Hati ya Mkataba na Waandishi wa Mradi*

Kucheleweesha utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa dharura kutasababisha kuongezeka zaidi kwa gharama za ununuzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa idara ya mtumiaji (user department) ya ZAWA inashirikishwa ipasavyo wakati wa maandalizi ya mahitaji na utoaji wa vigezo ili kuepuka kujitokeza kwa changamoto katika mchakato wa manunuzi.

# SURA YA KUMI NA SABA



# 17.0 MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU USAMBAZAJI WA MITAMBO YA KUCHIMBIA VISIMA

## 17.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi maalum kuhusu usambazaji wa mitambo ya kuchimbia visima (Combination Rigs Hammers) uliyohitajika katika utekelezaji wa miradi ambapo kampuni ya M/S Amtas Enterprise Supplier ilipewa tuzo ya zabuni hii inayohusu Loti 3 kwa mkataba nambari SMZ/IMF/No 104/G/IRNCT/2021/2022/05 wa tarehe 29 Januari 2022 wenye thamani ya shilingi 1,504,603,044 ambapo mzabuni alitakiwa kutekeleza kazi hiyo kwa muda wa wiki 10 kuanzia tarehe ya kusainiwa mkataba.

## 17.2 Dosari zilizobainika katika utekelezaji wa mradi

Katika utekelezaji wa mradi huo ukaguzi uliweza kubaini dosari mbali mbali kama zifuatazo:-

### 17.2.1 Kushindwa kuwasilisha dhamana ya benki na dhamana ya utendaji kazi kwa msambazaji

Kifungu nambari 9.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kilitaka kwamba, ndani ya siku thelathini (30) baada ya kupokea taarifa ya tuzo ya mkataba, Mzabuni aliyefanikiwa atato kwa Mnunuzi Dhamana ya Utendaji Kazi kwa kiasi kilichoainishwa katika kifungu Maalum cha Masharti ya Mkataba . Pia, Kifungu nambari 9.2 kinasema kwamba "kiasi cha dhamana ya utendaji kazi kitalipwa kwa Mnunuzi kama fidia kwa hasara yoyote inayotokana na kushindwa kwa Muuzaji kukamilisha majukumu yake chini ya Mkataba.

Masharti ya jumla ya Mkataba Kifungu nambari 9.1 kinasema kwamba "Kiasi cha dhamana ya utendaji kazi, kama asilimia ya Bei ya Mkataba, itakuwa asilimia 10 ya Bei ya Mkataba. Barua ya mwaliko yenye nambari ya kumbukumbu ZAWA/U:10/VOL.1/47 ya tarehe 21/12/2021 inasema kuwa "Zabuni zote lazima ziambatane na Dhamana ya zabuni (Tender Security) kwa kiasi na muundo uliotajwa katika mchanganuo wa taarifa ya zabuni (Zabuni data sheet)".

Ukaguzi ulifanya mahojiano na maafisa wa ZAWA pamoja na kufanya ukaguzi wa hati za malipo na kubaini kuwa malipo ya awali ya asilimia 50 yenye thamani ya shilingi 752,301,522 yalibainika kulipwa kwa mzabuni Amtas Enterprise bila kuwasilisha dhamana ya benki kulingana na mahitaji ya mkataba kama ilivyobainishwa katika Jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 75:Malipo yaliyofanyika kwa muuzaji bila kuwasilisha dhamana ya Benki**

| Nambari ya Hati | Tarehe ya Hati | Jina la msambazaji | Kiasi (Tsh) |
|---|---|---|---|
| PV2000194 | 24/02/2022 | M/S Amtas Enterprise | 641,091,732.00 |
| PV2000257 | 17/08/2022 | M/S Amtas Enterprise | 98,126,285.00 |
| PV2000204 | 01/03/2022 | M/S Amtas Enterprise | 13,083,505.00 |
| **Jumla** | | | **752,301,522.00** |

*Chanzo: Hati za Malipo*

Kutokana na malipo yaliyolipwa kwa mzabuni pasi na kuwasilisha hati ya dhamana kunaweza kupelekea kujitokeza kwa hasara pindipo mzabuni atakaposhindwa kutekeleza matakwa ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa malipo yote yaliyofanyika yanazingatia matakwa ya hati ya mkataba ili kunusuru kujitokeza kwa dosari katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

## 17.3 Ukiukwaji wa taratibu za utoaji wa zabuni

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa ukiukwaji wa taratibu za utoaji wa zabuni ambapo kwa mujibu wa Mapendekezo ya Ripoti ya Tathmini imempendekeza mzabuni M/S OSAJU COMPANY LTD (Mzabuni nambari 3) ambae amekuwa na sifa na uwezo wa kutekeleza Mkataba kwa loti Nambari. 2 na 3 kwa mujibu wa zabuni ya zabuni iliyowasilishwa.

Ukaguzi ulifanya mahojiano na maafisa wa ZAWA na kubaini kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba ZAWA/A/10/10/150 ya tarehe 21 Januari, 2022 ilibainisha mzabuni M/S Amtas Enterprise alipewa mkataba wa utoaji wa mashine za Rigs mbili (2) za kuchimba visima vyenye thamani ya USD 651,600 bila ya kodi ambapo hakuwa mzabuni aliyestahiki kupewa zabuni kulingana na mapendekezo ya ripoti ya tathmini ya zabuni.

Kupewa zabuni kwa mzabuni asie na sifa huwenda ilisababishwa na kutokuzingatiwa utaratibu wa ununuzi na uharaka wa utekelezaji wa mradi jambo ambalo lingeweza kupatikanwa kwa hasara ikiwa mzabuni atashindwa kutekeleza matakwa ya mkataba aliyoomba kulingana na mahitaji ya zabuni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa mapendekezo ya tathmini ya Bodi ya Zabuni yanapaswa kuzingatiwa na kufanyiwa kazi na pindipo pakijitokeza kasoro zozote za kutokutekeleza mapendekezo ya Bodi ya Tathmini ni vyema zibainishwe sababu za msingi zilizopelekea kufanyika uamuzi huo kwa maslahi ya taifa.

## 17.4 Kuchelewa kuwasilishwa kwa mashine za kuchimbia kisima (Riggs)

Kifungu nambari 17.5 kinasema kuwa "muda wa mkataba utakuwa wiki kumi (Miezi Miwili na Nusu)", Masharti ya Jumla ya Malipo ya Mkataba Kifungu nambari 18 cha Mkataba kinasema kuwa "Zabuni hizo zitawasilishwa katika Makao Makuu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar Barabara ya Malawi Msikiti Mabluu na Afisi ya Pemba Machomane Chakechake Pemba".

Kutokana na mapitio ya mkataba na rasimu ya hati ya usafirishaji wa mzigo yalibainsha kwamba mkataba ulisainiwa tarehe 29 Januari, 2022 na mzigo kuwasili tarehe 13 Disemba, 2022 katika Bandari ya Zanzibar jambo ambalo ni kinyume na vigezo na masharti ya mkataba husika.

Hata hivyo kutokana na majadiliano na maafisa wa ZAWA yalieleza kwamba mitambo ya kuchimbia visima bado ipo katika bandari ya Zanzibar tangu ilipowasili ingawa taratibu muhimu za utoaji wa mizigo hiyo zilifanywa lakini bado kulikuwa na uchelewaji wa utoaji wa mizigo hiyo kutoka bandarini na kuwasilishwa makao makuu ya ZAWA jambo ambalo lilipelekea kuwepo kwa gharama za ziada za uhifadhi wa mzigo zenye thamani ya shilingi 27,324,000 kwa mujibu wa ankara ya malipo namba 015/07 ya tarehe 13 Julai, 2023.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unafanya ufuatiliaji wa karibu ili kubaini mahitaji yanayohitaji kabla ya kuwasili kwa mizigo bandarini ili kuepusha kujitokeza kwa gharama za tozo zinazotokana na ucheleweshaji wa utoaji wa mizigo bandarini.

## 17.5 Dosari iliyobainika katika malipo ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) shilingi 98,126,285

Kwa mujibu wa kifungu 10(2) cha Sheria Nambari 4 ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya 1998 inaeleza kwamba VAT haitozwi kwa usambazaji wa msamaha, na punguzo au mkopo wa ushuru wa pembejeo kwa ununuzi uliofanywa kuhusiana na usambazaji wa msamaha.

Aidha, taarifa ya tuzo yenye kumbukumbu nambari ZAWA/A/10/10/150 ya tarehe 21 Januari, 2022 inasema kuwa "Hii ni kukujulisha kuwa mteja (ZAWA) amekubali ofa yako na umepewa mkataba wa usambazaji wa mashine mbili za kuchimbia visima (Rigs) vyenye thamani ya dola za Marekani 651,600.00 bila ya kodi.

Ukaguzi ulifanya mahojiano na maafisa wa ZAWA pamoja na uhakiki wa hati za malipo, stakabadhi za malipo na kubaini kuwa jumla ya shilingi 98,126,285.00 zililipwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kupitia stakabadhi namba 0992591 ya tarehe 01/03/2022 kuwa ni malipo ya kodi ya zuio.

Kutokana na dosari ya ufanyaji wa malipo uliobainishwa hapo juu huwenda ulitokana na kukosekana kwa umakini kwa watendaji wa ZAWA kufanya zuio kinyume na utaratibu jambo ambalo huwenda likapelekea kujitokeza kwa usumbufu juu ya urejeshwaji wa fedha zilizolipwa kinyume na utaratibu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unaongeza umakini katika ufanyaji wa malipo kwa kuzingatia hati ya zabuni pamoja na hati ya mkataba ili kuweza kujenga uaminifu na kuondosha usumbufu kwa wazabuni wakati wa kufanyika kwa malipo.

## 17.6 Malipo yaliyolipwa kwa msambazaji bila kuwasilisha dhamana ya benki shilingi 300,920,608.80

Kifungu nambari 18.4 (i) cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) kinasema kuwa "Malipo ya awali ni asilimia 50 ya bei ya mkataba , juu ya Utoaji wa Dhamana ya Benki' na Kifungu nambari 18.4 (ii) kinasema kuwa "Wakati wa uwasilishaji kamili, asilimia 50 ya bei ya mkataba italipwa kwa muuzaji ndani ya siku thelathini (30) baada ya kupokea na kukagua zabuni na baada ya kuwasilisha nyaraka zilizoainishwa katika Masharti ya Jumla ya Mkataba.

Mapitio ya Mikataba iliyosainiwa na wasambazaji wa mitambo ya kuchimba visima yalibainisha kuwa, kiasi cha malipo ya awali kilibadilishwa kuwa asilimia 70 ya bei ya mkataba badala ya asilimia 50 na kupelekea kufanyika kwa malipo ya shilingi 1,053,222,130.8 bila ya kuwasilisha dhamana ya benki na dhamana ya utendaji kazi.

Aidha,ukaguzi umebaini ZAWA imefanya malipo ya ziada ya asilimia 20 kwa hati namba PV2000253 ya tarehe 17 Agosti, 2022 yenye thamani ya shilingi 300,920,608.80 aliyolipwa mzabuni M/S Amtas Enterprise kama ni malipo ya awali bila ya kuzingatia matakwa ya hati ya zabuni.

Kutokana na dosari iliyobainishwa hapo juu ukaguzi umekitathmini kitendo cha kubadilishwa malipo ya awali kuwa asilimia 70 badala ya kile kilichonakiliwa kwenye hati ya zabuni ni kwenda kinyume na kanuni nambari 134(2) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 ambayo inazuia majadiliano ambayo yatasababisha kubadilisha vipengele na masharti ya mkataba ulioelezwa katika hati ya zabuni.

Kuongeza asilimia ya malipo ya juu baada ya mchakato wa zabuni hupunguza ushindani kwa wazabuni wengine kwani pindipo hati ya zabuni ikiainisha malipo ya awali ya asilimia 70 inaweza kupelekea kujitokeza kwa ushindani mkubwa na kuwapata wazabuni wenye sifa wa utekelezaji wa mradi kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa kiasi cha kutosha cha malipo ya awali kimeainishwa katika nyaraka za zabuni ili kushajihisha upatikanaji wa wazabuni wenye sifa na uwezo wa utekelezaji wa miradi iliyopangwa.

# SURA YA KUMI NA NANE



# 18.0 MATOKEO YA UKAGUZI JUU YA USAMBAZAJI WA "GPS RECEIVERS, GENERATORS NA ELECTROFUSION MACHINES"

## 18.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na usambazaji wa GPS Receiver, Electro Fusion Machine, na Pipe Fusion Machine kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya ZAWA kwa matumizi ya fedha za UVIKO-19.

Mkataba uligawanywa katika loti tatu ambapo M/S Sapphire Engineering (T) Limited ilipewa loti ya 1 na ya 3 na jumla ya shilingi 573,657,000 kama ilivyowasilishwa katika Jadweli hapa chini.

**Jadweli Nambari 76:Taarifa ya mkataba kwa usambazaji wa GPS Receiver, Electro Fusion Machine**

| **Kipengele cha Mkataba** | Matokeo ya ukaguzi juu ya usambazaji wa gps, jenereta, na mashine za umeme |
|---|---|
| Nambari ya Mkataba | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/02 |
| Jina la msambazaji | M/S Sapphire Engineering(T) Limited |
| Tarehe ya Kusaini mkataba | 29 Januari, 2022 |
| Taarifa ya tarehe ya tuzo | 21 Januari, 2022 |
| Taarifa ya Tarehe ya Kukubali | 25 Januari, 2022 |
| Muda wa Mkataba | Siku 21 |
| Tarehe inayotarajiwa kukamilika | 19 Febuari, 2022 |
| Tarehe halisi ya kukamilika kwa dhamana | 28 Januari, 2023 |
| Jumla ya kiasi cha Mkataba pamoja na VAT | Shilingi 573,657,000 |
| Jumla ya kiasi cha Mkataba uliorekebishwa pamoja na VAT | - |
| Maendeleo ya Malipo (%) hadi 30 Juni, 2023 | Asilimia 100 |
| Kuchelewa kukamilika kwa kazi | - |
| Riba ya kuchelewa malipo | - |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za Mkataba uliofanywa na Wakaguzi, 2023*

Ukaguzi huo unatambua juhudi zinazofanywa na ZAWA katika mabadiliko ya kusaidia huduma za maji za kila siku ili kuimarisha ufanisi katika utoaji wa huduma ya maji Zanzibar. Pamoja na jitihada zilizofanywa na ZAWA Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:-

## 18.2 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Kipengele cha Ununuzi

### 18.2.1 Kukosekana kwa Uwazi na haki katika Uteuzi wa Wazabuni

Kifungu nambari 8 (1) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinasema kuwa "Wakala wa Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma atahifadhi kumbukumbu za kutosha za maandishi za ununuzi ambazo zinahusika, na kumbukumbu hizo zitawaagiza wazabuni ambao wameitikia matangazo au walikaribia kutoa zabuni au kuwasilisha maelezo ya nia au pendekezo, wazabuni waliofanikiwa, wazabuni wasiofanikiwa na sababu (2) kulingana na kanuni ndogo (1), rekodi zitapatikana kwa mtu yeyote au bodi, na sehemu yake, kama ilivyoelezwa katika Kanuni hizi, itachapishwa katika gazeti na jarida maalum la zabuni. (3) Bila kuathiri kanuni ndogo (2), taarifa zinazohusiana na maelezo ya mradi zitapatikana kwa umma kwa namna na muundo kama itakavyoelekezwa katika miongozo iliyotolewa na Mamlaka.

Ukaguzi ulipitia ripoti ya tathmini inayohusiana na usambazaji wa vifaa vya mawasiliano ya kimtandao na zana za Mamlaka ya Maji Zanzibar na kubaini kuwa mchakato huo haukuwa wa wazi na wa haki. Dosari zilizobainika na ukaguzi ni kama zifuatazo:-

- Kukosekana kwa mzabuni M/S Sapphire Engineering (T) Limited katika hati ya zabuni iliyochaguliwa na kupokelewa lakini alikuepo katika kuwasilisha na kufungua zabuni.

- Mzabuni M/S Sapphire Engineering (T) Limited aliwasilisha bei za zabuni kwenye Loti ya 1 na Loti ya 2 wakati amepewa Loti ya 1 na Loti ya 3.

- Mzabuni M/S Sapphire Engineering (T) Limited alipewa tuzo dhidi ya ripoti ya tathmini na mapendekezo ya wajumbe wa kamati na kubainika kuwa ameshinda Loti ya 1 na sio na Loti ya 3.

- Kukosekana kwa ripoti ya tathmni iliyosainiwa kwa usambazaji wa Vifaa vya mawasiliano ya mtandao na zana zake.

Kukosekana kwa uwazi katika mchakato wa kumchagua mzabuni ni kwenda kinyume na masharti yaliyoainishwa katika muongozo wa fedha za Ahuweni ya UVIKO 19 na hivyo kupelekea kupunguza ufanisi katika mchakato wa ununuzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha kuwa unaongeza umakini katika kufanya uteuzi wa wazabuni ili kuongeza ufanisi wa mchakato wa uteuzi ambao utakuwa katika hali ya uwazi na haki kwa lengo la kuepusha kujitokeza kwa mgongano wa kimaslahi baina ya mzabuni na kamati ya tathmini.

### 18.2.2 Kukosekana kwa taarifa ya tuzo kwa wazabuni ambao hawajafanikiwa Zabuni zote

Kanuni nambari 10(3) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya 2021 kinasema kuwa "Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma haitabagua au miongoni mwa wazabuni kulingana na fomu ambayo wanasambaza au kupokea nyaraka, taarifa, maamuzi au mawasiliano mengine.

Ukaguzi umebaini kuwa kuna ukosefu wa taarifa ya tuzo kwa wazabuni wasiofanikiwa katika kazi zilizowasilishwa kuhusiana na utekelezaji wa mradi wa UVIKO-19.

Taratibu bora za manunuzi zinahitaji mzabuni asiefanikiwa kupewa taarifa ya tuzo, hakutakuwa na ubaguzi au upendeleo kwa mzabuni kwa kigezo cha fomu za maombi zilizowasilishwa au nyaraka zilizopokelewa, taarifa ya tuzo, maamuzi au mawasiliano mengine yoyote bila ya uwepo wa taarifa za kutokuwajuulisha wazabuni wasiofanikiwa, kwa mfano mzabuni M/S Sapphire Engineering (T) Limited amepewa mkataba wa usambazaji wa "GPS receiver, Electro Fusion and pipes fusion machine"

Kutokutolewa kwa taarifa ya tuzo kwa mzabuni asiefanikiwa juu ya usambazaji wa vifaa vya mawasiliano na zana ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZAWA kuhakikisha unatoa Taarifa ya tuzo kwa mzabuni asiyefanikiwa kwa usambazaji wa mradi wa Maji.